**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 3 Agosti, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:-**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH (K.n.y.MHE. WILLIAM J. KUSILA) - MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:-**

Maoni ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:-**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 335

**Ujenzi wa Daraja la Kishara**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imetambua umuhimu wa daraja la Kishara katika Jimbo la Muleba Kaskazini; na kwa kuwa, katika mwaka wa fedha uliopita Serikali ilitoa jumla ya Shs.milioni 30 kwa ajili ya kujenga daraja hilo hadi kukamilika lakini hadi sasa kazi hiyo haijakamilishwa:-

(a) Je, Serikali ina maelezo gani juu ya kucheleweshwa kwa kazi hiyo?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya kiwango cha Mkandarasi aliyepewa kazi hiyo?

(c) Je, Serikali inakiri ukweli kwamba, uwezo wa Mhandisi wa Wilaya ya Muleba dhidi ya uzito wa ujenzi wa daraja hilo umekuwa mdogo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, daraja la Kishara liko katika Wilaya ya Muleba, Kata ya Izigo na ni kiungo kati ya Kata ya Izigo na Kata ya Ruhanga. Barabara yenye daraja hili ina urefu wa kilomita 5.5 kutoka barabara inayoelekea Bukoba eneo la Katoke hadi barabara inayotokea Kamachumu eneo la Nyawaibaga. Mradi wa ujenzi wa daraja la Kishara ulianza tarehe 16/01/2005 na ulikadiriwa kugharimu jumla ya shilingi 30,927,000/= ambazo kati yake shilingi milioni 30 zimetolewa na Serikali na shilingi 927,000/= ni mchango wa Halmashauri. Kutokana na mapungufu yaliyojitokeza kwenye usanifu wa daraja ambapo awali makisio ya ujenzi wa kuta hayakujumuisha gharama za nondo zitakazotumika, jambohili lilisababisha gharama za ujenzi kuongezeka hadi kufikia shilingi milioni 53, na huo mradi kusimama. Fedha za nyongeza zilipatikana mwezi Mei, 2006 kiasi cha shiling milioni 23. Hata hivyo, mradi huu umechukua muda mrefu kukamilika kutokana na mvua kubwa iliyokuwepo kuanzia mwezi Machi hadi Mei, 2005 pamoja na mapungufu katika usanifu wa daraja hili.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mvua kuanza Mkandarasi alikuwa amefanikiwa kujenga kuta moja ya daraja upande wa Nyawaibaga na baada ya mvua akajenga kuta ya upande wa Katoke. Baada ya fedha kupatikana na mradi kusimama kwa muda merfu wataalamu walifanya tena uchunguzi kwa kazi zilizokuwa zimefanyika na kuona kwamba "*abutment*" ya upande wa Katoke haikidhi kiwango cha ubora wa daraja na wakashauri ivunjwe, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba imeunda Tume kutekeleza ushauri wa wataalamu. Kwa kuwa fedha zimepatikana Serikali inafanya juhudi ya kumalizia ujenzi wa daraja hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, Mkandarasi aliyepewa kuifanya kazi hiyo ni *MBAGO Enterprise*, Mkandarasi huyo anatambulika Serikalini na amesajiliwa na Bodi ya Wakandarasi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi alipewa kazi hiyo kwa kufuata taratibu zote za kutoa zabuni za Serikali. Kazi ilitangazwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mbao za matangazo, Mkoani Kagera pamoja na Wilaya zote zilizoko Mkoani Kagera. Wakandarasi watatu ambao ni *MBACO Enterprises Limited*, *Erastos Enterprises Limited* na Kanasho *Enterprises Limited* walijitokeza katika kazi hiyo kwa kufuata vigezo na sifa kama tangazo la zabuni lilivyoelekeza. Mkandarasi huyo alitimiza vigezo hivyo na kupewa kazi hiyo. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba uwezo wa Mhandisi wa Wilaya ya Muleba dhidi ya uzito wa ujenzi wa daraja hilo ulikuwa mdogo na ndiyo maana Halmashauri ililazimika kumtumia sasa Mhandisi wa Mkoa. Mhandisi wa Wilaya ya Muleba alisimamishwa kazi kuanzia tarehe 28 Februari, 2006 na hatua za nidhamu dhidi yake zinaendelea kuchukuliwa. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo mazuri aliyonipatia kuhusu swali hili.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda nilieleze masikitiko makubwa ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini. Daraja hili limekuwa likihitajika tangu tulipopata uhuru hadi leo. Kwa mara ya kwanza katika kipindi changu cha Ubunge Serikali ilikubali kutoa milioni 30 na Halmashauri ya Wilaya ya Muleba ikatoa Shs.927,000, lakini fedha hizo zikapotea kwa mazingira ambayo yalikuwa magumu mpaka wananchi ndio waliolalamika tukashirikiana kwenda kulalamika kuhusu daraja hili. Sasa milioni 30 zimetumika vibaya. Tumepata milioni 23, kwa hiyo kazi iliyokuwepo haiwezi kukamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inifahamishe na inithibitishie vipi wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini kwamba daraja hili litajengwa na likamilike?

Pili, Serikali imethibitisha kwamba uwezo wa Mhandisi wa Wilaya aliyekuwepo ni mdogo. Kwa hali hiyo ninaposema kwamba si kweli kwamba alitoa matangazo katika Mkoa mzima ili kushindanisha ujenzi wa daraja hili. Ninasema ukweli kwa sababu ni moja ya mambo ambayo yalikuwa kinyume mpaka sisi tukalalamika. Sasa napenda niiulize Serikali inaweza vipi kumwaajiri Mhandisi wa Wilaya ambaye hakika ana uwezo mdogo na akapewa majukumu makubwa ya kuiendesha Wilaya? Je, Serikali itarekebisha hili inapotuletea Mhandisi mwingine kuendesha Wilaya ya Muleba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, natumaini majibu hayatakuwa marefu kama maswali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Spika, Serikali imekiri hapa kwamba kulikuwa na mapungufu mengi katika mradi huo kwa maana ya kazi yenyewe ilivyofanyika na kusababisha hasara ambayo imepatikana kutokana na uwezo mdogo wa Mhandisi wa Wilaya.

Sasa Mhandisi tuliyekuwa naye wakati huo ndiyo huyo ambaye alikuwepo hapo Muleba na tulidhani angeweza kufanya kazi hiyo vizuri. Lakini baada ya kubaini mapungufu hayo ndiyo maana tumekiri hapa kwamba imebidi tumchukulie hatua za kinidhamu kama taratibu zinavyotaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ruth Msafiri kwamba daraja hilo itajengwa. Tumedhamiria kuisaidia Wilaya ya Muleba na wala asiwe na mashaka hata kidogo juu ya ukamilishwaji wa hilo daraja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, tukubali tu kwamba kulikuwa na matatizo *generally* katika Mradi mzima. Sasa mimi nafikiri katika hatua tuliyokwishafika hapa tukianza kujaribu kutafuta mchawi na nini na nini haitatusaidia sana. Mimi nadhani kauli ya Serikali ndiyo ya msingi zaidi *we will do everthing best as we can* kuhakikisha kwamba daraja hilo linafanyiwa kazi kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Na. 336

**Kugawa Kata zilizo kubwa Kurahisisha**
**Usimamiaji wa Maendeleo**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Jimbo la Kibakwe ziko Kata kubwa sana kiasi cha kusababisha ugumu wa utawala bora na usimamiaji wa shughuli za maendeleo ya wananchi kwenye maeneo hayo:-

(a) Je, ni vigezo na utaratibu gani unaotumika kugawa Kata?

(b) Kwa kuwa, Vijiji vya Mlimo, Lufu, Gwamhungile pamoja na vitongoji vya Maketa na Ilala viko katika ukanda wa milimani. Je, Serikali haioni hiyo ni sababu inayotosha kuigawa Kata ya Luhundwa na kufanya Kata za Luhundwa na Lufu?

(c) Kwa kuwa, Kata ya Rudi nayo ni kubwa mno na imekaa vibaya ki-jiografia. Je, Serikali haioni haja ya kuigawa Kata hiyo ili kufanya Kata za Rudi na *Mtera Staff?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachewene, Mbunge wa Kibakwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika kugawa au kuunda Kata ni pamoja na kuwepo na vijiji vilivyosajiliwa ambavyo haviko chini ya vitano (5), kuwa ni Makao Makuu ya Kata hiyo mnayoitarajia kuanzisha, kuwepo na Mahakama ya Mwanzo, kuwepo na huduma za kijamii na kiuchumi kama vile maduka ya rejareja yasiyopungua angalau ishirini (20), mambo kama soko, zahanati, shule za msingi na kama mnaweza mkawa na Posta hivi. Kwa hiyo, *generally* ni yale mambo ambayo yanaweza yakatoa huduma kwa wananchi. Kuhusu utaratibu unaotumika ni kuwa lazima wazo la kugawa Kata liwe limeibuliwa na wananchi wa eneo husika. Baada ya kuona umuhimu wa kugawa Kata hiyo. Vijiji husika huwasilisha ombi hilo katika Kamati ya Maendeleo ya Kata. Yakiridhiwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata maombi huwasilishwa kwenye Vikao vya Halmashauri na Mkoa.

Halmashauri husika inatakiwa sasa kutuma mapendekezo ya kugawa/kuanzisha Kata kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Maelezo ya ziada ambayo yanaweza yakasaidia ni pamoja na majina ya vijiji katika Kata mpya na ya zamani na sababu za kuunda au kugawa hiyo Kata.

(b) Mheshimiwa Spika, maombi ya kugawa Kata ya Luhundwa kuwa Kata mbili za Lufu na Luhundwa yamepokelewa katika Ofisi yangu kwa barua yenye Kumb.Na.HW/R.10/12/6 ya tarehe 9/4/2003. Hata hivyo, kutokana na kuwepo kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2004 Tume ya uchunguzi ilielekeza kuwa kusiwepo na mabadiliko ya maeneo ya Kata na Vijiji. Ofisi yangu imeanza tena kupokea maombi kwa wale ambao walikuwa bado hawajawasilisha kutoka Wilaya mbalimbali kwa lengo la kuyafanyia uchambuzi kama yanakidhi vigezo vilivyowekwa. Zoezi hili linahusisha Kata zilizoombwa kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2004 yakiwemo maombi ya Halmashauri ya Mpwapwa.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu hali ya kijiografia ya Kata ya Rudi. Na kama nilivyoeleza katika sehemu ya (b) hapo juu maombi hayo yatashughulikiwa kwa pamoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba ni vizuri Halmashauri za Wilaya ndiyo zitoe mapendekezo; na kwa kuwa mwaka jana kabla ya uchaguzi wa 2005, tulishakwishapeleka maombi ya Kata sita katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ambayo ina Kata 18. Sasa je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba hizo Kata ambazo ziliombwa Mkanana, Chipogolo, Malolo,

Igonji Kaskazini, Kata ya Mtera na hiyo ya Lufu yuko tayari kulishughulikia ombi letu kwa kuwa tulishalipitisha kwenye Halmashauri ya Wilaya?

La pili, Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna vitongoji ambavyo ni vikubwa na vimetimiza vigezo vyote, Nana, Majami, Chidwenya, Kazania, Mgogo na Namakawira. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kupokea ombi la Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa sasa vitongoji hivyo viwe Vijiji?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa walishawasilisha maombi ya Kata sita mwaka juzi na yalifanyiwa kazi na kati ya Kata hizo sita nadhani tulikubali Kata mpya tatu, na tulikuwa radhi kabisa kuzitangaza. Lakini kama nilivyosema ilikuwa ni karibu mno na uchaguzi na kwa sababu ile ile iliyotolewa mwaka 2003 wakati tunakaribia uchaguzi wa Kata na vijiji, sababu hiyo hiyo vilevile ilitumika katika zoezi hili.

Mheshimiwa Spika lakini hata hivyo, ziko Kata katika Halmashauri yake ambazo tulizikataa kwa sababu vigezo vyake vilikuwa havikutimizwa. Kwa hiyo, bado tuna nafasi na kwa kweli tungeomba Waheshimiwa Wabunge wengi mjitahidi kusukuma jambo hili.

Tusingependa lika-*spill over* tena mwaka kesho. Tungependa tumalizie zoezi hili mwaka huu ili tuweze kukubaliana ni maeneo yapi yana nafasi kulingana vilevile na uwezo wa Serikali utakavyoonekana. Kwa hiyo, tuko radhi na tutafanya hiyo kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala lake la pili, nataka tu niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba zoezi la vijiji lilishafanyika vilevile kwa maana ya kujaribu kugawa vitongoji vikubwa, kujaribu kuvitengenezea utaratibu mpya wa kuwa vijiji na lilikuwa ni zoezi kubwa kweli kweli. Tunachofanya sasa ni kujaribu kupitia upya hivyo vijiji vilivyokuwa vimetengenezwa tuone sasa kauli ya mwisho itasema nini.

Kwa hiyo, tutakuwa radhi hata kwa vitongoji alivyovitaja tutazingatia tuone kama wanaweza kubahatika angalau baadhi yake vikawa ni maeneo ya vijiji.

Na. 337

**Utoaji wa Huduma ya Posta na Benki**

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi nyingi duniani, Mashirika na Kampuni za Posta hutoa huduma za Benki na Posta kwa Pamoja na walengwa ni wananchi wa kawaida hasa Vijijini:-

(a) Je, ni kwa kiwango gani kutenganishwa kwa Shirika la Posta na Benki ya Posta mwaka 1992 kumeathiri utoaji wa huduma hizo muhimu kwa wakazi wa Vijijini?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, huu ni wakati muafaka wa kuziunganisha huduma hizo muhimu ili kukidhi kiu ya wananchi hasa wa Vijijini vya kuhudumiwa na mtandao mzuri wa Posta na Benki yake?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja napenda kwanza, kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, huduma ya Benki ya Posta ilianza tangu mwaka 1927 wakati huo ilikuwa inajulikana kwa jina la *Tanganyika Postal Office Savings Bank*; na ilikuwa chini ya Utawala wa Uingereza na ilitoa huduma za posta, *telegraph* na za benki. Mwaka 1967 baada ya Uhuru, huduma hizi zilianzishwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAPTC).* Baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, huduma za Benki ya Posta zilikuwa chini ya umiliki wa Hazina yaani Wizara ya Fedha na kuendeshwa kwa njia ya Uwakala kupitia Shirika la Posta na Simu Tanzania. *(Makofi)*

Benki ya Posta iliendelea kutoa huduma hizi hadi mwaka 1991/1992 wakati ambapo Bunge hili lilipitisha Sheria Namba 11 ya 1991 na kurekebishwa na Sheria Namba 12 ya mwaka 1992 ya kuunda upya Benki ya Posta Tanzania sambamba na mkakati wa urekebishaji wa Sekta ya Taasisi za Fedha na mabenki hapa nchini. Kufuatia maekerebisho hayo ya kisheria, Benki ya Posta Tanzania imeweza kufungua matawi yake ya kisasa nje ya mtandao wa Ofisi za Posta na kuweza kuendesha huduma mpya ambazo hapo awali hazikuwa zikitolewa kupitia Uwakala wa lililokuwa Shirika la Posta Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kutenganishwa kwa Shirika la Posta na Benki ya Posta mwaka 1992 hakukuathiri kwa kiwango kikubwa utoaji wa huduma hizo muhimu kwa wakazi wa Vijijini, bali kulileta ongezeko la ufanisi wa utoaji huduma na kukidhi matakwa ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Huduma za Mabenki na Taasisi za Fedha. Benki ya Posta Tanzania imeweza kujiendesha vyema na imeweza kukuza huduma na kuongeza idadi ya matawi yake hapa nchini. *(Makofi)*

Hata hivyo, tatizo ndogo lililojitokeza ni pale wananchi walipolazimika kufuata huduma za Uwakala wa Benki katika Ofisi za Posta za Wilaya au zile zilizobaki katika uendeshaji wa wafanyakazi wa kudumu wa Shirika la Posta Tanzania.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni wakati muafaka wa kutafakari namna ya kuzidi kuboresha utaratibu wa utoaji wa huduma za Posta na Benki ya Posta ili ziwafikie wananchi walio wengi nchini, hususan wale waishio vijijini kama tunavyoelewa kuwa huduma za Benki ya Posta ziko chini ya Wizara ya Fedha na zinadhibitiwa na kuratibiwa na Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* kulingana na Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Mabenki na Taasisi za Fedha.

Kwa upande mwingine Huduma za Posta zinasimamiwa na Wizara ya Miundombinu na kudhibitiwa na kuratibiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano nchini *(TCRA).* Mikakati inakamilishwa ya majadiliano juu ya kuanzisha mfumo utakaoziwezesha taasisi hizi mbili (Posta na Benki ya Posta) kutoa huduma kwa kushirikiana kwa lengo la kumhudumia mteja wao ipasavyo. *(Makofi)*

Na. 338

**Uboreshaji wa Barabara za Dar es Salaam**

**MHE. IDD M. AZZAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jiji la Dar es Salaam limekua kwa kasi sana na hivyo Miundombinu iliyopo kushindwa kukidhi mahitaji ya wakati huu hasa barabara ambapo kumekuwa na msongamano mkubwa wa magari katika barabara kuu za Morogoro na Bagamoyo *(Ali Hassan Mwinyi Road)* nyakati za asubuhi na jioni:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuondokana na tatizo hilo?

(b) Kwa kuwa, zipo barabara za Mitaani kama vile barabara ya Kigogo hadi Tabata, Magomeni Mikumi, Magomeni Kota, Makumbusho, Kijitonyama na Mabatini. Je, ni lini Serikali Kuu kwa kushrikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni itaziboresha barabara hizo ili kupunguza msongamano kwenye barabara kuu za Morogoro na Bagamoyo *(Ali Hassan Mwinyi Road)?*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napeanda kujibu swali la Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na msongamano wa magari katika barabara nyingi za Jiji la Dar es Salaam ikiwemo barabara za Morogoro na Bagamoyo. Serikali inaliona tatizo hilo na kama tulivyoeleza humu Bungeni mara kadhaa, Serikali imeandaa mikakati mbalimbali ili kupunguza msongamano huo.

Mikakati hii ni pamoja na mradi wa mabasi yaendayo kasi, upanuzi na ukarabati wa barabara kuu muhimu za Kilwa, Sam Nujoma na Mandella utakaonza hivi

karibuni, ukarabati wa barabara viunganishi na barabara za pembezoni mwa Jiji, uanzishaji wa usafiri wa boti majini kandokando mwa ufukwe wa bahari na uboreshaji wa taa za barabarani na za kuongezea magari. Aidha, Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali katika kutafakari tatizo hili ili kupata ufumbuzi wa pamoja na pia inawasiliana na wafadhili mbalimbali ili kupata fedha za kutekeleza miradi hii. *(Makofi)*

(b) Mhesimiwa Spika, Serikali Kuu itaendelea kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni pamoja na Manispaa za Ilala na Temeke kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kuwa barabara za mitaa katika Manispaa hizo zinaimarishwa ikiwa ni pamoja na kukabiliana na tatizo la msongamano Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali hili limekuwa likiulizwa mara nyingi sana hapa Bungeni na kwa kuwa mara nyingi majibu yamekuwa yakitolewa kwamba utekelezaji utaanza, lakini haijasemwa ni lini utaanza.

Lakini kuulizwa sana swali hili hapa Bungeni inaonyesha ni jinsi gani Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Dar es Salaam wanavyokerwa na msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Je, Serikali inaweza ikatuambia ni lini hasa ujenzi na ukarabati utaanza na lini hasa tatizo lile litaisha katika Jiji la Dar es Salaam? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Idd Azzan, Mbunge wa Kinondoni, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine wote wale wa Mkoa wa Dar es Salaam akiwemo Mbunge wa Ukonga, kwa namna wanavyoshughulikia na kuhangaikia barabara za Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza tatizo la msongamano wa magari ni tatizo ambalo kwa kweli Serikali kwa ujumla inaliona na inahangaika sana kuhakikisha kwamba zinapatikana fedha kwa ajili ya kuondoa kero hiyo.

Sasa sio Wizara tu kwa maana ya Waziri wa Miundombinu, lakini hata Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais nao wanatusaidia katika kuhangaika kuangalia tunawezaje tukapata fedha za kutekeleza mradi huo.

Mimi nadhani kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam na wananchi wa Dar es Salaam wavute subiri, wakati Serikali inatafuta fedha hizo ambazo kama nilivyosema katika jibu langu hapa Bungeni siku chache zilizopita zinakaribia bilioni 12 mpaka bilioni 15.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Idd Azzan namwomba avute subira na Waheshimiwa Wabunge wengine ili Serikali ikamilishe zoezi hili. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la Miundombinu limekuwa sugu kwa muda mrefu na Serikali katika miaka mitatu iliyopita ilikuja Bungeni ikasema kwamba itaweka utaratibu wa *BOT* yaani jenga, endesha, halafu rudisha. Kwa kuwa Serikali mpaka leo haijatoa utaratibu wa hiyo *BOT*.

Je, Serikali iko *serious* katika kutatua tatizo hili? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU(MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** : Mheshimiwa Spika, mpango wa *BOT* ni mmoja wa mipango ya kutekeleza miradi ya barabara na Serikali inachongojea kwa kweli ni kujitokeza kwa wale wawekezaji ambao watakuja na mpango mzuri wa *BOT* utakaokubalika na Serikali na ambao una manufaa kwa Serikali na sisi tuko tayari kupokea mwekezaji wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningemshauri Mheshimiwa Mbunge kama anajua wawekezaji wanaoweza kuja na mpango huo utaokubalika kisera na Serikali, sisi tutampokea. *(Makofi)*

**MHE. SAMEER I. LOTTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa barabara nyingi zinazungumziwa urefu hata hii barabara inayolalamikiwa hapa.

Lakini hazijazungumziwa barabara upana wake na tunavyofahamu ni kwamba barabara ndefu kama inayotoka Morogoro au ya Bagamoyo au barabara nyingine hizi. Kama Wakandarasi watakuwa wamepunguza inchi moja ama mbili katika upana wa barabara zile basi inakuwa ni hasara kubwa sana katika nchi?

Je, Naibu Waziri anaweza kuniambia upana wa barabara hizi hasa barabara ya Morogoro kuja Dar es Salaam au barabara ya Morogoro kuja Dodoma zina upana gani na je, ananiruhusu mimi kutembea na futi na kupima wakati wowote unaofaa? Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Nasikitika swali hilo liko nje ya swali la msingi. Kwa sababu swali la msingi limehusu barabara ya Dar es Salaam.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni muda umefika wa kuandaa mpango kabambe wa kushughulikia hili tatizo la usafiri Dar es Salaam pamoja na hizi hatua zinazochukuliwa za kujenga barabara ndogondogo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ndio Serikali inaona umuhimu huo na nadhani kuna

haja wadau tukae tuweze kutekeleza kuangalia tatizo hili in *totality* pamoja na huu ambao tunauzungumzia.

Mimi na yeye kama Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam kuna haja tukae kama Wabunge lakini na wadau wengine ili tuangalie mapendekezo hayo na yeye kwa sababu ameshashughulikia suala la maendeleo ikiwepo na barabara katika Jiji la Dar es Salaam nadhani atatusaidia sana kutupa *input* zitakazowezesha kutekeleza mradi huo ambao anaupendekeza.

Na. 339

**Tofauti ya Maendeleo Katika Maeneo Nchini**

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mipango ya maendeleo inatofautiana kati ya Mkoa mmoja na mwingine; na kwa kuwa, wafadhili wana tabia ya kuchagua miradi na maeneo ya kupeleka miradi hiyo:-

(a) Je, Serikali inayo mipango gani ya kusukuma maendeleo kwa ile Mikoa ambayo wafadhili hawakuichagua kupeleka miradi yao?

(b) Je, ni Mikoa mingapi imefaidika kwa misaada na miradi ya wafadhili kutoka nje na kwa miradi gani katika kipindi cha 2003 – 2005?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mbunge wa Ole, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ina dhamira ya kutoa fursa sawa kwa maendeleo kwa mikoa yote, iwe kwa kutumia wahisani au kwa kutumia fedha za ndani ya nchi. Hata hivyo, ufinyu wa Bajeti na wingi wa mahitaji unatutaka tuanze sehemu fulani na halafu tuhamie eneo jingine. Vigezo vya utoaji wa fedha za maendeleo vipo, kama vile takwimu za maendeleo ya watu *(Human Development Index)* ambazo husaidia kubaini mikoa iliyo nyuma kimaendeleo, ili iweze kuongezewa raslimali zaidi. Vigezo vingine ni kuangalia mikakati mipya ya kuendeleza kazi zilizokwishaanza; kuendeleza miradi iliyo na matokeo zaidi ya moja; kuangalia miradi/kazi inayoweza kupunguza tofauti zilizopo kati ya mikoa, na pia kuangalia miradi inayozingatia masuala mtambuka. Vile vile Serikali kwa kushirikiana na mikoa, hutayarisha Taarifa za Hali ya Maendeleo ya Mkoa (*Regional Development Profile*), ambazo hutumiwa na Serikali pamoja na wahisani kuona ni miradi gani (kutegemeana na hali ya mkoa kiraslimali) ipelekwe mikoa ipi na kwamba nchi itapata maendeleo yapi kutokana na miradi hiyo. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, Mikoa iliyokwishafaidika kwa misaada na miradi ya wahisani kwa kipindi cha 2003 – 2005 ni kama ifuatavyo:-

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004, mikoa yote ilipata fedha za wahisani isipokuwa mikoa ya Kigoma, Shinyanga, Tabora, Dar es Salaam na Rukwa. Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, mikoa yote ilipata fedha kutoka kwa wahisani na mwaka wa fedha 2005/2006 ni mikoa ya Arusha, Kigoma, Tabora na Ruvuma ambayo haikupata fedha kutoka kwa wahisani.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango imejitokeza wazi kwamba Mkoa wa Tabora ni miongoni mwa mikoa ambayo imekuwa haipati misaada kutoka kwa wafadhili. Kwa bahati nzuri mwaka huu kuna kijiji kimoja Tabora kilipata bahati ya kuwa Kijiji cha *Millenium* kwa maana kwamba kijiji hicho kitakuwa ni kitovu cha maendeleo na mfano mzuri wa kuendeleza vijiji. *(Makofi)*

Swali je, Serikali haioni ni vizuri kwa kutumia utaratibu huo huo wa Kijiji cha *Millenium* kufanya Mji au Tabora iwe ni Mkoa wa *Millenium* ili iweze kupata faida za kuendelea kama Kijiji cha *Millenium?*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kijiji cha Mbola kilichopo katika Mkoa wa Tabora kimeteuliwa na Umoja wa Mataifa kiwe Kijiji cha *Millenium*.

Lakini vile vile iko miji ya *Millenium* na Serikali inaendelea kuwasiliana na Umoja wa Mataifa kupitia Prof. Jefrey Sykes ambaye ndiyo Mratibu wa Miji na Vijiji vya *Millenium* Duniani ili aweze kufikiria kuifanya Tabora iwe moja ya miji ya Millenium.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa chini ya Mpango wa MKURABITA na kwa mujibu wa ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 – 2010 ya Chama cha Mapinduzi mashamba ya wananchi yatapimwa na kutoa hatimiliki ikiwa pamoja na nyumba zao na kwamba hati hizo zitatumika kuomba mikopo kwenye Mabenki.

Kwa kuwa sasa iko mikoa ambayo iko nyuma sana mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kigoma, Singida, Dodoma, Rukwa, Lindi na Mtwara. Je, Serikali sasa na kwa kuzingatia kwamba suala la upimaji lina gharama kubwa. Haiwezi kufanyika pamoja nchi nzima. Serikali kwa makusudi iko tayari kuanza upimaji katika mikoa niliyoitaja ili wachukue mikopo ili waanze kuondoa umaskini ili twende pamoja?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imebuni mpango kabambe wa MKURABITA. Na kwamba shabaha ya mpango huu ni kuwawezesha wananchi wote katika nchi yetu hasa wanyonge mali zao zitambuliwe rasmi. Mali kwa maana ya ardhi, nyumba na kadhalika

lakini vile vile hata biashara zao. Ndiyo maana MKURABITA inaitwa Mkakati wa Kurasilimisha rasilimali na Biashara Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo mkakati huu una mpango mahsusi tayari umeshakubaliwa ambao utachukua maeneo fulani ambayo yataanza kushughulikiwa. Kwa hiyo, mpango utaenea nchi nzima kwa kuzingatia vipaumbele vilivyokwishawekwa. Najua vile vile kwamba kuna maelekezo ya Rais ya baadhi ya mikoa sita ya nchi kupewa kipaumbele. Mikoa hii itaendelea kupewa kipaumbele hata katika utekelezaji wa MKURABITA lakini hata katika utekelezaji wa MKUKUTA. *(Makofi)*

Na. 340

**Sehemu ya Mapato ya Hifadhi ya Taifa kwa Vijiji Jirani**

**MHE. PHARES K. KABUYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina mpango wa vijiji na Wilaya zinazopakana na Hifadhi za Taifa kupata sehemu ya mapato yanayotokana na hifadhi hizo:-

Je, Wilaya ya Biharamulo ambayo inapakana na Hifadhi ya Burigi inapata fedha kiasi gani na ni vijiji gani vinafaidika na mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabuye, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kuanzia 2000 hadi 2004, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilipata jumla ya shilingi 26,082,088.00 zikiwa ni mgao wa 25% ya mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii.

Vijiji vya Wilaya ya Biharamulo vinavyozunguka Mapori ya Akiba ya Burigi na Biharamulo vinafaidika na mgao huo ni Vijiji vifuatavyo:- Nyabugombe, Mohingora, Mabare, Lusahunga, Kiruruma, Musenyi, Ruziba, Katerela, Rugondo, Katete, Kazunguti, Kabukome, Ichwankima, Kasenga na Bupandwampuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho cha miaka mitano (5) Makampuni ya Uwindaji wa Mapori ya Akiba ya Biharamulo na Burigi yamechangia jumla ya shs. 18,237,354.00 katika Miradi ya Maendeleo.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza. Hizo pesa asilimia 20 wanaipima anaweza akaniambia kwamba kinatokana na kiasi gani kilichokuwa kimekusanywa kutokana na mapato yanayopatikana katika hifadhi hiyo?

Pili, hizo fedha kulingana na vijiji hivyo vilivyotajwa anaweza akaniambia ni kiasi gani cha maendeleo hata deski moja linaweza likatengenezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kiasi cha fedha ni kama ifuatavyo:- Kuhusu kiasi cha fedha zilizochangiwa ikiwa ni asilimia 25 kutoka kwa Makampuni ya Utalii naomba kumfahamisha kwamba kwa hapa sina hiyo taarifa lakini ipo ofisini.

Mheshimwa Spika naomba baada ya hapa tuongozane na Mheshimiwa Mbunge nitakwenda kumpatia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na vijiji ambavyo nimevitaja na kiasi ambacho nimesema vimetolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo naomba nitoe mfano mmoja. Kampuni ya Kilimanjaro *Game Trailers* imeweza kutoa vifaa vya ujenzi na kusafirisha vifaa hivyo vya ujenzi ikiwa ni sementi, mbao, mawe na vifaa vingine kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari na Shule ya Msingi katika Kijiji cha Ruhita Wilayani Karagwe. Kwa hivi nasema hizo fedha zinafanya kazi.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda tu kumwomba Mheshimiwa Naibu Waziri aweke wazi kwa sababu suala la mapato bado kuna usiri. Kwa sababu vijiji vinavyopatikana na hifadhi hizi hazijui ni kiasi gani cha fedha kimekusanywa. Inakuwa mtu unapewa hujui kimekusanywa kiasi gani.

Je, Serikali haioni ni vyema kuweka utaratibu wa kuweka bayana juu ya mapato yanayopatikana ili wanavijiji wajue kwamba *stake* yao ni kiasi gani katika mapato hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa kusema kweli wananchi pamoja na Halmashauri ambazo zinapakana na vitalu hivi vya uwindaji vina umuhimu wa kufahamu mapato ambayo wanastahili kuyapata kutoka katika Makampuni haya. Naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba tangu sasa tutafuata mpango huo tutaeleza Halmashauri husika zimepata kiasi gani kutoka katika Makampuni haya ya Utalii tutawagawia Waheshimiwa Wabunge.

**SPIKA:** Kabla hatujaachana na swali hili. Ningeomba Mheshimiwa Kabuye aendelee kuwasiliana na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu amepewa mwaliko wa kuongozana naye. Lakini kwa bahati mbaya Mheshimiwa Naibu Waziri hakutaja ni saa 4.00 baada ya maswali, au ni saa 7.00 baada ya kusitisha shughuli za Bunge au ni saa 2.45 usiku. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 341

## Kuanzisha Mashamba ya Miti ya Kuni

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Ili kuzuia wananchi wasikate miti ovyo ovyo na kuharibu mazingira na uoto wa asili:-

Je, kwa nini Serikali kwa kushirikiana na uongozi wa Mikoa, Wilaya, Miji na Vijiji usianzishe mashamba makubwa ya kuni (*fuel wood plantation*) katika kila Mji na Vijiji nchini ili kupunguza ukataji wa miti ya asili kwa ajili ya mkaa na kuni za kupikia au kwa matumizi mengine?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazi, ninaomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa uharibifu wa mazingira unachangiwa kwa kiasi kikubwa na ukataji miti kwa ajili ya utengenezaji wa kuni na mkaa. Wizara yangu imeliona hilo na imeandaa mikakati ya muda mfupi na muda mrefu ya kuzuia uharibifu huo. Moja ya mikakati ya muda mfupi ilikuwa ni kusimamisha utengenezaji mkaa katika misitu ya asili ili kuandaa mpango wa uvunaji endelevu wa miti katika misitu hiyo kwa ajili ya mkaa, kuni na mazao mengine ya misitu.

Pamoja na Mpango huo upo tayari na utaanza kutumika hivi karibuni. Mpango huo utaainisha maeneo maalum ya kutengenezea mkaa kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya kupata mkaa mwingi kwa kutumia miti kidogo.

Mkakati wa muda mrefu ni pamoja na utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Vyanzo vya Maji uliotangazwa na Makamu wa Rais mwezi Aprili, 2006 na Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu Nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Makwetta kama ifuatavyo:-

Katika utekelezaji wa mkakati wa kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji, Wizara yangu imepewa jukumu la kuzitaka taasisi zote zinazotumia mkaa na kuni kwa wingi kuanzisha mashamba yao ya miti ya nishati. Katika utekelezaji wa mkakati huo Miji na Vijiji vinatakiwa kuanzisha mashamba ya miti ya nishati ili kupunguza kasi ya uvunaji wa miti katika misitu ya asili.

Aidha, katika dhana ya usimamizi shirikishi wa misitu, Wizara yangu inashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutenga

maeneo ya vijiji kwa ajili ya uanzishwaji wa mashamba ya miti ya nishati. Wizara yangu inaendelea na zoezi la kupitia sheria ndogondogo za usimamizi wa misitu ya vijiji.

Wizara yangu pia itaendelea kutoa maelekezo kwa njia ya ugani kuhusu aina ya miti inayostahili kupandwa katika sehemu mbalimbali nchini. Mbegu za miti ya kupandwa zinakusanywa na Wakala wa Mbegu za Miti – Morogoro, ili zipatikane za kutosha kwa mahitaji yatakayoongezeka. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wakati fulani Waziri Mwandosya wakati anatembelea mikoa alitoa pendekezo kama hili. Na kwa kuwa hatuna mifano ya mashamba kama hayo katika miji ya Dodoma au Dar es Salaam. Je, isingekuwa vizuri tukajua wapi mkakati kama huu umeanza ili kunusuru nchi yetu isigeuzwe kuwa jangwa?

Pili, kutokana na uamuzi wa Serikali wa kuzuia ukataji miti ovyo kwa lengo la kutengeneza mkaa ili kuhifadhi mazingira. Uamuzi huo umesababisha bei ya mkaa katika miji kama Dar es Salaam kuwa mara mbili ya bei yake na hivyo kufanya wanyonge washindwe kabisa kununua mkaa au mafuta?

Kwa nini kama wazo hilo anaona ni zuri kule Njombe kuna miti ya miwati, mikaratusi ambayo inakuwa kwa haraka na hivi sasa inaangamizwa kwa kuchoma ili kulima mashamba kwa nini kusiwe na mkakati wa kuwashauri wahusika ili kutumia TAZARA na kusafirisha miti ile ya miwati kupeleka Dar es Salaam na kuwa na vituo maalum mahali pa kuuzia kuni kama ilivyo kwa mafuta ili wawe na mbadala kuliko kukazania kuzuia tu wakati hakuna *substitute*. Naomba majibu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Makwetta na Bunge lako Tukufu kwamba tayari Serikali inalo shamba la miti kwa ajili ya kuni na mkaa katika Pori la Ruvu. Na tayari katika shamba hilo wananchi kaya 1,000 zimepatiwa ekari 20,000 ambazo pia huzitumia kwa kupanda miti kwa ajili ya kuni na mkaa na tayari wameshaanza kujipatia fedha kutokana na miti hiyo. Shamba hilo hasa lilipandwa miti hususan kwa ajili ya kuni na mkaa kwa Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam. Kwa hivi shamba lipo. *(Makofi)*

Vile vile kulikuwa kuna shamba la Serikali Mbeya kwa ajili ya kuni na mkaa. Lakini kutokana na kupanuka kwa mji wa Mbeya waliomba sehemu ya shamba hilo ili waweze kupima viwanja kwa ajili ya makazi.

Kuhusu swali lake la pili, kutokana na taarifa kwamba kuna mikaratusi huko Mbeya ambayo ingeweza kutumika kwa ajili ya kutengeneza mkaa na kuni wazo hilo tumelipokea tutafanya utafiti tuone jinsi gani tunaweza tukatumia mikaratusi hiyo kwa njia inayofaa.

Na. 342

**Kumkwamua Kiuchumi Mwanamke wa Kijijini**

**MHE. ZAYNAB M. VULU** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali pamoja na jitihada zake za kumsaidia na kumkomboa mwanamke katika kujikwamua kiuchumi kwa kuwapatia mikopo kupitia Serikali, Asasi zisizo za Kiserikali kwa kutumia dhamana za aina mbalimbali. Je, ni hatua zipi zinazochukuliwa ili kumkwamua ki-uchumi mwanamke wa kijijini ambaye hana dhamana zitakazomwezesha kupata mkopo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Zaynab Vulu kwa kutambua jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali za kumsaidia na kumkomboa mwanamke katika kujikwamua kiuchumi. Jitihada hizo ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake *(WDF)* katika ngazi ya Halmashauri. Mfuko huo umeanzishwa kwa lengo la kuwafikia wanawake wengi waliopo vijijini. Masharti yake na riba ni nafuu ikilinganishwa na Mifuko mingine na wanachama wanajidhamini wenyewe kupitia vikundi vyao. Huu ni Mfuko pekee unaowalenga wanawake nchi nzima.Mifuko mingine ambayo Serikali imeanzisha ili kumwezesha mwanamke kiuchumi na kuongeza ajira ni Mfuko wa Mikopo kwa Wafanyabiashara na Wajasiriamali wadogo wadogo *(SELF),* na Asasi ya mikopo kwa wanawake wazalishaji *(CREW-T)* ambayo huwasaidia pia wanawake wa vijijini.Aidha, zipo jitihada mbalimbali zinazoendelea kufanywa na Serikali ili kuona kila Mtanzania hususan mwanamke anashiriki kikamilifu katika kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Kwa mfano katika mwaka 2006/2007 Serikali imetenga wastani wa shililngi milioni 500 kwa kila mkoa ili zikopeshwe kwa wananchi hususan wanawake wajasiriamali. *(Makofi)*

Pamoja na kuanzisha Mifuko hiyo, Serikali imechukua hatua za makusudi za kuwahamasisha wanawake kujiunga na Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS).* Vyama hivyo ni mojawapo ya mbinu muhimu inayotumika ya kuwakomboa wanawake na wanaume kiuchumi. Serikali pia inaendelea na hatua za mwisho mwisho za kuhakikisha kwamba Benki ya Taifa ya Wanawake inaanzishwa. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba anihakikishie kwamba katika majibu yake amezungumzia suala la kuhamasisha wanawake kuanzisha vikundi huko vijijini. Wakati tunafanya Kampeni na ilani yetu ya Uchaguzi imetuelekeza kwamba kinamama na vijana waanzishe vikundi ili waweze kupatiwa mikopo na vikundi hivyo kwa sasa vimeshaanzishwa. Je, ni mkakati gani waliouweka katika kuwapatia hiyo mikopo hivyo vikundi? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**: Mheshimiwa Spika, ni kweli tumekuwa na jitihada za kuhamasisha akinamama na vijana kuanzisha vikundi na ninashukuru kupitia kaulimbiu ya Mwenge mwaka huu tunahamasisha pamoja na masuala ya kujihadhari na UKIMWI na Madawa ya Kulevya lakini pia suala la *SACCOS* kuimarisha na kuendeleza *SACCOS* kwa maendeleo endelevu. Kwa hivyo, sisi tunawahakikishia tutazungumka katika jitihada zetu pamoja na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuhakikisha kwamba *SACCOS* hizi mara zinapoanzishwa basi zitapata fursa ya mikopo hiyo ya shilingi milioni 500 kila Mkoa lakini vile vile zinaweza zikapata mikopo hii ya maendeleo ya Jamii *(WDF). (Makofi)*

Na. 343

**Kupeleka Umeme Makao Makuu ya Wilaya**

**MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro yaani Orkesumet:-

(a) Je, ni vijiji gani katika Wilaya ya Simanjiro vitafaidika kutokana na kupitiwa na umeme huo na kazi hiyo itaanza lini?

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuvuta umeme kutoka Nyumba ya Mungu ili vijiji vya Lemkuna, Lendanai, Naberera na Namalulu viweze kufaidika na umeme huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Serikali ya kupeleka umeme Simanjiro ipo pale pale kwani Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo *(SIDA)* limetoa fedha za utekelezaji wa mradi wa umeme Simanjiro. Mshauri wa Mradi ni *SWECO Internationa AB* ya *Sweden.* Umeme utakaopelekwa Simanjiro utatokea kwenye kituo cha umeme cha Same ambapo njia ya *KV 33* itajengwa na kupita katika vijiji vya Muungano na Ruvu Mferejini vilivyopo katika Wilaya ya Same. Vile vile umeme huo utapita katika Kijiji cha Loborosoit Wilayani Simanjiro ambapo Wilaya ya Simanjiro inataka kuweka pampu za kusukuma maji kwa ajili ya mji wa Orkesmet. Umeme ukishafikishwa mjini Orkesmet njia za umeme zitajengwa kuelekea Namalulu na Naberera. Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa upelekaji umeme Wilaya ya Simanjiro Orkesmet zilitangazwa tarehe 6 Julai, 2006 na itafunguliwa tarehe 15 Septemba, 2006 saa 8.00 mchana Makao Makuu ya *TANESCO.*Baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Kama nilivyoeleza hapo awali umeme utafikishwa kwanza kwenye mji wa Orkesemet na vijiji vya Loborosoit, Namalulu na Naberera.

(b) Iwapo fedha za ziada zitapatikana umeme wa *KV 33* utapelekwa katika vijiji vya Lemkuna na Lendanai kutokea Nyumba ya Mungu.

Na. 344

**Tatizo la Umeme Nchini**

**MHE. USSI AMME PANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu inakabiliwa na tatizo la umeme, hasa pale kina cha maji kinapopungua katika mabwawa yetu mvua zinapokosekana:-

(a) Je, kwa nini Serikali haianzishi matumizi ya umeme wa "*Solar Panel*" ambao unatokona na nguvu ya jua?
(b) Je, kwa kutumia teknolojia hiyo, Serikali haioni kuwa, ingewapunguzia wananchi wake gharama kubwa wanazolipia umeme kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Amme Pandu, Mbunge wa Mtoni, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nishati itokanayo na jua ni mojawapo ya vyanzo mbadala vya umeme. Hata hivyo usanifu wa kiasi cha umeme kinachoweza kupatikana kinatokana na mambo mengi mojawapo ikiwa ni umeme huo utatumika kwa matumizi gani. Serikali kwa kupitia Kitengo cha Nishati Mbadala (*Renewable Energy Section*) kinaendelea na tafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa upatikanaji wa vifaa vya kuzalisha umeme utokanao na jua na kadhalika. Vile vile, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iko katika mchakato wa kuendeleza umemenuru. Huko Mwanza mradi wa umeme wa jua unafadhiliwa na *Global Environmental Facility* kupitia *UNDP.* Mradi mwingine wa umemenuru unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA)* na utatekelezwa katika mikoa mingine ya nchi yetu. Kwa kuanzia, mradi huo utatekelezwa katika mikoa ya Iringa, Morogoro na Kigoma. Baada ya maelezo hayo hapo juu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mipango ya matumizi ya umeme utokanao na jua kama nilivyoeleza hapo awali. Umemenuru unaweza kukidhi mahitaji ya umeme vijijini kwa maeneo ambayo umeme wa gridi haujafika. Hata hivyo, kwa sasa gharama za umemenuru ni kubwa kwani ni kati ya senti za marekeni 25 hadi 125 kwa *kWh* kutegemeana na ukubwa wa mtambo, ikilinganishwa na bei ya sasa ya senti za Marekani 8.5 kwa *kWh* ya umeme wa gridi. Katika maeneo mengi yasiyo na umeme wa g ridi gharama ya mafuta ya taa kwa ajili ya mwanga, betri kwa ajili ya tochi, *radio* na mawasiliano ni kubwa kuliko ya umemenuru.

Kwa hiyo, ni kweli yapo maeneo ambayo umemenuru unaweza kuwapunguzia wananchi gharama za nishati na ndiyo maana Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iko katika mchakato wa kuendeleza umemenuru.

Mradi mwingine wa umeme nuru unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Sweden (*SIDA*) na utatekelezwa katika Mikoa mingine ya nchi yetu. Kwa kuanzia mradi huo utatekelezwa katika Mikoa ya Iringa Morogoro na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo hapo juuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa matumizi wa umeme utokanao na jua kama nilivyoeleza hapo awali. Umemenuru unaweza kukidhi mahitaji ya umeme vijijini kwa maeneo ambayo umeme wa *grid* haujafika. Hata hivyo kwa sasa gharama za umemenuru ni kubwa kwani ni kati ya senti za Marekani 25 hadi 125 kwa *Kilowatt*, kutegemeana na ukubwa wa mtambo ikilinganishwa na bei ya sasa ya senti za Marekani 8.5 *KW/H* ya umeme wa *grid*.

Katika maeneo mengi yasiyo na umeme wa *grid* gharama ya mafuta ya taa kwa ajili ya mwanga, betri kwa ajili ya tochi, redio na mawasiliano ni kubwa kuliko ya umemenuru. Kwa hiyo, ni kweli yapo maeneo ambayo umemenuru unaweza kuwapunguzia gharama za nishati na ndiyo maana Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iko katika mchakato wa kuendeleza umeme nuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Ninayomatangazo, nafurahi kutangaza wageni nikianzia wageni ambao ni familia ya Meshimiwa Waziri wetu wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Prof. Juma Kapuya. Waheshimiwa Wageni nikiwataja naomba msimame ili mtambuliwe. Kwanza ni Mama Tatu Kapuya, Mkewe Mheshimiwa Waziri, watoto wake, Zawadi, Baraka, Athumani, Kulwa na Doto wale pale. *(Makofi)*

Halafu kuna vijana waliyooa binti zake Waziri, Ahmad Mohamed, Nazar Taji na Musa Kitoi wale pale. Wapo pia ndugu zake, Shigela, Said, Ali, Suleiman, Nicolaus na Cosmas. Pamoja na hao wako viongozi kutoka Urambo katika Jimbo la Urambo Magharibi, Ndugu Elias Kaseko, Mwenyekiti wa Kata ya Kashishi Jimbo la Urambo Magharibi, Ndugu Salum Nassoro, Katibu wa Kata hiyo hiyo na Ndugu Salum Mwagi, Diwani wa Kata hiyo hiyo ya Kashishi. Karibuni sana mtawasalimia nyumbani maana yake Spika anatoka huko huko.

Mheshimiwa Janeth Masaburi, anatutangazia kwamba yupo mgeni wake anaitwa Dr. Didas John Masaburi, ambaye ni mume wake yeye. Tunakushukuru sana Dr. Masaburi kwa kumtunza mama vizuri. Mheshimiwa Amer Ali Ameir, Mbunge wa Jimbo la Fuoni, Zanzibar ana wageni watano kutoka Tawi la CCM Maungani, pia ni Wajumbe wa Kamati ya CCM Jimbo la Fuoni, wale pale. Karibuni sana Waheshimiwa.(*Makofi*)

Kwa upande wa kushoto kuna vijana wetu ambao ni wanachuo, pamoja na wakufunzi wao wa chuo cha ualimu. *Silesian Seminary* naomba msimame. Ahsate sana tunawapongeza sana wakufunzi kwa kuwaleta vijana waone namna demokrasia ya nchi yetu inavyoendeshwa, karibuni sana na karibuni tena.

Mheshimiwa Ligalama ana mgeni wake ambaye ni Diwani wa Kata ya Chita, Wilaya ya Kilombero, Ndugu John Chelele, yule pale. Kutoka Zanzibar tena Jimbo la Kiwajuni la Mheshimiwa Hoogan tunao Bi. Sepetu Mohamed Nassoro, Mwenyekiti wa Kudhibiti UKIMWI, Zanzibar.

Huyu alistahili kukaa *Speaker's Gallery* kama anaendelea kukaa naomba *Serjeant At-Arms* amsindikize pale, ni mtu mashuhuri huyu. Pia amefuatana na Bi. Salama Mzee Majaliwa, Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mjini Magharibi. Karibuni kule *Speaker's Gallery* kama mnaendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ameniomba nitangaze kwamba katika Uwanja wa Jamhuri Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imeandaa maonyesho ya juhudi zinazotekelezwa na serikali katika kuongeza kasi ya kutokomea magonjwa matatu. Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kutembelea mabanda hayo. Sielewi haya maonyesho yataendelea kwa siku ngapi, lakini nadhani ni vizuri kuwahi leo na kujifunza mambo hayo.

Taarifa ya Kikao, Mheshimiwa Adam Kigoma Malima, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, ameniomba nitangaze kuwa leo Alhamisi tarehe 3 Agosti, 2006, kuanzia saa tano asubuhi katika Chumba Namba 231, ghorofa ya pili jengo la utawala, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Harisson George Mwakyembe anaomba Waheshimiwa Wabunge wote wanaounda Chama ch Uhamasishaji wa Ushirika nchini wakutane saa saba leo siku ya Alhamisi tarehe 3 Agosti, 2006 saa za mchana, ukumbi wa zamani wa Bunge letu. Tangazo hili ni kwa ajili ya maandalizi ya Mkutano wao na Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, anatangaza kwamba Kamati Kuu ya *APNAC*, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo leo saa nne na nusu baada ya maswali. Kikao kitafanyika Ukumbi Namba 227.

Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo mwisho wa matangazo niliyoyapata kwa leo. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, samahani Mwongozo wa Spika.

**SPIKA.** Mwongozo wa Spika, endelea Mheshimiwa Mbunge na mwongozo wako.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Nadhani mhusika ameghafilika, mbele yangu kule na hapa juu kuna wapiganaji wetu. Bila shaka wamekuja kwa sababu ya nia ile ile. Nadhani ni vizuri wangetambulishwa na kusimama kwa heshima ya Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Spika.(*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Spika hutangaza wageni wale ambao nimeletewa taarifa. Lakini kwa kuwa wapiganaji wamevaa sare, basi nafurahi kutangaza kwamba Ndugu zetu Wapiganaji wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ambalo tunajivunia sana sisi wazalendo wote wa nchi hii, nao wako hapa. *(Makofi)*

Naomba Maafande msimame ili Wabunge waweze kuwaona. Ahsante sana. Kumbe wanaongozwa na mwenyewe Jenerali Waitara. Karibuni sana. Katibu tuendelee na *Order Paper. (Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007
### Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, iliyochambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha kupitia Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kuyapitia kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na hatimaye kuwasilisha Taarifa kwenye Bunge lako Tukufu. Wajumbe wa Kamati hii wamekuwa wepesi katika kuyaelewa majukumu ya Wizara, matarajio yetu, kushauri, kutuasa, kuelekeza na kutetea hoja za Wizara pale ilipobidi, nawashukuru sana.(*Mkofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia, kuwapongeza Viongozi wa Kitaifa waliochaguliwa kwenye nafasi mbalimbali kufuatia Uchaguzi Mkuu wa mwezi Desemba, 2005. Awali ya yote nawapongeza kwa dhati kabisa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tazania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wake Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kwao kupitia CCM kwa kura nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa katika uchaguzi mkuu wa mwezi Oktoba 2005. Kuchaguliwa kwake kumemwezesha kuendelea kwa kipindi cha pili kuwa Rais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi. Pia nampongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na Rais na baadae kuthibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu. Nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuliongoza Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa Hotuba yake ya kina ambayo imeelezea mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka 2005/2006. Nawapongeza pia Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa kwa Hotuba zao zilizoelezea Bajeti ya Serikali na Mwelekeo wa Uchumi wa Taifa. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu kwa hotuba zao ambazo zimekwisha kujadiliwa na kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochaguliwa katika majimbo yao, waliochaguliwa na Jumuiya zao kupitia Viti maalum na walioteuliwa na Mheshimiwa Rais. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda binafsi kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Heshima niliyopewa na Mheshimiwa Rais ni kubwa, hivyo napenda kumhakikishia yeye, Chama changu na wananchi wote kwa ujumla kuwa nitafanya kazi niliyopewa kwa uwezo wangu wote na ninamwomba Mwenyezi Mungu anisaidie.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Urambo Magharibi kwa imani waliyonayo juu yangu kwa kunichagua kuwa Mbunge wao ambako pia kumemuwezesha Mheshimiwa Rais kuniteua kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nawaahidi kuwafanyia kazi kwa moyo na ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mipango ya Mwaka 2005/2006, baada ya kusema hayo sasa naomba kutoa muhtasari wa tathmini ya hali ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Mipaka ya Tanzania na Uimarishaji Jeshi la Ulinzi Kiutendaji. Ulinzi wa Mipaka ya Tanzania ni jukumu kuu la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kuongoza na kusimamia ulinzi na usalama wa mipaka ya Tanzania dhidi ya adui kutoka nje ili nchi yetu, watu wetu pamoja na mali zao waishi kwa utulivu na amani. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (Jeshi la Ulinzi) ndiyo watendaji wakuu wa jukumu hilo na katika mwaka 2005/2006 lilitekeleza jukumu hilo vilivyo na kwa ufanisi mkubwa. Kwa sababu hiyo, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka yote ya nchi yetu kwa mwaka huo kwa ujumla ilikuwa shwari na tulivu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utulivu huo, yamekuwepo matukio mbalimbali ya kiuhalifu katika mpaka wetu wa magharibi yanayosababishwa na athari ya mapigano ya wenyewe kwa wenyewe na migogoro ya kikabila katika nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo *(DRC)* na Rwanda. Matukio hayo yamekuwa yakihatarisha usalama wa wananchi wetu waliopo katika maeneo ya mpaka huo pamoja na mali zao. Yamekuwepo pia matukio ya uvukaji haramu wa mpaka wetu na nchi ya Kenya unaofanywa na watu toka nchi za Eritrea, Ethiopia na Sudan kuingia Tanzania.

Hata hivyo, Jeshi letu la Ulinzi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama waliweza kuyadhibiti matukio hayo na baadhi ya wahalifu na wavukaji haramu wa mipaka wamekamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria. Aidha, vikao vya ujirani mwema vilivyohusisha mikoa ya mipakani ya nchi yetu na nchi jirani vimefanyika kama hatua mojawapo ya kukabiliana na matatizo yanayohatarisha usalama wa mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile lipo tatizo la baadhi za alama zinazotambulisha mpaka wetu na nchi ya Kenya kuharibiwa. Hata hivyo, Mamlaka zinazohusika zimekumbushwa na kuhimizwa kuweka upya alama hizo muhimu.

Mheshimiwa Spika Uimarishaji wa Jeshi Kiutendaji, wakati huu wa amani, Serikali imeendelea na juhudi za kuliimarisha Jeshi letu la Ulinzi kiutendaji na kuliongezea kiwango chake cha utayari kukabiliana na adui katika jukumu la ulinzi wa nchi wetu na pia kuliongezea uwezo wa kutekeleza majukumu mengine ya kitaifa. Hii ikiwa ni pamoja na kulipatia zana na vifaa mbalimbali.

Kama ilivyoelezwa katika Hotuba ya mwaka jana, juhudi za Serikali kwa sasa zimelenga zaidi katika kulijengea Jeshi la Ulinzi uwezo wa usafiri na usafirishaji wakati maeneo mengine yakiendelea kushughulikiwa hatua kwa hatua kutokana na uwezo uliopo kifedha. Juhudi zilizofanyika katika mwaka 2005/2006 ni pamoja na:-

Kukamilisha taratibu na kulipia malipo ya awali ya mkataba wa ununuzi wa magari mapya ya kijeshi. Mkupuo wa kwanza wa magari hayo unategemewa kupokelewa kati ya mwezi Oktoba na Novemba, 2006.

Kulipia malipo ya pili ya mkataba wa ununuzi wa Helikopta kwa ajili ya shughuli za uokoaji. Baadhi ya Helikopta hizo zimekwishapokelewa na ifikapo mwisho na mwaka 2006 Helikopta zote zitakuwa zimepokelewa.

Kufufua, kukukarabati na kuboresha zana za kijeshi na vifaa mbali mbali.

Kuunganisha boti za doria hapa nchini kwa kutumia wataalam wetu wanaosimamiwa na wataalam wa Kampuni moja toka Falme za Nchi za Kiarabu (*UAE*) tuliyoingia nayo mkataba wa kutuuzia boti hizo. Boti zingine zinaendelea kuunganishwa na Kampuni hiyo huko *UAE* na zinategemewa kupokelewa kabla ya mwisho wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kuliimarisha Jeshi la Ulinzi kiutendaji imehusisha pia kuwawezesha wanajeshi kufanya mafunzo na mazoezi ya kijeshi ili kuwaandaa na kuwaimarisha kimapigano. Katika mwaka 2005/2006, Serikali imeliwezesha Jeshi la Ulinzi kuendesha mazoezi mbalimbali katika ngazi ya Kamandi, Brigedi na Vikosi kwa kufuata muhtasari wa Mwongozo wa Mafunzo ulioandaliwa. Mazoezi hayo yameendelea kuwajengea wanajeshi wetu umahiri wa kutumia zana na vifaa, utimamu wa mwili na mbinu za kisasa za kumkabili adui katika jukumu la ulinzi wa nchi yetu. Aidha, Serikali imeliwezesha Jeshi la Ulinzi kutoa mafunzo kwa maafisa na wapiganaji wake katika Vyuo na Shule za Kijeshi ndani na nje ya nchi ili kuwaendeleza kitaaluma katika fani zao na kuimarisha uwezo wao wa uongozi.

Mheshimiwa Spika, jukumu lingine la kiutendaji la Jeshi la Ulinzi ni kusaidia Mamlaka za Kiraia wakati wa dharura na katika kukabiliana na athari za majanga. Jeshi la Ulinzi linalipa umuhimu wa juu jukumu hili na Serikali imeendelea kuliimarisha kiuwezo. Hii ikiwa ni pamoja na kulipatia nyenzo kama vile Helikopta kwa ajili ya shughuli za uokoaji, magari na madaraja ya kijeshi ambayo yametumika pia katika barabara mbalimbali hapa nchini baada ya madaraja yaliyojengwa katika barabara hizo kusombwa na mafuriko.

Lengo la Serikali ni kuliimarisha Jeshi la Ulinzi ili liwe na uwezo wa kuitikia na kutoa msaada kwa haraka kwa mamlaka mbalimbali za kiraia pale linapohitajika kufanya hivyo. Kutokana na kuimarika katika kutekeleza jukumu hili, katika mwaka 2005/2006 Jeshi la Ulinzi limeitikia na kushiriki katika kukabili dharura mbalimbali hapa nchini zikiwemo:-

Utoaji wa huduma za matibabu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili wakati Madaktari na Wauguzi wengi katika Hospitali hiyo walipogoma kufanya kazi mwezi Novemba, 2005.

Ujenzi wa daraja lililobomoka eneo la Msata katika barabara ya Chalinze kuelekea Segera mwezi Februari, 2006.

Kuhifadhi na kusambaza mitihani ya shule mbalimbali katika baadhi ya maeneo nchini wakati wa mitihani ya Taifa.

Kutoa taarifa kwa mamlaka za polisi kwa suala zima la kupambana na ujambazi nchini.

Uokoaji katika Jengo la ghorofa tatu lilipoporomoka huko Chang'ombe, Dar es Salaam mwezi Machi, 2006.

Kusambaza vifaa mbalimbali vya uchaguzi wakati wa Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Desemba 2005.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Kijeshi na Kiulinzi na Serikali na Nchi nyingine Duniani kuendeleza na kudumisha ushirikiano katika nyanja za kijeshi na kiulinzi na Serikali za nchi nyingine na Jumuiya mbalimbali za Kimataifa ni jukumu lingine lililotekelezwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa kutekeleza jukumu hilo kwa mwaka 2005/2006 tumeendelea kufanikisha mambo muhimu yafuatayo:-

Kuendelea kuijengea nchi yetu mazingira ya kuishi kwa utulivu na amani na nchi nyingine duniani na hasa nchi jirani.

Kutekeleza wajibu wa nchi yetu katika ushirikiano na nchi nyingine katika Jumuiya za Kimataifa kwa madhumuni ya kudumisha usalama na amani katika Kanda yetu, Afrika na duniani kote.

Jeshi letu la Ulinzi limeshiriki katika mazoezi ya pamoja ya kuwapatia wanajeshi wetu taaluma na uzoefu katika fani zao.

Jeshi letu la Ulinzi limepata misaada ya kiufundi, teknolojia mpya na vifaa vya kijeshi pamoja na vya huduma za kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, ni kwa misingi hiyo katika mwaka 2005/2006 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali yetu na Serikali za nchi za Jamhuri ya Watu wa China, Shirikisho la Ujerumani, Falme za Nchi za Kiarabu, Ufaransa, Uingereza, Marekani, Canada, Nigeria, India na Shelisheli. Aidha, Wizara imeshiriki kikamilifu katika kutekeleza makubaliano ya ushirikiano wetu na nchi nyingine katika Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sasa naomba kutaja mambo muhimu yaliyotokea katika mwaka 2005/2006 katika ushirikiano wetu na baadhi ya Serikali na Jumuiya hizo:-

Ushirikiano na Nchi Moja Moja *(Bilateral Cooperation)* (a) Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China

Serikari ya Jamhuri ya Watu wa China imetoa msaada wa zana na vifaa mbali mbali vya kijeshi vyenye thamani ya Maendeleo ya Vyama vya Michezo milioni kwa ajili ya Jeshi letu la Ulinzi. Aidha, baadhi ya Maofisa wa Jeshi la Ulinzi limepewa nafasi za mafunzo ya kijeshi nchini China. Katika kudumisha uhusiano uliopo baina ya nchi hizi, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali George Waitara, alifanya ziara ya kutembelea China mwezi Septemba, 2005. Serikali ya Shirikisho la Ujerumani. Tanzania imetembelewa na Wajumbe wa Kamati ya Fedha ya Bunge la Ujerumani mwezi Aprili, 2006 ili kuona miradi inayofadhiliwa na nchi yao inavyotekelezwa ambayo ni:-

·Ukarabati wa Hospitali Kuu ya Jeshi, Lugalo.
·Uimarishaji wa Karakana Kuu ya Magari ya Jeshi, Lugalo.
·Ujenzi wa Hospitali ya Bububu, Zanzibar.

Vile vile Serikali ya Ujerumani imelipatia Jeshi la Ulinzi nafasi mbali mbali za mafunzo ya kijeshi nchini Ujerumani na kutoa huduma za matibabu kwa maafisa, askari na familia zao nchini Ujerumani. Serikali ya Falme za Nchi za Kiarabu. Serikali ya Umoja wa Falme za Kiarabu imeanza maandalizi ya awali ya kusaidia ujenzi wa Chuo cha Ukamanda na Unadhimu kwa Maafisa, Arusha. Serikali ya Canada imetoa nafasi za mafunzo ya kijeshi na mafunzo ya kulinda amani kwa Jeshi la Ulinzi. Serikali ya India imetoa nafasi za mafunzo ya kijeshi na mafunzo ya kulinda amani kwa Jeshi la Ulinzi na pia kuwapatia matibabu maafisa, askari na familia zao nchini India.

Serikali ya Uingereza Serikali ya Uingereza imetoa nafasi za mafunzo ya kijeshi na ukufunzi wa ulinzi wa amani na ulinzi wa Ukanda wetu wa Uchumi katika Bahari ya Hindi kwa Jeshi la Ulinzi. Kikundi cha Maafisa 18 toka Chuo cha Kijeshi cha Nigeria kilifanya ziara ya kimafunzo hapa nchini mwezi Mei, 2006 kwa mwaliko wa Jeshi la Ulinzi.

Serikali ya Marekani imetoa nafasi za mafunzo kuhusu kupambana na ugaidi na mafunzo mengine ya kiwango cha shahada kwa Jeshi la Ulinzi. Aidha, Mwezi Juni, 2006 Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alifanya ziara ya kutembelea nchi ya Marekani kufuatia mwaliko wa Waziri wa Ulinzi wa nchi hiyo. Ziara hiyo ililenga kuimarisha uhusiano baina ya majeshi ya nchi hizi mbili.

Serikali ya Afrika Kusini Mwezi Aprili, 2006 Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alitembelea nchi ya Afrika Kusini kufuatia mwaliko wa Waziri wa Ulinzi wa nchi hiyo kwa lengo la kuimarisha ushirikiano baina ya majeshi ya nchi mbili hizi. Serikali ya Shelisheli Serikali za Tanzania na Shelisheli zimefikia makubaliano ya uendeshaji wa mafunzo kwa maafisa na askari wa majeshi yao ikiwa ni pamoja na kubadilishana wakufunzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuratibu utekelezaji wa makubaliano ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika yanayohusu nyanja za ulinzi na kijeshi hapa nchini. Baadhi ya mambo yaliyoshughulikiwa katika mwaka 2005/2006 ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa na Mawaziri wa Ulinzi wa nchi za Jumuiya hii kwenye mkutano wao uliofanyika Nairobi, Kenya tarehe 7 Machi, 2003. Baadhi ya mambo hayo ni:-

Kuendelea kubadilishana wanafunzi na wakufunzi wa kijeshi.

Majeshi ya nchi hizi kufanya mazoezi ya pamoja ambapo mwezi Septemba, 2005 Majeshi ya nchi hizi yalikuwa na zoezi la pamoja kuhusu operesheni ya Ugaidi wa Kimataifa lililoitwa *"Trend Maker"* na kufanyika Nairobi, Kenya. Kwa sasa majeshi hayo yanajiandaa na zoezi lingine liitwalo "*Hot Spring"* lililopangwa kufanyika Kampala, Uganda kati ya mwezi Agosti na Septemba, 2006.

Kushirikiana katika masuala ya kiufundi baina ya majeshi ya nchi hizi ambapo Timu ya pamoja ya Wataalam wa Kijeshi, mwezi Agosti, 2005 ilitembelea Taasisi za kijeshi za Tanzania kama ilivyofanya kwa nchi za Kenya na Uganda. Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeshiriki vikao vya maandalizi vya Sekretariet ya Jumuiya hii na kisha kushiriki katika Mkutano wa Mawaziri wake uliofanyika Windhoek, Namibia, tarehe 13 – 15 Juni, 2006 na uliofanyika tarehe 17 – 21 Juni, 2006. Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee aliongoza ujumbe wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mikutano hiyo miongoni mwa mambo mengine ilizungumzia masuala ya Uchaguzi uliofanyika *DRC* mwishoni mwa mwezi Julai, 2006.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania kwa sasa inashikilia nafasi ya Mwenyekiti wa *SADC Organ* chombo kinachoshughulikia masuala ya Ulinzi na Usalama katika Jumuiya hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kushiriki na kutoa mchango wake kuhusu masuala ya ulinzi na kijeshi katika Jumuiya za Kimataifa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa wajibu wa Tanzania katika Jumuiya hizo kulingana na makubaliano yaliyofikiwa. Jumuiya hizo ni kama vile Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika. Aidha, ushiriki wetu katika Jumuiya hizo umeendelea kuwa wa manufaa kwa nchi yetu. Kwa mfano Umoja wa Mataifa umetoa nafasi za kozi mbalimbali za kulinda amani kwa Jeshi letu la Ulinzi ili kuwaandaa maafisa na askari kuweza kushiriki kikamilifu katika operesheni mbalimbali za kulinda amani duniani.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha mahusiano ya kijeshi na nchi mbalimbali duniani, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatarajia kuboresha Ofisi za Waambata Jeshi katika Balozi zetu nchi za nje na kufungua Ofisi mpya katika Balozi zetu zilizopo Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Malawi, Marekani na Nigeria. Pia inatarajiwa kufungua ofisi za Uwakilishi katika Jumuiya za Kimataifa ikiwemo Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na *SADC*.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Umma, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kuwa ulinzi wa Tanzania ni jukumu la kila Mtanzania. Ni kwa msingi huo Serikali inatambua kuwa umma wa Watanzania ni nguzo mojawapo ya kusaidia nguvu ya Taifa ya kudhibiti ulinzi na usalama wa nchi yetu. Ili kuuimarisha katika jukumu hilo, Serikali imeuhamasisha na kuuwezesha umma wa Watanzania kufanya mafunzo maalum ya kiulinzi au mafunzo ya mgambo. Jeshi la Ulinzi ndilo linalowajibika katika kuendesha na kusimamia mafunzo hayo kwa malengo maalum ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005/2006 malengo yaliyowekwa ya idadi ya wanamgambo waliopata mafunzo ya awali imeweza kufikiwa kwa kila Mkoa wa Tanzania Bara. Aidha, kwa madhumuni ya kuimarisha Kada ya Viongozi wa Mgambo, katika mwaka huo, Jeshi la Ulinzi liliendesha kozi mbili za Uongozi Mdogo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006/2007 mafunzo ya ulinzi wa umma yataendelea kutolewa kwa kufundisha Wanamgambo katika kila Mkoa Tanzania Bara. Sambamba na hilo, upo mpango wa kuendesha kozi moja ya Uongozi Mdogo na nyingine ya Uongozi Mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuoanisha nadharia na vitendo katika mafunzo ya mgambo, kuanzia mwaka 2006/2007, Jeshi la Ulinzi litaendesha kila mwaka, Zoezi la Medani la Batalioni moja katika Kanda moja kati ya Kanda Nne za Mgambo.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana wa Kitanzania, jukumu lingine la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kusimamia uendeshaji wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wa Kitanzania. Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ndilo lenye wajibu wa kuwachukua vijana hao katika makambi yake na kuwapatia mafunzo ya ukakamavu, ulinzi, uimarishaji wa umoja kitaifa na kuwajenga vijana katika uzalendo wa hali ya juu. Aidha, JKT huwapatia vijana hao mafunzo ya ufundi stadi, uvuvi, kilimo na ufugaji bora ili wamalizapo mafunzo yao waweze kujiajiri wenyewe au kuajiriwa na kuweza kujitegemea na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005/2006, JKT ilikuwa na vijana 3374 wa Operesheni Jiajiri waliochukuliwa katika makambi yake mwezi Machi, 2005. Vijana hao wanatarajia kumaliza mkataba wao wa mafunzo ya miaka miwili mwezi Machi, 2007. Baada ya kupatiwa mafunzo ya awali ya miezi sita ya ukakamavu, ulinzi na uzalendo, vijana hao kwa sasa wanaendelea kupatiwa mafunzo ya ufundi stadi, kilimo, ufugaji bora na uvuvi katika makambi mbalimbali ya JKT.

SUMA JKT ni Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa lililoanzishwa kwa lengo la kuendesha miradi katika sekta ya kilimo, ufugaji, uvuvi, uhandisi na ujenzi, viwanda na biashara ili kuzalisha mali na faida itakayopatikana isaidie Serikali katika gharama za uendeshaji wa shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa. Ili kufanikisha jukumu hilo, SUMA JKT inawajibika kuandaa mipango ya aina mbalimbali kwa lengo la kuongeza tija, kuboresha teknolojia na kuimarisha shughuli zake. Hivyo, miongoni mwa shughuli zilizotekelezwa na SUMA JKT katika kipindi cha 2005/2006 zilikuwa zifuatazo:

Mwaka 2004/2005, SUMA JKT ilingia ubia na Kampuni ya *Maoming Sino Tanzania Great Wall Industrial Development* toka Uchina kuendesha Kiwanda cha Ushonaji Nguo cha Ruvu JKT. Ili kutekeleza ubia huo, katika mwaka 2005/2006, miundombinu pamoja na majengo ya kiwanda hicho yamefanyiwa ukarabati, mashine zimefungwa na wataalam toka Uchina waliwasili nchini kwa ajili ya kuwafundisha vijana watakaohusika na uzalishaji. Uzalishaji wa majaribio umekwisha anza. Gharama ya ubia huu ni shilingi 735.3 milioni.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kuingia ubia kati ya Kampuni ya *CAMI Textile* Tanzania *Ltd* na *SUMA* JKT katika kiwanda kipya cha kushona nguo cha *CAMISUMA*, Mgulani JKT yamekamilika. Ukarabati wa majengo ya zamani na ujenzi wa jengo jipya

la kiwanda umekamilika, mashine zimefungwa, na mafunzo kwa vijana 100 watakaoajiriwa katika kiwanda hicho yamefanyika na uzalishaji wa majaribio umeanza. Kiwanda hicho kinatarajiwa kufunguliwa rasmi mwezi Agosti, 2006 na kimegharimu shilingi 1.09 bilioni.

Mheshimiwa Spika, pia SUMA JKT inaendesha kiwanda cha kutengeneza madawa cha TANZANSINO kilichopo Chang'ombe, Dar es Salaam kwa kushirikiana na Jimbo la Shanxi la Jamhuri ya Watu wa China. Katika mwaka 2005/2006-kiwanda hicho kilifanyiwa ukarabati wa maghala yake ili kiweze kufikia kiwango cha kimataifa. Aidha, kiwanda hicho kiliendelea na utafiti wa dawa ya kutibu malaria ya *ARTECOM* na taratibu za kupata vibali kutoka Tanzania *Drugs and Food Authority* (*TDFA*) kuweza kuzalisha na kuuza dawa hiyo hapa nchini zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya kilimo jitihada za kuboresha sekta hii zimelenga sio tu kutosheleza mahitaji ya Jeshi, bali pia kwa ajili ya kuuza ndani na nje ya nchi. Ili kujiimarisha katika kufanikisha lengo hilo, SUMA JKT inaendelea kutafuta wawekezaji wengine kuingia nao ubia, kutafuta mikopo, kwa ajili ya kununua matrekta na zana za kilimo, kuongeza idadi ya wataalam, upimaji wa maeneo ya mashamba na kuendesha semina za mafunzo ya uendeshaji na uongozi wa miradi kwa wataalam wake.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya ujenzi, SUMA JKT imeendelea na utekelezaji wa miradi iliyopewa na Serikali mwaka 2004/2005 ya ujenzi wa nyumba 250 za Watumishi wa Serikali, Dodoma, ambapo nyumba 98 zimekamilika; ujenzi wa nyumba 91 za Viongozi wa Serikali Dar es Salaam, ambapo nyumba 50 zimekamilika; na ujenzi wa ghorofa 25 za kuishi Watumishi wa Serikali, Dar es Salaam, ambapo ujenzi huo unaendelea. Katika mwaka 2005/2006 SUMA JKT ilipewa na Serikali kandarasi ya ujenzi wa miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa nyumba 42 kwenye Makao Makuu ya Wilaya mpya za Chato, Siha, Mkinga na Nanyumbu yenye thamani ya shilingi 2.8 bilioni.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya ujenzi, SUMA JKT imejiimarisha kiasi cha kuwa na dhamana ya kupata mkopo wa mitambo ya ujenzi kutoka Kampuni ya *Hyundai* wa "motor *grader*, *vibrating roller* na *wheel loader*" yenye thamani ya shilingi 389.5 milioni. Mitambo hiyo itaiwezesha SUMA JKT kujenga barabara kwa ufanisi zaidi na hata kufikia kiwango cha lami. Sera ya SUMA JKT ni kujielekeza katika ujenzi wa barabara za vijijini ambazo wakandarasi wengi wanakwepa kuzijenga kutokana na mazingira yake kuwa magumu. Aidha, jitihada zinafanyika kuimarisha sekta hii kwa kuipatia mitambo zaidi ya kisasa, hasa "graders, bulldozers, stone crushers, rollers, dump trucks" nk. kwa ajili ya ujenzi wa barabara

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, SUMA JKT ilitumia kiasi cha shilingi 399.1 milioni katika kujiimarisha zaidi kwa kununua viwanja vitatu (eneo la Mbweni), kupima eneo la Kimbiji, kuthamini mali za SUMA JKT, kununua trekta na zana zake, kujenga *"golf course"* Lugalo na kuendeleza shamba la Bugwema.

Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 10.36 zilitumika kwa ajili ya chakula na kununulia sare za maafisa, askari na vijana wa JKT walioko makambini. Haya ni baadhi

ya mafanikio ya SUMA JKT katika jitihada za kujiendesha kibiashara na kuzalisha faida inayotumika katika kuendesha shughuli za JKT na kuleta unafuu kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Viwanda vya Utafiti na Uendelezaji wa Teknolojia ya Kijeshi jukumu lingine la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kusimamia viwanda vinavyoshughulika na utafiti na uendelezaji wa teknilojia ya kijeshi vinavyoendeshwa na Shirika la Mzinga lililoko Morogoro, na Shirika la Nyumbu *(Tanzania Automotive Technology Centre (TATC)* lililoko Kibaha, Mkoa wa Pwani.

Pamoja na kuzalisha bidhaa za kijeshi, kulikuwepo pia na dhamira ya Taifa kuvifanya viwanda hivi, vilivyoanzishwa zaidi ya miaka ishirini iliyopita, kuwa chimbuko la utafiti na uendelezaji wa teknolojia hapa nchini ili kuweza kujitegemea katika sekta ya viwanda. Hata hivyo, kutokana na uwezo mdogo kifedha uwekezaji katika mitambo na miundo mbinu ya viwanda pamoja na wataalamu umeshindikana na kukwaza kuwepo kwa utafiti na uzalishaji endelevu kama ilivyo dhamiriwa. Lipo pia tatizo la teknolojia ya zamani ya mitambo na mashine zinazotumika katika viwanda hivyo inayokwaza ufanisi katika uzalishaji. Hivyo, katika mwaka 2005/2006 baadhi ya shughuli zilizotekelezwa na Mashirika ya Mzinga na Nyumbu katika jitihada za kufanikisha malengo ya awali ya kuanzisha viwanda hivyo zilikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Mzinga linashughulika na utafiti na uzalishaji wa bidhaa za kijeshi. Katika mwaka 2005/2006, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea na juhudi za kupata mitambo ya kisasa kwa ajili ya kiwanda cha Shirika la Mzinga kama hatua ya kukarabati kiwanda hicho ili kukiimarisha katika jukumu lake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo shughuli za uzalishaji katika Shirika hilo haikuweza kufikia viwango vinavyohitajika. Hata hivyo, katika mwaka huo, Shirika hilo limeendelea kufanya shughuli za utafiti na uboreshaji wa bidhaa na vifaa mbalimbali kwa matumizi ya Jeshi la Ulinzi kwa kushirikiana na Makao Makuu ya Jeshi, ambapo zana mbalimbali zilizoharibika na kutokufanya kazi zimefufuliwa na kuanza kufanya kazi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumbu linafanya utafiti na uendelezaji wa teknolojia ya magari ya kijeshi. Katika mwaka 2005/2006 jumla ya magari 14 ya Nyumbu yamekamilika kutengenezwa na kugawiwa katika vikosi vya Jeshi la Ulinzi ili kuyafanyia majaribio na kupima uwezo wake. Hii inafanya idadi ya magari ya Nyumbu yaliyopo katika majaribio kuwa 21 baada ya magari mengine saba (7) kama hayo kugawiwa vikosini katika mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na utafiti endelevu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea na juhudi zake za kutafuta nchi marafiki zitakazokubali kushirikiana katika kuimarisha shughuli za utafiti na kuendeleza teknolojia hasa katika uzalishaji wa gari la Nyumbu kwenye Shirika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Awamu wa Tatu Mradi wa Mtandao a Mawasiliano ya Pekee *(ITN),* utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa Mtandao wa

Mawasiliano ya Pekee *(Independent Telecommunication Network (ITN)* una malengo mawili. Lengo la kwanza ni kuimarisha huduma ya mtandao huo kwa Jeshi la Ulinzi pamoja na JKT; na lengo la pili ni kuwezesha ujenzi wa Mfumo wa Serikali-Elektroni ndani ya mtandao pamoja na kutoa huduma kwa Watumiaji wengine mbali ya Serikali. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na kusimamia sehemu ya Mtandao wa kuhudumia majeshi, pia ina jukumu la kuratibu shughuli za kiufundi za ujenzi wa Mfumo wa Serikali-Elekroni ulioanza mwaka 2005/2006. Aidha, fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mfumo wa Serikali-Elektroni zimetengwa katika Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo katika mwaka 2005/2006 umehusisha uimarishaji na usimikaji wa mtambo chotara na kuukamilisha. Kwa upande wa ujenzi wa Mfumo wa Serikali Elektroni, muundo mbinu wa pete ya nyaya za *fibre optic* umesimikwa. Hatua hiyo imewezesha kuunganishwa kwenye muundo mbinu huo kwa Vituo vya Wizara za Fedha, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Bunge (Dar-es-Salaam). Kazi iliyosalia ni kufunga mitambo. Vile vile, katika mwaka huo mafunzo ya awali kwa wataalamu wetu watakaohusika na mtandao huo yalitolewa.

Mheshimiwa Spika, usimikaji wa muundo mbinu wa pete za nyaya za *fibre optic* utaendelea katika mwaka 2006/2007 ambapo Wizara zote zilizosalia zitaunganishwa kwenye muundo mbinu huo sambamba na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na *Ocean Road.* Pia ujenzi wa Vituo 21 vya Serikali - Elektroni katika Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa unategemewa kuanza katika mwaka huu. Vile vile katika mwaka huu inatarajiwa kujenga vituo 10 vya Serikali - Elektroni (vinavyotumia masafa ya "C" na "KU") Dodoma (Ofisi ya Bunge), Arusha, Tabora, Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mafia na Nachingwea; mpaka wa Kasumulo, Tunduma na Kyaka,. Sambamba na kazi hizo, mafunzo ya awali kwa watumiaji wa Serikali - Elektroni na wataalam yatafanyika.

Mheshimiwa Spika, Huduma na Mahitaji Muhimu kwa Wanajeshi na Vijana wa JKT, Serikali imeendelea na mipango ya kuimarisha utoaji wa huduma na mahitaji muhimu kwa wanajeshi na vijana wa JKT kwa lengo la kuboresha maisha yao na kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kwa upande wa utolewaji wa huduma na mahitaji muhimu ya chakula, tiba na sare katika mwaka 2005/2006 hali ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, juhudi za kuimarisha na kuendeleza mfumo wa utoaji wa huduma ya chakula kwa kutumia utaratibu wa mzabuni zinaendelea. Kwa ujumla mfumo huu umekuwa wa mafanikio tangu uanzishwe miaka miwili iliyopita, hasa kuwepo kwa matumizi mazuri ya fedha za Serikali. Hata hivyo, zilikuwepo kasoro chache zilizosababishwa na upungufu wa fedha baada ya bei za vyakula kupanda. Hatua za dharura na za muda zilichukuliwa ili kudhibiti hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa sare kwa wanajeshi na vijana wa JKT umeendelea kuwa mzuri na kuimarika. Maafisa, wapiganaji na vijana wamepatiwa sare kulingana na stahili na kwa wakati. Katika hili napenda kueleza kwamba katika muda mfupi ujao baadhi ya sare kwa ajili ya wanajeshi na vijana zitaweza kushonwa na viwanda vyetu kama vile Kiwanda cha Ushonaji cha Ruvu JKT Kiwanda cha *CAMISUMA* cha Mgulani JKT nilivyovielezea hapo awali na Kiwanda cha Chang'ombe ambacho kitaimarishwa. Hii ni mojawapo ya hatua zinazochukuliwa na Serikali kuimarisha mafanikio yaliyopatikana katika upatikanaji wa huduma ya sare kwa ajili ya majeshi yetu. Hatua nyingine ni kuandaa makadirio sahihi ya mahitaji ya sare na kutenga fedha za kutosha katika bajeti. Aidha, hatua nyingine ni kununua mali ghafi za kutengenezea sare kutoka katika viwanda vya hapa nchini badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi. Hata hivyo, uzoefu umeonyesha kuwa suala hili linahitaji juhudi na dhamira ya pamoja ya wadau wote nchini vikiwemo vyombo vya Serikali na wenye viwanda.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma za Tiba katika majeshi yetu (Jeshi la Ulinzi na JKT) kwa maana ya kuboresha Hospitali na Zahanati zilizopo ikiwa ni pamoja na kuzipatia vifaa bora vya kisasa, kuimarisha upatikanaji wa dawa za kutosha kwa vijana wa JKT, wanajeshi na familia zao pamoja na wananchi waishio jirani na Hospitali hizo. Aidha, madaktari na wauguzi wamepatiwa nafasi za mafunzo ili kujiendeleza katika fani zao. Hospitali na Zahanati hizo pia zimeendelea kutoa huduma kwa wananchi wanaoishi karibu na makambi. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 70 ya wanaotibiwa katika Hospitali na Zahanati za Jeshi ni raia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uboreshaji wa Hospitali za Jeshi, napenda kueleza kuwa baada ya kusaidia ukarabati na ujenzi wa Hospitali mbalimbali za Jeshi la Ulinzi zilizoko Tanzania Bara, Serikali ya Shirikisho la Ujerumani imeanza kusaidia ujenzi wa Hospitali ya Kanda Bububu, Zanzibar. Kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa, Serikali ya Tanzania itakarabati majengo ya zamani pamoja na kuweka miundo mbinu.

Mheshimiwa Spika, Uboreshaji wa Mazingira ya Kufanyia Kazi ili majeshi yetu (Jeshi la Ulinzi na JKT) yaweze kutekeleza wajibu wao ipasavyo, Serikali ina wajibu wa kuyawekea na kuyahakikishia mazingira bora ya kazi. Hii ikiwa ni pamoja na nyumba za kuishi na za kutosha kwa ajili ya wanajeshi na familia zao; miundo mbinu ya maji safi na majitaka, umeme na simu; ofisi, mabohari, maghala, vitendea kazi, vyuo na shule, viwanja vya michezo pamoja na maeneo ya kufanyia mazoezi ya kijeshi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uwezo mdogo kifedha, Serikali haijaweza kufanikisha mahitaji yote hayo na hivyo upo upungufu kwenye maeneo mengi. Serikali inayo dhamira ya kupunguza upungufu huo, hatua kwa hatua, kadri uwezo wa kifedha unavyoruhusu. Hata hivyo, maeneo yenye upungufu mkubwa kiasi cha kuathiri utendaji wa majeshi yetu na wanajeshi wenyewe umepewa kipaumbele kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za Kuishi, Mabweni, Miundo Mbinu ya Majisafi na Majitaka.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2005/2006 katika ujenzi wa nyumba za kuishi, mabweni, mifumo ya maji safi na maji taka yapo kama ifuatavyo:-

·Ujenzi nyumba 3 za kuishi Maafisa wa ngazi ya juu huko Mkalama, Dodoma uko katika hatua za mwisho. Mpango wa kupeleka maji safi unafanyika.

·Nyumba 2 za ghorofa za kuishi familia 12 za Maafisa 12 huko Tanga zimenunuliwa. Kazi za matengenezo ya ghorofa moja ziko katika hatua ya mwisho kukamilika.

·Jengo moja la kuishi familia 4 huko Nguvumali, Tanga limefanyiwa matengenezo na limekamilika.

·Ujenzi wa nyumba 6 za kuishi Maafisa huko Lugalo, Dar es Salaam upo katika hatua za mwisho.

·Ujenzi wa nyumba 44 za kuishi Maafisa na askari huko Makambako, Iringa zimefikia hatua ya kuezekwa.

·Nyumba za kuishi 36 huko Pemba ziko katika hatua za umaliziaji.

·Mabwalo 6 ya kuishi askari huko Bububu Zanzibar), Kagera, Pande na Tongoni (Tanga), Rukwa na Kigoma yamejengwa. Mabweni ya huko Kagera, Bububu, Tongoni na Pande yako katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Mabwalo, bwalo moja la Maafisa huko Kiluvya, Pwani na moja la askari huko Monduli, Arusha yamejengwa na yote yamekamilika. Pia mabwalo mawili huko Kiabakari, Musoma yamefanyiwa ukarabati mkubwa na yote yamekamilika. Aidha, Bwalo moja la askari huko Makao Makuu ya Brigedi, Zanzibar linafanyiwa matengenezo.

·Mfumo wa maji safi katika Hospitali ya Jeshi iliyoko huko Mwanza umefafanyiwa matengenezo makubwa na kazi imekamilika.

·Mradi wa kuchimba kisima cha maji na kuyasambaza huko Kisarawe, Pwani upo katika hatua ya mwisho kukamilika.

·Mifumo ya maji taka sehemu ya Lugalo *Area C* na *D* na Keko huko Dar es Salaam, Nguvumali, Tanga, na Ihumwa, Dodoma imefanyiwa matengenezo makubwa na kukamilika.

·Matenegenezo makubwa ya mifumo wa maji taka na maji safi huko Mirambo, Tabora na Kigamboni, Dar es Salaam yamnaendelea. Aidha, uchimbaji visima,

usambazaji maji safi na utengenezaji wa mfumo wa maji taka huko Gongo la Mboto, Dar es Salaam unaendelea.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi mingine ya ujenzi wa majengo muhimu iliyotekelezwa katika mwaka 2005/2006 katika maeneo mbalimbali ya Jeshi. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa maghala 7 ambayo yamekamilika, Hanga kubwa la kuegesha ndege ambalo awamu ya kwanza ya ujenzi imekamilika, na maghala 8 ambayo yako katika hatua ya mwisho ya ujenzi Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Aidha, Hospitali ya Wawi huko Pemba imefanyiwa ukarabati. Ukarabati wa Hospitali ya Welezo huko Zanzibar umekamilika. Pia ujenzi wa Zahanati ya Jeshi huko Mtwara uko katika hatua za mwisho kukamilika. Vile vile ujenzi wa wadi ya Viongozi huko Kiabakari, Musoma pamoja na majengo ya utawala huko Msangani, Pwani umekamilika.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kutafuta, kuyaendeleza na kuyatunza maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za majeshi yetu. Pamoja na shughuli mbalimbali za maendeleo zinazofanyika ndani ya maeneo hayo, lililo muhimu pia ni kuyamiliki kisheria. Kwa sababu baadhi ya maeneo ya Jeshi yaliyopo bado kumilikiwa kisheria, kumekuwepo na migogoro ya umiliki kati ya Jeshi na wananchi wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa migogoro hiyo, tangu mwaka 2003/2004, Serikali imekuwa ikitekeleza programu maalum ya kuyapima maeneo yote ya Jeshi hapa nchini kama hatua ya kuweza kuyamiliki kisheria. Katika mwaka 2005/2006 maeneo ya majeshi yaliyopimwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili kutekeleza programu hiyo ni yale yaliyoko katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Lindi, Mbeya, Mwanza, Tanga na Tabora. Kazi za upimaji wa maeneo hayo zimefanywa na wataalam wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kupima maeneo hayo linaendeshwa kwa kuzingatia taratibu zote za kisheria na tumepewa ushirikiano mkubwa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Uongozi wa Mikoa, Wilaya, Serikali za Mitaa na Vijiji ambako maeneo hayo yamo. Aidha, mawasiliano yamefanyika kati ya Wizara Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili kuharakisha usajili wa ramani za maeneo yote yaliyokwishapimwa na kupata umiliki wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa programu ya kupima maeneo ya Jeshi utaendelea katika mwaka 2006/2007 kwa kuhusisha maeneo yaliyoko katika Mikoa ya Tanga, Mara, Dodoma, Kigoma na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo yaliyochukuliwa na Serikali kwa ajili ya shughuli za kijeshi ni mali ya wananchi waliokuwa wakiyamiliki hapo awali. Wizara inaendeleza juhudi za kuwalipa fidia. Jumla ya shilingi 917.24 milioni zimelipwa kwa wananchi katika zoezi hili la fidia.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa mapungufu hayo, katika mwaka 2005/2006, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imefuatilia suala la fidia kwa wananchi wa Tondoroni na Msangani (Pwani), Oldonyo Sambu (Arusha), Kawe (Dar es Salaam) na Welezo/Kinoni (Tanzania Visiwani) ambao maeneo yao yalichukuliwa kwa ajili ya shughuli za Jeshi na kuwalipa jumla ya shilingi 917.24 milioni walizokuwa wakidai.

Mheshimiwa Spika, Vita Dhidi ya Maradhi ya UKIMWI, vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI na maradhi nyemelezi ni yetu sote na sisi katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Taasisi zake tunaipa umuhimu mkubwa. Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, *TACAIDS*, Mashirika ya Kimataifa na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali tumeendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa kasi ya kuenea kwa maradhi hayo inapunguzwa kwa kadri iwezekanavyo katika Wizara na Taasisi zetu. Elimu kuhusu UKIMWI imesisitizwa na Wanajeshi wengi pamoja na Watumishi wa Umma wanaelewa ipasavyo athari za maradhi hayo na jinsi ya kujikinga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za kutoa elimu kuhusu maradhi haya, imehakikishwa kuwa dawa kwa ajili ya kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI *(Anti Retrovirus)* zinaendelea kutolewa kwa watu waliothirika wakiwemo Watumishi wa Umma na Wanajeshi pamoja na familia zao. Ili kufanikisha majukumu ya kutoa elimu kuhusu UKIMWI katika mwaka 2005/2006, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake ilipewa shilingi 845.7 milioni kwa shughuli za UKIMWI kutoka mfuko wa *TMAP.* Aidha, Jeshi la Ulinzi lilipewa shilingi 158.0 milioni kutoka *TACAIDS.*

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha vita dhidi ya maradhi ya UKIMWI na magonjwa nyemelezi itaundwa Kamati ya pamoja ambayo itakuwa na wajumbe kutoka Wizarani, Jeshi la Ulinzi na JKT ambayo itakuwa na jukumu la kuratibu masuala ya UKIMWI katika Taasisi zetu.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatekeleza vyema msingi wa Utawala Bora. Msingi huu ni muhimu kwa kila Mwanajeshi na Mtumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yao yaliyoelezwa bayana katika Kanuni za Majeshi ya Ulinzi na katika Kanuni za Utumishi wa Umma. Misingi hiyo ni pamoja na uaminifu kwa nchi ambao hauna kasoro, utii, uhodari na ushujaa. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inapiga vita vitendo vyote vya rushwa, wizi, ubadhirifu wa mali ya umma, na matumizi mabaya ya madaraka. Wakati huo huo, Wizara inahimiza katika ngazi zote za utendaji kazi, uaminifu, nidhamu na utii wa sheria na Kanuni. Ili kutekeleza suala la Utawala Bora Wizarani, kwa mwaka 2005/06 Wizara iliandaa mafunzo kwa Watumishi wa Umma 140 juu ya Rushwa, madhara yake na jinsi ya kupambana nayo.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora ni pamoja na kuwepo matumizi bora ya vifaa na fedha za Serikali zinazotengwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Katika mwaka 2005/2006 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuimarisha kanuni na taratibu za udhibiti wa matumizi ya fedha na vifaa; na uwajibikaji wa Viongozi wanaofanya maamuzi ya matumizi ya fedha katika ngazi mbalimbali. Katika kutekeleza

suala hilo, Viongozi wa Taasisi na Idara chini ya Wizara wamekuwa wakitoa maelekezo yanayopaswa kwa Makamanda wa Kamandi, Brigedi, Vikosi na Vitengo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Wizara ya Fedha na hasa Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa juhudi zao za kusaidia kujenga uwezo wa kiutendaji kwa Idara za Uhasibu ndani ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kuwezesha mafunzo ya mtandao wa kompyuta, ukarabati wa ofisi za malipo na upatikanaji wa kompyuta, jenereta na kazi ya kusambaza mtandao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, matarajio katika mwaka 2006/2007 ni kwamba Vituo vya Malipo vinavyojitegemea kwa mtandao na vitakavyoanza kulipa kwa mtandao vitaongezeka kutoka vitano (5) hadi kumi na nane (18) hususan vya mikoani. Ni matarajio yetu kwamba hatua hiyo itaimarisha udhibiti na uwajibikaji katika fedha za Serikali na hasa upatikanaji wa taarifa za fedha kwa wakati. Aidha, ni matumaini yangu kwamba Wizara ya Fedha itaendelea kulipa umuhimu suala hili la kujenga uwezo wa udhibiti wa fedha za Serikali ndani ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo na Haki za Watumishi wa Umma, ili kuboresha kazi, katika mwaka 2005/2006, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliwapatia baadhi ya Watumishi wake mafunzo mbali mbali ndani na nje ya nchi ili kuongeza ufanisi katika utendaji. Wengine walihudhuria semina za muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi. Kwa kuzingatia mpango wa mafunzo wa Wizara kwa mwaka 2005/2006 Watumishi wa Umma 3 walipewa nafasi ya kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu ya shahada ya pili, Watumishi wa Umma 42 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika fani mbali mbali, na Watumishi 8 wa Umma wanaendelea na mafunzo ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kupatiwa mafunzo ya kazi, vile vile vitendea kazi vimeboreshwa hasa kwa kuwapatia watumishi nyenzo mbalimbali za kufanyia kazi zikiwemo kompyuta, mashine za kudurufu na sare za kazi. Aidha, Wizara iliwapandisha vyeo Watumishi wa Umma 122 na kujaza nafasi mpya za kazi 17.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Elimu kwa Jamii Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yameendelea kutoa huduma mbalimbali kwa jamii ya Watanzania ikiwemo Tiba na Elimu katika maeneo mbalimbali ya shughuli zao. Katika kutekeleza jukumu hilo wamejenga mahusiano mazuri na mshikamano baina yao na jamii ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, Jeshi la Kujenga Taifa, kwa ushirikiano na Halmashauri za Wilaya husika, limeendesha, kusimamia na kuratibu Elimu ya Msingi katika makambi yake ya Bulombora (Kigoma), Oljoro (Arusha), Makutopora (Dodoma), Maramba na Mgambo (Tanga), Chita (Morogoro) na Mlale (Ruvuma). Elimu hiyo inaendelea kutolewa kwa watoto wa familia za maafisa, askari na watoto wa familia za wananchi waishio jirani na makambi hayo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tumeendelea kutoa Elimu ya

Sekondari kwa jamii ya Watanzania. Majeshi haya hutoa huduma ya Elimu ya Sekondari katika shule tisa (9) za Sekondari wanazozimiliki ambazo ni *Makongo High School,* Sekondari ya *Airwing,* Nyuki, Kigamboni, Unyanyembe, Ruhuwiko, Kizuka, Kawawa na Jitegemee.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na kutoa Elimu ya ufundi stadi na uzalishaji mali kwa vijana wa kujitolea wanaochukuliwa katika makambi, pia imeendelea kuwapatia elimu hiyo vijana waishio maeneo ya jirani na makambi ya Maramba, Mgulani na Mlale kwa gharama iliyo nafuu.

Mheshimiwa Spika, michezo katika maisha ya binadamu na hasa kwa wanajeshi ni muhimu ili kuimarisha afya, akili, nidhamu na ukakamavu wa mwili. Michezo katika majeshi ni sehemu ya kazi na mafunzo. Aidha, kulingana na utaratibu uliopo, timu za majeshi zimeendelea kushiriki katika mashindano mbalimbali ya michezo ngazi ya Kitaifa na Kimataifa. Kwa mfano, Timu za Makao Makuu ya Jeshi za riadha, mpira wa miguu, mpira wa wavu na mpira wa mikono zilishiriki katika mashindano ya michezo ya majeshi ya Afrika Mashariki yaliyojulikana kama *The 2nd East African Cultural and Sports Week* yaliyofanyika Nairobi, Kenya kuanzia tarehe 2 hadi 10 Mei, 2006. Timu za Tanzania katika mashindano hayo zilipata ushindi wa pili wa jumla. Mwaka 2007, mashindano haya yatafanyika Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo ngazi ya Kitaifa, Timu ya Makao Makuu ya JKT ya mpira wa kikapu (wanaume) imekuwa bingwa mwaka huu wa 2006. Timu ya JKT, Mbweni imekuwa mshindi wa pili katika mashindano ya mpira wa wavu ya *Nje Cup,* Timu za *Transit Camp* ya Jeshi la Ulinzi na Ruvu Stars ya JKT zinashiriki katika Ligi Kuu ya Vodacom kwa mwaka 2006. Aidha, Timu za Wizara za mpira wa miguu (wanaume) na mpira wa mikono (wanawake) zilishiriki katika mashindano ya Mei Mosi, Mjini Shinyanga na kupata ushindi wa kwanza wa jumla, wakati Timu ya wanawake mpira wa mikono ilipata ushindi wa kwanza na Timu ya wanaume mpira wa miguu ilipata ushindi wa pili. Vile vile, Timu hizo za Wizara zilishiriki katika mashindano ya Shirikisho la Michezo Wizarani yaliyofanyika mjini Morogoro.

Mheshimiwa Spika, katika mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika nchini Astralia mwezi Machi, 2006 mwanariadha wa Tanzania Koplo Samson Ramadhani aliipatia Tanzania medali ya Dhahabu baada ya kuwa mshindi wa kwanza katika mbio za kilomita 42 zilizofanyika Melbourne, Australia. Kwa ushindi huo, Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi chache zilizoibuka na medali za dhahabu. Nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa mwanariadha huyo na kumwomba aendelee kufanya vizuri zaidi katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ili alipatie sifa Jeshi na Taifa kwa ujumla. Katika kutambua juhudi zake hizi, jeshi lilimpandisha cheo Koplo Samson Ramadhani, toka *Private* hadi Koplo.

Mheshimiwa Spika, Mipango ya Utekelezaji ya Mwaka 2006/2007, mipango ya utekelezaji ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2006/2007 imelenga kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kuhusu jukumu la ulinzi

wa nchi yetu. Baadhi ya mambo yatakayoshughulikiwa katika utekelezaji wa bajeti hii yapo katika maeneo yafuatayo:-

Kuendelea kuimarisha uwezo wa majeshi yetu kiutendaji kwa kuyawezesha kuwa na kiwango cha juu cha utayari kijeshi kwa matukio yanayohitaji kushughulikiwa haraka, yanayohusu adui moja kwa moja, maafa au majanga. Eneo hili linahusu:-

Mafunzo ndani na nje ya nchi kwa wanajeshi wetu. Mazoezi ya medani na mazoezi ya Ulinzi wa Amani. Upatikanaji wa vifaa na nyenzo bora za kufanyia kazi.

Kuboresha mazingira ya utendaji, vitendea kazi, huduma na mahitajimuhimu kwa wanajeshi na vijana wa JKT. Eneo hili linahusu:-

Kuendeleza mipango ya ujenzi wa makambi mbalimbali ikiwemo kukamilisha ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi, aghala na mifumo ya maji safi na maji taka na umeme. Kupatikana kwa vyombo vya usafiri hasa magari.

Kuwapatia wanajeshi na vijana wa JKT sare za kutosha kulingana na stahili na kwa wakati.Kuwapatia vijana wa JKT, wanajeshi pamoja na familia zao huduma za tiba.Kuwapatia wanajeshi na vijana wa JKT huduma ya chakula.Kulipia kikamilifu huduma za maji, umeme na simu.

Kuendelea na upimaji wa maeneo ya Jeshi na JKT na kuyapatia Hati Miliki yake pamoja na kuendeleza taratibu za kulipa fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao kwa ajili ya shughuli za Jeshi la Ulinzi na JKT.

Kuwapatia wanajeshi na watumishi a umma stahili zao za kisheria kwa wakati na kikamilifu zikiwemo mishahara na likizo. Hii ni pamojana kuendelea na udhibiti wa kerozilizokwisha kuondolewa Jeshini hasa zinazohusu madeni binafsi kwa wapiganaji.

Kuendeleza juhudi za kupambana na janga la gonjwa la UKIMWI.

Kuendeleza ushirikiano wa kijeshi kati ya nchi yetu na nchi jirani na rafiki katika nyanja zinazohusu mafunzo ya pamoja, taaluma mbalimbali na kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa katika mashirikiano kiulinzi ndani ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Kuendeleza tafiti na uboreshaji katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali toka viwanda na mashirika yetu kwa matumizi ya majeshi yetu.

Kuendelea kutoa mafunzo ya JKT kwa vijana wa Kitanzania yanayohusu ulinzi na ujenzi wa nchi, uimarishaji wa umoja wa kitaifa na kuwajenga vijana katika uzalendo wa hali ya juu.

Kuendelea kutoa mafunzo ya mgambo kwa umma wa Kitanzania kwa madhumuni ya kuimarisha ulinzi wa umma.

Kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya mradi wa Mtandao wa Mawasiliano ya Pekee. *(ITN).*

Kuboresha Utumishi wa Umma kama ilivyoelekezwa katika *Public Service Reform Programme.*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza Hotuba yangu napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioniwezesha kufanikisha na kutekeleza jukumu la kuongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tangu niteuliwe kushika wadhifa huu mwezi Januari, 2006.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Makamanda, Maafisa, Wapiganaji na Watumishi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuleta matumaini mapya ndani ya majeshi yake.

Amiri Jeshi Mkuu alipotutembelea mwezi Februari, 2006 aliahidi kuendeleza kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, juhudi zilizokwishaanza za kuyaimarisha majeshi yetu ili yaweze kutimiza majukumu yake ya kulinda nchi yetu, watu wake pamoja na maslahi yetu. Tunamshukuru sana Amiri Jeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Waziri wetu Mkuu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa na Mawaziri wenzangu wote. Napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa William Kusila na Wajumbe wa Kamati yake kwa msaada wao walioutoa kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kutoa shukrani zangu kwa Serikali za nchi mbali mbali kwa ushirikiano wao na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, shukrani za kipekee nazitoa kwa Serikali za Jamhuri ya Watu wa China, Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani na Falme za Kiarabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri aliyenitangulia Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mbunge wa Rorya kwa kuniachia msingi mzuri wa kutekeleza majukumu yangu. Napenda Kumshukuru aliyekuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Luteni Generali Idd Gahhu aliyestaafu mwishoni mwa mwezi Juni, 2006. Natoa shukrani za pekee kwa wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nikianzia na naibu Waziri Mheshimiwa Omar Yusufu Mzee, Katibu Mkuu Bwana Abel Mwaisumo ambaye sasa hivi yuko India, anaumwa, lakini anaendelea vizuri, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Ulinzi Generali George Waitara, Mnadhimu Mkuu Mpya wa Jeshi, Luteni Generali Davis Mwamunyange, Mkuu Mpya wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Generali Abdulrahman Shio, Makamanda. Maafisa, Wapiganaji na watumishi wa Umma

wote. Nawashukuru kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa na ushauri uliojaa ukweli na uaminifu.

Ulinzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani na nje ya nchi siyo tu umeleta usalama na amani, bali pia umekuwa kichocheo muhimu na msingi wa hali ya amani, utulivu na maendeleo ya nchi yetu. Kwa sababu hiyo, ulinzi wa nchi yetu ni jukumu la lazima lisiloweza kukwepeka na Serikali inayowajibika kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hili, Watanzania wote bila kujali tofauti zetu za kiitikadi, hatuna budi kuelewa na kuunga mkono juhudi zinazochukuliwa na Serikali wakati huu wa amani kuyajengea majeshi yetu uwezo zaidi wa kudhibiti ulinzi wa nchi yetu. Ni heri nchi ikaingia gharama sasa katika kujiimarisha kiulinzi ili kumzuia adui kupata kishawishi cha kuingia nchini mwetu na kutuharibia hali yetu ya usalama, amani na utulivu tuliyonayo kulio kumsubiri aingie. Tukisubiri hadi wakati huo ufike, gharama ya kukabiliana naye na kisha kurejesha usalama, amani na utulivu pamoja na maendeleo tuliyoyapata itakuwa kubwa zaidi, chungu zaidi na tutalazimika kuibeba kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake kwa mwaka 2006/2007. Ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Taasisi zake iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kama ilivyoelezwa katika hotuba hii kwa mwaka 2006/2007, naoa Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 287,546,476,000/= fedha za hapa nchini ambazo kati yake Shilingi 241,301,487,000/= zitatumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 46,244,989,000/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mgawanyo ufuatao:-

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 38 – Jeshi la Ulinzi la Ulinzi la Wananchi … 189,569,241,000/=
Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa ........ 45,608,996,000/=
Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa … 6,123,250,000/=

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 38 – Jeshi la Ulinzi la Wananachi ........ Tshs. 200,000,000/=
Fungu39 – Jeshi la Kujenga Taifa Tshs. 200,000,000/=
Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa…45,844,989,000/=

Mheshimiwa Spika, tumegawa vitabu, vina rangi nyekundu, Wabunge wakaniangalia, lakini nataka kusema si kutokana na ushabiki wa aina yoyote ile. Ndani ya Jeshi haturuhusiwi kuwa mashabiki. Kwa hiyo, hiyo ni rangi ya Jeshi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. COL. SALEH ALI FARRAH (K.n.y. MHE. WILLIAM J. KUSILA - MWENYEKITI KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu wangu kwa nema zake kwangu na kuniwezesha kuvuta pumzi hadi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, vile vile naishukuru sana Familia yangu, hususan Mke wangu Masha Farrah na makinda yangu kwa faraja wanayonipa wakati wa dharura.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa heshiima na taadhima, naomba kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Raha leo kwa imani kubwa waliyonionyesha, naahidi na mimi sitawaangusha.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa William J. Kusila, Mbunge, kunipa nafasi hii adhimu nisome Maoni ya Kamati kwa niaba yake.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha wa 2005/2006; Pamoja Na Maoni na Ushauri wa Kamati Juu ya Makadirio na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Taarifa na Maoni ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Mwaka wa Fedha 2005/2006 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwa Wizara hii, kwa niaba ya Kamati napenda kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa ushindi mkubwa alioupata katika Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge. Napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar kwa ushindi mkubwa alioupata katika uchaguzi mkuu uliopita. Nampongeza pia Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge. Kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu uteuzi ambao ulithibitishwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa nakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa na Bunge hili kwa kura nyingi. Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mbunge, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Vile vile pongezi mahsusi ziende kwa Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Job Y. Ndugai kwa kuchaguliwa kwao katika wadhifa huo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama inampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa CCM Taifa. Aidha

naungana na wasemaji waliotangulia kuwapongeza wale wote walioteuliwa kushika nyadhifa mbali mbali katika Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi. Natoa pongezi za dhati kwa waheshimiwa wafuatao:

Mheshimiwa Luteni Mstaafu, Yusuf Rajab Makamba, kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu Mkuu wa C.C.M, Mheshimiwa Kepteni Jaka Mwambi, kuwa Naibu Katibu Mkuu Tanzania Bara, Mheshimiwa Rostam Aziz, kuwa Katibu Uchumi na Fedha, Mheshimiwa Aggrey D. Mwanri, kuwa Katibu Itikadi na Uenezi, Mheshimiwa Dr. Asha Rose - Migiro, kuwa Katibu wa Siasa na Uhusiano wa Kimataifa na Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, kuwa Katibu wa Oganaizesheni wa CCM.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kwa juhudi zake na hatua anazochukua katika kusuluhisha migogoro ya ndani na nje ya nchi kwa sababu bila ya kufanya hivyo amani ya nchi yetu itaathirika.Wakati Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma alipokuwa akiwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007 aliliambia Bunge lako tukufu kuwa viwango vya Mishahara kwa watumishi walio katika vyombo vya Ulinzi na Usalama, vitapanda zaidi kuliko vile vya watumishi wengine wa kawaida. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi huo wa kuboresha viwango vya mishahara ya watumishi hasa katika vyombo vya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru Mheshimiwa Profesa Juma A. Kapuya, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Waziri, Ndugu Abel Mwaisumo Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wataalamu wa Wizara hii kwa kushirikiana vema na Kamati hii wakati wote tulipoichambua bajeti ya Wizara. *(Makofi)*

Aidha kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, napenda kumpongeza Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali George M. Waitara kwa kazi nzuri anayoifanya. Naomba pia kumpongeza Luteni Jenerali Iddi Saleh Gahhu, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Mstaafu kwa ufanisi katika kazi yake kwa kipindi chote alipokuwa akilitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inampongeza kwa dhati Luteni Jenerali Davis Adolf Mwamunyange kwanza kwa kazi nzuri aliyokuwa akiifanya akiwa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa na Pili kwa kuteuliwa kwake kuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kamati inaamini kuwa ataendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi kama ilivyokuwa utendaji wake akiwa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na pongezi hizi, Kamati inampongeza kwa dhati Meja Jenerali Abdurahman Amir Shimbo kwa kuteuliwa kwake kuwa Mkuu mpya wa Jeshi la Kujenga Taifa. Naomba pia kuitambua kazi nzuri inayofanywa na Maafisa wa Jeshi na askari wa Jeshi letu saaa na utiifu walionao kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa jinsi walivyotoa ushirikiano katika kupitia na kujadili Taarifa ya Wizara hii. Kwa hakika utendaji kazi wa Wajumbe hawa ni wa kuzingatia muda, kufanya kazi kwa muda mrefu, na uvumilivu wa hali ya juu jambo ambalo ni muhimu sana katika Sekta ya Ulinzi. Naomba niwatambue Wajumbe hawa kwa kuwataja majina:-

Wajumbe wenyewe ni Mheshimiwa William J. Kusila, ambaye ni Mwenyekiti na Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika, ambaye ni Makamu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Spika, wajumbe wengine ni Mheshimiwa Mohamed A.Abdulaziz, Mheshimiwa Kanali Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Kanali Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya na Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninamshukuru sana Katibu wa Bunge Bwana Damian Foka na Makatibu wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Ndugu Elisa Mbise na Ndugu Athuman Hussein kwa kuihudumia vema Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama yanatokana na Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tarehe 29 Mei, 2006, Jijini Dar-es-Salaam. Katika kuichambua taarifa hiyo, Kamati ilipitia mafungu yafuatayo:-

Fungu 38 – Ngome.
Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa.
Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006. Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 na kupitia kwa undani. Naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kabla ya kupitia taarifa hiyo, katika kujiridhisha juu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati ilitembelea vikosi mbali mbali vya JWTZ Tanzania Bara na Visiwani. Kamati imeridhika na utekelezaji wa mipango ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Mambo Muhimu kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Utekelezaji wa Majukumu yake. Kamati ilielezwa majukumu ya Wizara pamoja na mambo muhimu yanayotakiwa ili Wizara iweze kutekeleza kikamilifu majukumu yake. Katika maelezo hayo, Kamati ilielezwa kwamba mambo yafuatayo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Wizara:-

(i) Uwezo wa kuajiri watumishi wenye ujuzi kulingana na mahitaji.

(ii) Uwezo wa kupambana na adui wakati wowote.

(iii)Teknolojia bora ya Kijeshi kutokana na shughuli za utafiti na uzalishaji mali katika Mashirika ya Mzinga na Nyumbu.

(iv) Mazingira bora ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati: Kamati ilitembelea vikosi vya JWTZ, Bara na Zanzibar ili kuona utekelezaji wa majukumu ya ulinzi. Baada ya ziara hiyo, Kamati ilipata fursa ya kujadili kwa kina Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Pamoja na kupokea taarifa ya Wizara na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2006/2007, Kamati ina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa hali ya Mipakani ni shwari, Kamati inashauri kwamba hadhari kubwa ichukuliwe ili kujiandaa vilivyo katika kipindi hiki cha amani. Aidha kuhusu mpaka wa Malawi, Kamati inashauri kuwa Viongozi wa Tanzania na Malawi waendelee kukutana ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la mpaka kati ya nchi hizi mbili kutokana na mto Songwe kuhamahama. Vilevile Kamati inashauri kuwa Jeshi la Wananchi Tanzania liimarishe Ulinzi katika Wilaya za mipakani katika mikoa ya Kigoma, Rukwa na Kagera.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda vizuri mipaka yetu, Kamati inashauri kuwa katika mipaka yote baina ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo, ziwekwe alama za kudumu *(Beacons)*. Pamoja na ushauri huu, alama zitakazowekwa zipitiwe na kukaguliwa kila baada ya muda maalumu. Kamati pia ilibaini tatizo la maeneo ya kijeshi kuvamiwa na wananchi jambo ambalo ni hatari kiulinzi. Ni maoni ya Kamati hii kuwa kuna umuhimu wa kuzuia maeneo ya Kijeshi kuvamiwa. Sambamba na ushauri huu, mazingira ya kambi za jeshi yaboreshwe ikiwa ni pamoja na kupanda miti kambini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipoteelea vikosi vya Jeshi la Wananchi Tanzania ilijionea jinsi Jeshi letu lilivyojipanga kikamilifu katika kutekeleza majukumu yake ya kulinda mipaka ya nchi yetu. Kamati inashauri kwamba jeshi letu liendelee kupatiwa vifaa bora vya kisasa kulingana na mahitaji ya Kijeshi.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti ulinzi wa rasilimali zetu zilizopo bahari kuu masafa ya ali, *(Exclusive Economic Zone)* Kamati inashauri kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania litumike kulinda ukanda huu wa bahari ikiwa ni pamoja na kuongezewa mafuta ya kutosha kufanya hivyo. Aidha Operesheni za pamoja kwa vyombo vyote vya Ulinzi vikishirikiana na Idara ya Maliasili, zitasaidia kulinda rasilimali zetu.Kamati ilibaini kuwepo kwa tatizo la Wataalamu wengi wenye taaluma adimu kufikia muda wao wa kustaafu kwa mujibu wa Sheria. Ni maoni ya Kamati kuwa ufikiriwe uwezekano wa maafisa na Askari wa namna hiyo kuajiriwa kwa Mkataba mara baada ya kulipwa stahili zao zote.Vile vile ni vizuri kuwa na utaratibu wa kurithisha majukumu *(succession plan)* ili kuondoa tatizo la upungufu wa wataalam mara wataalam hao wanapoondoka kwenye utumishi. Aidha, utaratibu wa kuwapeleka Maafisa wa Jeshi na askari nje ya nchi kwenda

kusomea utaalamu ambao haupo hapa nchini, uendelezwe na uboreshwe zaidi kuliko ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tarehe 24 Aprili, 2006 mbele ya Kamati hii, pamoja na taarifa iliyowasilishwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Jeshi la Wananchi Tanzania, Kamati inashauri kuwa Serikali iandae mpango wa kumaliza tatizo la makazi ya Askari. Katika ushauri huu ni maoni ya Kamati kuwa mpango wa ujenzi wa maghorofa kwa ajili ya makazi ya askari unafaa kufikiriwa na kutekelezwa kwa kuishawishi mifuko ya Hifadhi za jamii kama vile *NSSF*, *LAPF* na mingineyo, kushiriki katika ujenzi na baadae kulipangisha Jeshi katika nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuwa na Jeshi linalokwenda na wakati, Kamati inashauri kuwa uwepo utaratibu wa JWTZ na JKT kutembelea Vyuo vya Elimu ya Juu ili kueleza utendaji wa JWTZ na JKT kwa madhumuni ya kuwavutia wataalamu kujiunga na JWTZ na JKT. Kufanya hivi kutasaidia kuliwezesha Jeshi kupata watu wenye uwezo wa kupata mafunzo ya Kijeshi yatakayowafanya waweze kutumia utalaamu wao Kijeshi na kuleta ufanisi zaidi katika ulinzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la madeni ya askari, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua na uamuzi mzuri wa kulipa madeni yote ya askari. Hata hivyo ni maoni ya Kamati kuwa askari anapopangiwa kazi maalumu ya kufanya, iwe ni sambamba na malipo ya stahili zake ili kuepuka mlundikano wa madeni ya askari.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa moja ya mambo muhimu kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika kutekeleza majukumu yake, ni uwezo wa Kuajiri watumishi wenye ujuzi kulingana na mahitaji, na kwa kuwa Jeshi la Kujenga Taifa linafanya kazi nyingi ikiwemo kazi ya kuwafundisha vijana Ulinzi na Uzalendo, Kamati inashauri kuwa ajira katika vyoo vya dola itoe kipaumbele kwa vijana waliohitimu mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuipongeza sana Serikali kwa jitihada zake za kuboresha hali ya maisha ya Wanajeshi na vyombo vingine vya Dola. Tunafahamu hali na matatizo yanayolikabili Taifa; Pia tunafahamu kuwa si rahisi kuyatatua matatizo yote kwa mara moja; Hata hivyo ni maoni ya Kamati hii kwamba, juhudi ya Serikali ya kuyaondoa matatizo yote yanayovikabili vyombo vyetu vya dola ikiwemo JWTZ, ziendelezwe na ziungwe mkono kwa dhati. Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kamati, na kwa niaba yangu mwenyewe binafsi, napenda kusema kazi uliyotutuma Mheshimiwa Spika, tumeifanya kwa kadri tulivyoweza. Naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, Naunga mkono hoja ya Wazri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c) na 81(1) Toleo la 2004 kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa leo, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie sote tuendelee kuwa wazima na afya njema.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwako binafsi kwa jinsi unavyoonyesha utendaji wako wa hali ya juu, pamoja na Naibu Spika wako na bila kuwasahau Wenyeviti wote wawili kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge letu kwa ufanisi mkubwa. Napenda kuwashukuru Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Msaidizi wake Dr. Wilbroad Peter Slaa, kwa kuona ninafaa kuwasaidia kazi hii ya kuwa Msemaji Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Pongezi za pekee ziwafikie wapiga kura wangu wa Jimbo la Mtambile, kwa imani yao waliyonipa kwa kunichagua kwa kura nyingi sana. Aidha nakishukuru chama changu cha *CUF* kwa mashirikiano na imani kubwa walionipa na kuniwezesha kuwa Mbunge, ninaahidi tutaendelea kushirikiana.

Mheshimiwa Spika, haitakuwa vyema kama sikumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Al Hajj Juma Athman Kapuya na Naibu wake Mheshimiwa Alhaj Omar Yusuf Mzee kwa kuanza vizuri. Pongezi Ma- Ali Hajj. Pongezi pia zimfikie Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali George Marwa Waitara na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Wananchi Luteni Jenerali Davis Adolf Mwamunyange pamoja na Mkuu Mpya wa jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Abdrahman Amir Shimbo.

Mheshimiwa Spika, majeshi ya nchi ziliozoendelea mbali na kujishughulisha sana katika medani za kimataifa katika kulinda amani na operesheni mbali mbali bado yameweza kuwa kiini cha kukuza technologia katika nyanja mbali mbali, kwa mfano kuweko na maabara endelevu ambapo tafiti za chanjo na tiba za magojwa mbali mbali zinafanyika. Mfano mzuri ni jeshi la Marekani na kitengo chake cha *United States Army Medical Research Institute of Infectious Diseases* kilichoanzishwa mwaka 1969. Kitengo hiki kinafanya utafiti na kutengeneza chanjo na tiba kwa magojwa ya wanyama na binadamu.

Mheshimiwa Spika, tunashauri, Jeshi kuanzisha na kuimarisha vitengo kama hivi kwa sababu, tumeona utendaji wa hospitali yao Lugalo na jinsi madaktari wao walivyoweza kuchukua nafasi ya madaktari ulipotokea upungufu Hospitali kuu ya Muhimbili mwishoni mwa mwaka 2005 na kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa. Wanastahili hongera kwa kazi hiyo nzuri. Askari wataalamu katika jeshi wana mafunzo ya ukakamavu, wepesi kupokea chochote kinachojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapongeza ushiriki wa majeshi yetu katika operesheni za ndani na nje ya nchi hasa katika operesheni za umoja wa Mataifa za kulinda amani ambapo askari wetu wameshiriki kwa uaminifu mkubwa na kuipatia sifa kubwa nchi yetu. *Keep it up*.

Mheshimiwa Spika, wakati sasa umefika wa kuunda Jeshi la Kisasa. Wanazuoni wa nadharia ya kihalisia katika Siasa za Kimataifa, wana usemi kuwa, ukitaka amani jiandae kwa vita na sisi hatuwezi kulikwepa hili na ndio maana Kambi ya Upinzani inatoa wito wa kuudwa kwa Jeshi la Kisasa. Pamoja na mambo mengine, tunashauri mambo yafuatayo yazingatiwe:-

(a) Kuajiri vijana wenye taaluma maalum, wenye rekodi nzuri na tabia nzuri na upendo kwa nchi yao na ambao wakifunzwa wanafunzika. *(Makofi)*

(b) Kuimarisha mafunzo kwa kuwapa askari wetu mafunzo na mbinu za kisasa sambamba na nyenzo za mafunzo yenyewe. *(Makofi)*

(c) Mafunzo yaboreshwe kwa vikosi maalum ili nchi ipate askari wenye uwezo wa Kimataifa . *(Makofi)*

(d) Vifaa vya kisasa zaidi vinunuliwe na askari wawe wanafanyia mafunzo vifaa hivyo ili waendane na dunia ya utandawazi. Wakati umefika sasa kwa askari kufundishwa matumizi ya kompyuta vikosini sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

(e) Mafunzo ya Jeshi yaboreshwe, yawe ya kisasa zaidi ili yawavutie wataalam mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jeshi limeanza utaratibu wa kuajiri vijana wenye taaluma mbalimbali kama Sheria, Udaktari, Uchumi, Utawala, Ualimu, Uhandisi, Sayansi na Ujenzi katika ngazi za Shahada ya Kwanza na ya Pili, pia wapo Mafundi Mchundo na vizuri zaidi vijana wa Kidato cha Sita waliofaulu Daraja la Kwanza na la Pili.

Mheshimiwa Spika, vijana hawa wazalendo walioamua kujitolea kulitumikia Taifa ni hazina ya Taifa. Katika habari zisizo rasmi, inasemekana kuwa, vijana wengi waliofanya mafunzo ya awali katika *intake* ya mwaka 2002, walikimbia Jeshi, si kwa kushindwa mafunzo, ila ni baada ya kuona matarajio waliyokuwa nayo ya kuendeleza taaluma zao hayapo.

Je, kuna ukweli wa hili na kama ni kweli Serikali haioni imepata hasara kubwa?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara itoe maelezo ni askari wangapi wataalam na wale wa Kidato cha Sita wa Daraja la Kwanza na la Pili, walioajiriwa mwaka 2002 bado wanalitumikia Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Wizara kuwa, Jeshi liwatumie vijana hawa wenye uwezo mkubwa kielimu katika mpango wa kudumu wa kufanikisha lengo la kuunda Jeshi la Kisasa na kukuza teknolojia kwa kuzingatia mambo yafuatayo: -

(a) Kuanzishwa kwa maabara za kisasa zaidi za Jeshi zitakazofanya uchunguzi wa magonjwa ya binadamu na mifugo yaliyopo na ile ya milipuko ili baadae chanjo na tiba za magonjwa haya zitengenezwe hapa hapa nchini. Ni aibu kuingiza dawa za kienyeji kutoka China ili kutibu malaria Tanzania. *(Makofi)*

(b) Jeshi lianzishe miradi ya kisayansi, inayolenga kutengeneza nyenzo za kazi na vyombo vya kisasa ikiwa ni pamoja na kuboresha utendaji wa Mradi wa Nyumbu, yaani *Tanzania Automotive Technology Centre (TATC),* utakaozingatia kuongeza idadi ya wataalam na vitendea kazi na kuleta mitambo mipya na ukarabati wa majengo.

(c) Jeshi (mathalani katika kitengo cha JKT), liwe na vikosi maalum vya wahandisi, wenye utaalam wa hali ya juu waliosomeshwa katika vyuo maarufu duniani katika fani za barabara, madaraja, majengo na kadhalika. Kwa kutumia wahandisi hawa, kungekuwa na uwezekano wa wananchi kujengewa nyumba za kisasa kwa bei nafuu na ndio kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

(d) Kuboresha marupurupu ya kiutaalam mbali na mishahara ya askari watakaofanya kazi katika vitengo hivi muhimu ili wapate motisha ya kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua ya kuwa, katika Majeshi haya kuna kikosi kinacho jishughulisha na masuala ya uzalishaji, ambacho ni Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Kwa utaratibu waliojiwekea Jeshi ni kwamba, JKT imepewa kufanya uzalishaji wa mazao ya kilimo na ufugaji kwa asilimia kubwa na mambo ya kijeshi asilimia ndogo. Vivyo hivyo, Jeshi la Wananchi wa Tanzania wamepewa asilimia kubwa kufanya mambo ya kijeshi na asilimia ndogo katika mambo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika tunashauri kuwa, uzalishaji wa chakula ulenge kulipatia Jeshi mahitaji yake badala ya kutumia wazabuni binafsi. Zabuni ipewe Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa ili izalishe hicho kinachohitajika. Aidha, Jeshi la Wananchi wa Tanzania libuni kazi za kufanya Wanajeshi wetu wakati wa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mishahara ya askari wetu hasa wapiganaji wa ngazi za chini zaidi ni lazima iangaliwe ili kuwaepusha na tamaa za kujiingiza katika vitendo viovu. Kama vyombo vya habari vilivyoripoti, kuna habari kuwa, katika matukio ya ujambazi yaliyotokea miezi michache iliyopita, kati ya majambazi hao walikuwepo askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Inawezekana kabisa wanashawishika kujiingiza katika vitendo hivyo, kutokana na kuishi kwao uraiani au mishahara na posho ndogo. Kwa kuwa nchi imewapa dhamana kubwa walinzi hawa wa Taifa, ni vyema wakalipwa vizuri kwa kuboresha mishahara yao na marupurupu yao kwa wakati muafaka ili waweze

kukidhi mahitaji yao na watumie muda mwingi kulitumikia Taifa katika shughuli mbalimbali za kijeshi na za maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kufahamu ni kwa nini Wizara inachelewesha mafao ya wastaafu, huku wakijua orodha ya wastaafu wa kila mwaka na tatizo hili litapatiwa lini ufumbuzi wa kudumu? Kambi ya Upinzani pia inataka kujua kuna wastaafu wangapi hadi leo ambao hawajalipwa mafao yao na nini hatma ya wastaafu hao? Pia, ni wastaafu wangapi kati ya hao wameshafariki dunia bila kufaidika na haki yao hiyo na nini hatma ya warithi wa marehemu hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni la kuchelewesha fedha za uhamisho kwa Wanajeshi wetu. Pia kuna malalamiko ya Wanajeshi kutopatiwa haki zao wanapokwenda operesheni mipakani, hali ambayo inawafanya kuwa wanyonge wa kimawazo, wakizikifiria familia zao na hivyo kuathiri utendaji wao katika operesheni hizo. Je, ni vipi hali ilivyo hivi sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la kukosa nyumba za kuishi kambini kwa askari wa JWTZ na JKT ni la muda mrefu na bado halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Imedhihirika kuwa Wanajeshi wengi wanaishi uraiani, hali ambayo si tu inashusha hadhi ya ufanisi wa kiutendaji kwa Majeshi haya, lakini pia inapunguza uwezo wa kuwadhibiti kimaadili na kuna uwezekano wa kujisahau wakiwa uraiani na kujitumbukiza kwenye vitendo viovu. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, tunashauri kuwa, mahitaji ya vyombo vyetu vya ulinzi yatumie teknolojia ya *pre-fabricated,* ambayo tunaweza kujenga nyumba nyingi kwa muda mfupi na gharama nafuu ili kukidhi shida za nyumba za wapiganaji wetu.

Mheshimiwa Spika, haipendezi na inasononesha sana kuona nyumba wanazoishi askari wetu zimechakaa sana, hazina stara, kiasi askari walio na familia wanalala na watoto wao wakubwa bila ya stara yeyote. Tusishangae maadili yakiporomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, askari wanapoishi nje ya kambi inakuwa si rahisi pindi ikitokea dharura, kupatikana kwa urahisi. Hii ni hatari kwa ulinzi na usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni nyumba ngapi zinahitajika kwa makazi ya askari wake wote Tanzania. Hivyo, ushauri wetu kwa Serikali ni kuzikarabati nyumba zote chakavu haraka iwezekanavyo, sambamba na kuwajengea makazi bora Wanajeshi wetu, ambao sote tunakubali Jeshi letu ni imara, shupavu, jasiri, linajituma bila woga na ni watiifu wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, askari wetu wengi wanapostaafu, hali zao huwa duni sana hasa wale ambao hawakufikia ngazi za Umeja na kuendelea. Hili ni kundi kubwa hivyo, tunashauri kuwa kama Serikali ina nia njema na wapiganaji wetu kupata makazi mema wanapostaafu, kuwe na utaratibu wa kuwanunulia nyumba kupitia Mashirika ya Mifuko ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, ni kawaida kabisa katika Majeshi karibu mengi Duniani kuwa na vitengo vinavyoshughulika na kazi za uzalishaji. Katika Jeshi letu la Wananchi Tanzania (JWTZ), lina vitengo hivyo pia. Kitengo cha kuzalisha magari kinajulikana kama Nyumbu na kitengo kinachojihusisha na uchimbaji wa dhahabu kinajulikana kama Meremeta.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba za Wizara hii kwa miaka ya nyuma tumekuwa tukifahamishwa jinsi vitengo hivi vinavyoendeshwa. Kwa kuwa kitengo cha Meremeta kilikuwa na jukumu la msingi, pamoja na majukumu mengine, ilikuwa ni kuhakikisha Kitengo cha Nyumbu kinapatiwa msaada mkubwa sana kifedha ili Nyumbu ifanye kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua na kuitaka Serikali ilieleze Bunge lako ni kiasi gani cha fedha kimepatiwa kitengo cha Nyumbu kwa ajili ya kujiimarisha. Aidha, tunaomba tupatiwe maelezo ni jinsi gani kitengo cha Meremeta kinavyoendeshwa. Hapa hatuombi maelezo ya juu juu tu, tunaomba nyaraka kuthibitisha Waziri atakayotujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majengo ya Hospitali ya Nyumbu ni makubwa yaliyojengwa tangu mwaka 1980, kwa lengo la kuwahudumia Wanajeshi na raia. Kwa masikitiko makubwa majengo hayo yamebakia maonesho na hayatumiki kutokana na ukosefu wa vitendea kazi na vifaa zikiwemo mashine mbalimbali, ambazo zinajumuisha ubora wa kuitwa hospitali.

Mheshimiwa Spika, jengo hili hivi sasa ni chakavu hivyo, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni lini jengo hili litafanyiwa ukarabati na kukamilishwa kutumika kama hospitali. Hivi Serikali haioni kukamilika kwa matumizi ya Hospitali ya Nyumbu, kutapunguza matatizo makubwa ya wananchi wa Kibaha?

Mheshimiwa Spika, Kamandi ya *Navy* ni kiungo muhimu sana katika Jeshi katika ulinzi wa baharini, lakini uchache wa boti na boti ndogo zilizopo imekuwa ni kikwazo kwa boti hizo kwenda kwenye bahari kuu, ambapo imebainika kuna meli kadhaa za kigeni zinazovuna rasilimali zetu isivyo halali, huku tukijiuliza nini cha kufanya. Hivyo, Kambi ya Upinzani inataka kujua, Wizara ina mpango gani wa kuwapatia Kamandi hii boti kubwa na za kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi leo nchi yetu imeshindwa na kuwa na chelezo cha kukidhi mahitaji ya meli zetu zilizopo nchini, lakini baya zaidi hata vyombo vinavyotumiwa na vyombo vyetu vya ulinzi, havina chelezo kilichokamilika kwa matengenezo ya vyombo vyake.

Mheshimiwa Spika, mbali na kutokutumia vizuri rasilimali watu iliyopo katika kikosi hiki, pia tunakosa mapato ambayo kikosi chetu kingeingiza kwa kukarabati vyombo mbalimbali vya ulinzi na vya raia. Vyombo hivyo sasa vinakarabatiwa

Mombasa au Madagascar. Ni vyema Waziri akatueleza, kuna mpango gani wa kukifufua chelezo kilichopo au kutafuta mbia atakayekubali kuwekeza katika Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona posho wanayolipwa Wanajeshi kwa ajili ya chakula Sh.60,000/= kwa mwezi ni kidogo mno, kwani hii ni wastani wa Sh.2,000/= kwa siku. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali, kuwalipa angalau Sh.120,000/= kwa wastani wa Sh.4,000/= kwa siku; hasa ukizingatia bei ya vyakula imekuwa ikiongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na asilimia kubwa ya wapiganaji wetu kuishi uraiani, Serikali imelazimika kutafuta magari ya kuwasafirisha kwenda kwenye makambi yao. Kambi ya Upinzani inashauri Wizara, iboreshe usafiri wa askari kwa kununua magari mapya na ya kutosha. Magari mengi aina ya TATA yanayotumiwa na askari hawa, yamechoka sana. Labda ni nidhamu ya kiaskari tu inayowafanya askari wa usalama barabarani wasiyakamate magari hayo.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa watumishi wengine wa Serikali, askari wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, wanastahili kupewa nafasi ya kujiendeleza kielimu ili waweze kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Tunatambua ya kuwa, kuna sheria inayowataka askari hawa kutumikia Jeshi kwa miaka kadhaa, kabla hawajapewa kibali cha kwenda kusoma katika shule na vyuo vya uraiani. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atoe maelezo yafuatayo: -

(i) Katika kipindi cha mwaka wa masomo 2005/2006 kilichomalizika hivi karibuni ni askari wangapi kutoka katika Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa, waliomba kujiendeleza katika shule na vyuo mbalimbali?

(ii) Ni askari wangapi wa Majeshi hayo waliruhusiwa na mpaka sasa wanaendelea na masomo yao katika vyuo mbalimbali nchini?

(iii)Ni askari wangapi wanasomeshwa na Jeshi katika vyuo mbalimbali nchini na nje ya nchi katika mpango wake wa kudumu wa kuandaa wataalam wa taaluma mbalimbali zinazohitajika katika shughuli na Miradi ya Majeshi?

Mheshimiwa Spika, tunatambua kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania linapoajiri hufuata malengo kama kupata wataalam wa fani mbalimbali na wale ambao Jeshi linataka kuwaendeleza. Lakini Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuwa, uajiri wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni vyema ukaanza kwanza na askari wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa Tanzania Bara na Jeshi la Kujenga Uchumi kwa Zanzibar, kwa kuzingatia kiwango cha elimu na sifa zilizowekwa na Wizara. Tunatoa ushauri huo kutokana na ukweli kwamba, askari wa Majeshi hayo tayari wanakuwa wamejengeka katika nidhamu ya Jeshi na kwa namna nyingine, kuwafanyia upendeleo fulani kwa kujitolea kwao kulitumikia Taifa.

Mheshimiwa Spika, Rais wetu na Amiri Jeshi Mkuu, wakati alipolihutubia Bunge lako Tukufu, alizungumzia sana suala la kujenga na kuimarisha Utaifa wetu. Vyombo vya Ulinzi,Vyuo na Mashule,vimesaidia sana katika kutekeleza Sera hii.

Mheshimiwa Spika, katika msingi ule ule wa kutekeleza Sera ya Utaifa, Jeshi limekuwa likigawa nafasi za ajira kimkoa.

Mheshimiwa Spika, katika zoezi hilo, kumekuwa na malalamiko katika taratibu za kuwapata vijana kutokana na baadhi ya Viongozi wa Mikoa, kushindwa kutekeleza utaratibu huu kwa uadilifu hivyo, nafasi za sehemu moja zinaweza kwa makusudi kuchukuliwa sehemu nyingine. Kwa mfano, inawezekana nafasi za Mjini Magharibi Unguja au Shinyanga, zisiwafikie walengwa na hatimaye kuchukuliwa na vijana toka Mikoa mingine. Hivyo, ni vyema sasa wakati umefika Wizara iandae mkakati kwa nafasi hizo ili kupata Jeshi linalowakilisha sehemu zote za nchi, ili sera yetu ya kujenga Utaifa iwe endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, lina jukumu la kulinda mipaka. Tunapenda kulipongeza Jeshi letu katika ulinzi wa mipaka yetu. Tunaomba Vyombo vya Ulinzi vishirikiane ili kutatua hata matatizo madogo madogo kama yale ya wavuvi na kadhalika ili kuhakikisha mipaka yetu inazidi kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, sare zinazofanana na zile za Jeshi la Wananchi wa Tanzania, zimekuwa zikionekana mara kadhaa zikiwa zinaingia nchini kama ni miongoni mwa mitumba, ambapo taswira inaonesha sare nyingi za Wanajeshi duniani zinalingana. Hivyo tunajiuliza, kwa kuwa Serikali inalifahamu suala hilo, kama Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa alivyotuonesha Wanakamati wa Wizara hii mwezi Machi, 2006 hivyo, tunaomba ufafanuzi juu ya yafuatayo: -

(i) Ni kiasi gani cha sare hizo ziko mikononi mwa wananchi wasio waaminifu?

(ii) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kutoingizwa tena kwa sare hizo isivyo halali?

(iii) Serikali ina mpango gani wa kuzikusanya sare zote zilizo mikononi mwa raia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa zisizo rasmi kwamba, baadhi ya askari wetu wanaostaafu, wanaajiriwa nchi za jirani kama wataalam kama kule Uganda na Kenya na *DRC*. Je, kuna ukweli wa jambo hilo na kama ni kweli, Serikali imetumia kigezo gani?

Mheshimiwa Spika, taratibu za kustaafu kama watumishi kwa askari wetu wataalam, haziwezi kuepukika, lakini ninaishauri Serikali iangalie namna ya kuwaongezea muda wataalam, kwa mkataba maalum, baada ya kupata stahili zao zote ili waendelee kutoa taaluma, kurithisha vijana walio chini yao, ambapo bado vijana hao hawajapata ujuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Sheria inawataka askari wa Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa, kulitumikia Jeshi miaka sita tangu kuajiriwa kwao kabla ya kuoa au kuolewa. Sheria hii imekuwa kero zaidi kwa askari wa kike. Sheria hii pia imekuwa ikiwakatisha tama, baadhi ya vijana na wataalam wanaokuwa na moyo wa kujiunga na Majeshi hayo.

Kambi ya Upinzani inashauri muda huo upunguzwe katika kiwango ambacho hakitaathiri taratibu za Jeshi, lakini kuwapa nafuu askari hao ili walitumikie Jeshi pasipo kinyongo, sambamba na mapambano ya vita dhidi ya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa kwa nia njema kabisa na hadi leo nia hiyo inaendelezwa katika kuwapatia vijana wetu mafunzo ya ukakamavu na Kijeshi, kulinda Taifa na kupata stadi za ufundi mbalimbali mfano ujenzi, ufugaji, kilimo na kadhalika. Hivyo, tunaishauri Wizara ilifanye Jeshi hilo kuwa la kisasa zaidi kwa kulipatia nyenzo zinazostahili kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la Serikali ni kuifanya JKT iwe ni Taasisi ya Uzalishaji Mali inayojitegemea yenyewe na hivyo kupunguza mzigo wa uendeshaji, Kambi ya Upinzani inataka kujua SUMA JKT, imepata faida ya kiasi gani cha fedha na je, Shirika hilo limepanga utaratibu gani endelevu kwa manufaa ya Watanzania?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka kujua Kiwanda cha Kutengeneza Dawa za Binadamu cha *TANZANSINO* kinachoendeshwa kwa ubia kati ya SUMA JKT na Kampuni ya Shanxi ya China, kimeweza kuingiza fedha kiasi gani tangu kiwanda hicho kianze uzalishaji?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali, kupitia na kuangalia namna kiwanda cha *TANZANSINO* kinatengeneza dawa za aina mbalimbali kukidhi haja ya askari na hata raia.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imeona kwamba, si busara kuwa na idadi kubwa ya vijana waliomaliza mafunzo ya JKT na kubakia mitaani bila ajira kwa kipindi kirefu. Hii inawezekana wakajiingiza katika vitendo vya uhalifu kama ujambazi, kwani tayari wamekuwa na ujuzi wa kutumia silaha.

Mheshimiwa Spika, hivyo Kambi ya Upinzani inataka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuwaajiri vijana waliomaliza mafunzo tangu mwaka 2004 na hadi leo hawajaajiriwa, sambamba na agizo la Mheshimiwa Rais la kuwapatia ajira vijana wapatao 1,000,000.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni Jeshi la Watanzania na Kikatiba askari hawatakiwi kujihusisha na siasa au kufanya kazi zao kwa maslahi ya Chama fulani cha Siasa. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaona si busara kutawanya idadi kubwa ya askari wakati wa uchaguzi, huku raia wakijiuliza masuala kadhaa juu ya haki, sheria na utawala wa kidemokrasia katika mwamvuli wa Mfumo wa Vyama Vingi.

Wananchi wamekuwa na hofu katika kipindi hicho tete, ambacho demokrasia inataka kuchukua mkondo wake kwa njia ya uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa michezo mbalimbali Jeshini imekuwa ikichezwa, hivyo hatua ya Timu ya *Trans Camp* ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na JKT Ruvu, kufikia hatua ya kushiriki ligi kuu ya *Vodacom* ni dalili nzuri ya jinsi michezo inavyoendelezwa Jeshini, lakini inaonekana timu hizi bado hazijafanya vizuri. Hivyo, Kambi ya Upinzani, inaishauri Wizara husika kuanzia sasa, kuandaa mikakati ya ziada na kuhakikisha timu hizo hazipotezi hata mchezo mmoja katika mechi zilizosalia. Tunazitakia kila la kheri timu za *Trans Camp* na JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu mkubwa, kwa kuwa ulinzi hauanikwi kama karanga au mpunga, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Naibu wake, watafute namna ya kukutana na mimi mwenzao Waziri Kivuli, kwa manufaa ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, sasa mtaanza kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Orodha yangu iliyoko hapa kuna Waheshimiwa Wabunge 21 wameomba wachangie hoja hii. Ni dhahiri haiwezekani kuwapa nafasi wote hao. Kwa hiyo, nimetumia vigezo vyetu vya kawaida vya kuzingatia kwamba, nchi yetu ina pande mbili, Zanzibar na Bara, pia kuona hata huku Bara, maeneo mbalimbali yaweze kuwakilishwa na tunaongozwa na kanuni kwamba, wale ambao hawajasema wanapewa kipaumbele.

Baada ya kufanya hesabu zote hizo, wasemaji ambao inawezekana watapata nafasi ni wafuatao: Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mbunge wa Mtera, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mbunge wa Mpendae, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mbunge Viti Maalum, Mheshimiwa Ali Juma Ali, Mbunge wa Chaani, Mheshimiwa Abdallah Salim Sumry, Mbunge wa Mpanda Magharibi, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni na inawezekana tukamfikia Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, kwa saa za jioni, lakini nitaangalia hali inavyokwenda.

Sasa naomba namwita Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mbunge wa Mtera. Wakati huo huo wajiandae Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani na atakayefuatia baada ya hapo ni Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mbunge wa Mpendae.

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza, nikushukuru sana kwa heshima kubwa uliyonipa ya kunifanya kuwa msemaji wa kwanza

katika hoja hii. Napenda kuanza kwa kusema, ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuwasihi Wabunge wenzangu kuona kazi nzuri ambayo Jeshi letu inafanya na ripoti ya Waziri ambayo ameitoa kwa ufasaha, nawasihi wote tuipitishe bajeti ya Jeshi letu la Ulinzi na Kujenga Taifa, kwa sauti moja. Kwa kawaida huwa tunaanza kwa kupongeza Viongozi wa Ngazi za Juu. Mimi kazi hiyo nilikwishaifanya wakati nilipochangia kwenye hoja ya Waziri Mkuu, kwa hiyo, haitakuwa vizuri kuirudia tena. Lakini narudia tu kusema kwamba, ninakushukuru sana na kukupongeza wewe Spika wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda niende moja kwa moja kwenye suala la Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya na Mheshimiwa Omari Yussuf Mzee, kwa kazi kubwa na ya maana kwa nchi yetu, ambayo wamepewa na jinsi wanavyoiendesha. Mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, kwa kweli nataka niseme ninakubaliana na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati hiyo, kwa sababu nilikuwa mmojawapo. Nataka niwahakikishie Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwamba, tutawapa kila ushirikiano katika jambo hili. Pamoja na kuwapongeza, nataka niwahakikishie kwamba, kazi yao ni nzuri na tunaomba waendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza wapiganaji, nikianza na Mkuu wa Majeshi, Jenerali George Waitara na Mnadhimu Mkuu wa Majeshi, Luteni Jenerali Davis Mwamnyange. Kwa kweli ninataka niwapongeze sana, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa sisi Wanakamati, ambao tumeiangalia kazi yao kwa karibu zaidi na mara nyingine kwa undani zaidi na mara nyingine hata kwa mazungumzo na baadhi ya hawa viongozi, tunataka tuwahakikishie wenzetu kwamba, wanaifanya kazi hii safi sana na tunaomba wazidi kuendelea na mwenendo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Shimbo. Pia, nawapongeza Makamanda wote, Maafisa wote, wapiganaji wote na raia wote, ambao wanafanya kazi katika Jeshi letu, kwao ni pongezi na kuwatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye uchangiaji, napenda kuanza kuchangia katika Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda niseme kwamba, Jeshi la Kujenga Taifa kwa miaka mingi limefanya kazi nzuri. Ni kweli kulikuwa na wakati kidogo, mambo hayakwenda vizuri, kwa sababu walikuwa hawapati fedha za kutosha, lakini Jeshi la Kujenga Taifa ni chombo kimojawapo, ambacho kimeiwezesha Tanzania na kimetuwezesha Watanzania kuwa kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe wito kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; hivi kweli bado kuna umuhimu tena wa kuwa na JKT na JKU? Mimi napendekeza kwamba, wakati umefika kwa nchi yetu kuwa na Jeshi la Vijana moja tu na liwe ni JKT. Kwanza, JKT itasaidia kuwaweka vijana wetu pamoja, itawasaidia vijana wetu kuweza

kuijua Tanzania kwa upana kama ilivyo na itaweza kusaidia katika kuwaunganisha vijana wetu kupitia Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nimeona mifano hapa, mara nyingi sana vijana wanapokutana watakuambia, sisi tulikuwa pamoja Ruvu, tulikuwa pamoja Oljoro na kadhalika. Sasa napenda siku moja nikute vijana wanasema walikuwa kwenye Kambi ya JKT Visiwani au Pemba au Zanzibar penyewe. Kwa hiyo, hilo napenda nilitoe kama pendekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine ambalo napenda nilitoe ni kuwa, tungeiomba Serikali kwamba, JKT waendelee kupewa fedha nyingi zaidi ili waweze kupeleka vijana wengi, kwa sababu huko ndiko vijana wetu wanaweza kujifunza mambo mbalimbali na hata mambo ya kuwawezesha hawa vijana wakirudi kuweza kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulichangia ni suala la ulinzi wa mipaka yetu. Katika ulinzi wa mipaka yetu, napenda kusisitiza hasa kwenye mipaka ya bahari na maziwa yetu, kwa mfano, kwenye upande wa Bahari ya Hindi. Ni kweli kabisa, tunahitaji kuimarisha ulinzi kule kwa sababu hivi sasa mali yetu nyingi sana inaporwa na watu wa nje, kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kuilinda vizuri. Hali kadhalika kwenye maziwa na hasa Ziwa Tanganyika. Kwa kweli huku napenda ulinzi uimarishwe. Ulinzi uimarishwe kwa sababu wenzetu kule Serikali yao haina nguvu ya kutosha kuweza kuangalia mahali pote. Kwa hiyo, tunapata majangili tu ya kutoka Congo, wanakuja upande wa Tanzania wanapora watu wetu halafu wanarudi makwao na mara nyingi wanakuwa na vyombo vya baharini vilivyo bora kuliko vya kwetu. Napenda nipendekeze kwamba, Serikali iangalie umuhimu wa kuwapa Wanajeshi wetu vyombo imara vya kuweza kuangalia ulinzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye upande wa Hospitali za Majeshi. Naomba Serikali iangalie kwa makini sana Hospitali zetu za Majeshi, ingawa zinaitwa Hospitali za Majeshi, lakini utakuta asilimia 75 au 80 ya watu wanaohudumiwa katika hospitali hizo, wanakuwa ni raia wa kawaida. Kwa mfano, pale Dar es Salaam, Nachingwea na Mbeya. Ukienda katika Hospitali za Jeshi utakuta watu wengi wanaohudumiwa katika hospitali hizo ni raia wa kawaida. Sasa, naomba hospitali hizi zipewe nyenzo safi na zipewe dawa za kutosha, kwa sababu zinahudumia raia zaidi kuliko Wanajeshi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka niende kwenye upande wa kuwaenzi mashujaa wetu. Ni kweli kwamba, huko Mtwara tunayo sehemu ambayo tunawaenzi mashujaa wetu waliotoka Msumbiji. Lakini nina hakika kwamba, Tanzania imeweza katika suala zima la kusaidia ukombozi wa vijana wetu mashujaa ambao wamefia Zimbabwe, wako vijana wetu ambao wamefia Namibia na hata *South Africa.* Mimi nafikiri kwamba, wakati umefika wa kuweza kuwaenzi vijana hawa kwa kuwatengenezea mahali kama vile tulivyowatengenezea wenzetu waliofia Msumbiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kengele ya pili isinikute bado sijamalizia, napenda kuchukua nafasi hii, kwanza kuwashukuru wanajeshi wetu ni kweli wanafanya kazi katika hali ngumu sana. Lakini pia nataka nimshukuru Amiri Jeshi Mkuu, ambaye ni Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi alivyolipa kipaumbele suala la uboreshaji wa hali za wanajeshi wetu. Hata mkiangalia katika mishahara mtaona kwamba, ilitangazwa mishahara ya wanajeshi wetu imeongezwa kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko mishahara ya watumishi wengine wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka kumalizia kwa kuunga mkono na kusisitiza tena suala la nyumba za wanajeshi. Ni kweli kabisa vyombo vyetu vya fedha kama vile *NSSF, LAPF, PPF,* nadhani wakiwa pamoja, wanaweza wakasaidia sana katika ujenzi wa nyumba za wapiganaji wetu. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeongeza nidhamu kwa sababu askari anayeishi mtaani, hakika nidhamu yake kwa vyovyote vile, lazima itaporomoko tu na mara nyingine atajikuta katika shida ambazo angelikuwa kwenye makambi, hangeweza kupata shida za namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka tena nimpongeze Waziri kwa hotuba yake safi na ya kina na kuwaomba tena Wabunge wote, kwa sauti moja tuunge mkono hoja ya Wizara ya Jeshi la Ulinzi na JKT ili vijana wetu wakaendelee na kazi yao ya kulinda nchi yetu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea, nataka kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, kuhusu kanuni. Si kwamba kuna lolote limetokea hapa, isipokuwa tunakumbushana tu kwa hao wanaofuata, kanuni ya 49 (10) hizi ndiyo zinatawala mjadala. Inasema hivi: " Kila Mbunge atalisemea lile jambo ambalo liko katika mjadala tu na hata rudiarudia maneno yake au yale yaliyokwisha kusemwa na Wabunge wengine." Nasema hivyo ili tusaidiane kuokoa muda, tupate wachangiaji wengi zaidi. Kama jambo limesemwasemwa wewe unaunga mkono, ukirudia tena haisaidii na ni kinyume cha kanuni.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru asubuhi hii kwa kunipa nafasi hii. Lakini kwanza, nataka nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia mimi pamoja na wote, kuamka katika hali ya uzima na afya na tukaweza kushiriki katika shughuli za Bunge asubuhi hii. Baada ya shukrani hizo, pia nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Ziwani kwa mara ya pili, kwa kuniamini na chama kwa ujumla, kunirejesha kugombea na kushinda kwa asilimia kubwa. *(Makofi)*

Baada ya shukrani hizo, sasa najielekeza kwa yale ambayo nakusudia kuchangia katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kwa kusema kwamba, kwa kweli kazi ya jeshi ni ngumu mno na vijana wetu ambao wamekubali kuingia katika kazi hii ni wa kupongezwa. Ni kazi ambayo unaweka maisha yako mikononi mwa hatari. Sasa mpaka mtu kukubali kujiunga katika katika jeshi, kwa kweli ni wa kupongezwa. Ni vyema Serikali ikaona umuhimu huo na ikawaenzi wanajeshi. Hasa nakusudia kuwaenzi baada ya kumaliza kutumikia katika jeshi, askari wengi sana wanapomaliza au wanapostaafu,

maisha yao yanakuwa dhalili mno. Huwezi ukaamini kwamba, huyu ni mwanajeshi, katumikia katika jeshi kwa miaka 20, 30 au zaidi. Maisha yake yanakuwa ni dhalili. Hata huo utaratibu wenyewe wa kupata pensheni anapomaliza, inakuwa na usumbufu mno. Wengine imefika wakati wameondoka duniani, lakini bado hata hiyo pensheni hajaipatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hili nitoe mfano mmoja tu, katika jimbo langu kuna mpiga kura wangu alikuwa mwanajeshi, katumikia katika jeshi akafika muda wa kustaafu kutokana na maradhi (ugonjwa) akastaafu na kwa mujibu wa taarifa nilizopewa na Wizara, akalipwa hicho ambacho kalipwa. Ingawa kimekuwa ni kidogo mno, lakini kwa kweli baada ya kustaafu, kutokana na maradhi yale akaendelea nayo. Kaendelea na maradhi yale mpaka aka-*paralize,* ikawa sasa yeye hana mkono, hana mguu na yuko kitandani. Suala hili nikalileta hapa wakati huo Waziri alikuwa, Mheshimiwa Prof. Phillemon M. Sarungi, nikamweleza kumlalamikia hali ile nashukuru kwamba, alinisikiliza na nilichomwomba kwanza jeshi limkumbuke kwa kumpatia angalau matibabu. Nashukuru Waziri, alichukua juhudi kijana yule alichukuliwa na akapelekwa hospitali kwa matibabu. Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya familia yake, nachukua nafasi hii kulishukuru jeshi kwa kuchukua hatua angalau kwanza ya kumpatia matibabu. *(Makofi)*

Lakini kwa kuwa ambacho alikuwa amepewa kilikuwa ni kidogo mno, hakimsaidii. Maisha yake ni dhalili, askari huyu kapata matibabu lakini bado mpaka leo hali yake kwa kweli hanyanyuki ni hapo hapo. Mbaya zaidi muda wote kashindwa kujenga hata kibanda cha makuti, amekuwa akipangisha hapa na pale. Pamoja na kulipwa, nilikuwa naomba sana kwa kuthamini mchango wake, Serikali ingechukua huruma maalum kwa kiwete huyu, nasema ni kiwete mumfikirie. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, utakapofanya ziara ya Pemba uje umwone wewe mwenye, pamoja na hiyo familia yake na hapo alipoazimwa kukaa, wewe mwenyewe utaingia moyo wa huruma wa kumsaidia huyo kijana. Hilo nilitaka niseme na natoa changamoto kwamba, si huyu tu wa mfano huu, nasema hivi kwa wanajeshi wengine wote angalau Serikali kuanzia sasa ifikirie kuwapangia fungu maalum wanapostaafu ili angalau waweze kumudu maisha yao baada ya kustaafu. Hilo Mheshimiwa Waziri ni la kwanza. *(Makofi)*

La pili, nataka nichukue nafasi hii niwapongeze wanajeshi wa kikosi cha *Alhamisi Camp*. Hawa nawapongeza kwa kiasi kikubwa, walitusaidia kuweka hali sawa katika tukio lile katika uchaguzi uliopita. Baada ya kuona kwamba, hali imekuwa ni mbaya mno pale watu wamehama kabisa mji, tuliwaomba wanajeshi tunashukuru waliingilia kati. Ilikuwa ni siku ya sikukuu lakini waliweza kuvunja shughuli zao, pamoja na mimi mwenyewe, tukaweza kutanga nao katika mji mzima na katika vitongoji vya Piki kuomba watu warudi katika maeneo yao na kwamba hali ya pale sasa ni shwari. Baada ya kuondolewa vijana pale wa KMKM na JKU, jeshi walikubali tukaondoka pale na magari karibu manne au matano ya jeshi, tukatembea katika Kata zote za kijiji kile mchana mkutwa, nashukuru sana hali ikawa shwari. Kwa namna ya pekee, nataka nimshukuru kiongozi anayeongoza *operation* ile, Luteni Kanali Lingoe, sijui kama bado yupo Pemba au amekwisha hamishwa, lakini kwa kweli namshukuru sana kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Piki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu sisi Wabunge ni wawakilishi wa wananchi, ni vyema sana unajua sheria za jeshi zimekuwa ni ngumu mno kueleweka kwa wananchi wa kawaida. Kwanza, nilikuwa naomba jeshi jaribuni kutufanyia semina Wabunge, tuweze kufahamu taratibu na sheria za kujiunga na jeshi ili sisi tuweze kupata nafasi ya kuzungumza na wapiga kura wetu. Kule unakojiunga na jeshi lakini kuna moja, mbili, tatu, nne. Kwa mfano, sheria ya jeshi inasema kama unataka kujiunga ufahamu kwamba, unatakiwa usioe wala usiolewe kwa muda wa miaka mitano, ukae katika kambi. Sasa kwa kweli miaka mitano huoi wala huolewi, hapa Wabunge tunakaa miezi miwili tu na kama si mtu ambaye wa karibu ya Mungu kama Ali Said, huwezi kupona. Kwa nadra upate mtu ambaye yuko chini karibu na Mungu kama mimi ndio kwa kweli utasalimika hapa, vinginevyo lazima utaadhirika. *(Makofi/Kicheko)*

Miaka mitano au sita na kijana *self status* kwa hiyo, nafikiri hii sheria mngeitazama kwamba, mbona umekuwa ni muda mrefu mno na hasa *logic* yake nini kwamba askari akioa au akiolewa kitapungua kitu gani? Kwa nini wasiruhusiwe wakaoa, kwa sababu wakishaoa wakiwa na wake zao, wanakuwa kambini hawazunguki, hata udhibiti wa magonjwa unakuwa rahisi. Lakini unawaambia wasioe, wasiolewe, ina maana unawaambia kwamba, sasa msioe wala msiolewe, lakini namna nyingine ya kufanya mtajua wenyewe. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri hii sheria ni ngumu mno, kama ingekuwa mimi hata siku moja nisingekuwa mwanajeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nataka nizungumzie suala la JKT na JKU, kidogo kalisema Mheshimiwa John S. Malecela. Mimi naungana naye moja kwa moja kwamba, hakuna ulazima wote, Jeshi la Wananchi ni moja, hatuoni sababu kwa nini kuwe na JKT na JKU. Kwa hiyo, napendekeza moja kwa moja kwamba, JKU kule Zanzibar ifutwe na badala yake kuwe na JKT, ilimradi sasa vikosi vya JKU badals ya kufanya kazi za JKU kule wanakuwa wao wanafanyakazi za kisiasa zaidi, wanatumika katika shughuli za kisiasa wakati wa uchaguzi, sioni kama kuna shughuli nyingine. *(Makofi)*

Halafu kuna kikosi kinaitwa Kikosi cha Varantia, hiki nacho ni kikosi cha jeshi. Sasa nauliza kuna Majeshi mawili Tanzania? Hivi nilikuwa najiuliza sasa Kikosi cha Varantia kule Zanzibar ni cha nini, hakina shughuli yoyote zaidi wao ni kubugudhi watu hasa wakati wa uchaguzi. Kwa hiyo, kikosi cha Varantia na Kikosi cha JKU, napendekeza vifutwe mara moja na badala yake kuwe na JKT, ambayo inaanza Bara hadi Visiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumze ni suala la kuajiri katika jeshi. Jeshi kama tulivyosema ni letu sote Tanzania nzima, kwa hiyo, ni vyema mkazingatia kwamba, kuna pande mbili za Muungano, zikatengwa nafasi maalum kwamba hizi ni nafasi za Zanzibar, hizi ni nafasi za Bara. Lakini nakumbuka wakati fulani, Waziri aliulizwa suala hili akasema kwamba, tukifanya hivyo, tutakuwa tumeligawa jeshi. Hatuligawi, lakini tunafanya uwiano mzuri. Ni vyema ikajulikana kwamba, Mkoa wa Kusini Pemba nafasi zenu za jeshi ni hizi hapa, Mkoa wa Kaskazini Pemba ni hizi hapa, Kusini Unguja hizi hapa, Mbeya hizi hapa na kadhalika. Siyo kwamba, tunafanya hivyo kwa ubaguzi, lakini tunafanya hivyo ili sote tuweze kushiriki kutoka sehemu mbalimbali za nchi, jeshi lisiwe linatoka sehemu ya moja ya nchi. Hiyo, ndiyo dhamira yetu, naomba mtuelewe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la makazi ya wanajeshi. Nadhani sina hakika, lakini sheria inasema wanajeshi wanatakiwa wawepo kambini, sasa wanajeshi wengi wanaishi uraiani hii, ni kutokana na upungufu wa nyumba. Sasa wanapoishi uraiani, kwa vyovyote itakavyokuwa, basi maadili yataporomoka. Kwenye bajeti naona hela si kidogo, shillingi bilioni 280 na zaidi, Serikali nzima ya Unguja hawana bajeti hiyo, mmepewa nyie jeshi kwa nini msimege sehemu kubwa mkakahikisha kwamba, mnajenga nyumba za kutosha ili wanajeshi waweze kubaki kambini wakati wote, mdhibiti na hali ya dharura ikitokea, inakuwa ni rahisi wanajeshi kuweza kupatikana? Lakini kama tunawaacha uraiani, wataishi na raia wa kawaida, ndio mara kwa mara unasikia migongano imetokea baina ya wanajeshi na raia wamepigana, wamefanya hivi yote ni kutokana na kuwa wanajeshi tumeshindwa kuwadhibiti katika makambi. Ni vyema Serikali ya Awamu ya Nne, ikafanya jitihada za kutosha kuhakikisha kwamba, mnawapatia wanajeshi hawa makazi bora katika maeneo yao ili kuweza kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwa jinsi unavyojitahidi kuliendesha Bunge hili katika mfumo huu wa vyama vingi. Hongera sana na nadhani kwa utaratibu huu, utakuwa Spika wa maisha. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nashukuru kwa salamu hizo, lakini si vizuri kuwa Spika wa maisha, itakuwa si mfano mzuri. Ahsante.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kwa mara ya kwanza, kuweza kuchangia hoja iliyo mbele ya Bunge hili Tukufu. Vile vile napenda kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, vile vile nampongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Alhaji Amani Abeid Karume. Pia nampongeza Waziri Mkuu, kwa kuteuliwa na Rais na kukubalika katika Bunge hili kwa kura za kishindo. Pia sitakusahau wewe Spika, pamoja na Naibu Spika, unakwenda na viwango katika Bunge hili Tukufu, pamoja na Wenyeviti wako wawili wanaoliongoza Bunge hili. Vile vile sitawasahau wapiga kura wangu wa Jimbo la Mpendae, kwa kunipa nafasi hii leo kuzungumza katika Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nitazungumzia mambo yafuatayo; nitazungumza hasa kuhusu huduma ya askari, nitasema kwa uchungu utanivumilia. Wanajeshi ndiyo wanaotusababisha kulala na kutulia katika maisha yetu, tunahitaji kuwapatia huduma bora na malazi bora. Jeshi lilipoweka utaratibu wa kuweka *canteen* ni jambo la busara kwa sababu limepunguza matumizi ya fedha za nchi yetu, za walipa kodi wetu. *(Makofi)*

Lakini wakati taratibu hizi zinawekwa, hawakuangalia yule mtoa huduma ambaye ni mzalendo wa nchi hii. Wazabuni wanapata tabu katika kulipa huduma bora jeshi, kwa sababu kiwango walichopewa wanajeshi ni kidogo kuweza kulisha makambini. Ipo haja

kuweza kuangalia upya na kuangalia kule Zanzibar gharama za vitu zinavyopanda kila siku. Mimi naweza kuwatajia *scale* ya chakula cha askari anachotakiwa kula. Anatakiwa ale gramu 240 za nyama, Zanzibar kilo moja shilingi 3,500/=, unamlipa shilingi 2,000/= ili alishwe; je, kuna kitu gani? *(Makofi)*

Hakuweza kuangalia kwamba zamani walikuwa wakinununa kuni, wanajeshi wenyewe walikuwa wanajipikia, wanajeshi wenyewe walikuwa wanajihudumia, leo mzabuni anatakiwa anunue vyombo vya kuwahudumia askari na aajiri wafanyakazi wa kuweza kuwahudumia wanajeshi wale. Ni jambo zuri kabisa na wamestarehe buheri kabisa, lakini hawakumwangalia mzabuni; nyama kilo moja inam-*cost* askari mmoja shilingi 900/= kwa gramu 250 kwa kule Zanzibar, hapa Dodoma nyama kilo moja shilingi 1,500/=. Nyanya kule tunaita tungule, shilingi 1,000/= kwa kilo, leo hapa ndoo ya lita 20 ni shilingi 2,000/=. Wakae waangalie askari anatakiwa kutunzwa, kwa sababu ndiye anayetusababisha sisi tuwe huru. Mimi nalipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Afrika nzima hakuna jeshi lenye *discipline* kama la Tanzania. Hii ni uhakika kabisa, jeshi lina haja ya kutunzwa, huduma yake si chini ya shilingi 4,500/=, askari alipwe kwa ajili ya *ration* na yule mtoa huduma apate kukidhi matakwa ya kutoa huduma jeshini. *(Makofi)*

La pili, niliwahi kumwuliza Waziri anieleze kuhusu waliopewa kazi ya kutoa huduma kwenye maduka ya jeshini, hawa wanajitajirisha kwenye migongo ya askari wetu. awa ni watu ambao wanapewa msamaha wa ushuru na vitu vyao vikawa bei juu na leo mwanajeshi anafika *stage* ya kuacha jeshi, hana kibanda cha mgongo, ni aibu. *(Makofi)*

Leo tunasema tunawawekea maduka jeshini ili kuweza kupunguza makali ya maisha, tunawazidishia makali ya maisha; kwa nini? Mwanajeshi shamba lake ni jeshini, hana shamba hana, kikataa chake kiko kambini; kwa nini tuwaweke katika hali ya unyonge ndugu zetu?

Nasema haya najua si kwa kubahatisha, najua kamanda wa juu na huyu askari wa chini, kuanzia *private* mpaka *sergeant major* au *office number one* bwana *RSM,* hawa ni watu wenye dhiki jeshini. Wakisema hawa wanaambiwa ni wafitini wakubwa, Waziri nakuomba kupitia Bunge letu Tukufu, ufanye ziara uwe unazungumza kuanzia na askari mpaka bwana *RSM.* Makamanda kwanza waweke mbali, ukishapata taarifa za askari, nenda kazungumze na makamanda, utajua mbivu na mbichi. Hili nakuomba kupitia Bunge lako, uliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni nyumba wanazoishi askari na hasa Zanzibar. Mheshimiwa Waziri, nakuomba utembelee kuanzia Kambi ya Dunga, Makao Makuu ambako ni jimboni kwangu, Brigedi ya Nyuki, nyumba alizozijenga Marehemu Kanali Mussa Maisala hazijafanyiwa *repair*, pazia ni kanga, ni aibu. Karo hazikamatiki, utafiri kwamba, hawaishi wanajeshi. Tunaomba wazidishiwe ili wapate kutengezewa, kuna wanajeshi wazuri pale kwa sababu wa kila fani wapo. Mafundi wapo, ukija kwenye kikosi kinaitwa *field engineer,* hatari nacho mkiongezee zana. Palibomoka maghorofa

matatu, kamanda alitoa *time* Waziri Mkuu alipokwenda walishafagia kila kitu. Ni wajibu kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la Kambi ya Chukwani, hata vyoo haina, umeme hakuna, wala maji hamna. Mzabuni anayetakiwa kutoa huduma pale, inabidi atoe fedha yake mfukoni akateke maji, si aibu kambi ya jeshi kuwa haina maji wala umeme? Waziri nakuomba hiyo kambi, mimi nimefanyia depo hapo, nakuomba tena sana, ingawa Naibu Waziri ni jimbo lake, lakini nasema kwa uchungu kwa sababu ile kambi ndiyo iliyonilea, ipatiwe umeme, maji na vyoo. Ni aibu kwani ndiyo vyoo vyao askari, si jambo la kupendeza hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ajili ya muda na mimi ni mara yangu ya kwanza, naipongeza Wizara ya Ulinzi, pamoja na Makamanda wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na askari wa chini wote, nawapongeza na Mwenyezi Mungu atawajalia wawe imara waweze kutulinda katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, inabidi nimwombe radhi hapo, tumekuwa tukimtaja Mbunge wa Chaani kwamba ni Mheshimiwa Ali Juma Ali kumbe ni Mheshimiwa Ali Juma Haji.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi wake mkubwa alioupata. Hali kadhalika kwa kuweza kuendelea kuaminiwa na wanachama wa Chama cha Mapinduzi, Wajumbe wa Mkutano Mkuu, ambao pia wameweza kumpa ushindi wa kishindo katika nafasi ya Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, pamoja na Naibu Wake Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya katika kuhakikisha kwamba wanatekeleza Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa leo nataka kuzungumzia suala la JKT. Rais wetu amethibitisha na ameonesha nia ya kuendelea kufufua makambi ya Jeshi ili kuendelea kuwa-*train* hawa vijana wetu wa JKT. *(Makofi)*

Lakini mimi nilikuwa na tatizo moja, JKT jeshi ina-*train* vijana takribani 2,000 lakini vijana ambao wanaajiriwa ni vijana 1,200 tu, hiki ni kitu ambacho nadhani Serikali haina budi kukiangalia tena upya. Vijana hawa wanafundishwa vitu vingi, wanajengwa kuwa wakakamavu, wanajengwa kuwa wazalendo, wanajengwa kuwa waaminifu na vitu vingine vingi. Lakini licha ya hivyo vijana hawa wanafundishwa mbinu za kijeshi,

ikiwemo utumiaji wa silaha. Sasa najiuliza ikiwa kama JKT nia yetu ni nzuri, kuendelea kufufua haya makambi, lakini kwa nini mafunzo haya ya utumiaji wa silaha, yanaendelea kufundishwa katika hizi kambi za JKT wakati uwezo wa jeshi kuajiri hawa vijana, haulingani na idadi ya wanaofundishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukiangalia katika idadi hii, wanaokuwa *trained* ni 2,000 wanaoajiriwa katika jeshi ni 1,200; hawa wengine 800 wanakwenda wapi? Hizi silaha wanajua kutumia, nadhani Wizara hii haina budi kuanzia hivi sasa, ku-*stop* haya matumizi, hizi *recruitment* za matumizi ya silaha. Huwezi kuwafundisha tu vitu vingine na mambo mengine, wanakuwa wakakamavu, wazalendo na vitu vingine kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili mimi nataka kuzungumzia katika suala hili, Mheshimiwa Rais wetu ameahidi kuongeza ajira za vijana kufikia milioni moja. Nadhani umefika wakati sasa, Wizara hii au JKT ikatumiwa kama chanzo cha kuweza kupata idadi ya ajira nyingine za vijana kwa namna mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo suala kwa mfano, kuna Wizara ya Usalama wa Raia, kuna Wizara ya Magereza, kuna Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo ina magereza ndani. Hizi mbili peke yake kama zikitumiwa vizuri, zinaweza kusaidia kuwachukua hawa vijana, kwa sababu mimi sioni sababu, kila siku wakati tunapitia Bajeti, ukiangalia vitabu hivi unakuta kwamba, kila Idara katika Wizara ina kifungu cha *training* kimewekewa pesa nyingi sana. Kila Wizara, yaani katika Wizara nzima, hakuna Wizara ambayo inakosa fungu la *training.*

Mheshimiwa Spika, haya mafungu ya *training* katika Magereza, mafungu ya *training* Wizara ya Usalama wa Raia, Polisi, yanaweza yakapunguzwa kwa maana ya kwamba, vijana hawa ambao tayari wameshakuwa *trained* kupitia JKT, wale ambao wanabakia ambao hawawezi kupata ajira jeshini, basi kama ikiwezekana, waweze au Usalama wa Raia waweze kuwachukua kutoka pale. La sivyo hii Wizara ya Mambo ya Ndani na Magereza, waweze pia kuwachukua vijana kati ya wale waliokuwa *trained.* Kwa sababu mafungu haya ya pesa ni mengi yanawekwa hapo, lakini mafungu haya ya pesa yanaweza yakapunguzwa katika namna ambayo vijana hawa kwa sababu tayari wameshapitia mafunzo fulani, basi kifungu chao kile kingine, kinaweza kikapunguzwa ili kuweza kutumika katika masuala mengine ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia suala la *security* na makampuni ya ulinzi, katika Wizara ya Mambo ya Ndani. Nadhani umefika wakati sasa, Wizara ya Usalama wa Raia, kuweza kuangalia na kuweka sheria madhubuti, ambayo iwalazimishe hawa watu ambao wanafungua haya makampuni ya ulinzi, moja ya sheria kubwa iwe kwamba, vijana watakaowachukua wawe ambao ikiwezekana wametokana huku JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili litaisaidia sana nchi yetu, kwa sababu nchi yetu hivi sasa binadamu tumeumbwa, wote tuko katika misingi ya kidini mbalimbali. Lakini wapo binadamu wengine ambao sasa hivi wameanza kubadilika na unaweza pia

kuwalinganisha na wanyama. Haya yameweza kutokea kutokana na matukio ya kihalifu, mabaya na ya kutisha, ambayo yamekuwa yakiendelea katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani kama JKT itaendelea kuwafundisha hawa vijana wetu, jeshi likachukua ile idadi, wakakabaki hawa wengine 800 au wakakabaki kiasi chochote, kwa sababu ninajua kwamba, kwa kadri tunavyozidi kufufua haya makambi ndivyo, idadi ya vijana ambao watakuwa hawana ajira itakuwa inazidi kuongezeka.

Kwa hiyo, Wizara ya Usalama wa Raia pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani, zishirikiane kwa dhati kabisa na kwa moyo mmoja na kuweka sheria kwamba iwe lazima kwa mfano, Wizara ya Mambo ya Ndani kwamba watu ambao wanakuwa wanafungua haya makampuni waweze kuwachukua wafanyakazi wa pale kutoka katika JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni la *Inter Connection* ya Wizara nyingine katika Wizara hii. Wizara ya Ulinzi kama alivyosema mzungumzaji aliyepita, ni Wizara ambayo ni tajiri kwa fani, ina fani za kila aina, kuna Madaktari, Walimu na *Engineers.*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi naomba hivi sasa kama ikiwezekana, hata kama najua hizo *Inter Connections* zilikuwepo, basi hizi *Inter Connections* ziboreshwe zaidi. Wizara hii ya Ulinzi inatusaidia katika masuala mbalimbali, kwa mfano, katika miundombinu, jeshi wamekuwa wakitumiwa sana kutusaidia endapo tunapata dharura. Mfano hivi karibuni kulikuwa kuna mafuriko huko maeneo ya Tanga katika Daraja la Msalata. Waziri wa Ulinzi alipoulizwa na Mheshimiwa Rais alisema kwamba, daraja litakamilika baada ya wiki mbili. Lakini wanajeshi walipopelekwa pale baada ya siku mbili, daraja watu wanapita. Mimi napendekeza kwamba, hizi Wizara nyingine ziwe ni Wizara ambazo zinajitahidi kwa kadri ya uwezo wao, kuweza kuhakikisha kwamba, zinakuwa na ushirikiano wa karibu sana na kuendelea kuitumia Wizara hii ya Ulinzi ili walau haya mambo ambayo yamekuwa yakisaidia, yaendelee kuboreshwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu katika kuangalia mkakati mzima, tunazungumzia masuala ya kuboresha uchumi, masuala ya kuinua uchumi, kumwinua Mtanzani, lakini tuangalie na *expenses* nyingine ambazo hazina ulazima. Wizara hii ikiwa kama jeshi, watakuwa wanatumiwa katika masuala ya kujenga haya madaraja na kufanya vitu kama hivyo. Wizara ya Miundombinu, walau kazi zake zitakuwa zimepungua na hizi gharama ambazo zingekuwa zipelekwe huko, zinaweza kufanya mambo mengine ya msingi. *(Makofi)*

Nikizungumzia katika hizo *Inter Connections* za Wizara, napenda pia kuzungumzia suala la huduma ya afya. Jeshi limekuwa likitoa huduma ya afya kwa kupitia hospitali zake mbalimbali, tuna mfano, Hospitali ya Lugalo. Lakini pia kutokana na mfano halisi nilioupata kwamba, wanajeshi wetu ni watu ambao wamefundishwa uzalendo, tukipata mgomo pale wanaokwenda kutuokoa mara nyingi wanakuwa wanajeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya nayo basi kama ikiwezekana katika *training* mbalimbali, iweze kuwashirikisha wanajeshi ambao wako katika hizo fani, lakini vile vile walau siku moja moja, Waziri wa Afya pale, aweze kuamua kwenda kuzitembelea hizi Wizara, akajua matatizo yaliyopo katika Idara ya Afya katika hizo hospitali ambazo ni za jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona muda wangu umekwisha. Napenda kuzungumzia pia suala la wakimbizi. Mwaka 2003 Waziri wa Mambo ya Ndani wa wakati huo, Mheshimiwa Ramadhani Omar Mapuri, alikuwa Rwanda katika kikao chake na mimi bahati nzuri nilikuwepo pale katika hicho kikao. Waziri wa pale alimwambia kwamba, Mheshimiwa Waziri, Tanzania ni nchi ambayo inajitahidi sana kwa ukarimu kwa maana ya kwamba, inaendelea kuwapokea Wakimbizi. Lakini Mheshimiwa Waziri hakuna mkimbizi ambaye unaweza ukamjua kwamba, huyu ni mhalifu au huyu ana hatari kiasi gani pale unapomwona ameweka mstari na bakuli lake kwa ajili ya kuchukulia chakula. Ni vigumu sana kuweza kumjua. Mimi nilikuwa nashauri, *Vienna Convetion* ipo, ambayo inawalinda hawa wakimbizi. Lakini Kigoma peke yake hivi sasa ina kesi 177 za mauaji, ambazo zimefanywa na wakimbizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri hili jeshi letu kama ikiwezekana, waweze kusaidiana na majeshi katika nchi mbalimbali, ambazo zina wakimbizi, kuweza walau kuwarudisha kwa sababu ingawa hii *Vienna Convetion* inawalinda, wako hapa wanaendelea kukaa, lakini tunakaa na wahalifu. Kuliko sisi tuendelee kufa humu ndani, kwa sababu ya hiyo mikataba, ikiwezekana Wizara ya Ulinzi iweze kusaidiana na Wizara za Ulinzi kutoka Congo, Burundi na Rwanda. Hata kimya kimya hawa watu muweze kuwachunguza, kuna *intelligence* katika jeshi ambao wanaweza wakajua kuwa huyu mtu hafai, huyu mtu ana makosa fulani huko alikotoka. Hawa watu ili waweze kuondoka kwa hiyo, nilikuwa naomba najua hapa nitajibiwa kwamba, *Vienna Convetion* lakini mimi nadhani utafutwe utaratibu wa kijeshi, hawa watu waweze kuondolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka kuzungumzia adhabu ambayo wamekuwa wakipata askari wanawake. Askari wanawake au JKT ambao wako katika mafunzo, wakipata mimba huwa wanafukuzwa. Mimi naiomba Wizara, sasa umefikia wakati iweze kubatilisha hii Sheria, kwa sababu hii sheria inamkandamiza mwanamke. Kwa sababu mwanamke akipewa ujauzito na mtu kutoka nje anafukuzwa. Lakini mwanaume ambaye yuko pale mafunzoni, akimpa ujauzito mwanamke ambaye yuko nje anaendelea kubaki. Hii siyo halali kabisa na ni uonevu kwa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, naomba tu kuuliza kuhusu suala la kuapa. Kiapo kinamfanya mtu awe *subjected* kwa yule ambaye anaapa. Hapa Waheshimiwa Wabunge, tunaapa tunawajibika kwa Serikali. Tunawajibika kwa Rais ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, *Chief of Staff* anaapishwa na Rais, pale ina maana kwamba, anawajibika moja kwa moja kwa Rais. Lakini *Chief of National Service* alikuja Mwamnyange hakuapa, sasa hivi ameingia Shimbo hakuapa. Naomba sasa kama ikiwezekana na huyu naye anakuwa ana mzigo mkubwa huku kwa sababu yeye yuko katika *National Service;* kwa nini na yeye asipewe mamlaka yake ili na aweze kuapa? Naomba niweze kujibiwa katika hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumalizia hapo, naunga mkono hoja lakini napenda kutoa pongezi zangu za dhati kabisa, kwa Mheshimiwa Mwamunyange kwa kuteuliwa katika hii nafasi pamoja na Fimbo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, umekuwa na mambo mengi sana mazuri tu. Wakati tunaendelea, napenda Waheshimiwa Wabunge mtambue kwamba, kwa sasa hivi Kiongozi wa Shughuli za Serikali humu ndani ya Bunge ni Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu. Nampongeza sana, si haba hata ukiwa kiongozi hapo kwa saa chache, basi kwanza inaashiria mazuri na pili kwa kuwa ni mwanamama, inasogea siku ambapo pengine tutapata Waziri Mkuu siku zijazo. *(Makofi)*

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja ya Bajeti kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa vile nimeshatoa huko nyuma pongezi zangu kwa viongozi wetu wakuu, kwa hiyo, naendelea moja kwa moja katika mchango wangu kwa Wizara hii.

Kwanza, nampongeza sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Naibu wake, Katibu wake Mkuu, Mkuu wa Jeshi la Ulinzi, Mkuu wa JKT, wapiganaji wote na watendaji wa Wizarani, kwa kazi yao nzuri waliyoifanya katika kuandaa hotuba hii ambayo mara nyingi huwa nasema, kama zitakuwa hotuba hizi zinatekelezwa kama zilivyoelezwa, basi zina mwelekeo mzuri sana wa mafanikio. Baada ya pongezi hizo, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa juhudi kubwa na Watendaji wote walioshiriki katika juhudi kubwa waliyoichukua katika ujenzi wa hospitali yetu ya Bububu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hospitali hii inatoa huduma kubwa sana kwa wanajeshi na wananchi kwa ujumla. Naweza nikasema ni hospitali ya pili, ukitoa ile ya Rufaa ya Mnazimmoja, basi hii inaweza ikachukua nafasi ya pili. *(Makofi)*

Ni hospitali ambayo ilikuwa katika hali mbaya sana. Huwezi kuamini wakati huo ukifika pale kwamba, ni jengo la hospitali ambalo linatoa huduma kubwa kwa wanajeshi na wananchi. Lakini nadhani Mheshimiwa Waziri, baada ya kulitembelea na Naibu Waziri wake na kuona hali halisi ilivyo, wameona kwamba ipo haja ya kuomba misaada kwa wenzetu hawa wa Serikali ya Ujerumani, kutusaidia kuijenga hospitali ile. Tunashukuru sana kwa hilo. Ninaomba kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, hii hospitali inaonesha itakuwa nzuri. Kwa hiyo basi, isiishie kwenye jengo. Namwomba Waziri uzuri huu utakaokuwa kwenye jengo, ufanane na huduma zake. Kwa kutuletea vifaa na madaktari wa kutosha, hapo tutakuwa tayari ile hospitali tumeikuza kwa kiwango kile ambacho kina mwelekeo wa ujenzi wake unavyokwenda sasa hivi.

Sambamba na utunzwaji huo, tunaiomba pia Wizara hii ya Ulinzi iangalie hata hospitali nyingine za kijeshi, kwa sababu kwa kweli majeshi yetu yanafanya kazi nzuri sana katika nyanja mbalimbali, hili tunalijua sote. Kwa hiyo, ziangaliwe hata na hospitali nyingine kuziombea misaada kama ziko hospitali nyingi tu za majeshi kama vile Tabora,

Kibaha na kwingineko. Nazo hizi ziombewe misaada ziweze kufanikiwa kama vile ilivyofanywa Hospitali ya Bububu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia juu ya ujenzi wa hospitali yetu ya Bububu, nije sasa kwenye Makambi ya wanajeshi wetu. Lazima tukubali kwamba, wanajeshi wetu wengi hapa wachangiaji wenzangu wamesha zungumza kwamba, wanajeshi wetu wanafanya kati kubwa na nzito katika Serikali yetu hii ya Muungano. Sote ni mashuhuda, walipogoma madaktari Muhimbili, wanajeshi walichukua nafasi kwa haraka sana, kuokoa maisha ya wananchi wetu na kazi zikaenda kama zilivyopangwa. *(Makofi)*

Sote ni mashuhuda panapotokea maharibiko ya madaraja, mvua zimeharibu madaraja, wanajeshi wetu wanachukua nafasi haraka haraka. Siku moja, mbili, daraja limeshajengwa. Wananchi wanapita na kufanya shughuli zao kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikiwa wanajeshi wetu wanafanya kazi nzito kama hizi, kwa nini na wao tusiwaweke katika hali nzuri, ya utulivu wakati ule wanaporudi katika shughuli zile nzito na za ziada? Kwa nini tusiwafanye na wao wakifika katika makazi yao wawe katika hali ya utulivu? Kwa sababu kwa kweli wanaporudi katika majengo au katika makazi yao wakakuwa katika hali mbaya sana katika majengo yao. Majeshi yetu yamekuwa na utamaduni hivi sasa wa kujenga majengo ya mabati *(full suit)*. Kwa kweli jeshi la ulinzi limezidi, hakuna kambi utakayopita usikute jengo la mabati.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, aondokane sasa na utamaduni huu, ajenge nyumba za kudumu, nzuri na za kisasa, ambazo zitawafanya wanajeshi wetu wanapokuwa katika makazi yao baada ya kurudi katika shughuli zao za kawaida, wajisikie kwamba na wao wako katika makazi mazuri na hasa wale wa vyeo vya chini kabisa.

Tumeona katika hotuba yake sehemu mbalimbali ingawa wapo askari wa kawaida, lakini majengo mengi utakuta ya Maofisa na askari wetu wanastahili kujengewa nyumba nzuri za kudumu na za kisasa.

Mheshimiwa Spika, mwenzangu aliyepita, alitoa mifano mbalimbali ya kule Zanzibar na kwa sababu hakuna haja ya kurejea tena mifano mingine, natoa kwa sehemu nyingine. Niliitembelea Kambi ya Lugalo Dar es Salaam, nilikwenda kwa shemeji yangu, nilipofika katika hiyo nyumba wanayoishi, mimi mwenyewe nilisikitika sana. Kwanza, inavyoelekea zile nyumba zilikuwa asili yake ni kwa askari ambao ni *single,* lakini kutokana na ukubwa wa jeshi letu linavyokua na hali halisi ilivyo, hivi sasa nyumba zile wanakaa askari ambao ni wana ndoa. Nyumba hiyo ni chumba kimoja, ina sebule ndogo moja, ambayo nafikiri kwa ukubwa inaweza kuchukua futi tano mpaka sita, hiyo sebule yenyewe. Papo hapo kapanga viti vyake, yaani makabati yako hapo hapo. Ukipita sisemi uongo, ni bora ule Ukumbi wetu ule wa zamani, unapita kwa raha, ukipita pale kutoka nje kulikoni ukipita nyumba hiyo kwenda chumbani, kupita hapo sebuleni kwenda chumbani, anapita askari wetu kwa tabu sana. Hilo nimelishuhudia.

Isitoshe huko chumbani, ukuta ule baina ya sebule pale na chumbani ni nusu. Nusu ukuta kwa kweli akizungumza kule chumbani, sisi tulikaa pale ndiyo wamepanga kule labda wageni tuwasaidie vinywaji gani wameingia chumbani na mke wake, ilibidi sisi tutoke nje tuwapishe kwanza wao wapange kule ndani, halafu tuingie sebuleni, ni hali mbaya. Tunaomba utamaduni huu uondoke. Hasa kwa vile Serikali imetenga fedha nyingi kidogo katika Bajeti hii, katika mambo ya ujenzi, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri aondokane na mambo hayo ya ujenzi wa nyumba za mabati.

Mheshimiwa Spika, lingine nakuja kwenye uajiri. Ni kweli sasa hivi tunataka wanajeshi wetu wawe wa kileo na wenye elimu nzuri kwa kila hali. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ni kweli tunayo haki ya kuajiri wanajeshi wenye elimu ya juu, lakini tuangalie jeshi ni kazi moja nzito ya kijeshi. Lazima tuangalie na wale vijana wetu wenye elimu ya chini. Kwa sababu kila tukimwajiri askari mwenye elimu ya juu, atakapofika pale jeshini, hachukui muda atakuwa na cheo cha juu vile vile. Sidhani kwamba, likitokezea gwaride la Sherehe kama ya Muungano au Mapinduzi kule Zanzibar, tutawachezesha askari wote wenye nyota mabegani. Sifikirii hili. Ni lazima tuajiri nyanja zote za elimu, kwa sababu kazi nyingine za nguvu hazitofanywa na Maofisa. Kwa hiyo, hili nalo naliomba tuliangalie na vijana wetu wale ambao wana elimu ya chini, wachukuliwe. Mfumo sasa hivi unaokuja, mwenye *Form Four* akifika jeshini na akimwona wa *Form Six* ni Ofisa na yeye anajiendeleza. Kwa hiyo na hawa wazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakuja kwenye upandishaji wa vyeo. Kwa kweli sijui huku Mheshimiwa Waziri atakuja kutueleza nini, huku jeshini kuna tatizo gani, askari wa chini au maofisa wanafika kukaa na cheo kimoja kwa miaka 10, 15 mpaka 20. Kuna nini huku jeshini? Kama askari yule hana nidhamu, kwa nini asiitwe akaelezwa baadaye akionekana anaendelea na utovu wa nidhamu, aachishwe jeshi. Lakini haiwezekani kukaa miaka 15 mpaka 20 na cheo kimoja. Katika hotuba yake, amezungumzia utawala bora, lakini hatujaona upandishwaji wa vyeo katika Wizara yake Mheshimiwa Waziri. Nadhani utawala bora hauwajibiki kwa askari tu kuwajibika kwenye kazi, lakini na Wizara nayo iwajibike kwa askari. Moja kati ya hayo ni kuwapandisha vyeo askari wetu. Hapo tutakuwa utawala bora tunakwenda nao vizuri. Alizungumzia mpaka kupata sare, imezungumzwa kwamba watapata kwa stahili zinazostahiki. Lakini vyeo hatujaona humu. Nafikiri katika kanuni zao kuna utaratibu. Naomba Mheshimiwa Waziri aje atuambie, ni utaratibu gani unatumika kuwapandisha vyeo askari, kama askari kwa kawaida anachukua muda gani kupata cheo na muda gani ofisa akae, cheo cha luteni mpaka muda gani na unatendeka kweli katika jeshi letu hili la wananchi?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nimeshaanza kujifunza na kengele ya mwanzo ilinililia, kwa hiyo na mimi naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH S. SUMRY:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi mchana huu wa leo na mimi niweze kuungana na wenzangu, kwa kuunga

mkono hoja ya Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi napenda niwapongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee, Katibu Mkuu, Bwana Abel Mwaisumo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali George Waitara, Mnadhimu Mkuu mpya wa Jeshi, Luteni Mwamnyange, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Abdulrahman Shimbo, Makamanda na Maofisa wote wa Jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Nne, ambayo imesikiliza kilio chetu kwa muda wa miaka miwili huko nyuma, cha kuomba Wizara hii aongezwe Naibu Waziri ili iweze kuwa na ufanisi mkubwa zaidi. Leo hii tumempata Naibu Waziri na tunaona mambo yetu yatakwenda vizuri kama ilivyo ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Kadhalika ndani ya Bunge hili kwako Mheshimiwa Spika, ndani ya *Standard and Speed. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi yangu ni machache tu, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa ziara yake aliyoifanya kwetu Mkoa wa Rukwa, kukagua mipaka yetu kule Rukwa katika eneo la Kasanga, Jimbo la Kalambo, mnamo tarehe 23 Mei, 2006 hadi tarehe 25 Mei, 2006. Katika maeneo ya Kasanga, Jimbo la Kalambo, Kirando Jimbo la Nkansi na kule kwangu Ikola, Tarafa ya Karema, Jimbo la Mpanda Magharibi na kukubali kupokea boti nililolitengeneza mimi mwenyewe kwa ajili ya doria ya askari wetu pale Ikola. Nakushukuru sana. Kweli ilioonesha moyo wa ujasiri wa kutaka kujua mipaka yetu na kutembelea maeneo yetu na kujua shida ya askari wetu katika maeneo yale. Namshukuru sana yeye na naishukuru Serikali ya Awamu ya Nne, ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto aliyoitoa Mheshimiwa Waziri, ya kuonana na wanajeshi wetu kule na kwa kuwapa moyo, pamoja na kukutana na viongozi wa Serikali zetu za vijiji na kamati zetu za ulinzi na usalama, imetia moyo mpya ndani ya ulinzi baada ya kuwa wamekuwa na shida nyingi na matatizo mengi, ambayo wachangiaji waliotangulia, wameweza kuyaongelea ndani ya kambi zetu. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, namshukuru kwa namna ya pekee, Mheshimiwa Waziri, alipokuta askari wetu wana hali ngumu katika maeneo yao, alichangia kila kambi shilingi milioni tano, kwa ajili ya kukarabati majengo ambayo yalikuwa hata madirisha hayana. *(Makofi)*

Hii ilionesha maumivu makali aliyonayo kiongozi wetu upande wa jeshi, kwa kutekeleza yale yale ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, ndani ya Jamhuri yetu na Vikosi vyetu. Isipokuwa napenda niseme, hakuchangia juu ya hilo kwa ajili ya majengo yetu ambayo yalikuwa hata madirisha hayana, pia aliweza kuwawekea *TV set* kwa kila kituo kwa Kasanga - Jimbo la Kalambo, Kirando - Jimbo la Nkansi na kule kwangu Ikola Tarafa ya Karema - Jimbo la Mpanda Magharibi. Vijana wetu hawazagai mitaani na hakuna vurugu Mheshimiwa Waziri. Vijana wetu wanashukuru sana juu ya hayo, sasa hivi wanaburudika. Majengo yale yamekarabatiwa, wanaishi kwa amani na kujiona

kweli wapo chini ya kivuli cha Serikali yao, ambayo inajali maslahi na inathamini sehemu ya kazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, bado ninaiomba Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, iweze kufikiria kwa dhati juu ya maeneo yetu ya mwambao wa Ziwa Tanganyika, yenye utajiri wa pekee, ambayo hayajaguswa na mtu yeyote. Tuna samaki wengi mno, waliokaa chini ya maji ya ziwa lile, tuna mipaka inayokabiliana kibiashara ingawa tuko katika maeneo ya vita kati yetu na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Burundi na Zambia. Askari wetu wana hali ngumu kwa ajili ya ulinzi, hawana zana za kutosha, ahadi ya *speed boat* katika nyakati zilizopita tuliahidiwa kwamba, tutapewa *speed boat* mbili kutoka Serikalini, kwa ajili ya ulinzi wetu ndani ya Mkoa wa Kigoma na nyingine iwe katika Mkoa wa Rukwa. Kwa hali hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Serikali ya Awamu ya Nne, atupe kipaumbele katika maeneo yetu yale na vilevile kikosi cha *Navy Marine*, kianzishwe katika maeneo yetu na zana za kisasa kwa ajili ya mipaka yetu na watu wetu waweze kujiajiri kwa kutumia ziwa lile, kwa uvuvi ambao utawapa utajiri na kuondoa umaskini.

Pamoja na hayo, kadhalika tunaiomba Serikali kutokana na vikosi vyake vya ulinzi katika maeneo yetu, iweze kufunguliwa barabara kwa kutumia vikosi hivi. Barabara hizi za kilometa nne, kilometa sita, tunaomba msaada wako Mheshimiwa Waziri, kupitia Bunge hili Tukufu, aweze kulifikiria shauri hili ndani ya Kata yangu ya Ikola, kule Karema, katika vijiji vya Ikola, Karema yenyewe, Sumbwa, Kaselamiaga, Kasangatongwe, Lwega, hadi hapo tunapopakana na Jimbo la Kigoma Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuchangia juu ya masuala ya huduma za tiba zinazotolewa na askari wetu. Tulipotembelea kule katika kambi yangu ya Ikola, Mheshimiwa Waziri, uliona wale askari ingawa ni wachache, lakini pia walikuwa wakitoa huduma za tiba katika maeneo yetu. Askari hawa ni watu ambao wamejiandaa tayari na wameandaliwa na Taifa letu kuwa wazalendo wa kweli, askari wema, askari wa umma wanaojitolea kuwatunza wazazi na kuwaangalia licha ya kulinda mipaka yetu. Mimi binafsi, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mpanda Magharibi, naipongeza Wizara na nalipongeza sana Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naingia katika nafasi nyingine inayohusu vijana wetu wa JKT. Vijana hawa wameelimishwa, wamepewa changamoto, wana nidhamu ya kutosha na wana uwezo wa kukabili maeneo mbalimbali. Jumla ya vijana 3,374 wa *operation* jiajiri, walichaguliwa katika makambi yake mwezi Machi, 2005. Vijana hao wanatarajia kumaliza mkataba wao wa mafunzo wa miaka miwili mwezi Machi, 2007.

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba Serikali, vijana hawa wanapata mafunzo ya ulinzi, wanapata mafunzo ya kilimo, wanapata mafunzo ya uvuvi, wanapata mafunzo pia ya ufugaji bora.

Hizi ni zana nzito na nzuri, tunaomba Serikali kupitia Wizara nyingine zote, wachukuliwe vijana hawa ili wawe maafisa ugani katika vijiji vyetu, ambavyo hatuna

changamoto hizi, kwa ajili ya kupunguza umaskini na kuleta maendeleo zaidi katika maeneo yetu, sambamba na ulinzi pia.

Pia napenda kukipongeza Kikosi cha SUMA JKT, kinachotengeneza madawa kwa kushirikiana na *TANZANSINO* kilichoko Mgul ani Dar es Salaam, huu ni ufanisi ambao tunapaswa kuunga mkono sisi sote.

Kadhalika kikosi chetu cha ujenzi ya miradi mbalimbali iliyopewa na Serikali, kiweze kutumika katika kutengeneza majengo yetu ya Serikali, katika kutengeneza barabara zetu na kadhalika. Nina hakika utakuwa ufanisi mkubwa na matengenezo yatakuwa imara, kama tunavyofahamu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, binafsi naunga mkono hoja, mia kwa mia ya Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii. Kwanza, naipongeza hotuba hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na maofisa wake wote, walioshiriki. Lingine nawapongeza wapiganaji wote, wakiongozwa na Mkuu wa Majeshi.

Mheshimiwa Spika, sitozidi kutoa pongezi kwa sababu hii ni mara yangu ya pili katika ukumbi huu mpya kuchangia. Kila mmoja anayekaa hapa, anasifu kwamba kazi ya wanajeshi wetu ni nzuri na kubwa, mimi nakiri hilo, kwa sababu niliwahi kuwemo kwenye nyaja hizo na ukiwa mwoga ukiingia tu kuna mambo mawili yanaweza kukurejesha nyuma. Ukiingia kwanza, unaelezwa kwamba kwa muda wote wa saa 24 uko kazini na ni kweli, lakini la pili unaelezwa kwamba, mengine tumia akili yako usiulize. La tatu na kubwa zaidi, tekeleza halafu lalamika. Mambo matatu mazito makubwa, lakini yanamfanya mtu awe mkakamavu. Utekeleze halafu ulalamike, umerudi kazini hujala, hujamwona mama watoto na watoto wako japokuwa wanaumwa, unaambiwa rudi kazini na wala usilalamike. Hivi ndivyo naamini wanavyofanya Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania. Wanafanya hivyo na hasa kwa vile wanavyoweza kuukabili Muungano wa nchi mbili hizi mpaka leo haujateteleka na mpaka leo tunakwenda kwa hali ya usalama na amani. Asante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia kwako, naiomba Serikali, tuwe na mfumo mpya, ambao wanajeshi wote wastaafu, wakishastaafu tuwatie moyo wajione wao ni wanajeshi wa akiba au jeshi la akiba. Lakini haya hayaji kama hatukuwatekelezea yale yaliyo muhimu, kuwalipa mafao yao kwa wakati, kupata pensheni zao inavyostahili, lakini kuandaa kabla ya hawajastaafu, akistaafu awe na mahali pazuri pa kuishi na hili linakuja ili tuwape mkopo wa kujenga nyumba. *(Makofi)*

Lakini leo mwanajeshi baada ya kustaafu hajapata pesa, anaanza kukopa ajenge nyumba, hata akipata pesa kwa muda wa mwaka mmoja hana chochote, huku anakuwa dhalili, kweli atakubali kuwa mwanajeshi wa akiba?

Nasema haya kwa sababu nimeyajua wakati tulipovamiwa, wakati ndio kwanza nastaafu, lakini nilitakiwa nirudi kwenye *waiting list,* wenzangu wakarudi wakaenda

uwanja wa mapambano, mimi nikasalimika kwa sababu wanajeshi wengi walifanya kazi haraka, kwa hiyo, ninaomba twende kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hospitali ya Bububu imeshazungumzwa, lakini na mimi nitazungumza kwa sababu ya muda wa miaka mitano yote ya nyuma niliyokuwa kwenye Bunge lako Tukufu, kila nikisimama nilikuwa naizungumzia Hospitali ya Bububu. Sasa leo ni wajibu wangu, kupongeza kwa sababu nimetembelea kule kibinafsi, inaendelea vizuri sana na natoa pongezi, izidi kuendelea vile, isipokuwa tu kazi iende haraka tupate wataalam, ili hospitali yetu ianze kazi mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumzia kuhusu ulinzi wa Zanzibar, ukiondoka Chwaka, ukipitia Pingwe, Bwejuu, Makunduchi, Mtende, Jambiani, hii ni Bahari ya Hindi. Lakini sehemu zetu hizi zote hazina jeshi na wakati wetu huu tunaujua ulivyo, kwa hiyo, pendekezo langu na ombi langu kupitia kwako Waziri na Wataalam, waende kule waone sehemu hizo, ili ijengwe kambi sehemu za Makunduchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa huzuni kabisa, nitazungumzia kuhusu vikosi vyetu viwili mpaka vitatu. Zanzibar ni nchi, imepindua na hatuiwezi kuifanya kuwa butu, kama ng'ombe asiwe na mkia, chofua asiweze kumuwinga winga. Haiwezekani hilo na mtu yeyote hasa Mzanzibari na mwenye imani na Serikali ya Zanzibar, hatoweza kusimama hapa akasema KVZ ivunjwe, JKU ivunjwe, KMKM isiwepo, hiyo haiwezekani. Kwa sababu ile ni Wizara kamili, pia imeajiri vijana wengi, ina maofisa, watalaam, walimu na kila fani, leo uje uivunje uilete kwenye JKT kuanza arifu kwa kijiti! Kweli hili naweza kusema halizungumziki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kupitia kwako, lazima ujue ndugu zetu Wapizani wana mtego, tulikuwa hatuna bendera wakalia sana hapa, baada ya kuipata bendera wakasema itiwe rangi nyekundu, tukawa hatuna timu ya mpira, kuipata timu ya mpira, tunajitegemea hawai-*support,* leo hii wanasema JKU isiweko, sijui KMK isiweko, sijui JKU isiweko, Valatia asiweko, tukishamaliza hayo watarudi nyuma watasema mshamezwa Wazanzibari hivyo, tusamehewe. Nimetoka nje, zaidi ya simu sita nimeshapokea, naambiwa hili halizungumziki, wala halina mjadala, hatuwezi kuifanya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikawa butu, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, kwa niaba yangu na niaba ya wananchi wa Jimbo la Mwanakweleke, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii. Napenda nimpongeze mtoa hoja, kwa jinsi alivyowasilisha hoja yake vizuri na vilevile nampongeza Mwenyekiti wa Kamati na Kamati zote kwa uwasilishaji wa hoja zao.

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa, kwa jinsi ambavyo imekuwa inasimamia moja ya majukumu yake makuuv kwa kuhakikisha kwamba, nchi yetu ya Tanzania ni shwari na ni tulivu. Pamoja na kwamba, kuna chokochoko ndogo ndogo za hapa na pale, lakini bado naendelea kuamini kwamba, haliwezi Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kwa jinsi ambavyo limekaa vizuri, uongozi

wake ni mzuri na askari wetu wako tayari kuwalinda wananchi na mali ya Watanzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie lingine kwamba, kwa kuwa nchi yetu ina ututlivu na ni shwari, jeshi letu la wananchi linalo wataalam wake, linalo askari ambao wamejifunza vizuri, wana utaalam mwingine wa ziada, ambao kutokana na kwamba nchi yetu haimo katika vita, inafanya baadhi ya utaalam usiweze kupata namna nzuri ya kutumika. Kwa msingi huo, napenda kushauri kwamba, pale katika ukurasa wa 22 na 23 wa kitabu, kumeelezewa na mashirika, lipo shirika kuna viwanda vya utafiti na uendelezaji wa teknolojia ya kijeshi, tuna Shirika la Nyumbu na Mzinga. Mashirika haya yamekuwa yanafanya kazi nzuri, Mziga wanatusaidia kutengeneza zana mbalimbali za kijeshi, muhimu kwa uendelezaji wa jeshi letu. Lakini vilevile Nyumbu wamekuwa wakisaidia katika usafiri na Mheshimiwa Waziri katika kuwasilisha hoja yake, amethibitisha kwamba, bado hali ya usafiri si nzuri na amethibitisha kwamba, katika mipango yake ya baadaye, Wizara itaendelea kuyasimamia haya.

Bado akakiri katika vifungu mbalimbali kwamba, malengo ya mashirika hayo hayakufikia kiwango walichokuwa wamekikusudia kuweza kufikiwa, lakini sababu alizozitoa, majengo ni chakavu na pesa ni kidogo. Ninashuri kwamba, kuhusu hayo mawili yafuatayo yaangaliwe uwezekano wa kufanyika.

La kwanza, ninaishauri Serikali ione uwezekano wa kutenga fungu kutoka katika pato la ndani ya nchi kusudi liweze kuimarisha vikosi, mashirika haya mawili yaimarishwe, shirika la Mzinga na Nyumbu, tuweze kupata zana hizi muhimu za usafiri na silaha za kijeshi, kadri inavyowezekana. Kwa hiyo, Serikali ihakikishe kwamba, mapato yake ya kila mwaka itoe ndani ya pesa za nchi, ziweze kusaidia tuondokane na tatizo hili.

La pili, ambalo naomba liangaliwe uwezakano wa kufanyika, ni kusaidia katika uongozi, siku zilizopita, mashirika haya mawili yalikuwa chini ya Ngome, baadaye yakawekwa chini ya Wizara yenyewe. Hali hii inaonesha kwamba, uongozi katika mashirika haya mawili, umekuwa ni uongozi wa kiraia, lakini watenda kazi ni askari. Kwa hiyo, hapa ni maeneo mawili ambayo ni tofauti. Sisi tuliopita walau Jeshi la Kujenga Taifa, tunajua jinsi raia ambavyo yuko mbali na askari na ndio maana ukifika kwanza, wanakubrashi wanasema toa uraia halafu uwe askari. Kwa hali hiyo, hili liangaliwe, iwezekane kabisa kwamba, uongozi mkubwa kabisa pale uwe ni wa kijeshi zaidi, ili kuweza kuweka ule msukumo na amri ya kijeshi itumike katika kufanya kazi katika haya mashirika muhimu, tuweze kuongeza usafiri na kuondokana na tatizo la usafiri kwa askari wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda niishukuru sana Serikali na nimshukuru Rais aliyemaliza muda wake, pamoja na mambo mengine, wakati anaaga Vikosi vya Jeshi Tanzania, alifika kukiaga Kikosi cha 21 KJ, ambacho ni kikosi cha Kaboya, kiko mkoa wa Kagera, lakini zaidi mno kipo katika Jimbo la Muleba Kaskazini na hawa ni wapiga kura wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mfululizo wa bajeti ya miaka mitatu, kwa kipindi kilichotangulia nikiwa Mbunge ndani ya Bunge lako Tukufu, nimekuwa nikieleza kilio cha askari wa Jeshi la Wananchi wa Kaboya, wakiwa ni askari, lakini wakiwa ni wapiga kura, wanayo haki ya kuwakilishwa sawasawa na wapiga kura wengine katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, askari wako hawa wanayo matatizo ya *ration* wanapokuwa wanakwenda katika mafunzo nje, maana yake mafunzo ya medani, wao na wa vikosi vingine uko utaratibu kwamba, hawalipwi pesa yao ya *ration* ambayo ni shilingi 60,000/=. Suala hili linaleta malalamiko, kwa sababu kwanza, pesa wanayolipwa ni kidogo, ambayo ningeshauri iongezwe, lakini pesa hiyo pia hawapewi. *(Makofi)*

Sasa sijui malalamiko haya ni ya nini, kwa sababu kama kutengwa pesa, wamekwisha tengewa, wanapokuwa wako ndani ama wako nje kwenye mazoezi, bado ni askari wale wale, orodha yao ipo katika ukurasa ule ule uliowahesabu. Naomba waendelee kupewa pesa hizi. Lakini vilevile nashauri Serikali ikae ifikirie kuwaongeza, milo mitatu kwa shilingi 2,000/= kwa siku ni kidogo, kusudi waweze kusimamia ushwari na utulivu wa nchi yetu ipasavyo. Lakini waweze kutoa mchango wao wa tija hata wanapopewa kazi nyingine na majukumu mengine kwa mujibu wa taratibu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, askari hawa pia wapewe mikopo midogo midogo ya kuwasaidia. Tanzania bado hatujafikia hatua nzuri kuhusu makazi, bado tunahangaika tunapokuwa katika ajira kutafuta kwamba ajira ile isaidie mtumishi awe na nyumba, kwa sababu baada ya kustaafu ni wachache walioweza kujenga nyumba. Kwa hiyo, wengi wanajaribu katika posho, kujibana kwa namna moja au nyingine mtu aweze kujenga nyumba. Sasa askari huyu naye apewe mkopo wa kujenga nyumba, anunue vifaa vya usaifiri vidogo vidogo. Kikosi cha Kambi cha Kaboya kiko kilomita 45 toka Bukoba Mjini, ambako ni Makao Makuu ya Mkoa na kiko kilomita 37 kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Kwa hali hii wanapokuwa katika uhitaji kwenda Makao Makuu ya Mkoa ama ya Wilaya, usafiri wao ni mgumu na wa magari, naweza kusema bado haujaboreka. Nilikuwa nimepata ahadi za kusaidiwa lakini haikufikia hali ya kuboreshwa na mimi naomba wapewe basi la usafiri, wapate basi la kuwasafirisha kwenda Bukoba Mjini, Makao Makuu ya Mkoa, ambapo ndio shughuli zao nyingi zinafanyika kule. Wapewe basi liwasaidie kwenda pia Makao Makuu ya Wilaya. *(Makofi)*

Lakini vilevile, niliwahi kuomba sana kwamba, katika kipindi cha mashambulizi ya vita vya Iddi Amini pale kulikuwa na zahanati, ilikuwa inasaidia sana ilipigwa bomu, ikasambaratishwa. Zahanati ile si kwamba, inahudumia askari wa kikosi cha Kambi ya Kaboya tu, hapana, hospitali ile inahudumia maeneo yote yaliyozunguka Kambi ya Kaboya, Kata za Mayondwe, Kata za Muhutwe, Kata ya Izigo na vijiji vilivyozunguka pale, vyote vinahudumiwa vizuri na hata wanaotoka nje ya maeneo hayo, wanahudumiwa vizuri pale kambini katika zahanati ya Kambi. Zahanati ile ni ndogo, ninaomba tena Serikali, iangalie zahanati ya Kikosi cha Jeshi cha Kaboya, kama Mheshimiwa Waziri atakwenda kuangalia *Hansard* ambazo nimechangia, kasoro mwaka 2005, siku ya bajeti

ya Wizara hii sikuwa Bungeni, lakini bajeti zilizotangulia nilikuwa nikilieleza hili na ninaomba Serikali iliangalie, itusaidie kujenga zahanati ya Kambi ya Kaboya kwa ajili ya askari, lakini hasa kwa ajili ya raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maombi hayo, naomba pia daktari, tuweze kupata daktari, atoe huduma hizi. Kwa msingi huo, napenda nitoe shukrani za wananchi waliozunguka Kambi ya Kaboya, wanapata huduma nzuri japokuwa ni kwa kiwango hicho kilichopo, ambacho bado ni cha hali halisi niliyoieleza, lakini wanapofika pale wanapata huduma nzuri na gharama safi na lugha safi, wanaanza kupona hata kabla hawajapata dawa walizofuata pale. Mimi naomba Kaboya waendelee kutoa huduma nzuri kwa wananchi na sifa hii iendelee kuenea kwa sababu ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninaposoma kitabu hiki nimeona Serikali imesema kwamba, imepima mipaka ya vikosi vyake na ikataja miongoni mwa mikoa na Mkoa wa Kagera ukatajwa. Sasa kwa msingi huo, nikakumbuka hii 21 KJ, sina hakika kama wananchi waliozunguka kikosi hiki cha Kaboya wakiwemo wa vijiji vya Mayondwe, Itoju, Bugasha, Bisole, kama kweli wanafahamu mipaka na mimi mwenyewe Mbunge wao, kama kweli tunaifahamu mipaka ya Kambi ya Kaboya. Nasema hivyo kwa sababu juzi Kata ya Mayondwe, walitaka kujenga shule ya sekondari baadaye wakaambiwa kwamba, pale watoke ni eneo la jeshi. Sasa mipaka hii inayokuwa inaoneshwa wakati tu kunapokuwa na sababu isije kutokea siku moja mipaka ikatengwa kumbe ukakuta kundi kubwa la raia linakaa ndani ya kambi na pengine ikawa si wakati muafaka wa kuweza kuwaeleza habari ya kuwahamisha. Mimi nilikuwa naomba mipaka ieleweke kwa majirani wa kambi, kama wamo ndani ya kambi, waeleweshwe watafidiwa vipi na watakwenda wapi, waanze kutafuta mahali pa kwenda mapema.

Lakini vilevile wakati wa *range*, risasi huwa wakati mwingine zinajeruhi wananchi kwa sababu Kambi ya Kaboya, sasa hivi iko katikati ya maeneo wanakoishi watu. Kwa hiyo, ni vizuri mipaka ile ikaeleweka isije ikatokea madhara kwa namna zote, madhara ya risasi au kuja kuwahamisha wananchi wakatimuliwa kwa kutumia nguvu. Lakini nataka niseme mpaka leo hii navyozungumza, ninapenda niusifu uhusiano mzuri uliopo kati ya wananchi wa vijiji vilivyozunguka Kambi ya Kaboya na kambi yenyewe ya Kaboya, ni mzuri sana. Pale iko shule ya msingi ambayo inatumiwa na wananchi pamoja na wanajeshi, tuna mahusiano mazuri, napenda kushukuru kwa hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninarudia kusema ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, nimefarijika mno kwa kupata nafasi hii ambayo ni aghalabu sana kuipata. Napenda kusema kwamba, ninaiunga mkono hoja kwa asilimia mia, asante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hauwezeshi kutosha kumpa nafasi Mheshimiwa yeyote aweze kuchangia, ni muda mfupi sana.

Nina matangazo machache tu kwanza kuhusu wageni, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wataona kwamba au wamebaini kwamba, Spika hajawatangaza wageni wao. Hii ni kuzingatia kwamba, hatuwezi kuendelea kupokea majina ya wageni

wakati wote wakati shughuli zinaendelea, itakuwa vigumu sana. Si rahisi kukatiza hotuba ya Waziri ama wachangiaji ili utangaze wageni. Kwa hiyo, nakumbusha tena, kabla ya kipindi cha maswali saa tatu, mtu ambaye ana mgeni aliyekusudia atangazwe hapa, basi awe amefika mezani kwa Spika, kabla ya saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

La pili, kumekuwa na manung'uniko miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge, kuna baadhi ya huduma wameomba kutoka Serikalini na hawajapata majibu. Napenda niwahakikishie kwamba, mimi binafsi na ofisi nzima, tunafanya jitihada kubwa sana isionekane kwamba, tunatabasamu hivi basi tunaridhika. Jitihada ni kubwa, lakini mnajua unapozungumza na Serikali, kuna mipaka yake na kwa maana hiyo, napenda niwafahamishe tu kwamba, Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge, tutakutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, siku ya Jumatatu, kufuatilia mambo hayo hayo. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kukubali kuwa nasi ili tuweze kupata ufafanuzi. Baada ya hapo, tutawajulisheni wote kilichowezekana. *(Makofi)*

Kwa jioni nitakuwa na wachangiaji wawili, saa kumi na moja nitamwita Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni na saa kumi na moja na robo nitamwita Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mbunge wa Kyela. Baada ya hapo itakuwa ni zamu ya Wizara kuanza kujibu hoja, nitamwita Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee, Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wote kwa robo saa, itatufikisha saa kumi na moja na dakika arobaini na tano, nitamwita Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili aweze kuongea kwa muda usiozidi saa moja, akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, itatufikisha saa moja kasorobo au kabla ya hapo, ndio tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi. Nimeweka saa moja tu nahisi kwamba, Wizara hii haina matatizo yoyote, kwa sababu hata michango yenyewe unapokaa kwenye kiti hiki, unapima na aina ya mchango, nimeona kabisa saa moja inatutosha kabisa kumaliza Kamati ya Matumizi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06:58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotamka mapema ilikuwa wachangiaji wawe wawili baada ya hapo zianze kujibiwa hoja, kwa hiyo, namwita sasa Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, atafuatiwa na Msemaji wa mwisho Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa jioni ya leo kuchangia machache juu ya hotuba ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea mbele namshukuru Waziri wa Ulinzi na Naibu wake na maafisa wote ambao walishirikiana kuiweka katika hali nzuri hotuba yao waliyowasilisha asubuhi ya leo na kuendelea mpaka leo inachangiwa.

Mheshimiwa Spika, suala zima ambalo nataka kulizungumzia kwanza namshukuru sana Waziri kukubali matakwa ya Wabunge wakiwepo Bungeni siku za Jumamosi na Jumapili kwenda kupiga shabaha JKT Makutupora, kwa kweli kwa haya tunamshukuru sana Mheshimwa Waziri kukubali ombi la Wabunge kuhakikisha kuwa na Wabunge wanapatiwa mafunzo rasmi ya kijeshi wakiwepo hapa Bungeni. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kulikubali ombi la Wabunge.

Suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu mjadala mzima ambao nimeusikiliza asubuhi kuhusu JKT na JKU Zanzibar. Lile ni suala ambalo kwa kweli linahitaji makubaliano au sera rasmi ambalo linaweza likazungumzwa kwa sababu linaweza likazungumzika.

Mheshimiwa Spika, lakini suala ambalo kwa kweli nataka kulizungumzia kwa hivi sasa kuingia JKT kutoka Zanzibar ni watoto wachache sana ambao wanaingi. Idadi ni ndogo sana kwa sababu wanaingia watoto 50 kutoka Zanzibar wakati ambapo kama itaongezwa idadi hii tunaweza kupunguza tatizo kubwa la ajira kwa vijana kwa sababu JKT wanapata mafunzo mengi ya mali ambayo huenda yakawasaidia katika maisha yao ya baadaeye. Kwa hili, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie ile idadi iliyopo hivi sasa kuingeza ili angalau kulifikia kama 200 au hata 500 kuhakikisha kwamba wanaingia katika Jeshi la Kujenga Taifa na kupata mafunzo na ujuzi ambao utawasaidia vijana wa Zanzibar ambao kwa kweli hawana kazi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri kuwa hivi sasa sekta ambayo imebakia kimichezo Tanzania ni katika Jeshi au katika Majeshi yetu yaliyopo Tanzania ambayo hivi sasa ndiyo yenye nidhamu ya kuhakikisha kwamba michezo inakuwa nchini Tanzania.

Kwa hiyo, ipo haja Meshimiwa Waziri asizitupe mbali hizi timu zetu zilizo katika Majeshi na kuziangalia na kuziwekea bajeti nzuri ambazo zinaweza zikafanya vizuri. Michezo uraiani hivi sasa ni migogoro tu au kitega uchumi ambacho kinavutiwa na wengi ambapo hivi sasa wajanja wanakitumia kama kwa kujinufaisha wao wenyewe. Lakini Majeshini bado nidhamu ya michezo ipo na inaendelea kuwepo kwa sababu ni watii sana wa nidhamu za Kijeshi kwa hiyo, michezo inaendelea vizuri kwa hiyo, ipo haja Mheshimiwa Waziri kuliangalia hili suala la kimichezo katika majeshi yetu na kulipa uwezo au kuwapa motisha wanamichezo wetu ili kuhakikisha kuwa wanailetea medali nchi yetu na sifa na ajira kwao vile vile kuhakikisha kuwa iko katika michezo ambayo wanashiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba namshauri sana Mheshimiwa Waziri kuwa aje kutembelea makambi ya Jeshi Zanzibar na akiyatembelea afike na kule vijijini ambako mengine yapo ambayo hivi sasa yanafanya shughuli zao za kiulinzi. Kwa hiyo, namwomba sana atakapofika aige mfano mzuri wa

Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi wakati uliopita Waziri wa Ulinzi alifanya hivyo na tukampongeza sana na yale ambayo tuliyatarajia alipokuja yalifanikiwa kwa sababu waswahili wanasema mkaa chini ya muasumini haachi kunukia, kwa hiyo, angalau unapokuja yale mengi wanajeshi wanaweza wakayaeleza na Wabunge wanaweza wakapata faraja na huenda hata na kura zikaongezeka kwa wakati ule. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ufanye ziara ya makusudi katika Kambi moja ambayo inaitwa Potoa. Kambi hii kwa kweli kila mwaka naipigia kelele na mafanikio yake kwa kweli tuliyaona kipindi kilichopita alipokuja Waziri walifanikiwa kwa baadhi ya matatizo yaliyokuwepo wakati ule na kuna baadhi ya matatizo ambayo mpaka hivi sasa bado hayajakamilika. Kwa hiyo, nashauri kuwa ipo haja na tatizo kubwa ambalo hivi sasa linawakabili ni tatizo la maji katika Kambi ile na barabara ya kwenda kule ambapo wanaishi wao wenyewe ni mbovu kwa hiyo ipo haja Mheshimiwa Waziri kuliangalia hili na ni vizuri hasa kuja kule tukashirikiana kuiona hiyo hali halisi kama walivyofanya hawa Mawaziri waliopita katika kipindi kilichopita.

Lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuwa nyumba zile zilijengwa mwaka 1972 na zikazinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Kwanza wa Zanzaibar Mheshimiwa Marehemu Abeid Aman Karume. Lakini kulingana na hivi sasa mpaka leo ni nyumba zile ukarabati wake kwa kweli si mzuri kwa hiyo ipo haja ya kuzifanyia ukarabati nyumba zile ambazo wanaishi wanajeshi na kuziongezea kwa wingi yaani wahakikishe kuwa zinaongezeka hata idadi ya zile nyumba zilizopo kule kuhakikisha kuwa zina mazingira mazuri kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru kipindi kilichopita waliwahi kukarabati lakini bado hazijakarabatiwa vizuri na nyumba ambazo wanaishi hivi sasa ambazo ziko katika kijiji kimoja kinaitwa Kivunge, vile vile tuziangalie kwa jicho la huruma tuhakikishe kuwa na nyumba zile zinafanyiwa ukarabati ili kuhakikisha kuwa zinakwenda na wakati tulionao hivi sasa kuacha ile hali tuliyonayo ya magofu na kuwa ni nyumba za kileo na za kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu malalamiko au matatizo ya Wanajeshi wetu hapa nchini. Yapo malalamiko mengi ambayo yameshazungumzwa na yanaendelea kuzungumzwa na Serikali inapopata uwezo inajaribu kuyapunguza lakini bado yapo ambayo yanahusiana na mambo ya likizo.

Mheshimiwa Spika, likizo kwa mfanyakazi wa Serikali au Wanajeshi ni kila mwaka aende likizo, lakini inafika mahali miaka mitatu wanajeshi bado hawajaenda likizo lakini suala linakuja je, katika hii miaka miwili zile pesa ambazo zinatengwa zinakwenda wapi ambapo haendi likizo, lakini pesa hazipati yaani ile azma au kusudio lililokusudiwa katika kipindi kile na hii ni haki yao ambayo kila mwaka wanaingia likizo lakini miaka mitatu hawajaenda likizo.

Mheshimiwa Spika, lakini fedha iliyopo pale sijui inatumikaje au haiingii au haitoki Hazina kwenda kwa Wanajeshi na hili ni lalamiko ambalo nalalamikiwa na

Wanajeshi wa chini zaidi ukilinganisha na wale wa juu ambao siku nyingine maslahi yao ni mazuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu kupandishwa vyeo. Hili linachukua muda mrefu kwa kweli na linalalamikiwa na wengi, kijana anaingia Jeshini ana sifa zote za kielimu lakini kwa nini anakaa muda mrefu hajaenda kozi ya Jeshi. Kwa hiyo, ipo haja kuwa tuwaangalie kwa miaka kama sita au saba anakaa bila ya kupatiwa nafasi yoyote katika Jeshi kwa hiyo, ipo haja ya kuliangalia kwa sababu ukiangalia vigezo vya mwanzo wanapoingia Jeshini utaona ni elimu ina *matter* lakini tatizo linakuja kuwa baada ya muda suala kama lile halifanyiki na wanalalamika kuwa hawaendi au hawapandishwi vyeo kwa muda wote huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba kuna mwaka ajali ya treni ilivyotokea hapa Dodoma, kuna wanajeshi wa Ihumwa walikwenda pale na kuweka Kambi. Walipoweka Kambi kwa bahati nzuri wakawa wanapewa posho kutoka kwa Mkuu wa Mkoa, lakini ile posho yao ya siku saba waliyokaa pale inaonyeshwa kuwa walikatwa. Sasa hili ni lalamiko mpaka leo wengine wanadai kuwa kwa nini hawakulipwa fedha ile na fedha ile ilikwenda wapi na kwa nini wakatwe wakati ile ilikuwa ni ajali iliyotokewa au ni janga la Taifa lililotokea kwa wakati ule? Kwa hiyo, ipo haja kuliangalia suala hili au wale ambao walishughulikia tatizo lile wakati ule walipwe yale mafao yao au warejeshewe fedha zao kwa wakati ule.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili linakuja kuwa wale ambao waliteseka pale na bado kuteseka kwao wakakatwa zile pesa za siku saba eti kwa sababu wamefidiwa na mfuko wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa kipindi kile.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo linazungumziwa kuhusu wanajeshi wetu kuhusu kuishi uraiani na suala kubwa ambalo linawafanya waishi uraiani ni kwa sababu hawana nyumba katika makambi. Lakini ile pesa ambayo wanalipwa kwa kujikimu na masuala ya nyumba au pango la nyumba ni ndogo ni shilingi 9,000/= kwa kweli ni ndogo sana ukilinganisha na mazingira tuliyonayo. Kwa hiyo, ipo haja kwa hili kuliangalia upya au wanajeshi wetu wataishi katika maisha duni au kuishi katika nyumba ambazo kwa kweli hazistahili au hazina sifa za kuishi wanajeshi na hivyo ni kudhalilika sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hili naliomba kuwa wanajeshi wetu wanaoishi uraiani kwa hii fedha ambayo wanapewa basi iongezeke na kama haitaongezeka basi wapewe kwa wakati na vilevile tunakikishe kuwa muda ambao wanapewa basi ulingane na mahitaji yao kwa sababu lipo lalamiko kuwa wanadai masurufu ambayo yalipita nyuma na hawajapewa mpaka leo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la *Ration Allowance* ambayo hivi sasa wanapewa shilingi 60,000/=. Kwa kweli hii ni ndogo sana namwomba Mheshimiwa Waziri iangaliwe kwa jicho la huruma iende na wakati angalau itoke hapa iende kwenye mfumo angalau kulingana na wakati tulionao kama shilingi 100,000/= au na zaidi ya hapo. Kwa hiyo, ipo haja ya wanajeshi wetu waangaliwe kwa sababu wanafanya kazi nzuri lakini maslahi bado ni duni, tuhakikishe kuwa tunawaenzi wanajeshi wetu kwani

kukasirika kwa wanajeshi ni tatizo la nchi kwa hiyo, tuone hii hali ambayo kwa kweli wanajeshi wetu wanaikabili hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache niliyoyasema na zaidi suala zima nasisitiza kwa Waziri ni kwamba afanye ziara tufuatane akitoka hapa twende Kambi ya Potoa tukaangalie yale mazingira waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja na ninakushukuru. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii kama msemaji wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze pengine kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Juma Athuman Kapuya, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Naibu wake Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na uongozi mzima wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri na vile vile kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kipindi kifupi sana toka wameapishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii vile vile kulipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kutumiza miaka 42 yenye historia ya kujivunia na historia iliyotukuka. Si vibaya kujikumbusha kuwa katika miaka ya mwanzo toka Jeshi letu lianzishwe upya mwaka 1964, Jeshi letu lilifundisha karibu vikundi vyote Barani Afrika vya kupigania Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mwalimu yeyote anavyojivunia na anavyojihusisha na mafanikio ya mwanafunzi wake anapofaulu basi ushindi wa vita vya Ukombozi Barani Afrika ni ushindi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Nduli Iddi Amini alipodhani tumechoshwa na vita vya ukombozi, akaona aah, basi huu ndiyo muda wa kuivamia Tanzania na kuimega vipande. Dunia ilishuhudia ari, uzalendo na utayari wa hali ya juu wa Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania pamoja na Watanzania wenyewe walionyesha ari isiyo na kifani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisemi haya kutokana na kusoma magazeti pengine na kusoma vitabu vya historia bali nilishiriki na nilikuwepo kwenye mchakato huo mkono mmoja nikiwa nimeshika silaha na mkono mwingine nimeshika *note book* na kalamu kama mwandishi wa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie pongezi zangu kwa kumnukuu Rais wetu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa aliyesema mwaka 2000 kuhusu Jeshi letu kwamba: “Jeshi letu ni dogo kwa idadi ya askari, lakini ni kubwa kwa uzalendo wake, ni kubwa kwa utii wake na ni kubwa kwa utayari wake katika Ulinzi wa Taifa letu.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nisahau kuhusu suala moja ambalo Mheshimiwa Waziri ameligusia katika hotuba yake kuhusu mchango wa Jeshi yanapotokea majanga ya Kitaifa. Kwa kweli hata mimi nayapongeza sana Majeshi yetu, mimi nadhani ni wajibu wetu kama Bunge ni kuliongeza uwezo mkubwa zaidi kila inapobidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu JKT niongelee kidogo tu. Naipongeza sana Serikali kwa jitihada za kulifufua Jeshi la Kujenga Taifa ingawa wengi tungependa liwe katika hali kama ilivyokuwepo kule awali. Leo hii naziona sababu nyingi zaidi kwa vijana wetu wanaomaliza Sekondari, wanaomaliza *High School* kupitia Jeshi la Kujenga Taifa kuliko hata ilivyokuwa huko zamani. Naamini JKT itasaidia sana kuondoa vichwani mwa vijana wetu na watoto wetu athari za *internet, video,* athari za televisheni za leo na kusaidia kuwajengea moyo wa uzalendo, umoja na kujituma na ushirikiano, vile vile kuwandaa kwa uongozi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 17 wa hotuba ya Waziri nimeguswa sana na *Operation* Jiajiri ambayo Mheshimiwa Waziri ameielezea vizuri sana. Naambiwa kwamba mwaka 2005 waliingia vijana 3,374 katika hii *Operation* Jiajiri na baada ya kupatiwa mafunzo nasoma huo ukurasa wa 17: "Baada ya kupatiwa mafunzo ya awali ya miezi sita Ulinzi na Uzalendo hao kwa sasa wanaendelea kupatiwa mafunzo ya Ufundi Stadi, Kilimo,Ufugaji Bora na Uvuvi katika Makambi mbalimbali ya JKT."

Mheshimiwa Spika, kama ingewezekana ningemwomba hata Mheshimiwa Waziri Mkuu zile shilingi milioni 500 zinazokwenda kwenye kila mkoa kwa ajili ya vijana zingepelekwa JKT kwa ajili ya *Operation* Jiajiri mimi nina hakika zingekuwa na *impact* kubwa kweli kweli kwa vijana wetu wengi ambao wanamaliza Darasa la VII, *Form Four* na *Form Six* ambao hawana ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nigusie kidogo kuhusu tatizo nililonalo Kyela ambalo naiomba Wizara ilitupie jicho katika mwaka huu wa fedha. Miaka ya 1970 wakati tunasumbuliwa na Iddi Amini huko Kaskazini Kamuzu Banda naye alilkuwa analeta chokochoko kwenye mpaka wetu na Malawi. Sasa hali ya usalama ikawa mbaya sana Kyela ndipo Serikali ikaamua kuweka kikosi cha Jeshi la Wananchi wa Tanzania sehemu za Ipyana Kyela.

Mheshimiwa Spika, kazi imefanyika nzuri sana na Jeshi letu pale Kyela lakini Banda alipoona kwamba tumemshughulikia Iddi Amini hadi Arua Kaskazini ya Uganda akajua kwamba sasa zamu imefika kwa yeye kushikishwa kidogo adabu kwa hiyo akaufyata moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, toka kipindi hicho mpaka wetu na Malawi umekuwa shwari na kutokana na hali ya usalama kuwa mzuri na hali ya kikosi chetu cha Jeshi kuzidi kuzingirwa na wananchi na bila kuwa na eneo kubwa zaidi *for expansion,* Wizara katika miaka ya 1990 ilishafanya mchakato wa kukihamisha kikosi hicho kukipeleka sehemu kubwa zaidi nafikiri mpakani mwa Wilaya ya Kyela na Ileje. Eneo hilo jipya mimi nalifahamu ni kwamba tayari lilisha hata pimwa, sasa utekelezaji wake ndiyo unaosuasua.

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kupitia Bunge lako hili niiombe Wizara kama imefikiria vingine kutokukihamisha hicho kikosi basi tungeomba litamkwe hilo wazi kuliko kuwaweka wananchi wa Kyela hasa Kata ya Kajunjumele na kwenye kijiji cha Kapamisya wasiwe na dukuduku kwa sababu walitoa mashamba yao makubwa sana kwa ajili ya kuliweka Jeshi pale na wana dukuduku kwamba kama Jeshi litaondoka pale basi watatumia yale mashamba kuweza kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Spika, lakini kama Serikali inaona kama nilivyosema uamuzi huo haukuwa mzuri, basi naomba Wizara vile vile inisaidie kupunguza shauku ya wananchi kuhusu maamuzi ya viongozi wa Jeshi katika kikosi hicho sasa hivi kwamba maeneo ambayo hayatumiki na Jeshi wananchi wakitaka kuyatumia kwa kilimo wanaambiwa walipie fedha, wayakodishe, mimi nadhani hiyo siyo nzuri. Ningeomba Mheshimiwa Waziri unisaidie kwenye hilo, maeneo yale ambayo Jeshi haliyatumii ningeomba wananchi waruhusiwe kuyatumia kwa kilimo tena ni cha mpunga bila kuwatoza hela yoyote.

Mheshimiwa Spika, moja ya sifa kuu ya Jeshi letu ni kwamba ni Jeshi lililo karibu na wananchi kwa ajili ya wananchi, tusiiharibu hiyo hali ya hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri au pengine Mheshimiwa Naibu Waziri waje Kyela wajionee hali wenyewe ili maamuzi ya kuhamisha hicho kikosi au lah yazingatie hali halisi iliyopo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 inazungumzia kuendeleza Sera ya CCM ya kuwa na Jeshi dogo lenye taaluma, lenye zana za kisasa. Kwa hiyo, litakuwa ni Jeshi kwa kweli la wasomi ambalo ndiyo kawaida kwa dunia yote ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wasomi hao hawatakuja kushika vyeo vya juu vya uongozi ikiwa Jeshi litarefusha mno vipindi vya *promotion*. Kwa muda mrefu nimekuwa na marafiki wengi Jeshini kwamba vipindi vya *promotion* vilikuwa vifupi miaka mitatu, mitatu, lakini sasa hivi nasikia vimeshakwenda mpaka miaka mitano au sita. Sasa hii *mark time* ni ya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba tusiwacheleweshe mno vijana katika Jeshi kupanda vyeo, changamoto yetu iwe ni kuwajengea maafisa wetu wanaostaafu mazingira mazuri ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, inauma sana leo hii ukikuta kwamba mtu ambaye alikuwa jana Afisa wa Jeshi unamkuta ameajiriwa kwenye kikampuni cha ulinzi wa jioni, inasikitisha sana. Inabidi kwa kweli tufanye maandalizi mazuri sana, hii nadhani ndiyo changamoto kubwa vile vile ambayo inakukabili Mheshimiwa Waziri katika uongozi wako wa hii Wizara.

Mheshimiwa Spika, leo hii napata faraja kubwa mno kuona Jeshi letu linaongozwa na Makamanda wasomi wazuri kweli kweli. Sasa nawaomba viongozi wetu wa Jeshi wa sasa msiwasahau wasomi ndani ya Jeshi wakajisikia ni wakiwa, nawafahamu

vijana wengi waliosoma vizuri sana ndani ya Jeshi, kuna *Ph.D.* nyingi sana Jeshini, kuna *Masters* nyingi tu, kuna *BcS* nyingi tu sana Jeshini. Lakini inakuwa kama nuksi Jeshini ukiwa umesoma sana unaoneka hufai pengine kupanda, kwa wale ambao hawaelewi basi nendeni pale *Mzinga Cooperation* kuna *Degree* nzito kweli kweli pale. Nilikuwa naomba uongozi wetu wa Jeshi sasa hivi uanze kuangalia hao vijana vilevile wasijisikie wakimya, tuwatupie jicho tuweze kutambua hazina waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mmoja mdogo wa mwisho hivi karibuni Serikali imetangaza kuwaongeza mishahara Madaktari Bingwa. Ah, sasa naomba sana mishahara ya Madaktari Bingwa pia Jeshini pia ipande vile vile kama haijapanda kwa sababu nina wasiwasi wanaweza wakawa wanapandishwa uraiani tu, lakini Jeshini wasipandishwe. Kwa hiyo, nilikuwa naomba iendane na mishahara ya wenzao vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,kwa hayo machache nilikua naomba nimpongeze tena Mheshimiwa Profesa Juma Athumani Kapuya, kwa hotuba nzuri sana na ninapenda niiunge hii hoja mkono. Ahsante sana.*(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu. Napongeza uongozi wote wa Awamu ya Nne wa Serikali ya Tanzania na uongozi wa Awamu ya Sita ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa wasimamizi wote Wakuu Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Rais Amani Abeid Karume,sina budi kupongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kusimamiwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Juma Athumani Kapuya na Naibu Waziri Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, nawatakia kazi ya kheri na mafanikio mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa ni jeshi letu na lenye dhamana kwa Tanzania yetu kulinda wananchi wote na nchi yetu yote kwa raia na mali zao zote na kuishi kwa usalama na amani. Naomba Serikali iipe uwezo wa fedha na nguvu zote ili idumishe amani nchini na kuajiri vijana wengi kwa kutumikia Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli JWTZ na JKT wote wapate huduma nzuri wakiwa kazini mwao na popote pale alipo kwa askari hawa wapo kazini saa zote 24 na pahali popote yupo kazini kwanza majengo yawe ya kijeshi, chakula, usafiri huduma za afya, dawa michezoni na kadhalika.

Kuhusu afya kwa majeshi yetu ni muhimu na dawa zipatikane. Majengo ya kambi ya Lugalo na kadhalika ni mabovu na huduma katika hospitali na vifaa vya utibabu bado haba na haviendani na wakati hasa kwa Jeshi letu kwani kupoteza askari mmoja ni sawa na kupoteza askari elfu moja.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Welezo Zanzibar (Mesaili) ina uhaba kwa jengo la kituo cha afya na dawa za kutosha na kuzigatia kambi hii ni muhimu na Jeshi lake, naomba Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi kukipa kipaumbele na fedha kwa kambi hii ili

zitolewe huduma na wanajeshi wetu kuwapa nguvu na uwezo wa kutumikia jeshi na wapewe vyeo haraka kulingana na sifa zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi Jimbo la Magogoni.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba yake nzuri ambayo inafafanua masuala mbalimbali muhimu yanayohusu Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa. Hivi ni vyombo muhimu sana katika kudumisha amani na utulivu na usalama wa Watanzania na mali zao.

Mheshimiwa Spika, nakusudia kutumia fursa hii kuzungumzia Jeshi la Kujenga Taifa na umhimu wake kwa Taifa letu. Kwanza, naipongeza sana Serikali kwa kurejesha mafunzo ya JKT. Jeshi hili ni muhimu sana katika kujenga uzalendo na Umoja wa Taifa wakati huo huo vijana wakifundishwa mbinu za ulinzi na yale mambo mengi mengine ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaorodhesha kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, bado hatujafikia viwango vile tulivyowahi kufikia. Hivi sasa tunachukua vijana wa kujitolea tu. Vijana wanaomaliza masomo kwenye shule za sekondari na vyuo hawapatiwi fursa ya kupitia JKT kama ilivyokuwa katika miaka iliyopita. Ni muhimu sana kwa dosari hii kurekebishwa hata kama vijana hao watatumia muda mfupi kwenye Jeshi kuliko wale wa kujitolea ambao watapewa nafasi za kujiandaa kwa maisha yenye manufaa kwenye Taifa, kama nitakavyoeleza hapa chini.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa na JKT kuimarisha uzalishaji katika kilimo na viwandani ni muhimu na zinazostahili pongezi. Fursa zinazotokana na hatua hizo zinapaswa kuchukuliwa kuwaandaa vijana wanaopitia JKT kwa ajira katika maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Spika, vijana wapewa mafunzo ya kina kwa nadharia kiasi na kwa vitendo kwa viwango vikubwa zaidi. Ni lazima mafunzo hayo yawape vijana ujuzi *(skills)* kwa kutosha na kutosha huko kupimwe kwa uwezo wao wa kutenda lakini kupimwe pia kwa viwango vilivyowekwa Kitaifa kwa sekta inayohusika. Kwa mfano, mafunzo ya kilimo yawawezeshe vijana kupata cheti au sifa nyingine ya juu kama zinazotolewa na vyuo vya Kilimo *(MATI).* Wanaosomea ufundi wafikishwe katika viwango vya kuwawezesha kushinda *Trade Tests* na hata kufikia *full technician certificate,* tusiridhike na viwango vya mafunzo vya ubora wa chini. Viwanda vya JKT vitumike kuwapatia vijana mafunzo kwa vitendo na kwa kweli hili liwe ndilo lengo kuu.

Suala hili la kuwapatia vijana ujuzi wa kina lipewe umuhimu wa juu sana na vijana wote wa kujitolea wanaojiunga na JKT watoke wakiwa wamebobea katika moja au zaidi ya fani za mafunzo yanayotolewa na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa kuwa vijana wa JKT watakuwa wameandaliwa vizuri na kwa kuwa viongozi wa JKT na JWTZ watakuwa wamepata nafasi nzuri sana za

kuwaelewa vijana hao, vijana wa kujiunga na JWTZ na majeshi ya Polisi na Magereza wachukuliwe kutokana na vijana hawa na taratibu nyingine ziachwe.

Mheshimiwa Spika, naiunga hoja mkono.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na hivyo kuweza kufika katika kikao cha leo cha Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wabunge wote kwa ushirikiano katika shughuli mbalimbali zenye kuhusiana na Bunge na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba yao iliowasilishwa leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa lina jukumu la kulinda na kuhakikisha usalama wa mipaka ya nchi yetu dhidi ya maadui kutoka nje ili nchi yetu, wananchi pamoja na mali zao wanaishi kwa amani na usalama. Je, Serikali ina mpango gani au mikakati gani kuhakikisha kuwa maslahi yao yanaboreshwa na wanaandaliwa mazingira mazuri ya kazi na makazi?

Mheshimiwa Spika, Wizara iajiri vijana wenye uwezo na ambao wako tayari kufanya kazi ya ulinzi wa nchi yetu. Wapatiwe taaluma na mafunzo ya mara kwa mara ili waweze kuifanya kazi yao kwa uhakika na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa linahitaji kupatiwa viwanja vizuri vya michezo vitakavyowawezesha kushiriki katika michezo ambayo itasaidia kujenga miili, afya zao pamoja na kuitangaza nchi yetu huko nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni jambo la kawaida sasa katika nchi yetu kuwa askari anapostaafu anakuwa na maisha duni kabisa. Hii inaleta udhalilifu kwa wastaafu hao pamoja na familia zao. Naiomba Wizara iandae mikakati maalum itakayohakikisha kwamba askari wanapostaafu wanapata mafao yao mapema iwezekanavyo, ili waepukane na udhalilifu.

Mheshimiwa Spika, askari wa vikosi vyote hapa nchini vinaonekana katika harakati inapofika wakati wa Uchaguzi Mkuu. Hii inatia hofu na wasiwasi kwa wananchi na hata kusababisha wengine waogope kufika vituoni kutumia haki yao ya kupiga kura kwa kuchagua kiongozi wampendae au wamtakae. Naiomba Wizara iliangalie suala hili na kulipatia ufumbuzi unaofaa. Asante sana.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba yake nzuri iliyoeleweka kwa urahisi na ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu uko katika masuala mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi za dhati kwa uongozi wa kikosi cha Wanajeshi katika kambi ya Mikumi kwa mchango wao katika ushirikiano muafaka na kikosi cha Polisi, Mikumi katika kupeana taarifa za siri na udhibiti dhidi ya vitendo vya ujambazi wa silaha vilivyokithiri jirani na Kambi ya Jeshi ya Mikumi katika barabara itokayo Mikumi kwenda Kidatu.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya ujambazi wa kutumia silaha katika eneo la daraja la reli ya *TRC* jirani na kambi ya Jeshi yalianza kwa mauaji ya mfanyabiashara maarufu mwaka 2004. Mauaji haya yalifuatiwa na mfululizo wa matukio ya ujambazi wa kutumia silaha dhidi ya watu binafsi mabasi ya abiria na ya mizigo. Katika miaka miwili iliyopita matuko yasiyopungua nane yametokea.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi katika eneo hilo limetimiza sehemu yake ya majukumu ya ulinzi wa raia na kufanya matukio hayo sasa yakome, kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Mikumi na wengine wote kwa ujumla tunatoa pongezi kubwa kwa kazi waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, licha ya pongezi hizi napenda pia kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Mikumi, kuwapongeza wanajeshi wa Kambi ya Jeshi ya Mikumi kwa mahusiano mazuri na wananchi wa vijiji jirani na kambi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri niliyoyaeleza lipo tatizo moja ambalo wananchi wa Kata ya Mikumi linawakera. Jambo hili ni kuchukuliwa kwa eneo la kitongoji cha Vikweme kwa ajili ya matumizi ya mazoezi ya kijeshi. Wananchi hawapingi kimsingi juu ya suala hili, ila wameondokewa kabisa na eneo pekee katika kata hiyo, lililokuwa ndio la kuilisha jamii nzima ya Mikumi kutokana na kilimo kilichokuwa kinazalisha mazao mbalimbali ya chakula.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa pekee wa eneo la Vikweme unatokana na ukweli kwamba eneo la Mikumi kwa jumla limekingwa sehemu zote nyingine na vikwazo vinavyozuia kilimo kisifanyike. Upande wa Mashariki ipo Mbuga/Hifadhi ya Mikumi, Magharibi ni Hifadhi ya Milima ya Udzungwa katika barabara iendayo Iringa, Kusini kuna Hifadhi ya Milima ya Udzungwa kuelekea Kidatu hadi Ifakara. Eneo pekee la Kaskazini pekee ambako kitongoji cha Vikweme kipo, ndiko wananchi wa Mikumi kwa miaka mingi wamekuwa wakijipatia riziki kutokana na kilimo. Kujiajiri na utekelezaji wa maisha bora kwa wakulima, MKUKUTA na kadhalika itaathirika kwa kiasi fulani endapo wananchi watanyimwa eneo hilo walilolitumia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa kila hali na mali.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, pongezi ni jambo la awali kabisa katika Wizara hii nyeti kwa kazi nzuri mnayofanya nikianza kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamanda na watumishi wote Wizarani.

Baada ya pongezo hizo naomba nitoe mchango wangu kwa haya machache yafuatayo:-

(i) Naomba tuzidi kuliimarisha jeshi letu la ulinzi siku zote kwa kuwa na wataalamu wenye uwezo pamoja na vifaa, kwani kuna msemo wa busara usemao tumia nguvu nyingi wakati wa amani kujiandaa ili nguvu iwe kidogo wakati wa vita!

Napendekeza kuimarisha vitengo vya tiba jeshini kwani ni muhimu sana hata kwa ajili ya tiba kwa viongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuendelea na utaratibu wa kuwajengea nyumba za kuishi makambini badala ya kuishi uraiani.

(ii) Napendekeza kurudishwa kwa utaratibu wa vijana wetu wamalizapo kidato cha sita iwe ni lazima kupitia Jeshi la Kujenga Taifa kwani faida zake zinaonekana wazi siku hizi ukilinganisha wale wa siku za nyuma waliopitia jeshi na hawa wa miaka ya hivi karibuni ambao hawapitii jeshini

Mheshimiwa Spika, pia napendekeza tuitumie JKT kwa ajili ya kutoa elimu kwa vijana kwa ajili ya uzalishaji mali katika fani zote kwani hata wale wa kujitolea wanaweza kuwa kichocheo muhimu sana katika kuimarisha uchumi pamoja na kupambana na umaskini warudipo makwao.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine nawapongezeni sana! Kwa niaba ya wananchi wa Wilaya na Jimbo la Hai, ninawaahidi ushirikiano wetu daima! Mwenyezi Mungu awabariki. Ahsanteni.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na uwezo wa kuchangia hoja hii ya hotuba ya Waziri wa Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, ulinzi katika nchi yoyote ni jambo la muhimu sana maana hizo nchi zinazosifika kwa amani na usalama tukiacha kando ule uvamizi wa kigaidi, basi huwa wa ulinzi imara katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima Serikali yetu itilie maanani sana juu ya suala zima la ulinzi. Hii ni pamoja na kuweka mazingira mazuri kwa wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Spika, wahenga walisema kwamba kama unataka amani, basi jiandae kwa vita. Suala la jeshi letu kuandaliwa kimaadili, kiuwezo, utayari na uimara wa hali zotre ni suala la msingi sana maana jeshi lililoandaliwa vyema kuwa na nidhamu na maadili mema na hivyo kuwa tayari kupokea na kutii amri yoyote inayotolewa na nchi yao.

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu uliopo sasa nchini petu, usitufanye tubweteke na kuona kwamba hali hii itaendelea kudumu milele. Ni wakati sasa Serikali kuimarisha ulinzi wa mipakani mwa nchi yetu na nchi za jirani kwa umakini sana bila

kutoa mwanya hata mdogo maana hatujui ni lini hali ya usalama inaweza kubadili. Kwa hivyo, hatuna budi muda wote tuwe-*standby.*

Mheshimiwa Spika, wastaafu wa jeshi letu ni watu muhimu sana katika nchi yetu. Kumekuwa na malalamiko mengi sana kuhusiana na stahili za wastaafu wa jeshi letu. Baadhi ya malalamiko ni kwamba wanajeshi wetu wanapostaafu huwa wanacheleweshewa stahili zao kwa muda mrefu sana kiasi kwamba wakati wengine wanakata tamaa.

Mheshimiwa Spika, tunayo mifano hai ya wastaafu wa jeshi ambao wamecheleweshewa stahili zao kwa zaidi ya miaka nane au kumi hivi. Hivi kuna sababu zipi za msingi zinazopelekea kufikia hali hii? Ni wakati sasa Wizara (Serikali) ieleze bayana hivi ni kwa nini wastaafu hawapewi stahili zao kwa wakati muafaka?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Serikali imeshaahidi kuwapatia wanajeshi na walinzi wengine mishahara mizuri, hapana budi Serikali iangalie tena uwezekano wa kuwaongezea marupurupu na stahili nyingine na muhimu katika hili ni utekelezaji wa yote ambayo kwa ujumla wake yataboresha maslahi ya wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira ni haki ya kila raia katika nchi yake. Kama ni hivyo basi, ajira popote pale yaani katika Idara, Wizara na Serikali ni lazima zaidi izingatie vigezo maalum kuliko kuangalia kigezo cha itikadi ya siasa kama inavyofanyika kule Visiwani, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ni vyema suala hili la ajira wasipewe mashehe dhamana ya kuwatafuta au kuwasaili vijana wanaotaka kujiunga na jeshi kama inavyofanyika Zanzibar na hasa Kisiwani Pemba. Ahsante sana.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimpongeze Waziri Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Naibu wake na Katibu Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo inaeleweka.

Mimi nikiwa Mbunge wa Kilombero, tuna kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa ya Chita. Madhumuni ya Kambi hiyo pamoja na mafunzo ya Kijeshi, yalikuwa kutoa mafunzo ya kilimo na kuwekeza kwenye kilimo cha mazao mbalimbali kama mpunga, mahindi, soya, migomba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hali ya uhusiano kati ya askari wa JKT Chita na wananchi wanaopakana nao katika vijiji vya Ikule na Chita kijijini siyo nzuri kwa muda mrefu. Chimbuko la matatizo lilitokana na jeshi kujiongezea eneo kwa kujipanulia mipaka na kubadili ramani ya awali bila kuwashirikisha wananchi na wengine kunyang'anywa maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, JKT Chita ni kambi ya Kilimo, ni mategemeo yangu kwamba jeshi hilo lingekuwa na uhusiano mzuri na wananchi, ili kama kuna uwezekano wa

kupata wawekezaji wa aina yoyote, wananchi waweze kunufaika na jeshi kuwa katika maeneo hayo, ndiyo nia ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba vijana wetu wa JKT Chita wapatiwe elimu ya siasa, ili kuelewa uhusiano wao na wananchi wanaowazunguka. Mimi mwenyewe kama Mbunge na baada ya kupata malalamiko yanayohusu ardhi, nilijaribu mara mbili kuomba kuonana na *Chief of National Service* pale Mlalakuwa bila mafanikio. Kwa vile moja ya mikakati ambayo imepangwa kutekelezwa mwaka huu wa fedha 2006/2007 ni kuendelea na upimaji wa maeneo ya JKT na Jeshi na kuyapatia Hatimiliki pamoja na kuendeleza taratibu za kulipa fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao kwa ajili ya shughuli za Jeshi na JKT.

Naomba shughuli hii itakapokuwa inatekelezwa JKT Chita, wananchi wa Chita na Ikule kwa maana ya Serikali za vijiji hivyo na vitongoji vyake washirikishwe ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni katika mwezi wa Julai, 2006, kule Chita, katika kijiji cha Chita, yametokea matukio mengi ya kupigwa na kuporwa mali wananchi wa kijiji cha Chita. Vitendo hivi vimefanywa na vijana wa Jeshi JKT Chita, katika tarehe 02 Julai, 2006, 07 Julai, 2006, 12 Julai, 2006, 15 Julai, 2006, 28 Julai, 2006 na tarehe 29 Julai, 2006.

Mheshimiwa Spika, katika matukio hayo mali kadhaa za wananchi ziliporwa na wanajeshi hao zikiwa na thamani ya shilingi 1,634,850/= na fedha taslimu shilingi 860,500/=. Jumla kuu ya mali na fedha na shilingi 2,495,350/=.

Mheshimiwa Spika, ombi na maoni, JKT ni mahali pa kujifunza na kutekeleza nidhamu. Msingi mkubwa wa kumjenga askari mzuri ni uadilifu, nidhamu, utii na ukakamavu. Ndiyo ilivyokuwa kwa JKT ya m iaka ya 1970 na 1980 wakati wetu baada ya kumaliza masomo ya kidato cha sita, ambapo tuliingia jeshi kwa mujibu wa sheria.

Naomba uongozi wa jeshi usisikilize upande mmoja, bali iunde Tume baada ya Bunge hili la bajeti, ili wananchi wakasikilizwe na viongozi wa kijiji wakasikilizwe pamoja na viongozi wa Jeshi waliokuwepo wakati wa matukio hayo niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa kutokana na taarifa iliyoletwa kwangu na Diwani wa Kata ya Chita Mheshimiwa John John Chelele, ni mbaya sana. Baadhi ya wananchi wameanza kuandaa silaha zao za jadi ili waweze kujilinda. Kwa nini tufike hapo? Kwa nini watu ambao wangeweza kufaidika na madhumuni ya kuweka kambi ile pale leo waone ni balaa kuwa na Kambi ya Jeshi Chita?

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo ya mahusiano mabaya, ni dhahiri uwekezaji utakuwa mgumu, kwani chuki baina ya makundi hayo mawili yanaweza yakazaa hujuma ya malengo mazuri yatakayowekwa.

**MHE. BAHATI ALI ABEID :** Mheshimiwa Spika, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wao ambao wameshiriki kuandaa hotuba

hii nzuri yenye kuwapa Watanzania matumaini ya kuishi bila hofu na maendeleo ya vijana yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna wastaafu wa Jeshi letu ambao walikuwa ni askari wadogo wanacheleweshwa sana kupewa kiinua mgongo chao hivyo hupelekea kupata matatizo makubwa yakukabiliana na maisha, kwa hiyo naiomba Serikali kuwa askari kabla hajastaafu aweze kufanyiwa taratibu zote zinazohitajika ili akistaafu aweze kupatiwa mafao yake bila usumbufu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ajira ya jeshi hili wana ajiriwa vijana waliomaliza kidato cha nne na kuendelea na kwa kuwa Serikali inajua kuwa kuna vijana wengi hawana ajira na wamemaliza darasa la saba kwa Bara na darasa la kumi kwa Zanzibar hata kama wakiajiri hawatapewa cheo lakini wanaweza kulinda Taifa lao kwa uzalendo mkubwa. Naiomba Serikali kuwa iwape nafasi vijana wetu hawa ili na wao waweze kuchanganyika na hao wasomi na wao wapate ajira.

Mheshimiwa Spika, mipaka ni kweli wanajeshi wetu wana jitahidi za kulinda mipaka yetu kwa jitihada kubwa lakini naomba wazidishe ulinzi ili wale wanaotaka kujaribu kuingia hata kufanya uhalifu wa ujambazi isiwezekane.

Mheshimiwa Spika, JKT hutoa mafunzo kwa vijana wetu kama vile ukakamavu, ulinzi, uzalendo,ufundi stadi, kilimo, ufugaji bora na uvuvi. Lakini vijana hawa wakishapata mafunzo haya wakimaliza wanarudi vile vile kwenye unyonge kwani wakimaliza mafunzo haya hakuna Serikali wala Taasisi yeyote inayowapa angalau mtaji au mikopo vijana hawa wakaweza kuendelea na yale mafunzo waliyoyapata, kwa hiyo, naiomba Serikali baada ya kuwapa mafunzo vijana hawa basi waajiriwe kwenye jeshi la wananchi wa Tanzania au JKT iwaajiri ili waweze kufanya hizi shughuli za uzalishaji mali majeshini kuliko kuwa wamefundishwa ukakamavu halafu wakaachwa wanazurura tu tutakuja kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, naomba niiunge mkono hotuba hii mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie ifuatavyo:-

Je, Wizara ina mpango wowote wa kuhifadhi maeneo muhimu yaliyotumika wakati wa vita dhidi ya majeshi ya uvamizi mwaka 1978/1979. Mengi ya maeneo hayo yalitumika kama *Holding Camps,* Ngome, *Division Headquarters* na kadhalika. Hoja yangu yajengewe *monuments* kwa kumbukumbu ya vizazi vijazo, maeneo hayo ni kama yafuatayo:-

(i) 14KJ kama kambi ya mapokezi kujiaandaa kwenda *Front-Line,*

(ii) Shinyanga kama *Holding Camp;*

(iii) Nyakibimbili -Katoro, MM ya *Division* kabla ya kuvuka mpaka;

(iv) Daraja la Kyaka lililobomolewa na majeshi ya maadui;

(v) Mutukula, sehemu gari la wahandisi lililipuka mabomu yaliyokuwa yamebebwa na kuua askari wetu;

(vi) Nyakanyasi baada ya kuvuka mpaka kikundi chetu cha wapiganaji kilikuwa *ambushed* na askari wetu takribani 14 waliuawa;

(vii) Bunena ambako ilikuwa *Mess* ya Makamanda wa juu walipofikia kabla ya kuendelea mpakani;

(viii) Rwamishenye – kama *Bn Svc;* na

(ix) Gereza la Rwamlumba lililotumika kuwahifadhi mateka.

Mheshimiwa Spika, miaka ya 1970 kulikuwa na mpango wa kutoa mafunzo ya uafisa *cadet* kutoka kwenye Chama Tawala au kutoka kwenye vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama. Lengo ilikuwa kutoa elimu ya kijeshi, faida yake tuliiona wakati wa vita. Wengi wao kama maafisa *Platoon Commanders* na *Staff Officers* kwenye MM ya Brigedi na *Division.* Nashauri utaratibu huu urejeshwe ili kuwa na maafisa wenye ujuzi wa mbinu za kijeshi *(military knowledge)* ambao watakuwa kwenye Jeshi la Akiba *(Reserve).*

Mheshimiwa Spika, maafisa wastaafu wanadhalilika sana mara baada ya kustaafu. Badala yake wanaishia kwenye makampuni ya ulinzi. Nashauri Wizara ifikirie kuwawekea utaratibu utakaowasaidi wasidhalilike.
Naunga mkono hoja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali George Waitara, Mnadhimi Mkuu mpya wa Jeshi la Wananchi, Luteni Jenerali Davis Adolf Mwamunyange, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Abdulrahaman Shimbo, Makamanda na watumishi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri sana. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi ni mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, sina mengi ya kuongeza kwenye taarifa ya Kamati ambayo imetoa ushauri na mapendekezo mazuri, yangu ni machache.

Natoa ushauri kwa Serikali kuharakisha utekelezaji wa ahadi yake ya Kujenga Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa kule Burigi, Muleba. Wananchi wa Muleba na Kagera kwa ujumla wanasubiri kwa shauku kubwa uanzishwaji wa Kambi hiyo ya Burigi. Tunaishukuru Serikali kwa kutuma maofisa wa Jeshi la Kujenga Taifa kukagua eneo hilo na kuridhika nalo. Kambi hiyo itaongeza usalama katika eneo hilo na kuwapa vijana mafunzo ya uzalendo na ulinzi ili waweze kulinda nchi yetu na kujitegemea pia.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuishukuru Serikali kufuatia hatua ya kuboredha maslahi ya askari. Lakini bado kazi ni kubwa. Bunge lina wajibu wa kuchukua hatua maalum kuunga mkono hatua za Mheshimiwa Rais ili bajeti ya ulinzi iboreshwe kadri mapato ya Serikali yanavyoongezeka.

Aidha namwombea Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Abel W. Mwaisumo, apone haraka maradhi yanayomsumbua ili aweze kurejea na kutekeleza majukumu yake. Naomba Mwenyezi Mungu amsaidie.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja tena.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vyema kabisa nimwombe Mwenyezi Mungu anipe uwezo nami nichangie katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naanza kutoa mchango wangu. Kwa kuwa nchi yetu imepakana na nchi nyingine ni kwamba tunaulazima wa kulinda mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, vijana wa Kitanzania ambao wameibeba nchi yetu ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Watanzania hawa ndio nuru ya nchi yetu kwani kuwepo usalama kunatokana na vijana wetu hao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa Wizara hii, pamoja na Serikali kutoa kipaumbele Wizara hii, bado vijana wetu wa Jeshi la Tanzania haki zao za msingi hawazipati ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kujua umuhimu wa vijana wetu wa Jeshi la Wananchi, imetoa changamoto kwa wanajeshi wetu utahafifu wa matumizi pale ambao watakuwa Mipakani ama *operation.*

Mheshimwa Spika, la kusitisha sana agizo hili limeachwa kiasi ambacho wanajeshi wetu wanapokuwa Mipakani ama *operation* hulazimika kutumia fedha zao mifukoni. Hili zaidi huwafikia wale wanajeshi wetu wa cheo cha chini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa nini haki hii ya msingi kwa vijana wetu huwaondolea? Kama haikuiondoa, ni utaratibu gani Serikali inayoutumia kwa kujua haki zao zinawafikia walengwa?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, wanajeshi hupatiwa motisha katika kambi zao, kama vile bia, soda na kadhalika kwa bei nafuu. Haki hii vijana wetu haiwafikii na matokeo yake ni faraja kwa wachache. Serikali ni vyema itoe haki kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii ni ya Muungano, ni lini basi Kiongozi Mkuu wa Jeshi atatoka Zanzibar? Ni vyema sasa Zanzibar nayo ikaonja ladha na cheo hiki.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tuna sababu za kutosha ya kujua umuhimu wa wanajeshi wetu. Pamoja na kulinda mipaka, lakini ni mara nyingi hunusuru maisha ya

wananchi wetu. Ni karibuni tu mgomo wa madaktari katika hospitali za Muhimbili na *KCMC,* ni wanajeshi ndio walookoa jahazi hilo na katika uvunjikaji wa madaraja wajenzi ni wanajeshi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iache yake yote iwaangalie wanajeshi.

Mheshimiwa Spika, raia yeyote aliyeamua kujiunga na JWTZ hupata heshima kubwa pale ambapo atakuwa ni mwanajeshi.

MheshimiwaSpika, la kusikitisha mwanajeshi anapofikia kustaafu Serikali haimjali tena kijana huyo. Hakuna sababu ya mtu kufikia cheo kikubwa katika Jeshi anapostaafu akawa mlinzi katika nyumba ya bwana. Hii ni dosari! Si udhalilishaji. Ni vyema Serikali iandae mpango mzuri wa maisha ya wanajeshi wetu wakati wanapostaafu. Pia na kuwapatia kiinua mgongo kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpangilio wa wanajeshi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, katika Zanzibar kuna Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) na Tanzania Bara kuna Jeshi la Kujenga Taifa. Nchi yetu ni ya Muungano, inakuwaje nchi moja kuwa na utofauti wa majeshi? Ni vyema sasa Serikali iandae mipango mizuri juu ya wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Spika, nalitakia jeshi maisha mema.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, ili kuepuka migogoro inayotokea kati ya Jeshi la Wananchi na raia, ni vyema Serikali ikafikiria kurudisha somo la Uraia Jeshini ili lisaidie kuelimisha askari kuwa kazi yao ni kuwalinda wananchi na sio kupambana nao.

Mheshimiwa Spika, linapotokea tatizo, utaratibu maalum utumike ili kushughulikia tatizo hilo na sio kuchukua uamuzi wa kupambana nao. Kupambana nao yaani kupambana raia ni kupoteza imani ya wananchi kwa Jeshi lao. Somo la uraia si somo la siasa ni somo la kujaza uzalendo.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 42 wa kitabu cha hotuba ya bajeti kuna kipengele cha saba, mipango ya utekelezaji ya mwaka 2006/2007, kipengele hiki kinaelezea kuendelea na upimaji wa maeneo ya Jeshi na JKT na kuyapatia hatimiliki yake pamoja na kuendeleza taratibu za kulipa fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao kwa ajili ya shughuli za Jeshi la Ulinzi na JKT. Naomba kipengele hiki kifahamike kwa wananchi na wanajeshi wenyewe ili kuondoa migogoro ya kugombania mipaka na inapotokea tatizo hili anayeathirika ni raia maana raia humwogopa askari na askari hutumia uwezo wake wa kijeshi kuchukua maeneo ya wananchi kwa kisingizio kuwa wanalinda usalama.

Mheshimiwa Spika, mfano ni mimi mwenyewe nimefungiwa barabara inayokwenda katika nyumba yangu kwa kisingizio cha usalama wa eneo la jeshi na wakati huo huo Ofisi ya Ardhi Wilayani yenye mamlaka ya kugawa ardhi, inasema kuwa lile eneo si la jeshi kwa mujibu wa ramani ya Mji wa Masasi, lakini kwa kuwa jeshi lina

nguvu ile barabara mpaka leo imefungwa pamoja na juhudi zote za uongozi wa Wilaya lakini askari hawataki kufungua barabara. Naomba msaada wako.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwanza kuhusu kuwaenzi wastaafu wa Jeshi. Serikali tunaomba iwaangalie wastaafu wetu wa Jeshi mara wanapostaafu, kuwaweka pamoja kiushirika na kufanya miradi mbalimbali na Serikali kuwapatia mtaji, hali hii itawaongezea imani ya nchi yao na kuendelea kuishi kwa matumaini.

Pili, Serikali iwapatie fidia/msaada wa kuwaendeshea maisha askari na familia zao, wale askari waliopata ulemavu wa maisha na kutoweza kujitegemea kutokana na kushiriki katika vita nje ya nchi yetu.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza hotuba hii kwa ajili ya utayarishwaji wake mzuri, kwa hiyo, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wake kwa ushirikiano wao mazuri pamoja na Makamanda na askari wote. Napenda kuunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja kwa upande wa nyumba za askari. Kwa heshima kubwa napenda kuishukuru Serikali kwa kuwajengea nyumba mia moja kwa Kikosi cha Jeshi cha 14KJ katika Jimbo la Wawi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu naiomba iendelee kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari. Kwa sababu askari kukaa uraiani si vizuri, ni vyema wakae *camps* kwenye nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia upande wa askari wenyewe, naomba kuuliza suala la ndoa kwa askari wa kiume na kike. Kwa nini askari wa kiume anapooa uraiani anakubalika kukaa na mke wake kambini *(Camp)* lakini askari wanawake wanapoolewa uraiani hawaruhusiwa kukaa na waume zao (raia) katika *camps?* Suali hili si haki.

Mheshimiwa Spika, napendekeza askari wa kike na askari wa kiume wakati wanapofunga ndoa na raia basi wasibaguliwe wote wakae pamoja katika *camp.*

Mheshimiwa Spika, suali la mwisho la kuchangia ni suala la mshahara wa askari. Naomba mishahara ya askari iongezwe kwa sababu mishahara bado ni midogo na hailingani na matumizi katika maisha ya leo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia moa moja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, Kambi ya Lugalo ijengwe vizuri Kambi hiyo ina majumba ya mabati yenye umri mkubwa zaidi ya Uhuru wetu. Mabanda haya yananikera na ni aibu hasa pale kuota *quarter guard* wanapokaa *military police.* Tutafute pesa tujenge majengo ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Meremeta ni ya nani na ina maendeleo gani mpaka sasa hivi maana inashindwa kulipa mishahara.

Mheshimiwa Spika, pale *Kunduchi Rifle Range* ni katikati ya makazi ya watu lakini jeshi wanaendelea kulenga shabaha pale je, ni lini wanajeshi wataondoka sehemu hiyo?

Mheshimiwa Spika, iliandikwa kwenye magazeti kwamba *radar* ya jeshi iliibiwa. Naomba maelezo kuhusu hilo.

Mheshimiwa Spika, wanajeshi wakafanye mazoezi kwenye mapori ya Kigoma, Shinyanga, Bukoba ambapo majambazi wanajificha ili wawatokomeze kabisa.

**MHE USSI AME PANDU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Naibu Waziri kwa kuchaguliwa kwao na Mheshimiwa Rais kuwa wao ndio viongozi wa Wizara hii, ni dalili tosha kwamba uwezo waliokuwa nao ndio uliomfanya Mheshimiwa Rais kuwateua.

Mheshimiwa Spika, pia nataka kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni Zanzibar kwa kunichagua kwa kura nyingi na mimi naahidi kuwatumikia kwa nguvu zangu zote.

Mheshimiwa Spika, nikianza kuchangia hoja ya Wizara hii kwanza nataka kuipongeza Wizara hii kwa juhudi zake kubwa za kulilinda Taifa hili mipakani nje na ndani na kuwapatia ulinzi Watanzaia wote usalama wa kuishi pamoja na mali zao.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye hospitali za majeshi naomba nizipongeza sana hospitali hizi kwa jinsi zinavyosaidia wanajeshi pamoja na raia wanaoishi maeneo ya karibu, hivyo natoa wito kwa Wizara hii ipatiwe nyezo ili iweze kuzidisha kasi za kutoa huduma hiyo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ili wanajeshi wetu wawe na hamu ya kazi yao hawana budi kupatiwa nyumba za kuishi. Jambo la kusikitisha kuna baadhi ya Kambi toka nyumba zilipoanza kujengwa wakati wa ukoloni mpaka leo hazijaendelezwa, hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa kujibu hoja anieleze kupitia bunge hili ni lini upanuzi wa majengo kwa wanajeshi wa kambi ya Mtoni, Zanzibar utashughulikiwa?

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niipongeze Wizara hii kwa ya pili na naunga mkono hoja kwa asilimia zote.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Waziri wa Ulinzi na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, pamoja na viongozi na Makamanda wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha

ulinzi na amani ya Tanzania kwa Watanzania kuwa ya uhakika zaidi na kupelekea nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi zenye amani na utulivu duniani. Mungu ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kuwasilisha kilio cha wananchi wa Jimbo la Kigamboni hasa wa Kata ya Somangila, Kata ya Kimbiji, Kata ya Pemba Mnazi na Kata ya Kisarawe II. Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limechukua maeneo ya mashamba ya wananchi wa Kata hizo kwa madhumuni ya kutumia maeneo hayo kwa kuanza mafunzo ya kijeshi. Eneo hilo JWTZ wameshalipima rasmi na kuwa chini ya miliki ya JWTZ. Pamoja na eneo hili kupimwa rasmi na kumilikiwa rasmi na JWTZ kwa masikitiko makubwa wananchi hawajalipwa fidia ya mashamba yao kusababisha kuwaongezea umaskini badala ya kupata maisha bora (kauli mbiu ya Serikali ya awamu ya nne).

Mheshimiwa Spika, nasikitika pamoja na kumuandikia rasmi barua ya malalamiko ya wananchi hao wa Kata hizo Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, mpaka leo hatujapata jawabu na mtazamo wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Tunaomba tujibiwe rasmi juu ya fidia ya eneo hilo. Lini Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi itawalipa fidia ya mashamba wananchi wa Kata hizo za Somangila, Kimbiji, Pemba Mnazi na Kisarawe II. Nakuomba Waziri uwatembelee wananchi wa eneo hilo na kuwafariji. Aidha, Jeshi la Kujenga Taifa linaendelea kumega maeneo ya wananchi huko katika Kata ya Kimbiji kinyume na makubaliano ya maeneo ya awali. Je, hilo Wizara inalielewa?

Mheshimiwa Spika, nashauri uongozi wa Wizara na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa kutembelea eneo hilo pia kuonana na wananchi kuzungumzia migogoro ya ardhi iliyopo.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi zangu kwa Waziri, Naibu Waziri, watendaji wote wa Wizara pamoja na Makamanda na askari wote chini ya uongozi wa Jenerali Geroge Waitara.

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi zinazoendelea kwa madhumuni ya kuwaweka askari wetu wote makambini. Lakini kuna haja ya kuongeza kasi ya kujenga nyumba nyingi za askari.

Kwa mfano, Kambi ya Milambo, Tabora imechakaa sana. Kwa hiyo, inahitaji matengenezo makubwa. Kambi ya Rada, Tabora, nyumba zake ni za hali ya chini sana. Nyumba zimejengwa kwa matofali ya udongo bila plasta. Kuna haja ya kuzijenga upya kwa zana za kisasa kama vile *cement* na rangi nzuri. *NSSF* iko tayari kusaidia ikiwa Wizara itaingia katika mkataba maalum kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nyingi za wanajeshi.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuiboresha na kuiwekea vifaa vya kisasa vya kupimia maradhi mbalimbali hospitali ya *Milambo Barracks,* Tabora.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zana za kijeshi, ili kuimarisha jeshi letu kuna haja ya kulipatia zana nyingi za kisasa kuanzia ardhini, majini na angani.

Mheshimiwa Spika kuhusu mafunzo, kutokana na haja ya kuwa na zana za kisasa za kijeshi, ni lazima kuwe na mfumo wa mafunzo kwa askari wetu ili kuweza kuzimudu zana zetu za kisasa katika majeshi yetu ya ulinzi.

Mheshimiwa Spika aidha, naipongeza Wizara kwa kuwa na utaratibu wa kuwaelimisha askari wake elimu ya sekondari ndani ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kiwanja cha ndege cha Tabora, kutokana na umuhimu wa kiwanja hiki kwa matumizi ya kijeshi na kwa hiyo, kwa ajili ya ulinzi wa nchi yetu, napendekeza Serikali ikipe kiwanja hiki umuhimu wa juu ili kulingana na jukumu hili la ulinzi. Aidha, jeshi lipewe nafasi maalum katika uwanja huo kwa ajili ya matumizi ya kiulinzi pamoja na kuegesha ndege za kivita.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema na kuniwezesha kuchangia hutuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote walioshirikiana na Waziri kwa kutayarisha hotuba hii ambayo ni nzuri na yenye matumaini kwa ulinzi wa nchi yetu. Kutokana na hutuba ya Waziri kumaliza kila kitu naomba kuchangia kidogo katika ajira. Kidogo sijaridhika na utaratibu unaotumika katika ajira ya kuajiri vijana waliomaliza darasa na kumi na mbili na kuendelea na kuwaacha wale waliomaliza darasa la saba kwa Tanzania Bara na darasa la kumi kwa Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu naomba uachwe kwani naona ni wa kibaguzi ambao hauwatendei haki wale wa darasa la saba na darasa la kumi kwa sababu kutokuendelea na masomo kuwa ndio sababu ya kuwa hawawezi kufanya kazi katika vikosi vyetu vya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, vijana hawa ni wengi sana wameenea mitaani na hawajui wafanye nini na mwisho kwa kuwa hawana na la kufanya hujiingiza na vitendo vya uhuni na wizi.

Mheshimiwa Spika, kushindwa kuendelea na masomo si kigezo cha kuwa hawana akili, lakini wameshindwa kutokana na hali ya mazingira na umaskini uliokithiri, lakini vijana hawa wamo wenye akili kama wanasomeshwa watakuwa wazuri kuliko hao wanaotajiriwa, naiomba Serikali kupitia Wizara hii na katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kutimiza ajira 1,000,000 na wakati macho ya Watanzania ya kutimiza ajira hizo yako katika vikosi vya ulinzi ambavyo huchukua vijana wengi kwa mkupuo, Wizara wawaangalie kwa jicho la huruma kuwaajiri vijana hawa katika vikosi vyetu.

Mheshimiwa Spika, vijana hawa tukiwaajiri pia ile dhana ya kupunguza umaskini itapatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa umahili wa viongozi waliochaguliwa kuiongoza Wizara hii naamini wataishauri Serikali katika kutekeleza wazo langu. Ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Spika, *Inshallah* Mwenyezi Mungu aniwezeshe kuchangia katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa naomba kutoa mchango wangu katika Wizara hii. Jeshi la Wananchi wa Tanzania limebeba imani ya nchi yetu pamoja na wananchi wake na mali zao kuishi katika amani ya nchi yetu. Hivyo basi Serikali yapaswa kujua umuhimu wa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, haki ya wanajeshi katika nchi yetu inabezwa sana kumpeleka askari mipakani ama *operation* ni majukumu ya Serikali. Kazi ya Serikali ni kumlisha askari huyu. La kushangaza askari anapopelekwa huko hujihudumia mwenyewe, hii si haki. Kufanya hivyo ni kumwonea askari huyo. Wanajeshi kambini mwao hupewa bei nafuu kwa baadhi ya mahitaji yao, kama vile soda na bia. Mara nyingi sasa vitu hivi wahusika hawafaidiki. Serikali yapaswa sasa haki hii iwasimamie wale wadogo ambao cheo ama vyeo vyao vidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara ya wanajeshi inaonesha wazi askari wetu wanashida kubwa sana jambo ambalo limepelekea askari wetu baadhi kujishughulisha na ujambazi. Kunusuru hili ni kuwaondolea matatizo vijana wetu, ili waepukane na kujishughulisha na vitendo viovu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wastaafu katika jeshi letu, baya ya hili ni pale mwanajeshi huyu anapostaafu akawa ni mlinzi wa nyumba ya bwana. Hii si haki, kwa nini wastaafu wetu tusiwahudumie. Haki ya mstaafu iko mbali katika Wizara yetu hii. Hakuna sababu ya usumbufu wanayopewa wastaafu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makazi ya askari wetu sio mazuri, jambo ambalo inaonekana kutokana na kazi ngumu za vijana wetu hawa huishi katika nyumba mbaya. Wanajeshi wameweza kutuokoa na maisha yetu, pale ambapo madaktari wetu walipogoma. Umhimu ni mkubwa mno. Ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa wanajeshi wetu.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote natamka rasmi kuwa naunga hoja ya Wizara mkono.

Pamoja na kuiafiki hoja hii, napenda nibainishe wazi kuwa yapo mambo machache ambayo nitapenda kuchangia na katika kufanya hivyo niombe Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho niweze kupatiwa majibu mambo hayo ni pamoja na:-

Ulinzi katika Mpaka wa Kigoma na huduma ya chakula kwa wapiganaji. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma, hususani wale wa Kigoma Kusini, natoa shukrani za dhati kwa Serikali kwa ujumla na JWTZ mahsusi kwa ulinzi unaoendeshwa na wapiganaji wetu eneo la mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Vipo vikundi vya askari upande wa jimbo la Kigoma Kusini (mwambao wa Ziwa) ambavyo vimekuwa vinajulikana kama *detache* za jeshi. Vikundi hivi vimekuwa vinafanya kazi nzuri ya ulinzi wa raia na mali zao badala ya polisi na kupambana na maharamia ambao wengi wao ni askari wa jeshi la *DRC* ambao wako upande wa Tanzania na kuwapora wavuvi zana na nyenzo za uvuzi ikiwemo mitumbwi, makarabai, nyavu na *engine* za kusukuma mitumbwi.

Kutokana na ulinzi *(patrol)* inayofanywa na *detache* hizi hasa katika Kata za Sumuka, eneo la Lugengela na Karago, Kata ya Sigunga, Kata ya Igalula/Bulugu na Kata ya Kalya, nathubutu kusema kuwa wavuvi sasa kwa takriban mwaka na nusu wamekuwa wanavua kwa amani. Bahati mbaya ni kwamba zipo kasoro mbili ambazo ni:-

(a) Hawana *patrol boats,* badala yake wanatumia mitumbwi ya kawaida ya wavuvi ambayo haina kasi ya kuwashinda wahalifu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ihakikishe inasaidiana Wizara ya Usalama wa Raia kupata *patrol boats* kama tatu kwa nia ya kuwadhibiti maharamia.

Kuhusu chakula cha askari, mara nyingi askari hutaka wapatiwe chakula toka kwa wanavijiji katika maeneo niliyoyataja hapo juu na ambapo *detache* hizi zipo. Ningependa kufahamu kama huo ni utaratibu sahihi. Hivi jeshi halina utaratibu

mahsusi wa kuwezesha askari kupatiwa chakula ama kutoka katika kasma ya jeshi au kutoka katika mishahara ya askari hao? Naomba nipate ufafanuzi kwa hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya ndege ya jeshi kusafirisha viongozi, mapema mwaka huu kuliibuka taarifa katika magazeti ambayo iliandikwa kwa ushabiki mkubwa sana pale Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi alipotumia ndege ya jeshi kuelekea Tabora, jimboni kwake. Nijuavyo mimi Mheshimiwa Waziri alikuwa bado ni muda mfupi madarakani hivyo hakuwa likizo bali alikwenda kikazi. Hivi kulikuwa kosa gani kwake kutumia ndege hiyo ya jeshi kwenda Tabora ambako kwa bahati na jimbo lake lipo huko? Kama sikosei katika jeshi la polisi viongozi wamekuwa wakitumia ndege au helkopta ya polisi. Kuna tatizo gani kwa Waziri kutumia ndege ya jeshi? Nitaomba nipate ufafanuzi wa hili maana napata picha kwamba vyombo vya habari havikumtendea haki Waziri wetu na huenda vilielekezwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpaka wa Tanzania na Kenya, nimefarijika kusoma katika hotuba ya Wizara kuhusu swala hili. Hata hivyo nashauri lishughulikiwa haraka kwani kwa uzoefu wangu nikiwa mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama mkoani Tanga (Kama Mkuu wa Wilaya ya Handeni) suala hili tumelizungumza sana lakini utekelezaji ni kuwa duni.

Mheshimiwa Spika, mgao wa vijana JKT kimkoa, nalipongeza jeshi kwa kurejesha mafunzo ya JKT na hivyo kuwezesha vijana kupata stadi za kazi/maisha. Hata hivyo nashauri kuwe na mgao wa uwiano wa haki kimkoa. Sio baadhi wanapata nafasi nyingi kuliko wengine. Aidha, kuwepo na muda wa kutosha kati ya kipindi cha usaili na kuripoti kambini ili wale watakaoshindwa hasa hatua ya vipimo hospitali, uwepo utaratibu wa mikoa husika kuipata fursa ya kujaza nafasi za mgao wao.

Mheshimiwa Spika namalizia kwa kusema tena kuwa naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini, pia nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi na Makamanda wote kwa ushirikiano wao katika kufanikisha hotuba hii.

Maoni na ombi langu ni kuwa kambi ya Mafunzo ya Huduma *(Logistic)* ya Morogoro ina umhimu wa kipekee, ambapo inahitaji mambo yafuatayo:-

(i) Mafuta ya Magari kwa wakati wote kwa ajili ya *operation* za mara kwa mara (mafunzo ya misituni).

(ii) Kutatua tatizo lililopo kwenye chanzo cha maji ambapo kuna muingiliano kati ya wananchi na kambi ya Jeshi. Wananchi waelimishwe athari zinazoweza kutokea wakiwa karibu na makambi ya kijeshi na kwa upande wa Jeshi, makambi yote yawekewe *fence* au wapande miti kuzunguka eneo lote ili kuepuka matatizo kama hayo.

(ii) Mabwalo yote ya maofisa na askari yaboreshwe, yafanane na hadhi ya mwanajeshi yakiwamo mabwalo ya Chuo cha Mafunzo ya Huduma *(Logistic)* Morogoro, Bwalo la Pemba, Lugalo Dar es Salaam (Maofisa + Askari) na mengine mengi hapa nchini ambayo ni mabovu sana.

Mheshimiwa Spika, nyumba za maofisa Lugalo ambazo zimegeuka mahame ziboreshwe pia zijengwe nyumba za askari makapera na askari wa kawaida. Pia askari wapatiwe usafiri kuepuka usumbufu wanaopata hivi sasa pia kuepuka kuwadhalilisha kwa kuomba *lift* kwa watu binafsi barabarani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kikosi cha Nyumbu kipatiwe fungu la kutosha ili kikidhi haja na pia ma-*engineer* wawe na kazi za kuzalisha maana wana ujuzi wa kutosha wa kutengeneza vipuri mbalimbali. Pia kikosi hiki kina teknolojia ya hali ya juu. JKT pamoja na mafunzo ya nidhamu na ukakamavu itumike kuwafunza ujasiriamali vijana sambamba na mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa lengo la kutengeneza ajira kwa vijana mara wamalizapo mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Spika, kikosi cha *Navy,* Kigamboni kinakabiliwa na matatizo mengi yakiwemo upungufu wa mafuta kwa ajili ya *operation,* upungufu wa askari wazamiaji, upungufu wa boti za doria, meli kubwa ambayo itasaidia kuzuia uhalifu unaofanywa na

meli za uvuvi za kigeni ambazo huvua samaki wetu bila malipo kisha hutoweka bila kuulizwa na mtu yeyote kutokana na kutokuwepo na meli kubwa ambayo inaweza kwenda kwenye kina kirefu. Kwa kukosa meli hiyo rasilimali za nchi yetu au mazao ya samaki yanavunwa na Serikali inakosa mapato mengi ambayo yangesaidia kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kikosi cha Anga kipatiwe Rada mbili zaidi ambazo zitaweza kukidhi haja kwa kuona kila pembe ya nchi yetu. Iliyopo hivi sasa haifiki mbali na ni hatari sana kwa usalama wa nchi. Kikosi pia kina upungufu wa askari na maofisa.

Mheshimiwa Spika, maduka yanayotoa huduma katika makambi ya Jeshi yanauza bidhaa kwa bei ya juu kama maduka ya Kariakoo. Naomba suala hili litatuliwe. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia machache tu ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ukubwa wa Jeshi lote la Wananchi wa Tanzania kwa idadi. Ni asilimia ngapi ya JWTZ ambao huwa hawana kazi za kufanya, kipindi chote ambacho hakuna vita? Na ni miradi gani inafanywa na Wizara hii ili kuboresha hali ya Uchumi wa wanajeshi?

Mheshimiwa Spika, ushauri, ni vyema jeshi libuni miradi mbalimbali hasa ya kilimo kwa mazao mbalimbali ili kuongeza kipato ambacho kitatumika kutoa motisha mbalimbali kwa watumishi wa Jeshi.

Mheshimiwa Spika, suala la usafiri wa wanajeshi (askari) limekuwa ni kero sana kwao, hata mara nyingine wamekuwa wakidhalilishwa na wenye magari, hasa kwa mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na kadhalika kwa sasabu wanapanda bure bila kutoa nauli. Naiomba Wizara iweke utaratibu wa kuwalipa askari fedha ya nauli kupitia mishahara yao, ili kuepuka mateso hayo na hata wakati mwingine ugomvi wa makondakta na askari hutokea.

Suala la askari kustaafu wakati wakiwa na umri mdogo, linatoa mwanya kwa wasio wavumilivu, kujiingiza katika masuala ya ujambazi. Muda uongezwe wa kuwa kazini, nashauri ufuatwe utaratibu kama wa Serikalini. Pia wanapotoka kazini, wengine huenda kuajiriwa katika nchi zingine.

Mheshimiwa Spika, naomba kuelewa Wizara ina utaratibu gani kwa wastaafu (wanajeshi) askari wanaoajiriwa nchi za nje. Je, huko si ni kuuza siri za nchi?.

Kuhusu kambi za jeshi, napenda kujua ni sababu zipi zilizoipelekea Wizara kutokuweka vikosi (kambi) za jeshi katika mkoa wa Singida tangu Uhuru wa nchi hii? Tafadhali nifahamishwe na je, ni kikosi gani sasa kinachohudumia mkoa huo?

Mheshimiwa Spiak, suala la askari kukaa kwenye kambi nje kwa muda mrefu, ni kwa nini? Suala la askari kukaa uraiani, kunawapunguzia hadhi yao na kunawapa

mwanya wa kujijengea ujirani na raia, askari polisi, askari magereza na hivyo kutoa mwanya wa kutetea na kulinda uhalifu kwa kuhofia kuvunja ujirani.

Mheshimiwa Spika, askari anapoajiriwa tu apewe mkopo wa kujenga nyumba mahali apendapo ili iwe *asset* yake mara atakapostaafu asihangaike, ahamie kwenye nyumba yake. Kutokana na uhaba wa madaktari bingwa wa magonjwa mbalimbali na pia *(AMO's)* jeshi kwa kupitia shuguli za jeshi la Ulinzi katika kusaidia mamlaka za kiraia. Zitoe waganga wake ili kusaidia maeneo ambayo hayana waganga kwa kusaidiana na Wizara ya Afya, ili mradi waingie mkataba, iwe ni mojawapo ya mradi.

Mheshimiwa Spika, Wizara itoe mafunzo ya ualimu kwa wanajeshi (vijana wa JKT) ili kuokoa jahazi la upungufu wa walimu na pindi itakapohitaji vijana wake, iwachukue (wakati wa maafa) pia kwa kuingia mkataba na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. ALI HAJI ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza pongezi kwa amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, askari, Makamanda na Mkuu wa Majeshi.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa na JKT, mbali na masuala ya ukakamavu, raia mwema, umoja, uzalendo na ulinzi, kwa maoni yangu naomba stadi na ujuzi mbalimbali ziimarishwe na uzalishaji katika fani mbalimbali uimarishwe na utoaji wa huduma mbalimbali pale inapowezekana. Kwa maoni yangu kufanya hivyo kutapatikana ajira kwa vijana waliopita JKT na kwa upande mwingine mapato ya Serikali yataongezeka na gharama za kikosi hiki zitapungua, ni sehemu ya kutekeleza MKUKUTA na utumiaji mzuri wa nguvu kazi watu.

Naomba ushirikiano kati ya JKT na JKU yaliyopo yaimarishwe na yaendelezwe na wabadilishane ujuzi, ukosefu na mbinu za kupata misaada toka nchi washiriki wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu michezo, JKT inafanya vizuri katika medani ya michezo. Ni mikakati gani mbali na mazoezi iliyopo inayoongeza ufanisi na ushindi na ari kwa wanamichezo, mcheza kwao hutunzwa. Ni wanamichezo wangapi ambao wameenziwa kwa kutuletea heshima Tanzania kutoka michezo ya Kimataifa na hata ya ndani na Kanda.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Muungano wa nchi zetu mbili Tanganyika na Zanzibar na kuzaliwa Tanzania shauri la dhamana na vyeo viliangaliwa kwa maslahi ya nchi na ustawi wa nchi yetu. Ombi langu nashauri hili lisipuuzwe, litaleta manung'uniko na kuzaa kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu kwa kuimarisha upeo wa kufahamu mipaka ya nchi yetu, si vyema kambi za Zanzibar kuundwa na askari wa Zanzibar pekee

au walio wengi. Naomba mchanganyiko wa askari uzingatiwe ndipo kambi hizi zitazaa JWTZ. Naunga mkono hoja.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Tifa, kwa hotuba nzuri. Aidha, nawapongeza wataalam wote hususan viongozi wakuu wa Jeshi la Wananchi na JKT kwa kazi nzuri ya kutayarisha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana wapiganaji wetu kwa utayari wao katika kukabiliana na dharura mbalimbali kama vile walivyowahudumia wagonjwa katika Hospitali ya Rufaa ya Taifa wakati wa mgomo wa madaktari na wahudumu wengine. Ushirikiano huu pamoja na utayari wao wa kutoa huduma za dharura umedhihirisha uzalendo wao. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Wizara iboreshe maisha ya spiganaji wetu ili tuweze kuendeleza nidhamu ya jeshi letu. Ni vyema Wizara iwapatie wanajeshi wetu makazi mazuri kambini.

Mheshimiwa Spika, nyumba za askari hazitoshelezi. Nafasi ni ndogo sana. Hazitoshi kwa matumizi ya familia ukizingatia utamaduni wetu wa Kiafrika wa kutembeleana na kutegemeana. Nafasi ya nyumba hizi inapunguza heshima za kifamilia kwani wazazi na watoto ni kama wanaishi ndani ya chumba kimoja.

Mheshimiwa Spika, wanajeshi wa vyeo vya chini wanastaafu wakiwa vijana bado. Aidha, vipato vyao havitoshelezi hata kidogo, hali hii iangaliwe upya ili hawa wastaafu vijana wasishawishike kuingia kwenye vitendo viovu, ikiwezekana uwepo mfumo wa kuwajengea wanajeshi nyumba za bei nafuu kwa njia ya mkopo ili nao waweze kuishi maisha yenye hadhi baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai kuhusu huduma za afya kwa askari wastaafu wa Jeshi la Wananchi na JKT hususan wale ambao wanastaafu wakiwa na matatizo ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, hawa ndugu wanashindwa kupata matibabu baada ya kustaafu, hivyo wanaishi kwa shida sana hata kupoteza uhai wao mapema *(pre-mature deaths)*. Mara nyingi wanatumia mafao yao kwa ajili ya matibabu hivyo wanashindwa kabisa kugharamia mahitaji mengine kama kuwasomesha watoto wao.

Mheshimiwa Spika, naomba Jeshi liendelee kuwapatia matibabu ya *ARV's* kwa mfumo endeleve ili waweze kuishi kwa matumaini.

Mheshimiwa Rais wa awamu ya nne amekuwa mstari wa mbele katika kuwaenzi wanawake kwa kuwapa nyadhifa mbalimbali katika Serikali yetu. Napenda mfano huu uendelezwe pia katika majeshi yetu.

Mheshimiwa Spika, wanawake bado hawajapewa nafasi za juu ndani ya majeshi yetu. Kama hawapo wenye elimu na viwango vya kijeshi vinavyohitajika naomba Wizara ichukue hatua za makusudi kabisa za kuwaendeleza wanawake pamoja na kuajiri wanajeshi wanawake wenye elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili mchanganuo wa kijinsia wa maofisa wa Jeshi la Wananchi na JKT. Maelezo haya yatasaidia sana kuwashawishi wanawake wengi waingie jeshini wakijua kwamba kupandishwa vyeo ni fursa sawa kwa jinsia zote.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba Wizara ya Ulinzi na JKT itazame upya swala la ajira kwa vijana wanaopitia mafunzo ya JKT. Je, kuna uwezekano wa Wizara ya Ulinzi na JKT pamoja na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kushirikiana ili wawezeshe hawa vijana waliopitia JKT kupata mtaji wa kujiajiri wenyewe?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja pamoja na kuwaombea wapiganaji wetu afya njema na busara katika kazi yao nzito ya kulinda mipaka ya nchi yetu. Namtakia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wengine wote kila la kheri katika utekelezaji wa maazimio na mipango yote iliyo katika hotuba hii ya 2006/2007.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jjimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Waziri wa Ulinzi na JKT kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa asubuhi hii. Naamini itatumika kama dira kwa maendeleo ya majeshi yetu. Naunga mkono hoja.

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Kwanza naipongeza Wizara kwa kazi inayoifanya ya kudumisha amani ya nchi, raia na mali zake, nimpongeze Waziri wa Wizara hiyo Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, pamoja na Naibu Waziri na wataalam katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nawaombea kila la kheri Mungu awasaidie kumudu majukumu magumu ya kuimarisha Jeshi la Ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi sina tatizo na Wizara hii isipokuwa tu kwa ile mimi ni mwakilishi wa jamii na hasa mkoa ambao mimi natokeo (Shinyanga), naomba sana jeshi hili au Wizara hii iiangalie sana Mipaka yetu kwa upande wa Wilaya za Bukombe, Kahama kwa Mipaka ya Burundi na Rwanda hasa kwa uhalifu na ujambazi unaojitokeza katika miji niliyoitaja wani wahalifu wa maeneo haya (majambazi) inawezekana kabisa wanao mtandao wa ujambazi na wakimbizi toka Mpakani hivyo ni vyema jeshi letu lisaidie jeshi la polisi katika maeneo haya. Kwa upande wa Wilaya ya Bariadi Mipaka ya Uganda (kwa Mji wa Mwanza) na Mpaka wa Kenya (kwa Mji wa Musoma) Mipaka hii iangiliwe zaidi kama tukio la wizi wa gari lililotokea Shinyanga hivi karibuni, wahusika walisemekana walikuwa mchanganyiko na watu wa nje hivyo ni

vyema Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa litowe ushirikiano na mbinu kali kwa jeshi la polisi ili kudhibiti matukio makubwa ya ujambazi unaohatarisha maisha ya Watanzania na mali zao. Hii ifanyike nchini kote kwani mtandao wa ujambazi ni mpana mno na ni hatari.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Serikali iboreshe makazi ya kambi za *Old Shinyanga* na Kizumbi zilizoko mkoani Shinyanga kwani kazi hii ni ngumu na iende sambamba na mishahara ya watu hawa na mafao mengine hapo tutakuwa tumeboresha Wizara hiyo na kudumisha amani ya nchi yetu. Ikumbukwe jeshi ni chombo nyeti nadhani kila mtu anafahamu ni jeshi linaweza kufanya hivyo, Serikali ilienzi vyema, ni mhimili wa nchi.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho naomba Wizara hii iwe na udhibiti kuhusu mavazi ya jeshi ambayo wakati mwingine yametumiwa na majambazi/wahalifu kufanyia vitendo vibaya na kulidhalilisha jeshi letu. Kufanyike udhibiti maalum mavazi haya yasitawanyike ovyo. Pia suala hili liendane sambamba na udhibiti wa silaha za kijeshi ambazo zimetumiwa na majambazi kwenye matukio mbalimbali yanayotokea nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia zote.

**MHE. MUHAMME AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia hotuba hii katika eneo la utaratibu au kanuni zilokuwepo za kustaafu kwa wapiganaji wetu katika JWTZ ziangaliwe upya hasa ukizingatia kwamba kuna askari wengi wastaafu ambao kiumri bado wana uwezo wa kutumikia jeshi. Kuna taarifa pia sijui kama ni za kweli kwamba askari waliostaafu mwaka 2003 wanapata mafao yao makubwa kulingana na wale waliostaafu 2004 hata kama waliacha wakiwa na cheo sawa na kuna wengine waliostaafu mwaka 2004 ambao wanacheo kikubwa basi wanapata fedha kidogo kuliko wenzao waliostaafu mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuchangia kuhusu ajira. Wakati wa ajira nashauri JWTZ izingatie sasa uwiano wa ajira baina ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani ili JWTZ iwe na muundo endelevu wa Kimuungano. Hali kadhalika kuhusu masomo ya uofisa pia yazingatie uwiano wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ni vyema nimwombe Mwenyezi Mungu aniwezeshe kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa naomba niende katika mchango wangu. Jeshi ni mwanga mkuu wa Taifa letu, kucheka, kucheza, kula, kutembea kunatokana na Jeshi katika nchi yetu. Kazi zao ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa ijue umuhimu wa wanajeshi wetu. Ipo haja kuangalia kazi zinazowakabili wanajeshi wetu hali ya kuwa maisha yao hayana uhakika. Nasema haya kutokana na maumbile ya askari anapostaafu ni kigezo tosha. Askari anapostaafu akirejea katika uraia anasikitisha, hana akiba na hana pa kukaa. Ni

kiasi gani askari wetu Serikali inalea na kuwapangia maisha ya baadae? Hivyo ni vizuri askari kustaafu akawa ni mlinda *gate?* Naiomba Serikali iwapangie pensheni zao askari anapostaafu kwa haraka sana kabla mstaafu huyu hajaadhirika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu askari kukosa imani ya kazi zao. Nchi yetu imejikuta na matatizo ya ujambazi, katika hili imebainika miongoni mwa askari wetu wanashiriki katika ujambazi ndani ya nchi yetu. Hii inatokana na posho wanayopewa askari wetu kuwa ndogo. Imani ya kazi kwa askari itatoweka na ndipo atapofanya biashara haramu ama machumi haramu kupitia taaluma yake. Ni vyema sasa Serikali ingewapa uwezo askari wetu.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza kwa kazi nzuri unayofanya ya kuliendesha Bunge letu Tukufu. Nampongeza Waziri wa Ulinzi na Naibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza jeshi letu la ulinzi kwa kulinda mipaka yetu kwa amani si kwa vita katika Mikoa ya Kigoma, Kagera na Rukwa ambako uharamia ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu limekuwa mstari wa mbele wakati wa majanga ya Kitaifa kwa mfano *El-Nino* ambapo barabara na madaraja yalikatika hivyo kuzuia usafiri wa mizigo na abiria, ajali kubwa kama za treni zinapoanguka husaidia uokoaji. Watu wanaofanya kazi kubwa kama hizi wakati wa amani na wakati wa vita wanastahili heshima kubwa kwa Taifa. Mheshimiwa Spika, sina hakika kuwa tunawapa heshima hiyo kikamilifu, tuchukua mfano wa nyumba. Kuna upungufu mkubwa kiasi kwamba wanalazimika kuishi uraiani jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa kwa wapiganaji wetu. Askari hawa baadhi yao wanaegemea *public transport,* hivyo mara nyingi wanafika kazini wamechelewa. Tunashauri kwa kuwa mafundi ujenzi wapo jeshini basi ujenzi wa nyumba liwe ni suala la dharura ili baada ya miaka mitatu wapiganaji wote waishi kambini.

Suala la maslahi ya wapiganaji ni muhimu kutokana na uzito wa kazi za ulinzi, maslahi ni pamoja mishahara na marupurupu kwa mpiganaji. Lakini pia kupandishwa vyeo ni motisha kwa wapiganaji wote.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia maslahi kwa wapiganaji nataka kugusia kitu kilichokuwa kinaitwa Pololo. Pololo zilianzishwa kwa nia nzuri ya kusaidia familia za wanajeshi ambapo vitu vyote vinavyoletwa kambini kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Pololo ilikufa kwa sababu wakubwa walikuwa wanachukua vyakula kwa wingi kinyume na taratibu. Baadae ukaja mradi wa kokoto kwa nia nzuri tu. Lakini wakaingia katika biashara ya kokoto watu ambao ni wanajeshi na hatimaye Pololo hii nayo ikafa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa dhahabu wa Mererani ingawa umeingiza *US$77.7 million* toka uanzishwe mwaka 2003 unasemekana nao unafuata mkondo ule ule wa Pololo. Makambi ya JKT yalianzishwa kisheria lakini yalipata matatizo hapo nyuma na

yakafa. Sasa yameanzishwa tena. Suala la kujiuliza hapa ni je, matatizo yaliyofanya haya makambi kufungwa yamejulikana na yameshapatiwa ufumbuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, JKT inatakiwa kuzalisha kwa 75% na mafunzo kwa 25%. Kwa hivyo, nafikiri JKT ni pahala pazuri ambapo programu zetu kama *Agriculture Sector for development Program(ASDP)* inaweza kuanzishwa pale tena kwa mafanikio. Kwa sababu kuna nguvu kazi nzuri yenye nidhamu ya kazi na yenye usimamizi mzuri. Tuangalie ni kiasi gani inaweza ku-*support budget* ya Wizara mwaka wa fedha 2005/2006 JKT imetumia 25% ya bajeti yake ya shilingi milioni 36.42 sawa na shilingi bilioni 9.15 kwa ajili ya chakula. Kwa mwaka 2006/2007 JKT itatumia 21% sawa na shilingi bilioni 9.53 ya bajeti yake ya shilingi milioni 45.608. Hii inaonesha kuwa bado JKT ni tegemezi. Tungeomba kwanza mkakati uwe ni kulifanya jeshi kujitegemea kwa chakula na kuzalisha ziada ili iuzwe kugharamia shughuli nyengine za Jeshi.

Mheshimiwa Spika , nataka nilipongeze kwa dhati kabisa Jeshi la Wananchi (JWTZ) kwa kusimamia vizuri chaguzi zote mbili: (i) Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na (ii) Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri na Wabunge. JWTZ walisaidia sana kule Pemba kuzima njama mbalimbali zilizoandaliwa na vikosi vya SMZ (KMKM, JKU, KVZ) wakati wa Uchaguzi. Ndio maana Uchaguzi Kisiwani Pemba ulikuwa huru na haki na wa amani. Lakini mambo yalikuwa tofauti katika Kisiwa cha Unguja ambako pamoja na kuwa kulikuwa na wanajeshi wengi, vikosi vya SMZ viliachiwa kufanya vinavyotaka hivyo kuvuruga uchaguzi wote Unguja. Tunachojifunza hapa ni kuwa tukitaka tunaweza kusimamia chaguzi zetu vizuri. Ahsante sana.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, kwa kazi nzuri anazozifanya za kusimamia Jeshi la Tanzania na JKT. Nchi yetu ni tulivu si kama nchi zingine kama Congo na Burundi wanapingana lakini Tanzania tu shwari. Namtakia kheri na afya njema katika kazi zake.

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kuchangia katika hoja hii, naunga mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nilete mapendekezo kwa jeshi letu kama ifuatavyo:-

(1) Benki wanayotumiwa kupewa mikopo ya Wanainchi iko Dar es Salaam inaitwa Benki ya Wanainchi Dar es Salaam, nashauri ziongezwe Benki zingine ili kuwapa ushindani wa riba ili wakopeshwe wengi.

(2) Benki ya *NMB* iko karibu maeneo mengi, nashauri Jeshi liwasimamie wanajeshi wa vyeo vya chini waweze kupata huko waliko kuliko wote wafuate Dar es Salaam.

(3) Elimu itolewe kwa wanajeshi wote kuhusu mikopo inayotolewa na Benki ya Wanainchi wengi hawafahamu.

(4) Vijana wanapomaliza ule mkataba wa miaka miwili JKT, Serikali iwaandalie nyenzo wanaporudi kwa jamii, waweze kuendeleza ujuzi walioupata JKT.

Naunga mkono asilimia mia moja na fedha apewe zote.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kikosi cha Mlale JKT, kikosi kilianza mwakka 1970 na kikosi kina kazi zifuatazo, *Mv mechanics,* umeme magari, uashi, useremala, fundi nguo, kilimo na mifugo na mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji mali, ekari 30 kahawa, ekari 50 za soya, mahindi, ufugaji ng'ombe, bustani na ufugaji samaki.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya kikosi hiki ni kwanza umeme, kulikuwa na *generator* limeharibika, tayari kikosi kiliomba fedha ili kuunganisha umeme toka chazo cha umeme wa maji kwa jirani wa kikosi (*Convent* ya Masisista Chipole) tunaomba Wizara izingatie hilo.

Pili, ni maji, kutokana na tatizo la umeme kikosi kinakabiliana na tatizo kubwa la maji na tatu ni tatizo la nyumba. Nyumba zote zilizopo kikosini ni za muda mrefu lakini nyingi ni mbovu hazijafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya kwenda mjini ni mbovu ingawa tatizo hili sasa linashughulikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri tunaomba sana matatizo haya yaliyoonyeshwa Wizara itusaidie kuyatatua. Nitaleta taarifa ya ziara yangu ofisini kwako. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja. Pili, naipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenye matumaini makubwa ya kutulinda sisi na nchi yetu pia.

Mchango wangu ni juu ya kushauri kurudishwa kwa mafunzo ya JKT kama ilivyokuwa miaka ya 1990 yaani ili kuwapatia watoto wetu mafunzo muhimu ya uzalendo, ulinzi wa nchi yao na kujilinda wenyewe mbinu na stadi mbalimbali za maisha ikiwa ni pamoja na uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, naamini mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa yakirudishwa Serikali, wananchi waajiri tutapata nafuu kubwa na muda wa kujiandaa kuwapokea kwa ajira vijana wetu. Aidha, mafunzo yale yaliweza kuwaweka vijana pamoja na hivyo kuondoa dhana ya matabaka katika jamii. Nchi kama Israel imeweza kwa kiasi kikubwa sana kuondoa kero kwa vijana wake kuzurura kwa sababu mafunzo yale ni muhimu kabla ya ajira. Kwa kufanya vile nchi ile haina kero ya vijana wasio na kazi kama ilivyo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mpango wa mafunzo hayo ukiandaliwa vizuri naamini kabisa nidhamu kwa vijana wetu itakuwa nzuri. Uzalishaji wa chakula utakuwa mzuri kwani vijana watafunzwa kulima kwa kutumia zana za kisasa na ufugaji wa kitaalamu. Ujambazi na uhalifu utapungua kwani vijana wengi watakuwa wamepata elimu na taaluma ya namna ya kujiajiri na kujiendeleza kimaisha wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara kuliona suala hili sasa kwani vijana wetu wako mahali pabaya na uzalendo wao utakuwa mashakani. Nawatakia kila la kheri na utekelezaji mwema wa bajeti yenu.

**MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, napaenda kuchangia kuhusu SUMA JKT kutumika katika ujenzi wa miradi ya kilimo na barabara vijijini.

Mheshimiwa Spika, nimefuatilia sana uwezo wa SUMA JKT katika kazi za ujenzi *(Civil works & Buildings)* na kuridhishwa na kazi zao.

Nashauri, SUMA JKT sasa ijihusishe na ujenzi wa miradi ya kilimo kama miradi ya umwagiliaji na barabara zake *(Service and Farm to Market Roads).* Ushiriki wa SUMA JKT utaongeza ufanisi wa ujenzi wa miradi mingi midogo na mikubwa ambayo wakandarasi waliopo katika soko hawatoshi na hawakidhi mahitaji. Aidha, kwa kuwa SUMA JKT ni kikosi cha Serikali, itakuwa rahisi kwa miradi ya Serikali kuwatumia moja kwa moja na kupunguza mlolongo wa utaratibu wa kupata wakandarasi katika soko huria.

Mheshimiwa Spika, kikundi kingine ambacho kinaweza kuisaidia Serikali na wakulima ni kile cha Magereza. Napendekeza tufanye kikao cha pamoja kati ya Wizara za Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Mambo ya Ndani kuona jinsi majeshi kupitia vikosi vyao wanavyoweza kuchangia kuendeleza miradi ya kilimo hususan miradi ya umwagiliaji.

**MHE. STANLEY K. YONO:** Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa hotuba yenu nzuri na bajeti kwa wewe Mheshmiwa Profesa Juma Kapuya, Waziri na rafiki yangu Naibu Waziri, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, pamoja na Katibu wetu, maofisa na watumishi wote wa Wizara yenu.

Nashauri kuwa zile kambi za JKT ziwe katika Wilaya zote na ikiwezekana mshirikiane na Halmashauri husika katika kuchangia kwa vile bajeti yenu ni kidogo mno. Hivyo TAMISEMI ihusike na wananchi wachangie ili vijana wetu waingie kwa wingi katika JKT na hivyo kuweza kuinua hali ya vipato vyao kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, pia wafanyakazi/wanajeshi wawezeshwe mikopo kwa njia ya *SACCOS,* vyombo hivyo vya fedha viwe karibu na wanajeshi na watumishi hao. Hawa askari wajengewe nyumba bora, walipwe vizuri mishahara na marupurupu kama ilivyo kwa watumishi wengine kwani kazi zao ni nyeti na wanafanya kazi nzuri kwa nchi yetu.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, JWTZ wanalo eneo Jangwani Beach, barabara ya Whitesands ambalo wanalitumia kwa mafunzo ta kulenga shabaha *(rifle range).* Eneo hili zamani lilikuwa nje ya mji, kwa sasa liko katikati ya makazi ya watu.

Mheshmiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni lini Jeshi letu litasitisha shughuli za *rifle range* katika eneo hili la makazi ya watu na kuzipeleka nje ya mji?

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuniwezesha kuchangi hoja ya Wizara hii. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri na wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Wizara hii inafanya kazi zake vizuri na mimi naipongeza sana kuhusu utoaji wa ajira za kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwatazame wale vijana tunaowaweka makambini na kuwatumia kwa sababu tunao vijana wengi katika kambi hizo. Hawa wameshapata mafunzo ya kila aina, kwa hili wafikiriwe hawa vijana wetu.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze Waziri, Naibu wake pamoja na makamanda na wapiganaji wote wa JWTZ na JKT kudumisha ari, uzalendo wa hali ya juu katika kuwalinda Watanzania kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu michezo na sanaa za maonyesho ndani ya JWTZ. Itakumbukwa kuwa miaka ya 1970 hadi katikati ya miaka ya 1980 JWTZ ilikuwa chuo na chimbuko la wasanii na wanamichezo maarufu hapa nchini walioliletea sifa kubwa Taifa letu la Tanzania. Awali jeshi hili lilikuwa likiogopwa na wananchi wake kutokana na maudhui na tabia ya kuogopwa kama ilivyo kwa majeshi yote duniani lakini kupitia michezo na maonyesho ya sanaa za maonyesho wananchi waliliona jeshi kama walinzi wao na pia kama kitulizo cha burudani na kutangaza heshima ya Tanzania duniani.

Mheshimiwa Spika, kipindi hicho ndicho wanariadha akiwa Filbert Bayi na Juma Ikangaa, walipopatikana. Wasanii maarufu kama akina Marehemu Issa Matona, Capt. John Komba na wengineo walipatikana. Timu za *netball, handball, hockey, football* na kadhalika zilipoipandisha chati nchi yetu katika medani ya michezo. Hali hiyo hivi sasa imepoa na kasi kupungua.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kuwa uongozi wa sasa ufufue jambo hili muhimu kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ili tuweze kuwapata akina Filbert Bayi wengine, akina Capt. John Komba wengine, maana michezo jeshini ni moja ya uanajeshi wenyewe. Jeshi likiamua nchi yetu itang’ara duniani.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana kulitokea vurugu mjini Songea maeneo ya *stand* ambapo wanajeshi waliwavamia raia na kuvunja vioo vya magari na kuharibu mali na samani za raia ikiwa ni pamoja kuwapiga raia wasio na hatia. Mkuu wa Mkoa wa wakati huo *Major General* Said Kalembo pamoja na JWTZ (uongozi) wakaunda Tume kuchunguza tuhuma hizo na kubainika kuwa wnajeshi wale walifanya makosa na ikaamuliwa kuwa raia wake na mali zao walipwe fidia ya shilingi 40,000,000/=. Hadi sasa hawajalipwa. Je, Wizara inalielewa hili na kama ndiyo fidia hiyo italipwa lini?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha ikiwa ni pamoja na kuunga mkono hoja.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangi kuhusu nyumba za kuishi. Wanajeshi wa Biharamulo hawana nyumba bora za kutosha. Nyumba za tope zilizojengwa na wanajeshi wenyewe ni mbovu na chache, wanajeshi waliooa na ambao hawajaoa huchangia nyumba moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafairi, wanajeshi Biharamulo hawana usafiri wa kuwapeleka kazini na kurudi. Wanajeshi hao huonekana wakizagaa barabarani wakati wa kwenda na kurudi kazini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo, mara nyingi pesa za posho huchelewa kuwafikia askari. Malipo ya pensheni, mirathi kwa wajane hailipwi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ulinzi naomba wanajeshi wasaidie kusaka pori la Burigi na kuwafukuza majambazi ambao wamegeuza pori hili makazi hasa wanajeshi wa Rwanda na Uganda waliokimbia nchi zao.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwenye *operation* za vita au zoezi la kijeshi kumetokea madhara ya matatizo ya kiafya kama vile *shell shock* au *post war traumatic stress syndrome (disorder),* maradhi haya humsumbua askari hata akiwa nyumbani kwa kuweweseka na kupata woga mkubwa, naomba maelezo kwenye Jeshi letu yametokea haya na kama yametokea ni msaada gani wamepewa.

Mheshimiwa Spika, jeshi lina mpango gani wa kununua ndege mpya za kivita za sasa? *Mig 19* zimepitwa na wakati. Pia kuna mpango gani wa kuanzisha kitengo maalum cha *Search and Rescue* kusaidia panapotokea dharura na kuokoa maisha ya watu. naunga mkono hoja.

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kazi nzuri na ya kizalendo inayofanywa na majeshi yetu iendelezwe.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hoja hii kwa kusema kwamba tunalipongeza Jeshi letu la Ulinzi kwa kazi nzuri wanazofanya za Ulinzi wa nchi yetu. Pia naomba nitumie fursa hii kumpongeza Ndugu Mwamunyange, kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Aidha, nampongeza Meja Jenerali Shimbo, kwa kuteuliwa kuwa Mkuu mpya wa Jeshi la Kujenga Taifa, nawatakia kazi njema.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tanzania wana imani kubwa ya majeshi yao kwamba wao ndio watawalinda na kuhakikisha usalama wao, lakini ni jambo la kusikitisha kwamba unapofika wakati wa uchaguzi askari wengi kutoka Tanzania Bara huletwa Zanzibar wakiwemo JKT, sijui ni kwa misingi gani kwamba ni kuongeza nguvu ama ni kuisaidia Serikali iliyoko madarakani au vipi, bali imani ya wananchi ni kwamba ni walinzi. Kinachoshangaza na cha aibu JKT huchanganyika na JKU kule Zanzibar wakawapiga raia, wakawanyanyasa na kuwadhalilisha kadri wawezavyo na hatimaye kuvunja milango ya nyumba za watu na kuiba mali za raia.

Mheshimiwa Spika, je, hiyo ndiyo kazi na wajibu wa Jeshi/majeshi yetu? Aidha, baada ya kadhia hiyo inayowapata Wazanzibari, mara baada ya Uchaguzi askari hao husafirishwa na kurudishwa wanakotoka bila hata Serikali kujali matatizo ambayo wanayapata raia.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, atumie fursa aliyonayo kuwakumbusha walinzi wetu majukumu yao kwa raia na kuwajali raia hao kwani bila ya wao tusingekuwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, wanajeshi ambao wanatumikia nafasi zao kisiasa, basi wavue sare za Jeshi waingie kwenye uwanja wa siasa kama alivyofanya Mheshimiwa Capt. John Komba, nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, majeshi yetu yana kazi ngumu sana ambayo wangestahili kupata faraja baada ya kazi ngumu (saa za kazi). Ni jambo la kusikitisha kuona kwamba wanajeshi wetu hawana makazi mazuri (nyumba za kuishi) hivyo wanahitaji kuboreshewa makazi yao/nyumba zao ili waweze kuishi vizuri na familia zao.

Aidha, naomba waboreshewe mishahara yao ili wasidhalilike wakati wanapostaafu, kwani mara tu mwanajeshi anapostaafu huanza kuhangaika sana na maisha na kuwafanya wadharaulika ndani ya jamii. Hivyo Serikali iangalie sana katika kuinua hali zao za maisha kuendana na hali halisi ya uchumi wa nchi yetu. Ahsante.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake pamoja na Makamanda na wapiganaji kwa kazi nzuri wanayofanya ya kulinda nchi na kudumisha amani. Bila amani hatuwezi kufanya lolote na wala hatuwezi hata kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri masuala yafuatayo: -

(i) Tujenge uwanja mkubwa wa kumbukumbu ya vita vya Tanzania na Uganda katika Viwanja vya Bunazi, Wilayani Missenyi. Katika uwanja huo tuweke masalia na kumbukumbu ya vita ya kukomboa ardhi ya Tanzania pamoja na kuwakumbuka

mashujaa wetu. Uwanja huo uwe kielelezo cha kazi nzuri iliyofanywa na jeshi letu kulinda nchi yetu.

(ii) Fedha nyingi zaidi zitengwe kwa ajili ya utafiti wa gari la Nyumbu na utafiti huo ulenge vile vile kutengeneza magari ya kuweza kutumiwa na raia, kumbuka hivi sasa tuna soko kubwa la Afrika Mashariki na magari ya Nyumbu yanaweza kupata soko hilo.

(iii) Wakati umefika kwa Mkoa wa Kagera kuwa na kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

(iv) Kadri itakavyowezekana tuendelee kuimarisha jeshi letu kwa kulipatia vifaa vya kisasa.

(v) Tuendelee kutoa mafunzo ya mgambo kwa vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Kwanza, kama Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Ulinzi na JKT ninaunga mkono hoja hii moja kwa moja na kuitakia Wizara kila la kheri. Pamoja na kustaafu najisikia ni sehemu yenu na ninaona fahari kwa mchango niliotoa katika ustawi wa Wizara katika miaka ya 1964 hadi 1968 na 1980 hadi 1991.

Pili, pamoja na hayo, ninaona katika bajeti kuwa matatizo yaliyokuwepo wakati wangu Shirika la Mzinga, Nyumbu na Jeshi kwa jumla dhahiri kwa kupanuka kwa majukumu na papo hapo kutokuwa na fedha za kutosha Kitaifa. Natumaini hali itazidi kuimarika kadri tunavyokwenda. Nitaendelea kuwa balozi wenu.

Mheshimiwa Spika, tatu, hata hivyo, jawabu linaweza kuwa katika ku-*commercialise* shughuli za kibiashara zisizo za kijeshi moja kwa moja. Kwa mfano, Kampuni moja ya Canada ilikuwa tayari kutoa *sub-contract* ya kutengeneza magurudumu ya gari moshi kupeleka India. Wakati ule mtaji ulikuwa shilingi milioni 365 tu lakini faida ilikuwa kubwa sana, tulishindwa tu kwa kukosa fedha hizo. Kazi hiyo ilikuwa itekelezwe na Nyumbu. Bwana Kurjit Nahal wa *Meeco* ambaye ni mkandarasi wenu upande wa mawasiliano na Hashim Ismail watakuwa na taarifa kamili za historia ya suala hili. Mfano mwingine ni Meremeta. Sijui tumekwama wapi ingawa upeo wake wa kufanikiwa ni mkubwa. Pengine tungetafiti na kujua tumeshindwa vipi na kuanza upya kwani Meremeta ilikuwa inaingiza fedha nyingi tu.

Mwisho, napongeza kurejesha JKT baada ya kulegalega na kusimama. Mimi nadhani inawezekana kurudisha vijana na kuwatumia zaidi kwa kuzalisha chakula na vifaa vingine kama inavyofanyika na SUMA JKT lakini kwa kiwango kikubwa zaidi. Najua hivi sasa SUMA JKT ni wakala wa Serikali na kwa hiyo, upeo wake wa kupanua usingekuwa na mipaka ya kijeshi wafanye mambo kibiashara.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwapongeza wewe Waziri, Naibu wako, Katibu Mkuu mpya, *CDF, CofS* mpya na makamanda na wapiganaji wote.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake. Pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa JKT na wanajeshi wote kwa kazi nzuri ya kulinda nchi yetu. Serikali iboreshe vyombo vya usafiri kwa wapiganaji wetu (wanajeshi) JWTZ na JKT katika vikosi vyote vikiwemo vikosi vya JKT Makutupora na JWTZ Ihumwa. Serikali inunue mabasi/magari kwa ajili kusafirisha wanajeshi wnapokwenda kazini kwa kuwa baadhi yao wanaishi uraiani.

Mheshimiwa Spika, Serikali ijenge makambi/nyumba ya kutosha ili wanajeshi wote wakae kwenye makambi badala ya kupanga uaraiani.

Pia Serikali iboreshe maslahi ya wanajeshi kwa kuwa wanafanya kazi katika mazingira magumu. Pia Serikali iendelee kuboresha mafunzo ya wanajeshi wetu kulingana na hali ya sasa ya karne hii ya 21 ya *Science and Technology.*

Mheshimiwa Spika, jeshi letu liimarishe ulinzi wa mipaka yetu na kudhibiti uingizaji wa silaha zinazoingizwa kiholela na wakimbizi pia kudhibiti wimbi la wakimbizi ambao huingia nchini kwetu na kutuletea athari nyingi, uharibifu wa mazingira, kuingiza silaha ambazo hutumiwa na majambazi yanayohatarisha maisha ya Watanzania na mali zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake ya Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2006/2007 kwa Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza watendaji wengine wa Wizara yake nikianzia na Naibu Waziri MheshimiwaOmar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Mkuu wa JKT, Makamanda wote, Maafisa, wapiganaji na watumishi wote wa Wizara yake kwa umakini na uaminifu mkubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi zangu hizo napenda kupendekeza yafuatayo, kwa kuwa mkoani Mtwara katika Wilaya ya Tandahimba maeneo ya Litemla ilikuwa kambi *(Camp)* iliyotumika kuwaandaa wananchi maeneo yale kiulinzi hasa mgambo kufuatia kuwepo vita nchi jirani ya Msumbiji na kwa kuwa maeneo hayo ni yenye rutuba sana ikizingatiwa kuwa eneo hilo lipo tu pembeni mwa Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa hata Halmashauri ya Wilaya ya Newala ilijaribu kwa mafanikio sana mradi wa kilimo cha matrekta siku za nyuma na kwa kuwa sasa Jeshi la Kujenga Taifa linarudia kuwapokea vijana kwa kujitolea na kwa mujibu wa sheria, je, Wizara haioni kama ni vyema eneo hilo la Litemla likafunguliwa kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa ili kuinua uchumi wa kilimo uliolala bila kutumika ipasavyo kwa sasa.

Kwa kuwa Jeshi linasaidia sana katika kuongeza mahitaji ya sekondari nchini kwa kufungua shule kama vile *Makongo High School, Jitegemee High School, Airwing* na kadhalika ni vyema basi jitihada hizo zikaangalia pia mikoa ya pembezoni ambayo ina matatizo mengi ya kijamii, hivyo Wizara ifikirie uwezekano wa kufungua shule ya sekondari angalau moja katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Kigoma, Rukwa na Pwani. Kwa kufungua shule maeneo hayo itakuwa ni kuunga mkono kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, la kulipa kipaumbele mikoa hiyo ya pembezoni.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi pamoja na wapiganaji wana tatizo kubwa sana la makazi, wengi wao hupanga *(rent)* uraiani. Ushauri wangu ni kuwa mkakati uandaliwe kuhakisha kuwa unaanzishwa mradi wa ujenzi wa nyumba kwa ajili ya askari/wapiganaji. Mradi huu utatia moyo *(motivation)* askari lakini pia utasaidia kulinda siri za kijeshi.

Mheshimiwa Spika, mkakati uanzishwe kuhakikisha kuwa askari wote ambao hawajifikia kiwango cha kidato cha nne sasa wanasomeshwa, hii ni kwenda sambamba na kuwa na jeshi lenye uwezo na utaalam wa kijeshi unaendana na matumizi ya teknolojia na sayansi endelevu.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, napongeza hotuba nzuri na mipango mizuri ya bajeti. Pia napongeza utendaji kazi mzuri. Majeshi yetu yanafanya kazi zake vizuri na sisi wananchi kwa imani katika jeshi tunaishi kwa utulivu mkubwa.

Kuhusu majengo ya askari, nashauri kasi ya kujenga nyumba za askari iongezwe ili watendaji hawa waweze kuishi vizuri zaidi na kuweza kuendelea kutenda kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nidhamu ya askari, nashukuru suala hili kila mara lilipojitokeza la askari kuchukua sheria mkononi na kuwapiga raia, jeshi limekuwa linachukuwa hatua za haraka. Naomba na kushauri utaratibu huu uendelee ili wanajeshi na raia waendelee kuishi kwa maelewano mazuri.

______Kuhusu wakufunzi wa mgambo toka jeshini, napendekeza Wilaya za Mpakani hususan Karagwe ambako ujambazi umekithiri hasa katika pori la Kimizi, tuongezewe idadi ya wakufunzi hawa waliopo tayari wanafanya kazi nzuri, wakiongezeka usalama utaboreka zaidi. Naunga mkono hoja.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pia naipongeza Serikali ya awamu ya nne

kwa ushindi mkubwa ulioupata katika Uchagizi Mkuu uliopita hivyo kuiongoza Serikali hii yenye sera nzuri ya amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Wizara hii kwa uwezo wake mkubwa chini ya Waziri na Naibu Waziri wake na makamanda kwa udumishaji wa nidhamu ya juu katika jeshi letu, aidha, naomba katika hili lizidi kusisitiza suala la nidhamu jeshini kwani hivi sasa dosari ndogo ndogo zimeanza kujitokeza katika ujambazi wa wizi kwa askari ambao umezuka hivi karibuni (vifaa vya mawasiliano ya *Radar)* lazima Idara ya Intelijensia ijidhatiti kabla ya matokeo ya uhalifu ndani ya jeshi haijachukua nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, nalishauri jeshi kwa kuwa ni chombo ambacho hakitakiwi kiwe na dosari za kipuuzi, naomba pia katika uajiri wawafuatilie kwa kiwango cha juu sana vijana hao watarajiwa kabla kuchukuliwa katika ajira vinginevyo jeshi letu litachafuka na kuwa jeshi lisiloaminika na wasioaminiana kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu la Majini *(Navy)* lazima lipewe kipaumbele sana kuimarishwa kimafunzo na kiuwezo wa vyombo ili liweze kuwa katika kiwango, kwani inafahamika jeshi hili lilivyofanya vizuri wakati wa vita vya Kagera. Jeshi hili linaweza kuwa pia ni chanzo cha kuingiza pato katika vyelezo vyake pale Kigamboni pamoja na uzalishaji wa vipuri.

Mheshimiwa Spika, bado nashauri kikosi hichi cha *Navy* kipewe pantoni yake kwani kusubiri pantoni ya kiraia itachangia ucheleweshaji wa harakati za kijeshi hasa ukizingatia pantoni zilizopo ni za kuzimika zimika.

Mheshimiwa Spika, katika wakati huu wa usalama nalipongeza sana jeshi katika kujifunza na kutoa maafisa waandamizi naamini hawa vijana watasaidia sana katika shughuli za kijeshi. Lakini bado nashauri yale mafunzo ya kivita manuva yapangiwe muda maalum kwa mwaka kwani mafunzo haya hupunguza woga kwa vijana wetu kuzisikia risasi za moto na *movement* za ndege zetu za kijeshi.

Mheshimiwa Spika, aidha yale mafunzo yaliyowashirikisha Wafaransa yangerudiwa rudiwa ili kuwazidishia ukomavu askari wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza *General* George Waitara, kwa uadilifu wake na hasa kuwa na lugha za kijeshi tu na kuachana na kuchanganya mambo yasiyomhusu inatia moyo sana na kuonyesha jinsi anavyofahamu majukumu yake lakini bado namshauri awe anatembelea makambi yake na kutoa maelekezo mazuri kwa maafisa na askari hasa katika kudumisha nidhamu za kijeshi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza mchango wangu nalipongeza jeshi hasa madaktari waliochukua nafasi ya wale waliogoma pale Muhimbili na kuonyesha umma jinsi gani uwezo wa jeshi ulionao.

Mwisho, naomba niwaombee wanajeshi wote waliofariki vitani au popote katika harakati za kijeshi na Mungu atawapa mapumziko mema ya peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, vituo vyote vya *Radar* vipewe kipaumbele cha aina yake kama macho na binaadam. Ahsante.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuchaguliwa kusimamia Wizara hiyo nyeti.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe taarifa ya masikitiko yangu kuhusiana na Wafanyakazi wa Meremeta walioko jimboni kwangu ambao waliachwa bila utaratibu wa kuishi. Ni muda mrefu hawapewi mishahara, wanateseka. Wamekuwa wakinisumbua tangu Uchaguzi Mkuu hadi leo. Nimekwisha mwona Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, akaahidi kuwa watalipwa, hadi leo hawajalipwa. Nilimuona Gavana wa Benki Kuu naye akasema pesa zimepatikana na wangelipwa mwezi Februari, 2006.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi hao walishatuma viongozi wao kuja hadi Dar es Salaam nao wakaelezwa kuwa warudi watalipwa lakini mpaka leo hawajalipwa. Hali ya watumishi hawa ni mbaya. Naomba majibu ambayo yameambatana na hundi ya malipo. Si vyema viongozi wa ngazi ya Gavana na Katibu Mkuu wa Wizara kutoa ahadi zisizotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleweke, Meremeta Jimboni kwangu ni tatizo kubwa. Kabla ya kupitisha bajeti ieleweke wazi kwa wananchi husika ni lini watalipwa.

Mheshimiwa Spika, napenda nieleze kuwa kazi za ulinzi kwa sehemu kubwa huwa ni siri ya nchi ikiwa ni pamoja na uwezo wa jeshi hilo. Kwa kuwa sehemu kubwa ya mambo ya jeshi ni siri si vyema watu wote wakafahamu kuna nini. Wakati Mgulani inaweka makao pale Dar es Salaam palikuwa ni pori, watu walikua wachache sana waliozunguka katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, mie naomba kwa nia njema ni vema wangetafutiwa mahali pengine nje ya Dar es Salaam, wajengewe vizuri na wapewe usafiri wa kutosha. Hali hii ifanyike kwa uangalifu na wajengewe shule na miundombini ya kutosha. Sasa wamebanana na hawana hata pa kufanyia mazoezi wala *range.* Tusiweke kila kitu wazi.

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja na ninampongeza sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana kuona katika ukurasa 15(24) maelezo ya dhamira ya Jeshi letu kufungua Ofisi za Wambata wa Jeshi katika Balozi zetu zilizopo Ujerumani, *UAE,* Malawi, Marekani na Nigeria.

Mheshimiwa Spika, nitafurahi zaidi iwapo jitihada za makusudi zitafanywa siku za baadae kufungua tena ofisi ya Mwambata Ottawa, Canada ambako miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka 1980, askari wetu hasa wa Mizinga, vifaru na *Pilots* wetu walikuwa wanapata mafunzo.

Aidha, Canada inajulikana sana duniani kwa shughuli za *peace keeping* na wana vyuo maalum vya kufundishia mafunzo ya *peace keeping,* Halifax. Isitoshe, Wa Canada walikuwa wametuuzia ndege za usafiri *(Transport planes)* na wakawa wanazifanyia *service.* Naamini kwa kufungua tena ofisi ya Mwambata Cananda, kutalinufaisha sana jeshi letu. Naomba sana hilo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga tena mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kuhusu kambi za Jeshi, kuna kambi nyingi za Jeshi zimesahaulika sana na kuna nafasi nyingi zinatoka lakini zikishatoka watu wengi hawapati taarifa ili kuweza kujiunga na Jeshi na unakuta kule kwenye kata, Halmashauri hawatoi taarifa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna kambi nyingi zimesaulika kabisa kama ifuatavyo, Rwamishenye, hiyo kambi ilikua kama Makao Makuu ya Jeshi lakini kama sio Makao Makuu iboreshwe pamoja na majengo ukiangalia majengo ni aibu kubwa kuona wanajeshi wanakokaa, inaleta aibu. Hivi Serikali haioni aibu Jeshi linasamaniwa kipindi cha upiganaji ndipo wanathaminiwa

Mheshimiwa Spika, maombi yangu ni kuwa nafasi za Jeshi zikiwa zinatoka ziwe zinatangazwa kuanzia kwenye Kata na Halmashauri. Ukumbuke matatizo yaliyotokea na waliyoyapata kipindi cha nyuma Serikali isingesahau kambi hizo za Rwamishenye, Kaboya na kambi zingine zote. Serikali isiwakatishe tamaa wale wanao penda kujiunga na Jeshi. Pia Serikali iwakumbuke na wale wastaafu wa Jeshi wote na kuwa na kumbukumbu ya siku ya mashujaa hasa Bunazi, Mtukula, Rwamishenye na Kaboya pawe panakumbwa kwa kuwaenzi wale walio poteza maisha ya hasa kila mwaka. Naomba kupata majibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kufanikisha matayarisho ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, pongezi za pekee ni kwa wapiganaji wote wa jeshi hili kwa kazi nzuri wanazozifanya za kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa na amani na utulivu licha ya kuzifanya kazi hizi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, niipongeze pia Serikali kupitia Wizara ya Utumishi na Menejimenti ya Umma, kwa uamuzi wake wa kuwaongezea maslahi wataalam wetu na wapiganaji wetu ili walau waweze kupunguza makali ya maisha. Naiomba Serikali iendelee kuwakumbuka kila mwaka wanajeshi wetu ili kuwapa motisha zaidi katika kuzifanya kazi zao hizo ngumu na za kujitolea.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara hii kwa juhudi zake za kuboresha huduma za tiba kwa kujenga au kuboresha hospitali ya Jeshi Kanda ya Bububu. Ukamilishwaji

wa ukarabati wa hospitali hiyo pamoja na miundombinu, kutawasaidia sana wanajeshi wetu na hasa raia wa Zanzibar kupata huduma ya matibabu itakayokuwa bora zaidi. Naishukuru pia Serikali ya Shirikisho la Ujerumani kwa kukubali kufadhili ukarabati wa hospitali hiyo pamoja na ujenzi wa mabwalo ya kuishi askari katika kambi ya Bububu ambayo ipo kwenye jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa uboreshaji wa hospitali hiyo hautaishia tu kwenye ukarabati wa majengo bali ni imani yangu kuwa miundombinu yote muhimu kama vile maji ya uhakika, barabara nzuri, umeme wa uhakika, zana za kisasa za uchunguzi wa magonjwa, mafunzo ya madaktari bingwa vile nayo yataboreshwa.

Mheshimiwa Spika, kambi nyingi za Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa upande wa Zanzibar maeneo yake hayana hatimiliki, namshauri Mheshimiwa Waziri katika zoezi la upimaji wa maeneo ya Jeshi Zanzibar ianze na maeneo hayo yakiwemo ya kambi ya JWTZ Mwanyanya na Bububu inapokarabatiwa hospitali.

Mheshimiwa Spika, kambi ya JWTZ Mwanyanya imezungukwa na makazi ya raia, hivyo nashauri eneo la kambi hilo lijengewe uzio ili kuliweka katika hali nzuri ya usalama. Kambi hiyo haina gari la kuaminika, gari dogo linalotumika kwa sasa ni kongwe na huharibika mara kwa mara, naomba wapatiwe gari jipya kwa kuzingatia hali halisi ya kisiasa katika jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, kambi ya Mwanyanya ina jengo la ofisi za utawala ambalo ni kongwe sana na ambalo linahitaji ukarabati mkubwa. Kutokuwepo na nyumba za kuishi askari katika kambi ya Mwanyanya kumewalazimu askari kupanga mbali na kambi na hivyo kuwasabsbishia usumbufu wa kwenda na kurudi kazini. Ni vyema Wizara ikachukua juhudi ya kuwajengea mabwalo wanajeshi hao.

Mheshimiwa Spika, askari wetu wanalalamika kuhusiana na posho ndogo (resheni) wanayopewa ambayo haikidhi hali halisi ya gharama ya vyakula na upandaji wa mahitaji kwa ujumla, posho hilo liongezwe. Kwa kuwa jeshi la wananchi ni chombo cha Muungano ni kwa kuwa JKT kwa upande wa Zanzibar hakuna kambi yoyote ya kikosi hiki, ninaishauri Serikali ianzishe kambi ya JKT sawia na JWTZ ili kulikamilisha Wizara hii ya Jeshi la Ulinzi na JKT. Kuanzishwa kwa Kambi za JKT huko Zanzibar kutapanua wigo wa ajira kwa vijana wetu wa huko Zanzibar na hivyo kutimiza azma ya ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira, kulijitokeza malalamiko ya ajira kwa vijana wetu huko Zanzibar wakati Jeshi la Wananchi Tanzania lilipotangaza nafasi za ajira mpya kwa Watanzania wote. Vijana wengi kwa upande wa Zanzibar waliitikia wito huu, lakini tatizo lilikuwa ni kuzipata nafasi hizo ambazo wingi wa nafasi hizo inasemekana kuwa zilichukuliwa na watoto, ndugu na jamaa wa askari ambao wengi wao walitoka Tanzania Bara. Naimani malalamiko haya Waziri anayafahamu kwa kina. Hivyo, ili kuondoa migongano ya ajira mpya kwa vijana wanaopenda kuajiriwa na jeshi la wananchi kutoka Zanzibar ambao wanakubalika kwa mujibu wa matakwa ya mwajiri, Wizara iweke utaratibu wa kueleweka ili jambo hili lisitokee tena.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pensheni kwa wastaafu wa jeshi hili wamekuwa wakilipwa fedha kidogo kama pensheni yao na kwa kuwa inasemekana kwamba katika miaka ya nyuma Serikali ilitangaza kuwa pensheni hiyo ingekuwa inaongezwa kila mishahara inapoongezwa, wastaafu wanalalamika kuwa pensheni yao imebakia ile ile kwa zaidi ya miaka minne sasa hasa wale wenye kima cha chini, je, Serikali inasemaje kuhusiana na hilo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika,naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenyewe binafsi, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Viongozi wa Majeshi, *General* George Waitara, *Lut. Gen.* Mwamunyange na *Major General* Abdulrahman Shimbo, pamoja na watumishi wote wa Wizara yako. Hakika jeshi letu la ulinzi ni jeshi la kujivunia sana.

Mheshimiwa Spika, limepigana vizuri kwa ushujaa mkubwa na ukombozi wa nchi za Msumbiji, Zimbabwe na Namibia na vita vya uvamizi vya Nduli Iddi Amini. Pia kuhusu majanga ya Taifa *(Civil works)* kama moto ulitokea *Tiper, u*jenzi wa madaraja wakati wa mafuriko kazi ya Wizara hii ni ngumu na nzito. Ama mzigo mzito mpe Mnyamwezi. Namshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kumteua Mheshimiwa Alhaj Profesa Juma Kapuya, kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, hoja zangu ni kwanza, naomba Serikali iongezee fedha Wizara hii kwani hii shilingi bilioni 287.5 hazitoshi kwa majukumu ya kisasa ya jeshi letu kwa sababu vita vya siku hizi vinapiganwa kwa kutumia vyombo na silaha za kisasa ambazo ni ghali zaidi. Askari wa miguu siku hizi wanaweza kuangamizwa na askari wachache wa adui wenye silaha za kisasa.

Kuhusu hospitali ya jeshi, Lugalo Mheshimiwa Waziri, tunaomba Serikali ikubali kuwa katika nchi zilizoendelea Hospitali ya Jeshi ndio Hospitali kubwa kuliko zote katika nchi. Ukubwa Hospitali ni kuwapo kwa watumishi bora yaani Hospitali hiyo iwe na mabingwa waliobobea wa fani zote za magonjwa ya binadamu. Hospitali lazima iwe na vifaa vingi vya kisasa na pia iwe na ubora wa majengo yake. Mheshimiwa Waziri, hospitali ya Jeshi ndio Hospitali ambako viongozi wetu wakuu wa Kitaifa wawe wanatibiwa. Hospitali hii ipewe fedha nyingi kwa ajili ya kutimiza majukumu niliyoyaainisha hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, watani zako Warufiji wanayo ardhi kubwa yenye rutuba ya mboji nyingi. Aidha, Mto Rufiji una maji tele, huu ni mto mkubwa, Bonde la Mto Rufiji ndio sehemu bora ya kilimo cha Mpunga, Pamba, Mahindi, Korosho, Ufuta na Mikunde na kilimo cha miwa vinastawi. Sasa naomba Wizara yako ianzishe rasmi kambi kubwa ya JKT katika jimbo la Rufiji kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, mimi Mbunge wa Rufiji natoa ahadi kuwa mimi mwenyewe na wapiga kura wa Rufiji tuko tayari kuwapokea JKT. Binafsi Warufiji watajifunza sana ukulima wa kisasa na elimu nyingine toka kwa JKT, kambi ya

Rufiji Mzee Kapuya wape watani zako JKT. Tuna ardhi, maji mengi na watu. Tusaidieni nasi tupate kuendelea.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru sana MMheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Tupe Kambi ya JKT Rufiji. Ahsante sana.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, nimeomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi Kujenga Taifa katika vipengele vifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu *ration allowance,* utaratibu wa Jeshi ni kuwalipa *ration allowance* ya shilingi 60,000/= kwa mwezi kama posho ya chakula. Yapo malalamiko ni kwa nini askari hawalipwi fedha hizo wanapokuwa kwenye medani na hata hivyo kiasi hicho cha fedha hakitoshi kufuatana na kupanda kwa maisha. Je, Waziri mwenye dhamana ana mkakati gani kuhusu hili linalolalamikiwa sana?

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya wataalamu wa kijeshi. Jeshi lilianzisha viwanda kwa ajili ya uzalishaji. Viwanda hivyo ni Mzinga cha Morogoro na Nyumbu cha Pwani. Uongozi wa viwanda hivi uko mikononi mwa raia zaidi kuliko Jeshi. Madhumuni ya Jeshi kuwasomesha wataalamu hawa ni kuonyesha utaalamu wao kwa maendeleo ya Jeshi. Kwa kutokuwatumia ni kusababisha wataalamu hao kutokutumika. Mbali na hiyo, nashauri viwanda hivyo viwili vya uzalishaji viwe chini ya Makao Makuu ya Jeshi kuliko kuwa chini ya Wizara kama ilivyo sasa hivi, kwa kuendelea kuwa chini ya Wizara kunasababisha malalamiko kutoka kwa wapiganaji.

Kuhusu nyumba za wapiganaji. Wapiganaji wengi wanaonekana kuishi mitaani. Kasoro kubwa inayojitokeza ni wapiganaji hao kuhusishwa katika matukio kadhaa yanayotokea na hasa yote ya ujambazi. Inawezekana kabisa Wizara kusimamia ujenzi wa nyumba za wapiganaji ili kuondoa tatizo la kuishi pamoja na familia zao.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo lingine ambalo ni usafiri kwa askari. Kwa mfano kutokana na askari kuishi nje ya kambi asubuhi wanatoka kila kona na hasa kwa Dar es Salaam ambako hukusanyika *stand* kubwa ya Ubungo. Waziri mwenye dhamana amejipangaje katika kuondoa tatizo hilo la usafiri? Yapo madai kuhusu fedha (Kasma) ya mafunzo kuwa wapiganaji hawalipwi wakati wanapokuwa kwenye mafunzo. Ni vyema sasa Waziri aeleze kuhusu Kasma hii kwa sababu hali hiyo ya askari kutolipwa imeshusha morali ya wapiganaji. Waziri anaeleza nini kuhusu Kasma hii ya mafunzo ambayo inalalamikiwa kwa kiasi kikubwa?

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa mtoa hoja amegawa dakika kumi kati ya dakika zake 60 zitumiwe na Naibu Waziri katika kujibu hoja za Wabunge, kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri nampa dakika 25 kuanzia sasa na Mheshimiwa Waziri mtoa hoja atamalizia kwa dakika 50. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe

binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Aidha, na mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Naomba pia kuungana na Wabunge wenzangu walionitanguli kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar kwa kuchaguliwa na wananchi walio wengi kuongoza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuchaguliwa kwao kunaonyesha ni jinsi gani Watanzania wanavyozikubali sera za Chama cha Mapinduzi na viongozi wake, aidha, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imani aliyonipa ni kubwa na napenda kumuahidi kuwa nitafanya kazi zangu za kulitumikia Taifa letu kwa uadilifu na uaminifu mkubwa na bila kuchoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na wananchi pamoja na wale walioteuliwa pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika Wizara mbalimbali, nawaahidi ushirikiano wangu katika kutekeleza majukumu tuliyopangiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Waziri wangu Mheshimiwa Alhaji Profesa Juma Athumani Kapuya, kwa kunishirikisha kwa ukamilifu katika masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Aidha, nampongeza Katibu Mkuu Ndugu Mwaisumo pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa utendaji mzuri wa kazi zao, namwombea kwa Mwenyezi Mungu amjaalie Katibu Mkuu wetu afya njema na aweze kurejea salama kutoka India alikokwenda kwa matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo nampongeza Kaimu Katibu Mkuu Ndugu Msongo, kwa kazi nzuri wanazozifanya, vile vile nawashukuru wanajeshi wote wakiongozwa na Mkuu wa Majeshi Jenerali George Waitara, Mnadhimu Mkuu wa Majeshi Luteni Jenerali Mwamunyange na Mkuu wa JKT Meja Jenerali Shimbo, kwa ushauri na msaada wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawaahidi wanajeshi wote wa Tanzania kuwa nitawatumikia kwa uwezo wangu wote na kwa heshima na taadhima. Nawaomba wasichoke kunisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Kiembe Samaki Zanzibar kwa kuniamini na kunichagua licha ya majukumu mengi niliyonayo nawaahidi nitawatumikia kwa uwezo wangu wote na sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Magharibi na Mkoa wa Mjini Magharibi kwa ushirikiano mzuri wanaonipa.

Mheshimiwa Spika, wahenga wanasema, kidole kimoja hakivunji chawa, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru sana mke wangu pamoja na watoto wangu kwa kuniunga mkono toka wakati wa kampeni ya Uchaguzi Mkuu hadi hii leo. Nawaomba kwa kushirikiana na Watanzania wote waendelee kunisaidia ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa kiwango na *speed* inayaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani na pongezi hizo sasa naomba kutoa ufafanuzi na hoja mbalimbali zilizoulizwa na Waheshimiwa Wabunge. Hoja ni nyingi na mimi nitazijibu baadhi tu na nyingine zitajibiwa na Mheshimiwa Waziri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze na hoja ambayo imeulizwa na Wabunge wengi, Wabunge 21 wameuiliza, wametaka ufafanuzi na wametaka kuelewa juu ya makazi ya wanajeshi.

Mheshimiwa Spika, nataka nikubaliane na Waheshimiwa waliouliza hoja hii. Ni kweli kwamba makazi ya Wanajeshi ni duni, lakini jitihada zinafanywa kwa kushirikiana na Wizara na Fedha pamoja na Taasisi mbalimbali za Fedha ili kuweza kupata fedha ambazo zitakuwa na riba nafuu tuweze kuwajengea Wanajeshi wetu nyumba za kisasa. Tunazo ramani zetu ambazo tumeshaanza ujenzi katika maeneo mbalimbali ya Tanzania. Kwa mfano, Lugalo, Makambako na Wawi Pemba. Hizo nyumba zina vyumba vitatu na vyumba hivyo vitatu kimoja kitakuwa ni *self container* na ramani hizo tunaendelea kuzitumia katika maeneo mbalimbali. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wavute subira ili kazi hii itakapokamilika waweze kuiona katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii kama nilivyosema ni 21 wakiwemo Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Issa Khamis Issa, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa John Malecela na Mheshimiwa Mariam Kasembe. Hao ndiyo waliochangia hoja hii, nawaomba wavute subira na mambo yetu yakikaa vizuri wataweza kuyaona katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengine walichangia hoja ya kuanzisha makambi mapya ya Jeshi la Kujenga Taifa katika maeneo mbalimbali.

Naomba kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hiyo kwamba, hivi sasa tuna makambi zaidi ya 24 ya Jeshi la Kujenga la Taifa ambayo tunayahudumia. Makambi hayo yana vijana zaidi ya 4,000 ambao tunawahudumia. Nia hiyo ipo ya kuanzisha makambi mengine katika Wilaya mbalimbali. Lakini kwanza tunataka kuimarisha haya makambi yaliyopo, hatuwezi tukaanzisha makambi mengine wakati haya mengine hali yake ni duni. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wavute subira ili tukishayaimarisha makambi haya, tutaanzisha makambi mengine katika maeneo ambayo yanahitaji kambi hizo kuanzishwa.

Mheshimiwa Spika, waliochangia hoja hii naomba niwataje. Ni Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza. Kwa hiyo, nawaomba wavute subira kidogo hali itakapokuwa nzuri tutaanzisha makambi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyozungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa maendeleo ya *SUMA JKT* kwa upande wa Kiwanda chetu cha Madawa, *TANZANSINO*. Hili limezungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, alitaka kuelewa ni kiasi gani cha faida kimeshapatikana kupitia kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka 2003/2004 kiwanda hiki kilipata faida ya Sh. 997,701,928/= katika mwaka 2004/2005. Kiwanda hiki kilipata faida ya Sh. 1,599,942,853/=. Napenda pia nimhakikishie kwamba mahesabu ya kiwanda hiki yako kwa Mkaguzi Mkuu yanakaguliwa na ninamwomba Mheshimiwa Mbunge anaweza kuja akakitembelea kiwanda hiki akaona shughuli za kiwanda zinavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo ilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ilikuwa ni suala zima la kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa ili iweze kuongeza tija. Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ni Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid na Mheshimiwa Jenista Mhagama. Nataka kuwambieni kwamba ushauri wao tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Issa Kassim Issa alitaka kujua suala nzima la Kambi ya Chukwani, bahati nzuri alieleza kwamba Kambi hii iko katika Jimbo langu. Namshukuru kwa kuliona hilo. Lakini nataka nimwambie tu kwamba hadi sasa hivi ninavyozungumza katika Bunge hili, kazi ya upelekaji maji katika Kambi hiyo inaendelea vizuri na kazi ya upelekaji umeme katika Kambi hii inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imetoa Sh. 44,596,988/= kwa ajili ya umeme na imetoa Sh. 49,536,000/= kwa ajili ya usambazaji wa maji katika eneo la Kambi.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na ustahimilivu kidogo pengine katika kipindi cha mwezi mmoja au miezi miwili hali itakuwa nzuri na ninamkaribisha katika Jimbo langu na ninamkaribisha katika Kambi aje anywe maji na sisi tutakayoyasambaza katika Kambi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wametaka au wameomba au wamependekeza *JKT* na *JKU* ziunganishwe. Nataka niseme hivi, katika suala hili, hivi vyombo viwili sio vyombo vya Muungano. *JKT* ina sheria yake inayo Gavana, *JKT* na *JKU* zina sheria yao inayo Gavana *JKU*. Tuziachie Serikali zetu mbili, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa upande wa *JKU* na Serikali ya Muungano kwa upande wa *JKT*. Watakapoona ni wakati muafaka vyombo hivi kuviunganisha, basi watatuleta ushauri huo au mapendekezo hayo au sheria hiyo ya kuunganisha ndani ya Bunge letu hili. Hapo sisi kama ni wasimamizi Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tutavipokea na kufanya navyo kazi.

Kwa hiyo, nasema kwamba hivi sasa ni mapema kulizungumza suala hilo. Waheshimiwa Wabunge tuwe wastahimilivu kidogo. Hoja hii ilizungumzwa na Mheshimiwa John Malecela na Mheshimiwa Ali Said Salim. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine lililozungumzwa katika upande wa *JKT* lilikuwa ni suala zima la kukitumia chombo hiki kama ni jiko la kutengenezea vijana ili waweze kuajiriwa katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Lucy Mayenga, kwa kutoa hoja hii. Nataka nimwambie kwamba huo ndiyo utaratibu ambao sasa hivi tunaufanya katika Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2001, hadi hii leo, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ukiachilia mbali hao ambao wako katika mafunzo walioanza katika mwezi uliopita, wamechukuliwa vijana 2,466 kutoka *JKT;* Polisi wamechukua vijana 21 kutoka *JKT*; Usalama wa Taifa wamechukua vijana 50 kutoka *JKT*; Magereza wamechukua vijana 461 kutoka *JKT*; *TANAPA* wamechukua vijana 200 kutoka *JKT* na vyombo vya ulinzi binafsi wamechukua vijana 1,174 kutoka *JKT*. Tutaendelea kuwahamasisha wenzetu wachukue vijana kutoka *JKT*.

Mheshimiwa Spika, lakini la msingi hapa, kila chombo kinategemeana na sifa wanazozihitaji kutoka kwa vijana wale. Inawezekana tukawa na vijana wengi wa *JKT*, lakini hawana sifa za kuweza kuingia katika chombo fulani. Lakini tutajitahidi vilevile kuwashauri vijana wetu na wananchi wetu wanaojiunga na *JKT* wajiunge wale ambao wana sifa ili sifa zile ziweze kuwafaidia hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wetu wa Bunge Mheshimiwa Jenista Mhagama alitaka kuelewa suala nzima la ukarabati wa Kambi ya Mrata *JKT*. Nataka nimhakikishie kwamba hakuna kambi ya *JKT* hata moja tutakayoiacha katika suala la ukarabati. Kitakachogomba hapa ni muda tu. Leo tutaanza kambi hii kulingana na hali yetu ya kifedha na kesho tutaanza kambi ile kwa kulingana na hali yetu ya kifedha. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe mstahimilivu. Lakini kama nilivyosema, kwamba, haya makambi ambayo *on going* tuliyonayo tutaanza nayo kuyafanyia ukarabati na

kuyaboresha zaidi kabla hatujaanzisha makambi mengine. Namwomba Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa heshima na taadhima awe mstahimilivu, atupe muda tuweze kutafakari mambo yetu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy Mayenga alitaka kuelewa hizi Taasisi za Ulinzi *(Security Companys)* zichukue vijana kutoka *JKT*. Nataka nimhakikishie kwamba utaratibu wa kuwachukua vijana kama nilivyoelezea upo na vijana 1,174 wameshachukuliwa. Lakini tutaendelea kuzihamasisha hizi *Security Company's* kwa sababu watakapochukua vijana kutoka *JKT* tayari yule kijana tumeshampika, ameshapikika na tunawaelewa vijana ambao sio wakorofi. Kwa hiyo, itakuwa ni vyema tutawapatia vijana ambao ni wazuri kuliko kwenda kuokota vijana wa vichochoroni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kuwahamasisha au kuyahamasisha haya Makampuni ya Ulinzi ili yaweze kuchukua vijana kutoka *JKT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala ambalo liliulizwa au kulikuwa na hoja iliulizwa kutoka kwa kaka yangu Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir. Alisema hivi, anaiomba *JKT* iongeze idadi ya vijana kutoka Zanzibar wanaojiunga na *JKT* badala ya kuwa ni vijana 60 tu. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir mawazo yake ndiyo tuliyonayo sisi pale Wizarani na *JKT*. Mwaka huu tumechukua vijana 112 kutoka Zanzibar ambao wamejiunga na *JKT,* sio vijana 60, tumeongeza kutoka vijana 60 mpaka vijana 112. Kwa hiyo, kila tutakapokuwa na nafasi, nataka nimhakikishie kwamba tutaongeza hawa vijana kwa sababu lengo letu ni vijana wote wapate mafunzo ya ulinzi na ukakamavu.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir alitaka vilevile kuelewa jinsi tunavyoimarisha michezo Jeshini. Nataka nimhakikishie kwamba hivi sasa tumeshaandaa Mkutano wa pamoja baina ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ili kuona ni jinsi gani tutakavyoweza kushirikiana katika kuimarisha michezo ndani ya Jeshi. Tuna imani kwamba tukiimarisha michezo ndani ya Jeshi, nchi yetu itapata medali za dhahabu nyingi, kwa sababu ya *discipline* iliyoko ndani ya Jeshi.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kama ana mawazo zaidi ya kuweza kuwasaidia wanamichezo waliomo ndani ya Wizara yangu, namwomba na ninamkaribisha Ofisini aje tushirikiane, tufanye uchambuzi wa mawazo yake ili tuweze kuyafanyia kazi kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kidogo nitoe maelezo ambayo Mheshimiwa dada yangu Getrude Mongella ametaka kuyafahamu katika mchango wake wa maandishi. Ameeleza kwamba, kuna vijana wa *JKT* Buhemba walipelekwa katika Kisiwa cha Kwerumto, akatuuliza sisi je, *JKT* Makao Makuu inayo taarifa hiyo? Kwa sababu hao vijana wamekwenda bila ya uongozi wa Wilaya kujulishwa. Nataka nimhakikishie kwamba, taarifa hiyo sisi tunayo. Hawa ni wavuvi na walikwenda katika Kisiwa kile, ndugu zangu wanaokaa katika Visiwa wanaelewa, wamekwenda kupiga diko kwa

maana ya kwamba kukaa pale ili kuvua na hatimaye kupata mazao mengi na mengine kuyatumia kwa matumizi yao kama ni *JKT* Kikosi na mazao mengi kuyauza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Getrude Mongella vilevile alitaka kujua kwamba hawa vijana walioko pale waligombana na wananchi. Amesema tutafanya nini ili kudumisha amani katika eneo hilo? Nataka nimhakikishie kwamba amani imesharudi. Lakini tutakachokifanya sisi ni ku-*sensitize* vijana wetu wa *JKT* waishi vizuri na wananchi katika maeneo waliyopo.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile, kwa kupitia Bunge hili Tukufu, nawaomba Waheshimiwa Wabunge ambao wana Kambi za Jeshi na Kambi za *JKT* wawa-*sensitize* katika maeneo yale kuishi vizuri na wanajeshi walioko katika maeneo yale. Kwa sababu hii inawezakana huyu akamchokoza yule na huyu akamchokoza huyu. Kwa hiyo, nataka tusaidiane. Kwa upande wetu sisi tutachukua jitihada hizo kuwaelimisha hao vijana wa *JKT* na kwa upande wenu Waheshimiwa Wabunge nawaombeni mchukue jitihada hizo kuwaelimisha wananchi wetu, kwa sababu hawa wote ni Watanzania na tuna imani kubwa sana ya maisha yao.

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie hoja ambazo zimekuwa *raised* na kaka yangu pale Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, nataka nimwambie ushauri wake wa kuboresha na kunyanyua hadhi ya *JKT* sio kama ilivyokuwa, nataka nimhakikishie kwamba lengo letu kuliko ilivyokuwa ndiyo lengo letu. Namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira kwa sababu ndiyo tumeanza na hii ari mpya na *speed* hii haitapungua, itakwenda hivi hivi. Kila mwaka aje, nitamwonesha mabadiliko ndani ya *JKT* na nataka atuamini. Nataka amwamini Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya aniamini mimi na Mkuu wa *JKT* mpya. Tutafanya kazi usiku na mchana kuboresha *JKT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe alieleza kwamba kama Shilingi milioni 500 wangepewa *JKT*, basi *impact* ingeweza kuonekana. Hili ni wazo lake, inawezekana ikawa hivyo na inawezekana ikawa vinginevyo. Lakini nataka nikubaliane naye na mimi nataka nimuahidi tu kwa sababu hizi Shilingi milioni 500 pamoja na ile *project* ambayo tumeipata kupitia Semina ya Kilimo iliyokuwepo juzi, sisi kama *JKT* tutazifuatilia tuweze kuona kama na sisi tunaweza tukashiriki katika miradi ya aina hiyo ili iweze kuwasaidia vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nimeshaunga mkono hoja, nawaomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri na sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi wa Kujenga la Taifa ili amalizie na kuhitimisha kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kufafanua hoja za Waheshimiwa Wabunge ambao kwa kweli zimekuwa tajiri sana na tutajitihidi kuzijibu. Kwa hali ilivyo, nitajitahidi kuzijibu karibuni zote. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nianze kwa kuishukuru sana Kamati yangu ya Ulinzi na Usalama kwa mchango wao ambao wameutoa hapa ambao umewasilishwa na Makamu Mwenyekiti ambaye alikuwa ameteuliwa na wenzake. Nashukuru sana, ni michango ambayo inatusaidia sana katika kufanikisha malengo ya Wizara.

Pili, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Kivuli, ndugu yangu Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim ametoa mchango ambao kwa kweli unaendelea kujenga na kuendelea kutupa mawazo mapya katika Wizara. Namshukuru sana na hii ni dalili kwamba tutaendelea kushirikiana kwa kila hali. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii kumbe inapendwa sana na Watanzania kwa sababu japokuwa tumepewa siku moja, lakini waliochangia katika Wizara ni Waheshimiwa Wabunge 82. Kwa hiyo, mimi inanitia moyo sana kwamba ninaoongoza Wizara ambayo Watanzania mnaipenda na mko tayari kutoa muda wenu kusoma na kutafakari ili muweze kuchangia na hatimaye kuboresha utendaji wa kazi katika Wizara. Nawashukuruni sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuwataja na kuwatambua Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo: Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa mdomo ni Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah ambaye ndiye alikuwa amewasilisha mawazo ya Kamati ya Ulinzi na Usalama. Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa John Samwel Malecela Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Abdallah Sumry, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee. Hawa ndiyo waliopata nafasi ya kuchangia kwa mdomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Mossy Sulemain Mussa, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Vuai Khamis, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Wilson

Masilingi, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Mwinchoum Musomi, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha na Mheshimiwa Aloyce Kimaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Mohammed Chombon, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Lucy Nkya, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na Mheshimiwa Esther Nyawazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu ni Mheshimiwa Mariamu Kasembe, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Chacha Wangwe, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Janeth Masssaburi, Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah na Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Kwa jumla ni karibu Waheshimiwa Wabunge 82. Nawashukuruni sana kwa michango yenu. *(Makofi)*

Meshimiwa Spika, yaliyochangiwa yote kwa kweli sisi yanatusaidia kama nilivyosema, nitajitahidi kujibu karibuni hoja zote baada ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuzipunguza, kama itakuwa hoja nyingine zimeshindikana, basi tutazijibu kwa utaratibu ambao Mheshimiwa Spika, umetuelekeza wa kutengeneza *table* hivi. Halafu tunatoa majawabu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Malecela katika hoja ambazo hazijajibiwa alishauri tushirikiane na *NSSF.* Huu utaratibu tumekwishaanza na hivi sasa mazungumzo yamefika hatua ya mbele sana.

Vilevile Mheshimiwa John Malecela alizungumzia ulinzi wa mipaka yetu. Inashauriwa kwamba, mwambao wa Ziwa Tanganyika pale tunaona kama kuna kitu kimelegalega. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa John Malecela uharamia wa Ziwa Tanganyika tunaujua. Tumeanza kuchukua hatua za kudhibiti uharamia huo na hatua za mwanzo ambazo tumeanza kuchukua ni kuhakikisha kwamba tunawapatia vijana wetu zana za kuweza kukabiliana na hao maharamia. Wanapokuja, wanakuja na boti kubwa zaidi. Sisi tumeanza kununua boti za *Horse Power 75.* Lakini hivi karibuni tumeongea tena na Serikali, tuangalie upya jinsi ambavyo tunaweza tukatoa boti hizo kubwa zaidi ili kuhakikisha kwamba tunapambana vilivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hospitali za Majeshi zinatibu asilimia 80 ya raia, ni kweli zipewe vifaa na madawa ya kutosha. Hili tutaendelea kulizingatia kadri ya uwezo wa Serikali unavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwaenzi mashujaa wetu ambao walifia Namibia, *South Africa,* Zimbabwe na kadhalika, hili nalo tunalipokea kama wazo, Mheshimiwa John Malecela tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ali Said Salim, amesema yupo Askari ambaye yupo kule Pemba, hali yake ni taabani, amenialika niende Pemba ili nikamwone. Napokea mwaliko huo, nitakwenda. Napokea pongezi zake kwa kile Kikosi cha Alhamisi ambacho kinafanya kazi nzuri wakati huu na yeye anatambua. Vile vile, alizungumzia nafasi za Jeshi zigawiwe katika maeneo yote. Sio kweli kwamba kwa kufanya hivyo kutaligawa Jeshi kama nilivyojibu siku ile. Siku ile labda sikueleweka sawasawa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nizungumzie kuhusu nafasi. Nafasi zinapotengewa na Serikali kwamba mwaka huu ajirini vijana kadhaa, tunachofanya kwanza tunaangalia ni nafasi ngapi tuzitenge na tuzipeleke Jeshi la Kujenga la Taifa kama wanavyoshauri Waheshimiwa Wabunge, zinazosalia tunazigawa kwa Mikoa yote 26 ya nchi hii. Kwa maana hiyo, ni Mikoa mitano ya Tanzania, Visiwani inakuwa imezingatiwa. Kwa hiyo, hapo hakuna kusema kwamba eti Jeshi litagawanyika, hapana. Hiyo ni *formular* ambayo tunaitumia kuhakikisha kwamba tunapata vijana wanaokuja kuunda Jeshi la Wananchi na liwe na sura kweli ya Jeshi la Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilichozungumza siku ile, ni ule utaratibu wa kutaka kulifanya Jeshi, tunapotaka kupandisha vyeo, tuanze kukaa na kusema Wazanzibar wangapi mwaka huu watapanda vyeo, Wakurya wangapi mwaka huu watapanda vyeo, Wanyamwezi wangapi mwaka huu watapanda vyeo, hicho ndicho tulichokataa. Kufanya hivyo ndiyo kutaligawanya Jeshi. Kwa sababu kufanya hivyo utakuwa na wanajeshi ambayo *loyalty* yao haiko Jeshini, au wana-*refer* huko Jeshini, bado wanakumbuka kambi walizotoka. Ndiyo hayo tunayoyaona yanayotokea Somalia, ni kwa sababu hiyo hiyo. Watu wanapelekwa Jeshini, lakini badala ya kuwa waaminifu na watiifu kwa Jeshi, wanakuwa watiifu kwa watu waliowatuma. Sasa hiyo tuikwepe sana. Hicho ndicho nilichozungumza siku ile, sikuzungumza kwamba ajira nayo iwe ya mahali pamoja, hapana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maduka ya Jeshi kwamba watu wanayatumia maduka ya Jeshi kujitajirisha, hawapunguzi bei na wala hawakopeshi. Udhaifu huu tumekwishau-*note* na tumeshapata taarifa kule katika vyombo vyetu na tatizo lililokuwepo ni kwamba tulikuwa na mikataba ambayo inatufunga. Wale walikuwa na mikataba ya miaka mitano. Kwa hiyo, kuivunja mikataba ile, pengine tungeshitakiwa, ingeleta matatizo makubwa. Kwa hiyo, tulichofanya, tumesubiri mikataba ile ambayo hivi sasa karibuni yote inakwisha. Kwa hiyo, mikataba ile tunaanza kuandaa taratibu mpya za kupata wazabuni wapya ambao watakuja kuhudumia maduka yale ya Jeshi. Tutakuwa waangalifu, tunashukuru na tunapokea ushauri wenu.

Mheshimiwa Spika, Kikosi cha Chukwani kipatiwe vyoo na umeme, kina matatizo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba matatizo tunayajua. Mheshimiwa Naibu Waziri alishakwenda akaandika ripoti aliporejea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy Mayenga, nataka nimpongeze sana kwa michango yake mahiri, kwa kweli nadhani alifanya utafiti katika majeshi yetu haya.

Mengi ameshayajibu Naibu Waziri. Lakini nataka nirejea pale aliposema *JKT* itumike kama moja ya vyanzo vya ajira. Naibu Waziri ameeleza jinsi ambavyo tunashirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama katika kuchukua vijana wetu. Lakini hatuishi hapo.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge kulikuwa na kundi kubwa la vijana wa *Operation* Miaka 40, walikuja hapa Dodoma karibuni 200, wanasema wao wamekuwa katika Jeshi la Kujenga la Taifa na wamekaa kule miaka minne, yaani baada ya miaka miwili ile ya mkataba, wakaendelea kuchukuliwa kwa miezi sita sita. Sasa walisema ajira imekuja Jeshini wameachwa.

Mheshimiwa Spika, ajira ya Jeshini ina vigezo, kwanza ni umri usiozidi miaka 23; pili, usiwe na Elimu ya Darasa la Saba, uwe na Elimu ya Kidato cha Nne. Sasa hao vijana walikuwa na Elimu ya Darasa la Saba na wengine walikuwa wameshavuka umri. Walisema, lakini kwa nini kama tulijua hayo, tuliendelea kuwaweka? Baada ya miaka miwili tungeliwaachia wakaanza kujitegemea. Kwa hiyo, nilizungumza nao nikawaambia, basi ngojeni, tuanze kuangalia kama tunaweza tukapata vyanzo vingine vya ajira.

Kwa bahati nzuri tumeweza kupata ambaye anaweza akawaajiri vijana wote wale 235 waliokuwa wamekuja hapa. Leo hii nasikia wawakilishi wao 20 wapo hapo nje wakiongozwa na Ndugu Wambura. Ndugu Wambura kama ananisikia, kama akija kesho nitampa anwani ili ndani ya siku 45 vijana wote 235 watakuwa wamepata ajira kwa mwajiri huyu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya iwe na ushirikiano na Wizara ya Ulinzi hasa kwa kutembelea Hospitali za Jeshi. Mheshimiwa Waziri wa Afya wa sasa analijua hilo na tunashirikiana kwa karibu sana. Tumeshamweleza hata namna ambavyo tunaweza tukasaidiana kutuongezea madawa katika hospitali zetu. Tukitoka hapa tunaendelea kwenda kulifanyia kazi tuone jinsi ambavyo tunaweza kushirikiana kwa sababu kwa kweli zile hospitali kwa kiasi kikubwa ni hospitali za wananchi.

Sasa hili lingine la Mheshimiwa Mayenga, Wakimbizi waondolewe kwa mbinu za Kijeshi. Hili kama alivyosema mwenyewe, lina mambo yake, lazima twende nalo kiutaratibu kwa sababu vinginevyo tutaharibu sura nzuri, sifa nzuri ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hii haitatusaidia sisi na wala haitamsaidia yeye.

Mheshimiwa Spika, ni lazima twende kwa utaratibu, tutajitahidi kila inavyowezekana tuone namna ambavyo kuwashawishi wenzetu na kutumia mbinu mbalimbali ambazo tutaweza kuhakikisha kwamba wanaondoka. Ni kweli lakini nataka nimhakikishie kwamba, wale wanaofanya makosa makubwa wanakamatwa na wanashtakiwa. Ndiyo maana huu ushirikiano mnaouona kati ya vyombo hivi vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, tuna ushirikiano mkubwa sana, tunapashana habari, tunawashughulikia. Kama kuna ambao bado wako *at large* hawajakamatwa, tuletee taarifa, hatutalaza damu.

Mheshimiwa Spika, kuna swali liliulizwa kwamba *Chief of National Service (CNS)* mbona yeye haapishwi na Rais? Watu wanasema mazoea yana taabu au kawaida inakuwa kama sheria. Ni kweli huko nyuma Makamanda au Wakuu wa Jeshi la Kujenga Taifa nao walikuwa wakiapishwa, lakini ilikuwa ni nje ya sheria. Kwa sababu Jeshi la Kujenga Taifa ni Kamandi kama zilivyo Kamandi nyingine. Tuna Kamandi ya *Navy*, Anga na hivi sasa tunaunda Kamandi ya Majeshi ya Miguu au Majeshi ya Ardhini. Sasa ukimwapisha huyu Mkubwa wa Kamandi hii ya Jeshi la Kujenga Taifa maana yake unataka na Makamanda hao wengine wote nao waapishwe kitu ambacho hakiendani na utaratibu wetu.

Tunajua kwamba ni wadhifa mzito, lakini wadhifa wa mtu anayesimamia ndege zote zile ambazo zinzkwenda kupigana wakati wa vita sio mdogo. Wadhifa anaobeba Kamanda wa Majeshi Ardhini sio mdogo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa hawa wawili wanaoapa, wanaapa kwa niaba ya wenzao. Lakini hata wao vile vile wanapoanza kuingia katika Uafisa wa Kijeshi wanaapa kutii kwa Amiri Jeshi Mkuu. Kwa hiyo, yote yamezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Haji Juma Haji, Askari waajiriwe hata Darasa la Saba. Darasa la Saba hivi sasa bado tunawaajiri katika nafasi chache zile za michezo, kwa sababu michezo haizingatii kusoma, inazingatia kipaji. Unaweza kuwa umefika mpaka Chuo Kikuu, una *PHD* lakini inapokuja kwenye kukimbia ukapambana na Mbarbaig mmoja kutoka Babati atakuacha tu. Kwa hiyo, hii tunaendelea kuzingatia. Tunatoa nafasi, lakini katika sehemu nyingine za Kijeshi inakuwa ngumu ndugu zangu, kwa sababu Majeshi ya Dunia hii yanabadilika, yanakuwa ni Majeshi ya kitaalamu kweli kweli.

Sasa umtoe kijana wa Darasa la Saba mpaka umfikishe mahali ambapo anaweza akaelewa *electronics* za Majeshi ya kisasa, ni kazi ngumu zaidi. Kwa sababu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi sasa hivi ina mkakati wa kujenga Sekondari katika kila Kata. Hili tatizo la kusema vijana wa Darasa la Saba ndio wawe wanaajiriwa katika Jeshi litajiishia lenyewe kwa sababu vijana wa Kidato cha Nne watakuwa wengi sana na baadaye mtaanza kupiga kelele tena Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abdallah Salum Sumri kwanza naomba nimpongeze kwa mchango wake, lakini hasa kwa mchango wake wa kutupatia boti ambayo ina *horse power* 75. Imetusaidia sana pale Ikola. Tunamwomba Mheshimiwa Sumri na Wabunge wengine waige mfano wa Mheshimiwa Sumri. Lakini suala la kujenga barabara, sasa hili ningeomba tu tuelekeze nguvu zote, sisi sote kuishawishi Halmashauri yetu, tukigeuza kwamba Jeshi liwe linajenga na barabara zile za kwenda kule katika vituo kama vile Ikola tutakuwa tumelipa jukumu ambalo ni jipya. Jeshi linaingia katika ujenzi wa barabara inapokuwa ni dharura, Jeshi linaingia katika ujenzi wa madaraja inapokuwa ni dharura na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, *JKT* waajiriwe kama Maafisa Ugavi wa Kilimo Vijijini kwa sababu kule *JKT* wanafundishwa masuala ya kilimo bora. Tunavyo Vyuo vya Kufundisha Maafisa Ugavi.

Mheshimiwa Spika, Labda nitashauriana na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwamba pengine na yeye angechukua hii *pool* akawa anaipeleka kule kama inawezekana kuongezewa utaalamu wa kuweza kuwasiliana na wakulima ili ndio waweze kuajiriwa kama Maafisa Ugavi. Lakini kuwaajiri moja kwa moja itakuwa kazi kwa sababu yako mambo mengi ambayo sisi hatufundishi kama Maafisa Ugavi. Sisi tunafundisha wakulima wakalime kwa utaratibu wa *modern agriculture,* kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, aliomba wastaafu walipwe mafao kwa wakati, pensheni stahili na wapewe mikopo midogo midogo. Mikopo midogo midogo wanapata, tatizo tulilonalo ni kwamba mpaka sasa bado wanaruhusiwa kukopa katika Benki moja tu na hili wameshaliwasilisha kwetu. Kwa hiyo, tunalifanyia kazi. Mikopo midogo midogo wanapata, bado hatujaingia katika mikopo ya kujengea nyumba. Hili tunalipokea kama wazo la Waheshimiwa Wabunge, tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tupate haraka wataalamu wa Hospitali ya Bububu, hilo tumelipokea. Ulinzi wa anga utembelee sehemu fulani fulani kwenda kuangalia kule Zanzibar jinsi ambavyo ziko wazi, hazina ulinzi wa aina yoyote.

Mwaliko wa kutembelea naupokea, lakini ulinzi au kufungua kikosi mahali, kunategemea kama eneo lile kweli itaonekana kwamba *strategic* angalau ki-*strategic* ni mahali ambapo tunaweza tukapata hatari ya Kitaifa. Mimi nitakuja kutembea, lakini siji na jawabu la kusema kwamba nakuja sasa kuhakikisha kwamba kikosi kinafunguliwa, hapana. Tutakayoyaona tutawasilisha katika Wizara na tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ruth Msafiri anasema Serikali itenge fungu la mapato ya ndani ya nchi ili kuyafufua Mashirika au kuyapa uwezo Mashirika yetu ya Nyumbu na Mzinga. Mheshimiwa Ruth Msafiri, hivi ndivyo tunavyofanya. Hizo fedha tunazozipata ni kutokana na Serikali kutenga mapato kutoka makusanyo ya ndani ya nchi. Uongozi wa Mashirika haya una wasi wasi kwamba umekuwa wa kiraia zaidi kuliko wa Kijeshi.

Nina hakika kama ningewapanga foleni hapa, ungewaona jinsi ambavyo hasa Nyumbu na mimi mwenyewe nimefika, ungeona jinsi ambavyo asilimia kubwa ni Wanajeshi kuliko raia. Raia wako katika zile *supportive posts*. Lakini katika zile nafasi za kuamua na kubuni ni Wanajeshi wenyewe. Kama ungemwona Col. Mashauri hapa, ungefurahi tu.

Mheshimiwa Spika, Askari wa Kaboya wana matatizo ya *ration.* Nadhani tutajibu katika mlolongo mwingine. Wapewe mikopo, nimeshazungumza, wapewe basi la kuwapeleka Mkoani na Wilayani. Usafiri kwa ujumla katika Jeshi letu la Wananchi kwa

muda mrefu umekuwa na matatizo kwa sababu magari yaliyokuwepo yamenunuliwa kwa muda mrefu na yamechakaa. Tukawa tunatumia fedha nyingi katika kuyakarabati.

Nilipokuwa nikisoma Bajeti hapa, nimesema katika kuimarisha Jeshi letu moja ya vitu ambavyo vinaendelea hivi sasa, tumeshalipa awamu ya kwanza ya malipo ya kununua magari. Magari yanayonunuliwa ni 628 yakiwemo na mabasi na magari ya kivita.

Kwa hiyo, tutaangalia katika kupanga kipaumbele tuone Kaboya tunaweza tukaifanyia nini. Ndiyo maana uliniona katika Mawaziri ninaosisitiza katika kuwashukuru Waziri wa Fedha. Sikumsahau kwa sababu kwa kweli ananisaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, sasa hili la kupiga shabaha sikulisikia sawa sawa. Kama alikuwa anashukuru, basi napokea shukrani, lakini kama alikuwa anaomba kwamba tutoe kibali, hili nilishaongea na Mheshimiwa Shellukindo. Kwa sababu nilikuwa nasafiri, nikamwambia jiorodhesheni Waheshimiwa Wabunge mumwone Mheshimiwa Naibu Waziri atawasiliana na Makutupora, mtakwenda mkashinde huko mnapiga shabaha, hatuna matatizo. Kama hali hiyo bado ipo mpaka leo, sisi tuko tayari.

Mheshimiwa Spika, suala kuhusu Waziri atembelee Zanzibar hususan Kambi ya Potoa, niko tayari kutembelea. Lakini taarifa, nataka nikuhakikishie kwamba ninazo, Mheshimiwa Naibu Waziri alishatembelea kule na ni hodari kweli kweli wa kuandika ripoti za kina.

Mheshimiwa Spika, suala la likizo wakati mwingine Wanajeshi wanaweza wakakiuka miaka likizo yao kutokana na jinsi ambavyo kazi zao zinavyowahitaji pale walipo. Sasa tusione kwamba ni tendo la ukatili. Lakini ni kweli kwamba wanastahili kwa kila mwaka kwenda likizo na wanapokwenda tunapaswa kuwalipa na kwa kiasi kikubwa tumejitahidi, ndiyo maana hatuna malimbikizo makubwa ya madeni katika Jeshi la Wananchi wala Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa kweli kwa hapo Serikali naishukuru jinsi ambavyo inawahudumia Wanajeshi.

Mheshimiwa Spika, *JKT* itaondoa *idle time* kwa vijana wetu, nadhani hili amelieleza Mheshimiwa Naibu Waziri. Suala la Shilingi milioni 500 amelieleza Naibu Waziri, Ndugu Mwakyembe. Hili la Shilingi milioni 500 tatizo lililopo ni kwamba mpaka sasa, sisi tunachukua sehemu ndogo ya vijana, tunachukua vijana 3,000. Zingatia vijana walioko katika nchi yetu hii. Ni wengi kweli kweli kwa sababu asilimia 60 ya Taifa hili ni vijana. Sasa wanaobaki kule, kama hizi fedha zote zikielekezwa katika Jeshi la Kujenga Taifa, wanaobaki kule wafanyeje?

Nadhani ndiyo maana hekima zikatumika na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu mwenyewe kuhakikisha kwamba wanajaribu kutafuta namna ambavyo wakasaidia vijana walioko Mikoani. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu

Waziri, nasi tutaangalia jinsi ambavyo tukashirikiana na wenzetu katika kuvuna Shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Spika, mpaka wa Malawi baada ya vita vya Nduli Idd Amin sasa uko shwari. Mheshimiwa Mwakyembe kwa Kiingereza wanasema *it is apparent*. Yaani ni *apparent peace which you are seeing*. Iko shwari kwa sababu Tanzania imeamua kukaa kimya, lakini wenzetu wanaendelea ku-*extend*.

Kwanza ziwa haliitwi Ziwa Nyasa, linaitwa Ziwa Malawi, halafu vile vile mpaka ule wameusogeza badala ya kupita katikati ya Ziwa uko nje ya Ziwa. Tumeunda Tume sasa ya nchi kadhaa ambazo nitazisoma huko mbele na kujaribu kuzingatia matatizo ya mipaka hii ili tuhakikishe kwamba tunapata ufumbuzi wa suala hili. Kwa hiyo, unaweza ukaona pametulia lakini kwa sababu sisi ni waungwana, tumeamua kusema tusigombane, kama linaweza kuzungumzika, kwa nini tusizungumze na hii ndiyo sera ambayo Tanzania iliyonayo Kimataifa na ndiyo inayoendelea kuipa heshima nchi yetu. tunaamini Malawi ni ndugu zetu, tutaelewana.

Yale maeneo ambayo unasema wananchi wanakodishwa, hiyo ni haramu na hilo ni kosa na kama unawajua wanaokodisha, tupatie ili tuwashughulikie. Ardhi ile ni mali yetu wote kwa maana ya Jeshi la Wananchi, lakini ule mtambo uliojengwa pale nataka kuhakikisha kwamba hatuna wazo la kuuhamisha. Ni rada ambayo inatusaidia sisi kuangalia maeneo yote yale yaliyoko pale na rada ile imelazimika kuwekwa chini kuliko rada nyingine zinazowekwa juu kwa sababu kule kulikuwa kuna ujanja wa kuleta baadhi ya ndege chini chini ili zisiweze kuonekana kwa sababu rada ina upeo fulani. Ukiweza kuruka chini kidogo, basi huonekani.

Mheshimiwa Spika, kama utakumbuka vile vita vya siku saba vya Israel walipokuwa wakipambana na Waarabu walipokwenda kuipiga Egypt, ndege zake zote ziliruka kiwango cha chini kabisa. Kwa hiyo, rada za Egypt hazikuweza kuona, wamekuja kushtukia adui ameshafika ndege zao zote zimeshapigwa na kiwanja kimefumuliwa. Ndiyo maana tunasema hatuwezi kuachia hapo na rada zitabaki katika ngazi hiyo. Lakini wananchi wenye hitajio kama ardhi ipo na sisi hatuitumii tutaendelea kuwaruhusu walime ila wasipande mazao ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, bado Mheshimiwa Mbunge anasema vijana waliosoma Jeshini hawajaliwi sana, kwa hiyo anaomba Wizara iangalie hili suala. Nalipokea na tutaendelea kuzungumza na Makamanda ili kuhakikisha kwamba kweli taaluma nayo inapata stahiki inayostahili.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge hoja zingine ambazo zilijitokeza za uwekaji wa mipaka ya Kimataifa na ulinzi kama nilivyozungumza tumeunda Kamati Maalum ambayo inasimamiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kuweka mipaka ya Kimataifa majini kwa nchi za Malawi, Msumbiji, Comoro na Shelisheli.

Lingine lililojitokeza ni uvamizi wa maeneo ya Jeshi unaofanywa na wananchi. Hili namshukuru sana aliyewasilisha hapa, kwa sababu angalau ameliweka katika sura ya sawasawa. Mara kwa mara huwa tunaambiwa sisi, ninaposema sisi maana yake ni Wanajeshi wetu ndio wanaovamia maeneo. Sio kweli . Wanajeshi kwanza hawaingii mahali mpaka wamepewa, lakini wanapopewa, kwa sababu wao mahitaji yao ni maeneo makubwa, wanapewa maeneo makubwa yanayotosheleza mahitaji yao ya leo na ya kesho. Sasa kwa sababu yanaonekana yako tupu, basi wananchi mmoja mmoja anaingia, mara huyu anajenga kama ka-*kiosk* cha kuuza biskuti, mwingine anajenga vitu gani, baada ya muda tayari unaona nyumba zimeanza kuenea pale, baadaye inaonekana kama Jeshi ndilo limevamia. Hatuvamii, Jeshi linapewa ardhi. Ndiyo maana zoezi la kupima maeneo ya Jeshi kwa ajili ya kumilikishwa kisheria linaendelea kama lilivyoelezwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuendesha operesheni za pamoja, Jeshi la Polisi na vyombo vya dola, hiki ni kitu cha kawaida katika nchi yetu. Nchi nyingine zinatushangaa, tunawezaje? Kwa sababu kwa kawaida, Jeshi la Polisi na Jeshi la Ulinzi huwa kuna mapambano ya aina fulani fulani ya kimya kimya, hawaelewani hawasemeshani, lakini hapa Tanzania kwa maelezo tuliyoyapata, Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi ni kitu kimoja. Wanakaa, wanazungumza kuendeleza mapambano. Nchi jirani hapa na Watanzania kazi yetu kusema. Kwa mfano wenzetu Kenya wanakuja kujifunza kwetu jinsi ambavyo Majeshi yao yanaweza yakafanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Spika, uhusiano wa Vyuo Vikuu kwa ajili ya kupata wataalamu zaidi, huu ushauri tunaupokea na tutaufanyia kazi, Wanajeshi kulipwa stahili zao hasa wastaafu na Marehemu. Stahili za wastaafu zinalipwa kwa wakati, kasoro zipo katika maeneo yahusuyo usahihi wa nyaraka na maamuzi ya wasimamizi wa mirathi, hili nalo tunaomba msaada.

Wakati mwingine, kweli makosa ni yetu, siwezi kukataa. Lakini wakati mwingine ni makosa ya wale ambao wanaotaka kuchukua mirathi, wanagombana kweli kweli humu, inakuwa ni matatizo. Hivi sasa tunayo kesi ya Lt. Kanali mmoja ambaye alifariki mwaka wa sita huu, baba ameng'ang'ania yeye ndiyo apewe mirathi wakati kuna mke na watoto.

Sasa Mahakama hiyo inashindwa kutamka na sisi tumeshindwa kulipa. Kila akija tunasema hatukulipi kwa sababu tunajua wewe utakwenda kuzitumia tu. Mahakama ikasema wakae Kikao cha Kiukoo kama ikimteua basi watampa yeye mzee, amekwenda amesema kama ni Kikao tu, hamna tatizo. Ameorodhesha majina akasaini. Sasa mambo kama haya lazima tuyaangalie.

Lakini la pili, vile vile tuna wale ambao tayari mirathi yao tumekamilisha na *cheque* zipo. Zaidi ya *cheque* 250 ziko pale zinasubiri watu kuja kuzichukua, hawaji. nyingine za miaka karibuni 14 iliyopita. Mwaka 1992 aliyekuwa Waziri wa Ulinzi akaleta akachapisha vitabu akaleta akawagawia Waheshimiwa Wabunge wasaidie katika kuwatambua wale wanaotafutwa kuja kupokea urithi, mpaka leo bado tunazo *cheque* hizo hazina wenyewe.

Ajira kwa Wanajeshi itokane na *JKT,* nadhani tumeshajibu. Wataalamu wanaostaafu waajiriwe kwa mkataba: Kwa sasa utaratibu tulionao ni kuongeza muda wa utumishi kulingana na mahitajio, wazo la kuajiri kimkataba litafanyiwa kazi. Aidha, juhudi za kuandaa Wanajeshi vijana zitaimarishwa. Kwa sababu kwa kweli unajua kama jinsi ambavyo sehemu nyingine zote zilikuwa katika ajira na Jeshi lilisimama. Sasa kumbe katika Jeshi ni hatari zaidi kwa sababu tulionao sasa karibuni wote wanatakiwa watoke, patabaki wazi kabisa.

Sasa mawazo kama haya mnayotupa Waheshimiwa Wabunge yatatusaidia sana. Lakini hiyo isiwe ndiyo mbadala wa kuimarisha juhudi za kuajiri Askari vijana. Huwezi kuwa na Jeshi lililojaa Askari wa Mkataba. Hivi kweli kila Mgambo Askari wa Mkataba ndio unategemea wapige mbio kwenda Rwanda, Burundi na *Congo*.

Mheshimiwa Spika, mafunzo nje ya nchi kwa taaluma ambazo hazipo nchini Waheshimiwa Wabunge, hili tunafanya kadri uwezo unavyopatikana kifedha. Jeshi kupata vifaa vya kisasa tunajitahidi tathmini imeshafanywa kuainisha mahitaji ya vifaa. Tunao mpango wa maendeleo wa miaka 15 ya Jeshi na Amiri Jeshi Mkuu alipokuja kututembelea tulimkabidhi na tumeshaanza kuutekeleza mpango huo, ndani yake tumebaini vifaa ambavyo tunavihitaji ili kuligeuza Jeshi letu kuwa Jeshi la Kisasa.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha ulinzi na usalama, mapambano dhidi ya ujambazi sare na Wanajeshi kukaa nje ya Kambi: Haya matatizo tunayajua, lakini suala la ujambazi naomba niongelee wakati mwingine, ni vyema tukafahamu kwamba mimi nafahamu, Waheshimiwa Wabunge mnafahamu, lakini tunao baadhi hasa Vyombo vya Habari wakati mwingine vinapotosha habari. Askari tulionao ni wengi, askari mmoja kwa ubinafsi wake anapoamua kufanya kitendo cha kijambazi halafu kichwa cha habari kinakuwa *JW* nao wahusika, ni kulidhalilisha Jeshi kweli kweli. Mawazo kama haya hatari yake yanaweza yakajenga uhasama kati ya Jeshi na wananchi. Kwa sababu wananchi watakuwa wanaona mtu aliyevaa *uniform* za Kijeshi badala ya kuwa ni mlinzi, wao kumbe ni jambazi ambalo linawasubiri usiku walale liende likawadhuru. Hali kama hiyo ikitokea ni hatari kubwa katika nchi. Tunaomba Vyombo vya Habari vitusaidie hawa wanaopatikana mmoja mmoja ni wao binafsi watakamatwa, watashughulikiwa kama watu binafsi kama walivyo katika Taasisi nyingine zozote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwingine kote duniani Vyombo vya Habari vinapoandika Majeshi ya nchi zao wanakuwa waangalifu kweli kweli. Sisi hapa baadhi ya Vyombo vyetu vya Habari vinataka kuleta kejeli katika Jeshi la Wananchi kama vile unazungumza habari za kawaida tu. Haiwezekani kabisa tuvumilie hali kama hiyo, hatutavumilia. Maendeleo ya vijana walioajiriwa mwaka 2002, utaratibu wa kuajiri vijana, nadhani hili tumeshalieleza.

Maendeleo ya Meremeta, Waheshimiwa Wabunge Meremeta lilikuwa ni Shirika kama yalivyo Mashirika mengine. Lilikuwa linajaribu kutafuta fedha kuisaidia Serikali ili kumudu majukumu fulani fulani ya Kiserikali na Mashirika yake, likagonga mwamba,

limefilisika. Kwa hiyo, hivi sasa kama alivyojibu Waziri wa Nishati na Madini, wakati fulani ndani ya Bunge hili hili hatua za kulifilisi kisheria zinaendelea.

Lakini wakati huo huo tunajua kuna wananchi walioko kule Geita wanahangaika, wanadai tumefanya nini? Tumeshapeleka *cheque* ya Sh. 190,584,970/= ili kulipa madeni yote ya Meremeta yaliyo katika eneo la Geita. Kama kutakuwa na madeni mapya, tutayabaini, tutashughulikia lakini hivi sasa ninavyozungumza na nyinyi Waheshimiwa Wabunge, tangu tarehe 28 mwezi Julai, *cheque* amepokea *DC* wa Geita kwa sababu tumeogopa kwenda kulipa kiholela tu. Akija mtu akasema mimi ndiyo Masanja mwana Shibiliti, simjui. Kumbe Masanja *proper* hayupo, unaweza ukamlipa asiyehusika. Sasa tunategemea *DC* kwa kutegemea vyombo vyake alivyonavyo hapo, aweze kumtambua Masanja Shibiliti ni nani aweze kumlipa huyo anayehusika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa Hospitali ya Nyumbu na maeneo mengineyo, juhudi za kukarabati maeneo yote zinaendelea kuzingatiwa kwa kutegemea uwezo uliopo wa kifedha. Hospitali hii nimeitembelea, ni kweli inasikitisha, lakini jinsi ambavyo fedha zinavyoendelea kuongezeka kutokana na makusanyo makubwa ya Serikali, ndiyo jinsi ambavyo Jeshi hili na Wizara hii inaongezewa uwezo wa kuangalia maeneo na ukarabati umeshaanza katika maeneo, ila ndugu zangu maeneo yalikuwa ni mengi ambayo yalikuwa yameharibika. Sasa tupeni nafasi ili hatimaye tuweze kufika katika Hospitali ya Nyumbu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha zilizotolewa na Serikali kwa mradi wa Nyumbu miaka mitatu iliyopita, Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani anapenda kujua fedha zilizotolewa kwa Nyumbu miaka mitatu iliyopita. Mwaka 2003/04 Shilingi milioni 240, mwaka 2004.05 Shilingi milioni 600 na mwaka 2005/2006 Shilingi milioni 800. Kwa hiyo, kwa miaka mitatu tumetoa jumla ya Sh. 1,640,000,000/=. Mahitaji ya kuendeleza Nyumbu kwa hivi sasa ni Shilingi bilioni saba kwa kipindi cha miaka mitano. Hili nalo tutaendelea kulizingatia polepole kutokana na uwezo ambao utaendelea kujengwa ndani ya Serikali.

Mafao ya wastaafu wa mirathi nimeyazungumza. Kuboresha mishahara na marupurupu kwa Wanajeshi, hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi tu. Kufuatia hotuba ya Waziri wa Utumishi, Serikali imewezesha viwango vya mishahara kuongezeka kwa asilimia 26 mpaka 47 ndani ya Jeshi. Ni nyongeza iliyo kubwa kuliko nyongeza Serikali iliyotoa katika makundi mengine yoyote. Kwa hiyo, tunaendelea na bado Tume ya Rais ambayo imeundwa kutazama mfumo wa mishahara itaendelea kutazama suala hili na kushauri hatua stahili. Nasi tumejipanga vizuri kushirikiana na Tume hiyo kuieleza matatizo yetu, matarajio yetu ili iendelee kutukumbuka.

Migogoro ya ardhi kati ya Jeshi na raia nimeizungumza, kwamba, Jeshi huwa halichukui, linapewa lakini pamoja na hali hiyo tunapobaini pengine bado tumefanya makosa, tunafidia. Ndiyo maana nikaorodhesha maeneo ambayo tumejitahidi kutoa fidia kuhakikisha kwamba wananchi hawa hawadhulumiwi haki zao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Castor

Ligallama, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro haya ndiyo ambayo tulikuwa tunayo ya kusema.

Wale ambao walichangia wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Lucy Mayenga alichangia tena anasema Askari ambao walichukuliwa na Taasisi za nje wanaporudi na ujuzi, uangaliwe utaratibu wa kuajiriwa na Jeshi. Taratibu zinazochukuliwa Ofisa au Askari kwenda taasisi za nje upo kisheria. Kanuni za Majeshi ya Ulinzi, juzuu ya kwanza utawala aya ya 6.09 imeelezea kwamba kwa fungu 44 la Sheria ya Ulinzi wa Taifa linasomeka kama ifuatavyo: "Afisa wa Askari aliyeambatishwa kushikizwa au kuazimishwa kwa madhumuni yoyote yale, ataendelea kuwa Afisa au Askari wa Majeshi ya Ulinzi. Kushikizwa au kuambatishwa au kuchukuliwa kwa Afisa au Askari nje ya Majeshi ya Ulinzi peke yake hakutadhuru muda unaotambulika wa utumishi wake."

Kulingana na maelezo hayo, hakuna Afisa au Askari anayeachishwa Jeshi kwa sababu ya kuchukuliwa na Taasisi ya nje. Mwanajeshi anaporudishwa kutoka alikochukuliwa huendelea na kazi. Ni kama vile umechukua *leave without pay.* Unakwenda kule unafanya kazi, muda ukiisha au kwa sababu zozote wame-*terminate contract* wamekatisha mkataba wako, ukirudi unaendelea katika nafasi yako. Kwa hiyo, hakuna tatizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chacha Wangwe alisema wastaafu Jeshini waongezewe pensheni na walipwe kila mwezi badala ya kulipwa kila badala ya miezi sita. Hawa ndio wanaokuwa majambazi baadaye kama hawajalipwa vizuri. Suala la malipo ya pensheni ni la Kitaifa na linategemea uwezo vile vile wa Kitaifa. Kwa hiyo, kuongeza malipo ya pensheni na utaratibu wa ulipwaji hutegemea maamuzi ya Hazina.

Mheshimiwa Benito Malangalila alishauri vijana wanaopelekwa *detach* mipakani, wasaidiwe kupewa posho ya mazingira magumu. Suala la posho hizi ndani ya Jeshi ni vyema tukawa waangalifu. Tunaweza tukalitumia vibaya tukaligeuza hili kuwa Jeshi la mamluki. Kwa sababu kwa jinsi kazi ya Kijeshi ilivyo, mazingira yao yote ni magumu. Hakuna mazingira rahisi ndani ya Jeshi.

Leo hii anaweza akaambiwa kwamba tuna tatizo Kagera haagi mke wala nani, hapo hapo alipo safari. Hata nguo zitamfuata baadaye. Lakini vile vile, mkumbuke kwa mfano tulipopigana vita hivi tulilipa vita *allowance?* Hatukulipa vita *allowance*.

Kwa hiyo, ni matatizo ambayo tunayajua yapo lakini ndiyo hali halisi, ndiyo mazingira halisi ya kazi. Sasa yapo madogo madogo ambayo tunaweza tukayaangalia, lakini tusisitize sana suala la posho. Ndiyo maana hii posho iliyokuwa ikiitwa Biharamulo *Allowance,* baadaye ilifutwa kwa kuogopa kuwa na Wanajeshi ambao hawawezi kwenda mahali kufanya kazi mpaka akuulize changu kiko wapi nilipe kabisa kabla sijakwenda? Ukiwa na Jeshi la namna hiyo ni hatari. *(Makofi)*

Wanajeshi wanastaafu na baadaye kuajiriwa na nchi jirani. Je, Serikali haioni kuwa hawa wanaweza kutoa siri za nchi? Hili lilichangiwa na Mheshimiwa Janeth

Massaburi. Kwanza Askari anapostaafu haruhusiwi kuchukua ajira yoyote nje ya nchi mpaka apate kibali cha Serikali. Kwa hiyo, akiajiriwa hajapata kibali ni kosa na akiajiriwa akatoa siri ni kosa la uhaini kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nikuhakikishie hawa watachukuliwa hatua za kushtakiwa. Kwanza anashtakiwa ndani ya Jeshi, halafu baadaye ndiyo anapelekwa katika Mahakama za kiraia na wenzetu wana sheria kali kweli kweli. *CDF* akisema mwekeni ndani huyu kama alivyozungumza nadhani kuna mtu amezungumza hapa Mheshimiwa Mbunge amezungumza hapa. *CDF* akisema mwekeni ndani unawekwa ndani, maswali yanakuja baadaye baada ya miezi mitatu, lakini umeshakaa ndani kwanza. Sasa mimi nawaombeni Waheshimiwa Wabunge kwamba haya ni masuala ambayo sisi kama waangalizi wa Jeshi tunayatilia maanani sana.

Kwa nini kwenye Jeshi kuna madeni wakati fedha za matumizi ya kawaida wanapewa Watendaji wa Jeshi? Waangaliwe. Waheshimiwa Wabunge, hili liliulizwa na Col. Saleh Ali Farrah, Mbunge wa Rahaleo. Zipo sababu nyingi zilizosababisha hali hii Jeshini ila zilizo kuu zaidi ni zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, utaratibu uliopo wa utoaji mafungu, fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida Serikalini ni utaratibu wa *cash budget,* yaani fedha hutolewa kulingana na Makusanyo ya Mapato ya Serikali na sio kutegemea maidhinisho pekee na hutolewa mwezi kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, Katika utaratibu huu, hakuna hakika ya kuwa *full funded,* yaani kupata malipo ya kutosheleza kwa migao yote ya mwezi. Mara nyingi *exchequer reliase* huwa chini ya wastani uliokadiriwa. Sasa shida zilizoko Jeshini wakati mwingine kuna shida za ghafla tu, zinazuka, matumizi lazima yaendeshwe. Kwa hiyo, inabidi tuingie katika madeni kama hayo. Lakini vile vile kuna baadhi ya madeni ya miaka ya nyuma ambayo kwa bahati nzuri Wizara ya Fedha ilisema itayalipa.

Sasa hayo nayo bado tuna tatizo nalo, lakini hivi karibu yanakwisha.

Tatizo lingine ni la kutosimikwa mtatandao wa malipo katika Jeshi zima ili kuhakikisha hati za malipo zenye fedha. Zoezi hili limefanyika kwa vikosi vya Dar es Salaam peke yake na hali ni nafuu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ninaposema mtandao wa malipo Jeshi zima, ni kwamba, anayelipa Tabora huku Dar es Salaam aonekane kwamba kalipa. Au anapotumia Tabora huku Dar es Salaam ili uweze kumdhibiti kwamba wewe unalipa una hela? Sasa mpaka tutakapokamilisha mtandao tuliouanzisha Jeshini bado kama hali hiyo inaweza ikajitokeza. Lakini kwa kiasi kikubwa hali imeadilika na ni ya nafuu zaidi.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni kutokana na asili yenyewe ya utendaji wa kazi za kijeshi, hujitokeza dharura nyingi kama nilivyozungumza hapo awali.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa tuliyoyapokea leo haya ndiyo ambayo mlikuwa mmechangia na naendelea kusema kwamba nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kupitia kwako, wewe mwenyewe kwa jinsi ambavyo umetusaidia kupata mawazo mapya.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishieni hakuna tutakachokidharau, hakuna tutakachokinyanyasa, tunakwenda kuyafanyia kazi kwa kuzama zaidi kwa kina ili tuhakikishe haya yanaendelea kuboresha hali ya Jeshi letu la Wananchi na kwamba haya yanaendelea kuboresha hali ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 38 – Ngome**

Kifungu cha 1001 –*Administration and General* … … … … shs 189,569,241,000/=

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote 38 - Defence, programme 10, sub-vote 1001*, kifungu kidogo 250100 - Mshahara wa Waziri. Nataka ufafanuzi mdogo tu. La kwanza,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo, nitakuruhusu kwenye fungu la Wizara kwa sababu hapa hakuna mshahara wa Waziri. Mshahara wake upo kwenye fungu 57, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Utaongea wakati huo na ninyi Waheshimiwa wengine kama mlikuwa mnauwinda mshahara wa Waziri, ni kwenye Fungu la 57 ndilo la Wizara.

Wizara hii muundo wake ni hivi, kuna Wizara fungu 57 - Ngome. Maana yake ndiyo Jeshi lenyewe. Fungu 38 halafu na fungu 39 ni Jeshi la Kujenga Taifa, ndiyo mgawanyo huo. Kwa hiyo, nadhani hata Mheshimiwa Kaboyonga, Mheshimiwa Zungu wote mnasubiri mshahara wa Waziri.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu cha 1001 – *The National Service Force* … … … … … shs 45,608,996,000/=

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. *Vote 39, programme 10 - National Service Force, sub-vote 1001*, *item* 260800 *Training Expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii kupitia kwenye Bajeti ya Wizara ya Fedha, nilifanya hivyo baada ya wewe na Naibu Spika kunipa maelekezo kwamba unaweza ukagusa Wizara yoyote kupitia Bajeti ya Waziri wa Fedha na Waziri Mkuu.

Pamoja na mambo mengine ambavyo nimechangia, lakini nilikuwa sijapata majibu yangu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, ninaomba ufafanuzi hapa kuhusiana na Jeshi la Kujenga Taifa katika upande wa mafunzo ambayo wamekuwa wakipewa vijana wetu.

Kwanza nianze kwa kulipongeza Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Wizara hii kwa mafunzo ambayo wamekuwa wakiyatoa kwa vijana, kwani yamekuwa yakiwasaidia vijana kupata mwongozo wa kulinda nchi yao. Lakini vile vile wamekuwa wakipata mafunzo mbalimbali ambayo yamekuwa yakiwasaidia maishani ikiwa ni pamoja na ajira, ujuzi na mambo mengine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia nilisema kwamba utaratibu huu wa kuandaa vijana wetu ili waweze kupata ajira pamoja na ujuzi ni mzuri. Vijana ambao wanapata mafunzo kupitia katika Jeshi la Kujenga Taifa wamekuwa wakifundishwa mambo mengi, ikiwa ni pamoja na kutumia silaha, kujilinda na maadui na mbinu mbalimbali ambazo zinawawezesha wao kulinda nchi. Lakini wakati huo huo kama wanataka kufanya mambo tofauti na nchi yao, basi wanaweza kufanya vitu vya hatari zaidi.

**WABUNGE FULANI:** Swali, swali…

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Nina dakika tano za kuelezea.

**MWENYEKITI:** Kweli kabisa. Hakuna mtu yoyote anayeweza kukuzuia. Ni Spika peke yake anayeweza kukuzuia.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijana hawa wamekuwa wakipata mafunzo haya na baada ya hapo wanapata ajira, labda Jeshini, *TANAPA*, Uhamiaji, Bandari na Makampuni mengine binafsi. Wasiwasi wangu mimi ni mmoja, kwamba, sehemu hii sawa ni nzuri inaandaa vijana. Lakini pia tusipoangalia sehemu hii ndiyo ambayo inapelekea vijana wetu baadaye kuja kugeuka na kuwa majambazi na zile pesa ambazo zimetumika kuwapa mafunzo vijana hawa, pesa ambazo ni za Serikali yetu zinatumika vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, wana mpango gani ama mikakati gani ambayo wameiweka ya kuwachukua vijana hawa kulingana na mahitaji ambayo wao kama *JKT* wanawahitaji. Yaani watoe

mafunzo haya kwa idadi kwamba tunahitaji vijana 100, baada ya mafunzo vijana 20 watapelekwa *TANAPA*, 20 watapelekwa Bandari na vitu kama hivyo ili tusilete tu vijana wengi tukawapa mafunzo bila kujua kwamba baadaye watakapokosa ajira watakuja kutumia mafunzo yao vibaya.

Juzi tu hapa kulikuwa na malalamiko ya vijana wengi tu ambao walikuwa hapa nje ya Bunge kama 60 ambao mkataba wao umesitishwa na Jeshi hili la Kujenga Taifa. Wenyewe kwa midomo yao na masikio yangu nimewasikia wanasema Mheshimiwa tumeshafundishwa jinsi ya kutumia silaha, jinsi ya kupambana na maadui kila kitu kuhusuiana na mambo ya Jeshi, leo unaturudisha nyumbani unatuambia kazi hakuna, tutakwenda kufanya nini na tumeshalitumikia Jeshi hili kwa muda wa miaka minne mfurulizo? Wamepata mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwamba, Serikali inawafanya nini vijana ambao imekuwa ikiwaacha na tayari wameshapata mafunzo? Je, kuna utaratibu ambao Serikali imeuweka huko wanakokwenda, kujua ni nini watakachokifanya? Labda mtagundua na majambazi wengine wanatokea huko! Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu, alilijibu. Ni vyema Waheshimiwa Wabunge tukarejea katika madhumuni ya kuanzishwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa. Madhumuni ya Jeshi hili ni kufuta ukabila, matabaka, kuleta umoja wa kitaifa na kuwaandaa vijana kujiajiri kwa kuwapa stadi za kazi. *(Makofi)*

Lakini vile vile uunganishe na Sera ya Ulinzi ya nchi hii. Sera ya Ulinzi wa nchi hii ni ulinzi wa umma, ndiyo maana tunaandaa Mgambo. Kwa maana hiyo, itabidi na Mgambo nao tukishawafundisha tuwape kazi, si nao wameshajua silaha? Lakini vile vile tukumbuke sisi sio peke yetu, hatuishi Kisiwani katika dunia hii. Nchi nyingi duniani zina mpango wa *National Service*, nenda Israel, nenda Egypt tena ni lazima, nenda Marekani wanafanya *National Service*. Sasa kama itakuwa kila kijana anakuja *National Service* lazima apate kazi, sio kweli. Mkataba hausemi hivyo. Kama hao aliokuwa anazungumza nao Mheshimiwa Amina Chifupa, wakakwambia sisi tumetelekezwa ghafla, kwa hiyo ndiyo maana tunasema wameshatufundisha silaha, basi ni *failure* labda katika utaratibu wenyewe wa kuwafundisha. Itabidi tukae tujichunguze tuangalie tunawafundishaje hawa vijana mpaka watoke na mawazo yaliyotarajiwa. Hayo ya kwenda kusema sasa tumeimarika, tunakwenda kuvamia nchi na kuwa majambazi, sio kweli. *(Makofi)*

Hao vijana uliokuwa ukizungumza nao Mheshimiwa Mpakanjia, ni vijana waliomaliza Mkataba na kwa hiari yao, wakawa wanaingia Mkataba wa miezi sita sita na *JKT*, wakati huo Jeshi la Kujenga Taifa linawapa mkataba wa miezi sita sita kwa sababu walikuwa na *contracts* nyingi za kujenga. Tumejenga nyumba za Dodoma za Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri. Kwa hiyo, ikawepo kazi ya kufanya, imekwisha, unaendeleaje kubaki nao?

Ukaja wakati wa kuajiari Jeshini, mwaka huu Serikali imetutengea nafasi za ajira 2000. Ndani ya 2000,elfu moja tumewapa Jeshi la Kujenga Taifa, waliokuwa na sifa stahili wamepata kutoka *JKT*. Wao wamekosa kutokana na upungufu wa sifa. Wakaja hapa tukazungumza nao, wananiambia pale, sisi tumekaa tunaona watoto wa wakubwa ndiyo wanaochukuliwa. Nikawaambia sawa, niambieni mtoto wa mkubwa mnayemfahamu kama ni Askari Jeshi nichukue hatua, kama ni mwanasiasa nimpelekee Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mimi siamini kwamba yupo mkubwa ambaye yeye mwenyewe anajua ukubwa wake kaupata kwa kusoma, leo hii akubali mtoto wake aishie Darasa la Saba ili asubiri nafasi ya kuvizia kwenye Jeshi. Walishindwa kunipa! Baadaye wakasema labda watoto wa ndugu zao. Mwishoni wakasema sasa Mheshimiwa Waziri tuchukulie sisi ni watoto wako, hebu tusaidie. Unafanyaje? Kwanza tupo hapa hatujala, tunaomba utusaidie hata Sh. 20,000/= au utupeleke Makutupora tukale. Makutupora chakula kinatolewa kwa *ration*, nitawapalekaje wakale? Kwa hiyo, badala ya Sh. 20,000/= nikatoa hela yangu mwenyewe Sh. 30,000/= nikawapa ili wakale. *(Makofi)*

Nikawaambia, ninyi ni viongozi sasa. Kaeni na wenzenu kule nje, mjiorodheshe, tujaribu kuangalia vyanzo vingine vya ajira, wakasema sawa. Wakajiorodhesha 235 na wakati najibu hoja za Waheshimiwa Wabunge hapa nimejibu kwamba kwa bahati nzuri kuna mwajiri mmoja ambaye ametukubalia kuwachukua vijana wote 235 na kwa kweli amenipa nafasi 250. Nimefanya kazi ambayo kwa kweli sikupaswa kufanya kwa sababu tumeshawapa stadi, wangepaswa kwenda kujitegemea. Lakini kutokana na mazingira yalivyokuwa na Bunge linaendelea, tena wakaenda kuzingira hata nyumba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wangu, nikaona bora nichukue hatua hii. Sasa bado Mheshimiwa Mbunge anauliza, mimi nifanyeje? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilidhani Mheshimiwa Amina Mpakanjia, maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanatosheleza. Bado naona hujatosheka na maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nina swali moja. Nimemwelewa vizuri Mheshimiwa Waziri labda na yeye pia atakuwa kidogo hakunielewa kile ambacho mimi nilikuwa nakitaka na kama amenisikiliza vizuri, wakati nilipoanza nilianza kwa kumpongeza na nimeipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa mafunzo ambayo wamekuwa wakiyatoa kwa vijana na nimeelezea baadhi ya maeneo ambayzo huwa wanaajiriwa. Lakini swali langu ni kwamba, naomba nieleweke, maana hata jana nilikuwa nauliza Mheshimiwa Waziri pia hakunielewa na leo kama nitakuwa sieleweki nitasikitika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anielewe, najua kwamba Serikali haiwezi kuwatafutia vijana ajira lakini swali langu la msingi ni kwamba, kwa sababu kule ambako walipokuwa wanawapa mafunzo wamewafundisha jinsi ya kutumia silaha, kwa hiyo, hata kama ndiyo wataondoka, ajira hawatapata. Mmeweka mpango gani au mkakati gani wa kuwafuatilia tena hasa wale ambao wamefukuzwa Jeshi kwa utovu

wa nidhamu, unafikiri watatoka wakiwa wanaipenda nchi yao kama walifukuzwa kwa utovu wa nidhamu na tayari wamekwishajua jinsi ya kutumia silaha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana kama hawa ambao wanaondoka kwa tofauti kama hii, wameondoka kwa kutoelewa na Jeshi mmeweka mpango au mikakati gani ya kuwafuatilia na kujua kwamba hawajihusishi katika vitendo vibaya? Hili ni Jeshi la Ulinzi, kwa hiyo mnatakiwa pia muweke ulinzi. Kwa hiyo, swali langu ndiyo lipo hapo, naomba majibu?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Ulinzi halishughuliki na usalama wa raia. *(Makofi)*

Mimi ninahakika, Usalama wa Raia wana mipango madhubuti ya kuendelea kuwalea wananchi wazuri na wale waovu wanawachukulia hatua zinazostahili za kisheria. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu cha 1001 – *Administration and General*… … … … … … Sh. 5,615,258,000/=

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana, *vote* 57, *programme 10, sub-vote 1001*, kifungu kidogo kingine 250100-Mshahara wa Waziri. Wakati tunachangia, tulizungumzia juu ya uboreshaji wa maslahi mbalimbali ya wanajeshi.

Mimi nataka kupata ufafanuzi juu ya mikakati iliyopo katika Wizara hii kuhakikisha kwamba familia za wapiganaji wetu ambao wanafanya kazi nzuri sana kutulinda katika nchi hii wanapoanguka wakati wa shughuli mbalimbali za kulinda nchi hii, au sehemu nyingine. Kuna mkakati gani wa kutunza hizi familia? Baadhi ya miongoni mwao baada ya wao kufariki kwa mfano inakuwa ni tatizo zaidi kwa familia ambazo zimebaki. Sasa je, kuna *Insuarance Policy* ya aina yoyote ile ambayo inaweza kusaida familia hizi? Hilo la kwanza.

La pili, nimeangalia katika vitabu hivi, Jeshi siku hizi linajishughulisha pia katika mambo ya uzalishaji mali kama ujenzi. Mimi nilifikiri kwamba baadhi ya fedha ambazo Serikali inalipa Jeshi kwa ajili ya kujenga kama nyumba za Magufuli zilizojengwa juzi, labda fedha hizo zingeonekana hapa kama *retention* ambazo Jeshi lingeweza kuzitumia. Lakini sioni mahali popote pale ambapo kuna *retention* ya aina yoyote. Kwa hiyo, mapato kama hayo yanakwenda wapi?

La tatu, ni kweli Mheshimiwa Waziri amejibu juu ya Meremeta kwamba imefilisika na atatoa bilioni kadhaa kulipa watu wa Geita. Kinachonisikitisha mimi ni kwamba inaonekana kuna *box* la fedha ambazo mtu anaweza akachukua tu akalipa kwa

makosa aliyofanya. Unapochukua Shilingi bilioni mbili kutoka *treasury* ndiyo kusema kuna bilioni mbili kwa ajili ya elimu. Sasa mimi nataka kuelewa kuna mikakati gani ya kuhakikisha kwamba Jeshi halijiingizi katika mambo ya kibiashara na vitu ambavyo vinaweza kuviletea Taifa hili hasara kama vile Meremeta inavyofanya?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Cheyo kwa kuguswa na matatizo wanayopata familia za Marehemu wapiganaji wanaobaki. Kwa kweli ni tatizo ni sugu, lakini moja ya hatua tunazozichukua ni kuhakikisha kwamba tunasaidiana nao kuhakikisha kwamba wanapata mirathi yao mapema.

Lakini kama nilivyosema kwamba, wakati mwingine tunapata matatizo kutoka ndani ya familia zenyewe, tunategemea vilevile kwamba jinsi mapato ya Serikali yanavyozidi kuboreka, Hazina wanavyoendelea kubadilisha *pension scheme* zao, ndiyo jinsi ambavyo familia za Marehemu nao wataendelea kupata unafuu. Lakini hatuna Bima za familia hizi. Lakini ni wazo ambalo tunalipokea na kwenda kuangalia kama linawezekana na utekelezaji wake uweje.

Fedha za ujenzi kubaki kama *retention,* kwa bahati mbaya hatuna utaratibu huo. Bado fedha inayopatikana inakwenda katika mfuko wa Serikali. Sasa tumesikia, kama tutaona tunaweza tutajenga hoja, tuone kama inawezekana, lakini mpaka sasa bado ni mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujiingiza katika biashara na kupoteza Shilingi bilioni mbili, nadhani labda bado tunaendelea kujifunza kwa sababu utakumbuka tulikuwa na sera ambayo Serikali ilikuwa inafanya mambo yote ya kutafuta hela, ya kufanya biashara na ya kufanya zile kazi za kawaida za Serikali. Mpaka tukafika mahali tukabadili mfumo, sasa haya ni mabaki tu ya falsafa kama ile.

Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Cheyo kwamba kwa mazingira tuliyokwishayajenga ndani ya Jeshi hivi sasa, suala la Jeshi kujiingiza katika biashara halipo na halitakuwepo. Isipokuwa Mashirika ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa sababu yale ni mashirika ya kiuchumi na kuzalisha na mapato yanabaki nayo yenyewe yanapanga matumizi yake yenyewe, yanakopa na kukopesheka, yakikosa yanashitakiwa kama mashirika mengine. Sasa kwa sababu tunalo jukumu la kuhakikisha kwamba vijana tunaowapata tunawafundisha si tu stadi za kazi pamoja na ujasiriamali, tunaomba hiyo kazi katika mashirika yetu ya kiuchumi ya Jeshi la Kujenga Taifa yenyewe iendelee, lakini ndani ya Jeshi *proper*, ndani ya Serikali *proper* hapana.

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu la 57, *sub-vote*, 1001, *item* 250100. Nataka ufafanuzi tu kidogo na ndugu yangu kama anakumbuka, niliwahi kumwandikia barua juu ya hali ya wanajeshi wa Biharamulo na leo hii nilipochangia kwa maandishi nilimwambia kwamba wanajeshi wa Biharamulo wanaishi katika vijumba vilivyojengwa kwa matope enzi za Twiga *Brigade*. Vijumba hivyo ni vya hovyo na havitoshi. Nikasema, Mwanajeshi aliyeoa anachangia nyumba na wanajeshi

ambao hawajaoa, nadhani hiyo ni hatari nikamwambia hivyo. Katika kujibu sikusikia hilo.

Pia, nikasema kwamba wanajeshi kwa kweli hawana usafiri wa kwenda kazini na kurudi. Mara nyingi unaona wamezagaa zagaa barabarani wakati wa kwenda Jeshini pamoja na kurudi, kwa mguu. Nalo hilo sikupata jibu, lakini pia nasema kwamba posho zao na hasa zile posho za chakula zinakuja zimechelewa, wanapata shida sana. Ndugu yangu naomba nipate maelezo kwa hayo machache.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyotuelekeza wewe jana, naomba kwa idhini yako Mheshimiwa Naibu Waziri ajibu haya maswali.

**MWENYEKITI:** Mambo mazuri haya.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Kabuye kwa hoja hizi ambazo ameziuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na lile la nyumba. Kama nilivyoeleza kwamba tuna mpango mzuri kushirikiana na mashirika ya fedha ya ndani na nje ili kuwajengea wananchi au wanajeshi wetu nyumba za kuishi na kama nilivyoeleza, *design* za nyumba ambazo tunataka kujenga tayari michoro tumeshachora, itakuwa na vyumba vitatu na chumba kimoja ni *self contained* kwa ajili ya wale ambao wameoa, ninamwomba Mheshimiwa Kabuye awe na ustahimilivu kidogo, hili suala tunalishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la usafiri Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kwamba, tunatarajia kupokea magari 628, ambayo tayari yameshanunuliwa na Serikali kwa ajili ya wanajeshi wetu na kuomba vilevile ustahimilivu, magari haya yatakapofika tutaangalia jinsi ambavyo usafiri ulivyo katika eneo ambalo unalizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la posho ya chakula kuchelewa, hili tunalichukua na tunalifanyia kazi kuona kwamba posho ya chakula isichelewe katika maeneo yote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *Vote* 57, *Programme* 10, *Sub-vote* 1001, Kifungu cha 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia katika hoja hii, miongoni mwa yale ambayo niliyachangia yalikuwa ni kuhusu usafiri wa Kaboya pamoja na kufahamu mipaka ya Vikosi vya Jeshi. Kuhusu Usafiri, kati ya hayo magari 628 ambayo Wizara imeagiza, Mheshimiwa Waziri amenihakikishia kwamba yatakapofika, wataliangalia Jeshi la Kaboya kupatiwa *bus*. Napenda nichukue nafasi hii nimshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niombe basi anisaidie kuhusu mipaka. Kambi ya Kaboya kwa sasa hivi imezingirwa na Vijiji. Nilivitaja Vijiji kadhaa. Sasa wasiwasi

wangu ni kwamba, wananchi wanaoishi katika vile Vijiji vinavyoizunguka ile Kambi, hakika hawafahamu mipaka yao mwisho ni wapi. Kwa hiyo, wanaishi kwa mashaka, hawafahamu ni lini ambapo wanaweza wakaambiwa waondoke.

Je, Kambi ya Kaboya na yenyewe imepimwa ikathibitika mipaka yake? Wananchi wanaozunguka maeneo hayo, ni lini watakapoweza kufahamishwa mipaka yao kusudi waweze kuacha kuingilia mipaka ya Jeshi na Vijiji vile ambavyo wananchi wanaishi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi kuhusu mipaka huko Kambi ya Kaboya na Vijiji!

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako, naomba kwanza nipokee shukrani za Mheshimiwa Ruth B. Msafiri kuhusu mambo ya usafiri. Ningeomba kwanza nifafanue la usafiri hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kulipa na mpaka wakamilishe mzigo wa mwisho wa magari hayo 628, tutachukua miaka mitatu. Sasa isije ikawa mwaka kesho tukaja kubanana hapa, uliniahidi, uliniahidi! Naomba tueleweke kwa sababu kama tunavyolipa kwa *instalments*, nao ndio wanatengeneza magari yale, kwa sababu gharama yake ni kubwa. Kwa hiyo, mpaka kufika mzigo wa mwisho, itachukua miaka mitatu. Naomba hili lieleweke na Mheshimiwa Phares K. Kabuye vile vile alielewe hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kuhusu mipaka, nilipokuwa nikizungumza, nimesema, zoezi la kubaini mipaka ya makambi yote ya Jeshi linaendelea hivi sasa. Katika Bajeti ya mwaka huu, tumetenga fedha za kuendeleza zoezi hilo. Lakini, kama hatua za muda mfupi, namuagiza Mkuu wa Kambi ya Jeshi ya Kaboya, hebu akae na wananchi wake, awafahamishe mipaka ya Kambi ya Kaboya mpaka hapo tutakapokuja kuweka mpaka ambao ni wa kudumu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, kumbe bado! Mbona liko wazi kabisa!

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo dogo tu la ufafanuzi. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, ametoa maagizo kwa Mkuu wa Kambi ya Jeshi ya Kaboya. Lakini ombi langu, isije kuwa ile amri tu anapoitoa, pale pale wananchi wanashurutishwa kuondoka. Naomba hilo niliseme ili isije kuwa ni matokeo ya amri hii, halafu ikaonekana kwamba ni vurugu. Taratibu zichukuliwe ili kuonekana kwa mipaka ile kueleweke kwamba ni kujulikana mwisho wa mipaka na *then* utaratibu unaoeleweka wananchi watakwenda wapi ueleweke vile vile kwa mujibu wa hali ya maelewano.

**MWENYEKITI:** Nina hakika haya yatazingatiwa na Wakuu wa Jeshi zima wako hapa wanasikia.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* 57, Proramu ya 10, *Sub-vote* 1001, Kifungu kidogo 250100 – Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alilieleza Bunge kuwa Meremeta ni Kampuni iliyoundwa ili iweze kuipatia mapato Serikali. Kwa sasa Waziri amesema, Kampuni hiyo imefilisika. Je, yuko tayari kulieleza Bunge hili, Wakurugenzi waliosimamia Kampuni hiyo hadi ikafilisika? Pili, Je, kama Kampuni imefilisika, ni lini itatangazwa mufilisi ili Watanzania wanaotaka kuinunua wanunue? La mwisho: Je, ni hasara kiasi gani Kampuni hiyo ilililetea Taifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aloyce Kimaro, la pili, kwa sheria za nchi yetu, Kampuni ikiwa mufilisi hainunuliki. Ni kwamba kilichosalia kinagawiwa kwa wenye hisa. Kwa hiyo, huwezi kununua Kampuni iliyofilisika. Utaratibu wa kufilisi ni kwamba Kampuni inakabidhiwa kwa mufilisi. Ile albaki iliyopo inagawiwa kwa uwiano kwa wadai na ikibaki labda kwa wanahisa, basi.

Mheshimiwa Waziri, labda la kwanza na la pili la kuuliza Wakurugenzi ni nani.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hilo nije nimuwasilishie kwa maandishi baadaye kwa sababu kwa kweli sina majina yao kichwani. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* 57, *Programme* 10, *Sub-vote* 1001, Kifungu Kidogo, Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka maelezo tu ya kuwa katika *events* na matukio ya majeshi. Kuna Askari hupata maradhi ambayo huitwa *Post War Traumatic Stress Disorder* na ni maradhi ambayo Askari hukaa nayo kwa miaka mingi sana kwa kuweweseka na kupata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua tu kama katika Jeshi letu kumetokea *incidents* kama hizi na kama zimetokea, walisaidiwa vipi kwenye *counselling* na kutibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua, ni lini sasa Serikali itakuwa na mpango maalum wa kuanzisha kitengo maalum cha *Search and Rescue*, kusaidia wananchi wanapopata matatizo kwenye Bahari au kwenye nchi kavu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo nilichangia lilikuwa Kikosi chetu cha Anga *Service* cha Ndege za Vita, Ndege zake zimepitwa na wakati. Ni lini sasa Serikali itakuwa na mpango wa kubadilisha hizi *Mid19* na kununua ndege ambazo zinakwenda na Jeshi lenyewe lilivyo?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, la tatu siwezi kuliruhusu kwa sababu linahusu kubainisha aina ya silaha za nchi yetu na nadhani hatuwezi kulizungumza hapa.

Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo labda ile *Syndrome* ya Wanajeshi kuharibikiwa na kuvurugikiwa baada ya vita ni *psychological* na kuunda *Search and Rescue* Kikosi. Sijui kitakuwa Usalama wa Raia ama kwako, sijui sasa!

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi. Ile ya tuseme kama mfadhaiko wa aina fulani, ilipata kutokea na Kitengo chetu cha Saikolojia *(Psychiatry)* kiko imara, kinakaa nao kwa muda mrefu. Kinajaribu kuwarejesha katika hali ya kawaida. Tulifanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivi sasa tuna baadhi ya wagonjwa wamelazwa katika Hospitali ya Lugalo wana matatizo hayo, wanaendelea kuhudumiwa. Sio vizuri kutaja majina, lakini wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hii ya *Search and Rescue Team*, ninaweza labda nikafananisha na jinsi ambavyo tunashiriki katika maafa kama jinsi ambavyo Treni ilivyoanguka, kama jinsi ambavyo madaraja yanabomoka, jinsi ambavyo majengo yanaanguka na matukio mengine ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini nimesema azma ya Serikali sasa, ni kujenga Kikosi Maalum Kabisa ambacho kinaweza kuwa na mwitikio wa haraka mambo kama hayo yanapotokea. Tunakusanya nguvu kuhakikisha kwamba hicho Kikosi tunakijenga. Hivi sasa tunafanya kazi hizo lakini kwa utaratibu wa kawaida. Ila, bado iko haja hiyo na sisi tumeishaitambua na tumeishaanza kujiandaa.

**MHE. SIRAJU S. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutaka ufafanuzi ufuatao kutoka kwa Waziri Mhusika wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi letu la Ulinzi katika moja ya Vikosi Muhimu ilivyonavyo, ni Kikosi kilichoko Tabora. Umuhimu wa Kikosi hiki ni pamoja na pale ilipojitokeza tulipokuwa na mapambano na Nduli Amin. Kikosi hiki ndio kilikuwa cha Kwanza kwenda Mstari wa Mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kihistoria, kiwanja cha Ndege cha Tabora, ni kiwanja cha Jeshi. Historia hii iko hivyo, akina Mzee Kingunge wanaweza kutusaidia kuiweka sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki ni kiwanja historia yake ni ya kijeshi. Tabora ni Makao Makuu ya Komandi moja Muhimu sana ya Jeshi. Ni mahali ambapo mvua zikinyesha, ndege zikitua zinazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili Jeshi letu likae vizuri, ninataka ufafanuzi. Serikali inaonaje kama ingelikiweka kiwanja hiki chini ya Mamlaka ya Jeshi kama ilivyo historia na kwa maana hiyo, ikitengeneze katika misingi ya kijeshi, hata kama ndege za raia zitatua, lakini tutajua kwamba ni cha kijeshi. Sababu tunazo nyingi. Hatuwezi

kuweka kiwanja kizuri cha kijeshi Mwanza, hatuwezi kukiweka Kigoma kwa sababu ya *Strategic Nature* ya Ulinzi wa Nchi. Tabora ni mahali muafaka. Naomba ufafanuzi juu ya suala hili kutoka kwa Waziri anayehusika. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hapa lazima Spika a-*declare interest*. Nadhani ni muhimu sana kiwanja hiki kiweze kuwekwa lami. Ni dhahiri tu, lakini Waziri labda una mawazo! Nadhani hata wewe utafurahia! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Ndugu yangu Mheshimiwa Siraju S. Kaboyonga. Aliligusia hili, mimi nikafikiri anazungumza habari ya kiwanja cha kuchezea mpira ambacho nilikuwa najua kwamba *traditionally* ni cha Jeshi, kinaitwa Vita *Stadium*, kumbe alikuwa anamaanisha habari ya kiwanja cha Ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha viwanja vilivyojengwa hivi sasa, viwanja karibuni vingine vyote, historia yake ni ya kijeshi. Vyote! Sasa, baada ya mabadiliko na kuingia katika Utawala wa Kiraia, viwanja vile vikaingizwa katika utaratibu wa kumilikiwa na Wizara ya Miundombinu hivi sasa, ambayo ilikuwa inaitwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefanywa hivyo makusudi kwa sababu ukikifanya kiwe kiwanja cha Jeshi, kutakuwa na *restrictions,* yaani kupangwa kwa matumizi ya aina fulani fulani kwa sababu Jeshi lina utaratibu wake wa namna unavyoweza kutumia maeneo yake, ambavyo mimi nina hakika ndugu zangu wa Tabora na mimi mwenyewe hatutapenda. Tungependa kiwanja hiki na hasa kama tutafanikiwa kupata amani ya kudumu Kongo, Burundi na Rwanda, kiwe ni kitovu *(hub)* cha kufufua uchumi wa Tabora. Ndege zitue na kuondoka zinavyotaka. Leo tupate amri ya Kamanda mmoja anasema: “Nasema mwisho ndege saa 12.00.” Itakuwa matatizo, tutakuja kulaumiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani, Waheshimiwa Wabunge wa Tabora, tusaidiane na mimi nikiwa mmoja wenu kujenga hoja, kuiomba Wizara ya Miundombinu itusaidie kujenga kuhakikisha kiwanja hiki kinapata lami. Hilo tuko pamoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninamwona Waziri wa Miundombinu yupo na anatabasamu. Labda anataka kuongeza kitu hapa! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba hiki kiwanja kiko chini yangu na ni kati ya viwanja ambavyo tunavitafutia fedha na ufadhili na mambo haya yakikamilika tutaendelea kukitunza kwa mujibu wa taratibu za kuendesha viwanja vya kiraia. *(Makofi)*

*(Kifungu Kilichotajwa hapo Juu Kilipitishwa na Kamati bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 1002 – *Finance and Accounts...* ...... … … … … … … … 126,676,900/=

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* 57, *Sub-vote* 1002, Kifungu kidogo 310300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia kwa maandishi na Mheshimiwa Waziri katika kujibu mawazo ambayo tulikuwa tumempa, alikiri kwamba wanajeshi hao wamewekewa utaratibu wa kupewa mikopo kupitia kwenye *Branch* moja tu ya Akaunti moja ya Wananchi ambayo iko Dar es Salaam. Sasa ninaomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri, wanasaidiwaje wanajeshi ambao wako Mikoa mingine ya nje mbali na Mkoa wa Dar es Salaam kwa kupatiwa mikopo kama hiyo? Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu maelezo madogo.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nampongeza Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa kwa kuguswa sana na jinsi matatizo ya mikopo yanavyoendeshwa katika Jeshi la Wananchi. Nimesema tunatambua tatizo hilo kwamba kwa kweli wana Benki moja tu, tena iko Dar es salaam. Tumeishalipokea, tukitoka hapa tunakwenda kukaa tuangalie namna ambavyo tunaweza tukawakwamua na wale walioko Mikoani waweze kukopa hata katika Benki nyingine. Lakini, ni vitu ambavyo lazima viwekewe utaratibu wa kueleweka.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 1003 – *Policy and Planning ... ...* Sh. 196,793,700/=

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamatiya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2001 – *Industries, Construction and Agriculture ... ... ...* 184,521,400/=

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu nami nihoji kidogo *Vote* 57, *Programme* 20, *Sub-vote* 2001 yote. Kwanza, napenda nikiri kwamba Jeshi letu ni zuri na Waziri pamoja na Msaidizi wake wanafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Napenda kwa niaba ya wananchi wa Busanda na wafanyakazi wa Meremeta, nishukuru kwa niaba yao kwa fedha zilizopelekwa kwa *DC*, nadhani ananisikiliza na atafanya kazi mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuchangia, kuna wazo nilijaribu kutoa na lilikuwa linanikereketa kwa muda mrefu. Nina imani kwamba Jeshi linapokaa, lina mambo yake mengine ambayo yanahusu umma yanaweza kuwa wazi lakini kuna mengine ambayo yanaweza kuwa ni siri yako *concealed* kwa sababu hayahitajiki kuonekana wazi wazi, mafunzo na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikiangalia Dar es Salaam, kwa mfano, Mgulani, Lugalo, wakati vinawekwa mahala vilipo vile vikosi, kulikuwa hakuna wananchi waliokuwa wanazunguka.

Sasa hivi wameshakuwa *encroached* na wamewazunguka sana. Sasa nilikuwa nimetoa wazo, hivi Serikali ina mpango gani kuanza kufikiria labda ili hawa wanajeshi kwa mfano hata Mgulani, kuanza kuafikiria kuwatafutia mahali pengine pazuri, kuwawekea miundombinu ili waweze kufanyakazi zao zaidi na nyingine ambazo sio lazima zionwe na kila mtu, waweze kuwa kule.

Kwa mfano, sasa hivi Lugalo, mahali pa kufanyia *range*; *range* unakuta wakati mwingine ni kati kati, inakuwa ni shida sana na shughuli zao za dharura. Nilikuwa nafikiri, Mheshimiwa Waziri Je, wazo hilo analifikiria?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nimekuhurumia tu. Ulichouliza hakifuatani kabisa na kifungu hiki. Lakini kwa sababu leo Spika kidogo amekuwa rahimu kupita kiasi, basi tuendelee. Waziri, naomba ufafanue!

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Nakushukuru tena kunipa nafasi na nampongeza Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba kwa kuona kwamba angalau sasa tumechukua hatua sasa ya Meremeta. Nadhani akirudi huko, atapokelewa vizuri tu. Matatizo tumeyamaliza.

Kuhusu suala la Lugalo na Mgulani kuwa katikati, hili ni Jeshi la Wananchi popote litakapokwenda, hatimaye litazungukwa na wananchi. Nimetoka Marekani juzi kwa nafasi ambayo nilipata. Nimekwenda kutembelea *Pentagon*. *Pentagon* iko katikati ya Mji wa *Washington* na imezungukwa na wananchi.

Kwa hiyo, uimara wa kutunza siri sio umbali unaokaa mbali na watu, ni mafunzo wanayoyapata na ya kuthamini nchi yao. Hii ndiyo kazi tunayofanya. Lakini vile vile suala la *range*, sidhani kabisa. Yuko Kamanda ambaye anaweza kuthubutu kuamrisha *Range* ipigwe pale Mgulani au ipigwe pale Lugalo.

Tunachukua tahadhari, tunakwenda maeneo ya mbali. Kama jinsi ilivyo hata hapa Dodoma, hatuwezi kupigia *range* hapa Mjini, tunapigia mbali. Hata pale Makutupora penyewe, hatupigii *range* pale pale Makutupora, tunakwenda mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunao utaratibu wa kujua maeneo ambayo yako salama katika kupiga *range*. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Dar es Salaam na maeneo mengine yote ambayo tuko karibu na Miji, tutahakikisha kwamba tunakwepa mahali ambapo raia wapo.

Lakini vile vile ukihamisha makambi haya sasa, gharama yake anabeba nani? Uhamishe Mirambo, uhamishe Lugalo, uhamishe Mgulani, Uhamishe Kaboya hiyo imezungukwa, yaani maeneo yote ya Jeshi yameshazungukwa. Itakuwa ni kazi ngumu sana na ni mzigo mzito ambao haubebeki hata kwa Mnyamwezi. *(Makofi/Kicheko)*

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu cha 1001 – *Administration and General* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 200,000,000/=
Kifungu cha 1001 – *The National Service Force* ... ... ... ... ... ... ... ... 200,000,000/=
Kifungu cha 2001 – *Industries, Construction and Agriculture*... ... ... 45,844,989,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2006/2007 Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha Bila Mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Makisio ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 01.23 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 04 Agosti, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*